**MONASTERI YA UTATU MTAKATIFU**
**OROPOS YA NJIMBO ATIKI**
**GREKIA (HELLAS)**

# ZAWADI YA WENYE ZAWADI

## KITABU YA TATU

**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE**
**KOLWEZI KONGO**
**2000**

## MWANZO

Zawadi ya Roho Mtakatifu ni mengi, kwa sababu na chemchem ya hile inatokea haikauke.

Mpaka sasa tunasoma ndani ya vitabu wa wili na jina umoja zawadi tisa. Hii zawadi inatoka ya Mungu. Kama itaingia neema ya Roho Mtakatifu ndani ya nafsi ya mwaaminifu moja orthodoksi, iko namna na huu mukristu kuwa mufazili na atapokelea ma faida ya zawadi ya Mungu.

Hii Kitabu wa tatu inatuelejea maonyesho ya zawadi wa fazila ya mbalimbali, na hii mafazila ni matendo ya Roho Mtakatifu.

# ZAWADI YA MA FAZILA

Mtume Paulo, mu barua wa kwanza kwa wa Korinto anaandika ma zawadi ya mbali mbali, kabisa bile ni ya kufanya matendo ya Kanisa. Anaandika pale ya kama zawadi ya ma fazila inatwaambia kabisa ya kama mukristu moja ni mukamilifu kama alipanda pa hii chogo. Vile anaandika: «Kama nikisema na lugha za watu na za malaika, lakini sina mapendo, nimekuwa kama shaba inayolia, ao upatu wa kuvuma. Na kama ikiwa nina unabii, na kufahamu siri zote na maarifa yote; na kama ikiwa nina imani yote, hata niweze kuhamisha milima, kama sina mapendo, mimi si kitu». (Wa Korinto 13, 1-2).

Basi, zawadi ya kusema ma lugha mengi, unabii na ufahamu wa fumbo, maono, mafunuo na miujiza, bila mapendo si kitu. Ni kusema hakuna maonyesho mazuri ya kama mukristu moja ni mtu muzuri na mukamilifu. Zawadi ya Mapendo ni chogo ya ma fazila yote, ni njia wa kweli na paka moja mu uzima wa Roho Mtakatifu.

Tena Mtume Paulo anatufundisha mu barua kwa WaGalatia (5, 22-23): «Lakini matunda ya Roho Mtakatifu ni mapendo, furaham salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, ujizuiza, hakuna sheria juu ya maneno ya namna hii».

Tena na Mt. Grigorio, askofu ya Konstantinopoli, vile anaandika mu kuhubiri yake, hile alisoma kwa lufu ya mt. Mutawa Efremi wa Siria: «Huyu mtakatifu alimaliza uzima usafi katika nafsi na mwili yake na hii ilikuwa zawadi ya Neema ya Mungu.. . »

Tena na mt. Mutawa Yoano wa Mugazi (Klimakos) anatufundisha hivi: «Hata mtu moja ahipashwe kuwaza ya kama alitenda hii uzima kitakatifu paka na nguvu ya ke. Hakuna namna mtu moja kushinda hali ya asili ya mwili yake, pasipo saidio ya Mungu.. . »Huyu aliyekamata mpango kugombana juu ya kushinda nguvu mubaya ya mwili yake, paka na nguvu ya maungo yake, anapashw akujua ya kama anakombana na anachoka kwa bure.. . Anafanya sala usiku na kigungo ya chakula kwa bure.. . ». Acha kwa Bwana Yesu Kristu mambo na zambi na ma zoezo mbaya ya mwili na uzima yako, sikia na famia ya kama nguvu yako ni kwa bure na kisha utachukua zawadi ya imani na saidio ya Mungu. Kisha Mungu atakupatia zawadfi ya uzima ubikira.

Kila fazila inaitumika mtu moja paka na nguvu kimutu, ni kusema bila tendo na neema ya Mungu, ni ya bure. Nabii Isaya anaweka ngambo ingine fazila inayetokea ya Mungu na fazila inayetokea ya mtu, anapaza sauti kusema: «Wa ngapi sisi wote tuko wasiyo safi na fazila yetu, bila neema ya Mungu ni kilako moja ya bure!

Katika fundisho ya mt. Nikolaos wa Kavasilas ma fazila ni zawadi hile inapandisha rohoni yetu Roho Mtakatifu katika Fumbo ya Kupakaa (Khrisma). Watu wingi walipokelea hii Fumbo pa umri yao ukubwa na hawakusikia zawadi gani Mungu aliwapatia. lakini hii zawadi, ni sawa begu ndani ya nafsi yao, kama watatumika muzuri ma fazila ya Mungu kufatana mapenzi Yake, iko namna kuleta na matunda mazuri.

Mulimaji ya mafazila ni Mungu, lakini mambo juu ya kuivya na kunenepa hii matunda inatokea ya mapenzi ya kila mukristu.

# MAPENDO

## «Mapendo yangu (Kristu) amesulubiwa»

Mtakatifu Ignatios Mumebaji wa Mungu, askofu ya muji Antiokhia wa Siria alijaza roho yake na mapendo kwa Mungu! Aliishi kabisa ndani yake neema ya Kristu, kwa sababu alimufuata na alitumika Kwake. Tena na jina lake maana ni moto, inatwaambia ya kama huyu alimupenda Kristu kabisa.

Wakati mutawala ya Roma Trayanos alipita ku mwaka 107, kisha ujalio ya Kristu mujini Antiokhia hile wakati ya nvita yake kupigana taifa wa Armenia, askofu ya hii muji Ignatios alisimama mbele yake na alikikisha, bila woga, imani yake kwa Yesu Kristu! Mutawala Trayanos alihamuru askari yake amubamba na amupeleke ya kufungwa mikono yake mu mji Roma kusudi kumutupa ndani ya ma nyama makali kwa kumukula.

Mt. askofu alimushukuru Mungu, kwa sababu katika mateso na lufu yake ataenda na haraka Kwake! Tena mara moja hivi ataonyesha na mapendo ukamilifu iliyekuwa ndani yake kwa Mungu. Joo vile, hile saa askari walimuvaa minyororo pa mikono yake huyu askofu alisikia furaha na shangilio munene ndani yake.

Wakristu wote waliisha kujua ya kama askofu wa muji Antiokhia walimupeleka mu Roma juu ya kumukula ma nyama makali. Hile muda askofu alipata «hatari» moja: Aliogopa kwani waaminifu wakubwa wa Parokie ya Roma, walifanya nguvu katikati na wakubwa ya Serkali (Inchi) yao juu ya kumutosha ya kifungo na kumuokoa. Huyu askofu alifanya nini? Aliandika barua moja, na aliwajulisha matakio munene yake hile ilikuwa ndani ya roho yake juu ya kufa kwa mateso ya mbalimbali kwa jina ya mapendo ya Kristu. Hivi aliandika: « Ninajulisha kwa wakristiani wote ndugu wangu ya kama, katika mapenzi yangu ninatembea njioa ya mateso.. . Ninamiomba, mapendo yenu haipashwa kuwa kizibiyo.. . Muniache kutimiza mimi matakio yangu kusudi kunikula kinywa ya nyama makali.. . Mimi ni gano (bego) ya Mungu na nitajitwaga na meno yao juu ya kuwa hivi mukate utamu na usafi mbele Yake! .. . Basi, musinizibiye kufata hii njia. Muacheni ma nyama, tena muwasukume juu ya kuja kwangu na kunikula na haraka.. . Ni faida yangu munene kwa kufa ya Kristu na hapana kutawala mu dunia mzima.. . Kama ma nyama watasita, mimi nitawasukuma juu ya kunibambna na kunikula.. . Muniacheni kuwa na mimi mufwasi ya Kristu wangu.. . »Mapendo yangu (Kristu) amesulubiwa.. . ». Basi, musinichukie wokovu yangu.. . Muniacheni kuteswa kwa ajili ya Kristu wangu».

Safari yake kutoka Antiokhia mpaka muji Roma ilikuwa urefu na miezi mengi. Kila siku mt. Ignatios aliteswa kwa ajili ya askari, wenye walimupeleka ya kufungwa na alipima mateso yake mpaka hile siku wa mwisho yake.. .

Mu tarehe 20 Mwezi ya kumi na mbili (Dekembrio) ku mwaka 107, ailijiongoza mu theatre Kolosieo ya Roma. Ma kiti ya ke ilikuwa na watu wingi. Zamu alifungula ma nyumba ya ma nyama makali.. . Kisha saa kidogo hile fasi ya theatre ilijaza na damu ya mushahidi mkubwa ya Mungu mt. askofu Ignatios.

## Wimbo ya mapendo kimungu

Mu Kitabu kizuri inaitwa: «Wimbo ya mapendo kimungu» ya mt. Mutawa Simeon wa Theologos Mupya (949-1022) anaandika matendo wa siri ya huyu mukristu alimupenda Mungu. Vile aliandika juu ya maungo yake:

Nilisikia sawa kilonda
ndani yangu kabisa kwa mapendo kimungu,
ninaomboleza, ninajilugua

mu akili na roho yangu.

Ninatembea na ninajilugua,
ninamutafuta hapa na kule,
lakini misiweze kumupata
Mupendwa ya nafsi yangu.

Ninapindula ma fasi yote ma macho yangu
kwa kuona Mupendwa wangu,
lakini Hule, Musiyeonekana,
anafuchama kwa siri.

Na, kwani ninalia na ninachungu
kumupata bila kitumaini,
kwa rafla anaonekana mbele yangu,
ninamuona na ninafurahi.

Ninashagaa kwa kuangalia
uzuri na utukufu kubwa yake,
wa shangilio na kimungu.

Ndani chini ya roho yangu
inajaza na mwangaza makao ya roho yangu
na chumba yangu pempeni
inajaza na nuru kimungu!

Alinimbatia, alinijaza
na neema isiyokusema,
mapendo na utamu
uzuri na furaha mnene.

Ninachukua katika roho yangu nuru
na uso yangu inaangaza
na inafanyika sawa uso ya Mupendwa wangu!

Na niko na mimi mkubwa
katikati ya dunia mzima
kwa utukufu, uzuri
mali na sifa wa Kristu.

## Wenye kuungana kwa uzima wa milele

Uwili kitakatifu Galaktioni na Epistimi walikufa katika mateso mengi ku mwaka 250, mu muda ya Mutawala ya Roma Dekios.

Waliishi sawa watawa pa Mulimani Sinaya na hile wakati kwa rafla mkubwa ya Serkali moja aliingia nyumbani yao na alimubamba Mukristu Galaktioni. Wakati alisikia hii mambo bibi yake Epistimi, alionyesha mapendo wa uwili wake: Alienda na haraka mukongo yake juu ya kumusidikiza kwa hile saa ya mateso yake, bila kuwaza hatari hile na yeye ilikuwa namna kupata. Alimukuta hile saa ma askari walimupeleka ya kumufungwa na alimwaambia na machozi:

-Tulikuwa sisi na uwazo na akili moja mu uzima yetu. Vile tunapashwa kubakia mpaka mwisho ya uzima yetu! Ninataka na mimi kukufa pamoja na weye kwa mapendo ya Kristu. Vile tutabakia na maungano na kisha lufu yetu na tutapata utukufu wa milele na shangilio.

Wa askari mara moja walimubamba, walimufunga na walimuongoza na huyu mbele ya mkubwa yao.

Hule ku mwanzo alihamuru kumupiga bwana wake Galaktioni na fimbo. Bibi yake, Epistimi, hasikuweze kuvumilia hii angalio. Mapendo yake nguvu ilimusukuma kupaza sauti na kusema:

-Ee Muzulumu musiyewema, usitaabu huyu kijana mwanaume, aliyeisha kukonda sana, kwa ajili ya uzima utawa wake mu jangwa?

Mkubwa alisirikia kwa ajili ya sauti ya bibi yake na alihamuru kumutosha manguo yake yote na kisha kumupiga nguvu.

Kisha alihamuru kupigilia misumari ya sibala ndani ya makucha ya miguu na mikono yao. Kisha hii mateso matata, ya kwanza waliwakata mikono na kisha muguu yao, kisha ulimi na ku mwisho vichwa vyao!

Vile, wote wa wili walistahiliwa kubeba pamoja ma taji wa utukufu. Ukumbusho yao Kanisa yetu inashangilia mu tarehe 5 ya Mwezi ya Kumi na moja.

## Muzee moja mugeni.. .

Wakati moja padri mutawa Agathon alikwenda mu muji kusudi kuuzisha vitu vyake na kununua mukate ya maisha yake. Karibu ya soko alipata mtu moja mskini, muzee na mwenye kilema.

-Kwa jina ya Mungu, ee ava (padri ya roho mkubwa), usiniache mimi bila saidio. Inibebe karibu yako.

Padri Agathon alimwaambia aikaa karibu yake, pa hile fasi aliisha kuweka vituga vyaka juu ya kuuzisha.

-Makuta wa ngapi ulibeba mpaka sasa, ee ava? Alimuuliza huyu muzee, wakati padri aliuzisha kituga wa kwanza.

-Makuta fulani, alimujibu padri Agathon.

-Ni muzuri! Hakuna namna kuninunua kitubula moja? Vile na Mungu atakubariki. Tangu jana usiku misikukula mara ingine.

-Na furaha mingi, padri alimujibu na alimutimiza mara moja matakio yake.

Kisha saa kidogo aliomba matunda, kisha kintu moja wa utamu. Vile padri, kisha kila kituga aliiuzisha, hule muzee wa kilema, alimuomba na kintu moja juu ya maisha yake. Ku mwisho aliuzisha vituga vyote na aliisha na makuta yake yote juu ya kununua vitu vya kula hule muzee. Mambo kabisa kubwa ni hii: Ya kama huyu padri alifanya hii kazi na mapendo mingi, bila huzuni ya roho zake na alijua ya kama atabaki huyu padri, bila mukate juma moja mzima!

Wakati aliuzisha na kituga yake wa mwisho alitayarisha vitu vyake kwa ondoko.

-Unaondoka sasa? Alimuuliza hule muzee wa kilema.

-Ndivyo, niliisha sasa kazi yangu.

-E, sasa utaonyesha mapendo ingine. Utanichukua na utanipeleka pa ribeka yako mpaka hile mupadanjia na kisha weye unaingia mu jangwa yako, alimuomba hule muzee mugeni.

Padri Agathon alimuweka pa ribeka yake na alimupeleka na ugumu mingi, kwani aliisha kuchoka kwa kazi yake tangu asubui.

Halafu, wakati walifika mu hile mupandanjia na alikuwa tayari kushusha chini uzito yake, alisikia toka mbingu sauti moja utamu:

--Ee Agathon, uwe mubarikiwa toka Mungu pa hii inchi na mbinguni.

Alinyanyua Mutawa ma macho yake yulu kuangalia nani alimwaambia hivi. Lakini mara moja huyu muzee aliisha kukimbia! . Alikuwa malaika ya Mungu, aliyemutuma Mungu kusudi kupima mapendo ya padri Agathon.

## Utoleo wa ngamia

Mutawa moja wa jangwa alituma mu mji mtoto wa roho yake juu ya kupanda mu fasi (mukini yao) ngamia (nyama) moja.

Hile saa alirudia huyu mtoto wa roho wake, alijikuta pa njia na mutwa mwingine wa jangwa, jirani yake, na huyu alimwaambia:

-Namna gani mimi misikukuone ya kama ulikwenda mu muji! Nilitaka kuniletea na kwa mimi ngamia moja kusudi niende na mimi na nyama yangu vituga vyangu mu soko ya kuuzosha.

Huyu mtoto wa roho alisema hii sauti kwa padri ya roho yake. Hule alimuhamuru mara moja amupatie hii ngamia yao kwa hule jerani na atamwaambia ya kama vitu vyao sisi tutapeleka na namna ingine.

-Uende pamoja naye mu mji na ngamia yetu; kama itaisha kazi yake ya kupeleka vitu vyake, kisha rudisha weye nyama na kisha sisi tutapeleka vitu vyetu mu soko.

Mwanafunzi wa roho aliitii na mapendo. Wakati aliisha ndugu yao kazi yake na ngami yao, kisha mtoto alibeba nyama na alimurudisha nyumbani yao juu ya kufanya na kazi yao.

-Wakati walifika mu soko, mtoto alibeba ngami na alianza kurudia. Jirani ndugu yao, alimuuliza huyu mtoto: ee, ndugu, unaenda wapi sasa?

-Ninaenda mkongo mu mukini yetu, juu ya kupeleka na vituga vyetu.

Hule mutawa mwingine alishangaa kwa hii mapendo ya ndugu wengine, kwani waliacha kazi yao juu ya kusaidia ya kwanza ndugu yao.

Wakati huyu mutawa jirani, aliisha kazi yake mu soko na alirudia jangwani, alienda kwa ndugu mwingine, alipika magoti mbele yake kwa shukrani kwani aliacha kazi yake na alifanya ya kwanza mapendo kumusaidia.

## Mukate wa sasa

Mutawa moja wa mukini (Skiti) ya jangwa aligonjwa wakati fulani na alitakia kula mukate kidogo wa sasa. Lakini atapata wapi mukate wa sasa ndani ya jangwa?

Mtawa moja kijana, wakati alisikia matakio ya hule mutawa mgonjwa, aliweka ndani ya mufuko yake mikate yake ya kukauka na alienda mu muji Aleksandria ya Msiri. Muji ilikuwa mbali kutoka jangwa ma siku wa wili kutembea na miguu. Huyu mutawa kijana, hasikuwaze muchoko yake! Paka aliwaza namna gani ataleta mikate wa sasa kwa hule mutawa mugonjwa. Aliacha hile mikate ya kuisha kukauka na alibeba mikate wa sasa nalirudia mu mukini yao mu jangwa.

-Ulipata wapi hii mukate wa sasa? walimuuliza na musagao ndugu wengie.

-Mu mji Aleksandria, aliwajibu kijana.

Wakati alisikia hule mugonjwa ya kama huyu mutawa alitembea ma siku wa wili juu ya amuletee mukate wa sasa, alikataa kuichunga hii mukate.

-Namna gani nitakula? Alisema. Hii mukate ni damu ya ndugu wangu!

Lakini ndugu wengine walimusukuma akule, juu hapana kupotesha hule mutawa kijana sandaka ya mapendo yake!

## Mapendo wa kweli

Wakati moja, mtoto wa roho yangu moja, anatweleja padri mutawa Zosimas, alinikaribia na aliniambia:

-Padri na baba wa roho wangu, ninakupenda sana!

-Mpaka sasa, nilimujibu, hasikuonekane mtu moja, mwenye anipende, sawa vile ninamupenda mimi. Sasa, unasema, ya kama unanipenda, na mimi ninasadiki. Lakini, kama

nitafanya kazi kimoja fulani, na hile wewe hautafurahi kwa hii kazi yangu, utabadilisha tabia yako mbele yangu. Lakini mimi, kila kazi kama utanifanyishia, nitabakia paka na tabia moja na nitakupenda daima.

Haikupite wakati mingi na mimi, bila kujua, alianza huyu mtoto wa roho yangu nichabula na matusi mbaya sana, mbele ya watu na watawa wengine. Mimi nilisikia hii matusi na machukio yake na nilisema ndani yangu: «Huyu ndugu ni moto ya Mungu». Mungu alinituma juu ya kuponyesha nafsi yangu, kwani ndani yangu ni utukufu wa bure. Huyu atanisadiai sana! Lakini, wale wananitukuza na ma sauti vizuri, hakuna namna kunisaidia. Basi huyu ni musaidizi na mufazili yangu».

Basi, nilimukumbusha na mu Kanisa na mu sala yangu sawa muganga wa roho wangu. Nilisema tena na kwa wale waliniambia matusi yake kupigana yangu:

-Ananichabula hivi, kwa sababu anajua paka zambi yangu hile inaonekana. Na hii zambi hasijue yoyote. Kama atafamia na zambi  yangu, hile haionekane, atasema nini?.. .

Kisha wakati ingine, alinikuta mu muji Kesaria. Katika zoezo yake, alikuja kwangu, alinimbatia na alinibusu, sawa  haikukuwe kintu katikati yetu. Vile, alifanya, kila wakati alinikuta na mimi misikumuonyesha uchungu ya roho yangu, lakini nilisikia matusi na ma sauti yake mabaya hile alisema kupigana yangu, katika watu wengine, wale waliniambia.

Lakini hii mara, alianguka mbele ya miguu yangu, aliikamata na aliniambia:

-Ee Muzee, baba wa roho wangu, unihurumie kwa jina ya Bwana Yesu. Mpaka sasa nilisema ma sauti mengi na wa matata kupigana yako.

Mimi nilimusimamisha, nilimubusu na nilimwaambia na furaha:

-Unakumbuka zamani, wakati uliniambia ya kama unanipenda? Mimi nilikujibu ya kama hasinipenda hata mtu moja sawa vile mimi ninamupenda? Tena nilikuwaambia ya kama, kama na weye utanichukia, mimi mitaendela kukupenda. Basi, sikia, sasa, ya kama hii matusi na ma sauti mabaya kupigana yangu ninajua yote, lakini misikusimamisha kukupenda! Misikuseme hata sauti moja mubaya kupigana yako mbele ya watu wnegine. Niulisema paka ma sauti mazuri juu ya weye. Lakini na ndani yangu nilichunga sifa hile nilikuwa zamani juu ya weye! .. .  Na, kama unataka kunisadiki sikia mambo moja wa ajabu: Siku moja richo yangu ilikuwa ugonjwa. Nilikukumbuka. Nilifanya pa richo yangu alama ya msalaba na nilisema: «Bwana Yesu Kristu, kwa maombezi ya ndugu wangu, uniponyeshe». Na mara moja niliponyeshwa! Basi, unashaka, juu ya mapendo yangu mbele yako?

## Mapendo ya padri mkubwa moja

Padi mkubwa ya monasteri moja, mweshimiwa na mufazili, alifanya kila siku hii sala:

-Bwana wangu, ninakuomba, usiniepuke toka watoto wangu wa roho mu uzima ingine wa milele, lakini unistahili kupata wote pamoja uzima wako wa milele Paradizoni.

Siku moja, alimujulisha Mungu ya kama kila mtu anatayarisha yeye wa pekee katika matendo yake, fasi ya utukufu yake mbinguni.

Ilikuwa karibu Siku Kuu mu monasteri moja wa pempeni na padri ya hile monasteri alimuita aende na kundi ya watawa wake mu monasteri ingine. Alikamata mpango hapana kwenda, kwa sababu  hasipende kufusifu kule. Lakini siku moja ya mukongo, alisikia ndani ya musingizi yake sauti moja na alimuhamuru aende bila kusita mu monasteri ingine ya Siku Kuu yake, lakini mbele atatuma kundi ya watawa wake na kisha ataenda na yeye. Padri mkubwa (Igumeni) alisikia hii amri kimungu.

Asubui mapema, alihamuru wanafunzi wa roho wake waende mu monasteri wa pempeni. Pa njia yao walipata muzee moja mupotevu. Walimuuliza mambo yake:

-Niko mugonjwa, aliwajibu na muchoko na maombolezo. Nilienda kwa munganga na punda yangu, lakini, wakati nilifika pa hii njia, punda yangu aliniangusha chiki. Na mimi misijue

juu ya nini alikuwa mukali na aliniangusha chini. Na mpaka sasa haikuonekana mtu moja kwa kunisaidia ya kusimama!

-Watawa walimujibu: Ee Muzee, sisi tutakufanyshia nini? Tuko mu njia na inapaswa kutembea na haraka.

Waliendelesha njia yao juu ya kufika kwa Siku Kuu ya monasteri ingine mukuacha katikati ya njia ndugu wao hule muzee mskini.

Kisha saa kidogo, alipita ya kule na padri mkubwa yao. Aliona hule muzee na hali kimbaya. Alinamisha yulu yake na mapendo. Alisikia mateso yake na alimuuliza na musangao:

-Muzuri, lakini hawakupite ya hapa, mbele ya saa kidogo, watawa vijana? Juu ya nini ulikataa kuwasimamisha wakusaidie? Ao, wale hawakukuone?

-Ndivyo, waliniona na waliniuliza, lakini waliniambia ya kama ni wenye safari na haraka na hawakuweze kwa kunisaidia.

Padri mkubwa alipata huzuni ya roho mubaya, alisikia haya kwa ajili ya watoto wa roho wake.

-Kama mimi nitakusaidia, utaweza kutembea?

-Hakuna namna kutengwa, padri wangu.

-Basi, kuja, nitakupandisha pa ribeka yangu, alimwaambia padri mkubwa na Mungu atatusaidia kufika pa hile fasi unaenda.

-Usiweze kunipeleka pa mabeka yako, kwa sababu njia ni murefu. Na weye uko muzee, isiwe kihana. Uende, Ava, mu kazi yako na usipotee saa yako. Umuombe paka kwa Mungu anisaidie.

-Misitakuache hivi pa hii hali yako, aliumujibu padri mkubwam mtu ya Mungu. Nitakupeleka mu muji!

Na muchoko mingi alimupandisha pa ribeka yake. Uzito ya mwili yake ilikuwa ku mwanzo munene sana. Na ugumu mingi alitembea pa njia, pole-pole. Kisha saa kidogo ilifanyika tendo moja wa ajabu. Uzito yake ilishuka pole-pole mpaka ilitoka ya ribeka ya padri mkubwa. Padri alinyanyua kichwa yake kuona mambo nini ilifanyika. Aliona nini? Pa hile fasi aliikaa hule muzee, aliikaa sasa malaika moja!

-Bwana Yesu alinituma juu ya kukujulisha, alimwaambia, ya kama paka hivi watastahiliwa wanafunzi wako kuishi na weye mu Ufalme Wake, kama watafata mwendo na matendo yako. Kama hawa hawatafanye hivi, wewe unaomba kwa bure. Mungu analipa kila mtu katika matendo yake.

Hii sauti alisema malaika ya Mungu na aliluka mbinguni. Padri mkubwa alirudia mu monasteri yake na mawazi mengi kusudi anza ushindani ingine mupya. Ilizimishwa tena kazi mingi juu ya kufundisha mapendo kwa wanafunzi wake.

## Padri mkubwa ya Khozevas

Padri moja muzee toka jangwa ya Khozeva ya inchi Palestini, wakati aliishi mu mukini yake, alienda kwa siri usiku na alirima na ma nyama yake, na bego yake ma shamba ya wamaskini waliokuwa ndani ya hii mukini yake.

Wakati alikuja mu jangwa na aliikaa mu chumba moja ya hile fasi Khozeva, kila siku alitembea hile njia inaenda kutoka muji Yerikho mu mji Yerusalema. Na, kama alikuta musafiri moja pa njia, alibeba vitu vyake na aliipeleka mpaka mulima ya miti Muzeitini. Kisha, alirudia pa hii njia juu ya kupeleka na vitu vya watu vingine, wenye walitembea hii njia na aliipeleka mpaka mji Yerikho.

Basi, uliona hule mutawa muzee kupandisha bile bintu pa mabeka yake, na muchoko na kutosha jashu, bila kupotesha kitumaini yake. Wakati ingine alipeleka na watoto wadogo. Wakati

ingine aliikaa na alitengeneza vilato vya wenye walisafiri, kwa sababu alikuwa na vitu vya hii kazi karibu yake.

Tena alikuwa na karibu yake kila siku mukate na maji kusudi kusaidia wale walitembea pa njia. Kama alikuta maskini moja, aliyevaa manguo mabaya, alimupatia nguo yake. Kama, tena, alipata na mufu moja, alimusoma ibada ya kuliyo yake na alimuzika.

## Mutumwa moja wa ajabu

Mu karne (milele) wa tano mu inchi Bulaya (Europa) taifa moja iliyeitwa Vandali, kwa mapiti yao katikati ya ma icnhi ya Bulaya, alibomoa kila kintu waliipata mbele ya ma macho yao. Inchi Italia iliteswa kupita. Ma muji yake mazuri walibomowa moja-moja na mustari yao. Vandali, watu mabaya na wanyanganyi walibamba mataifa ya Bulaya na waliwauzisha mu Afrika.

Pa hile miaka wa ngiza, askofu ya muji Kambania ya Italia, aliyeitwa Pavlinos, alitoa mali na uriti yake yote juu ya kununua watumwa na kuwapatia uhuru yao. Lakini hii kazi kibaya ilikuwa munene sana, na, kama huyu askofu, alibakia hata na manguo ya mwili yake, hakuna namna kusaidia watu watumwa wingi.

Siku moja alienda kumukuta mwanamuke balaka moja na huzuni ya roho yake mnene. Wanyanganyi walimubamba mwana wake wa pekee na sasa alikuja kwa askofu na aliomba makuta juu ya uhuru yake. Maombolezo yake walipasula tena na ma njiwe, sawa vile tunasema!

Hule askofu alimusikia mambo na sikitiko yake na aliliya pamoja naye. Alitafuta mara wa wili ndani ya nyumba yake kintu kimoja, lakini hakuna kitu. Kwa rafla ilikuja mu akili yake moja ingine uwazo nzuri.

-Unaona na weye, alisema kwa hule mama, ya kama misina na kitu juu ya kusaidia mtoto yako. Kama hii saa nikona kintu kimoja ni paka maungo yangu. Ninaitoa maungo yangu juu ya kubeba wetu karibu yako mtoto wako mupendwa.

Hule mama alishituka! Alizania ya kama huyu askofu alimuchekelea na alianza kuliya sana. Askofu alimwaambia amufate. Walienda pamoja kwa hule mkubwa munyanganyi, aliyekamata mtoto yake. Askofu alisema kwa hule mukubwa kumufunga na kutosha ya kifungo hule mtoto ya huyu mama.. .

Askofu mt. Pavlinos pamoja na watumwa wengine aliongozwa mu Afrika. Wakati wanyanganyi walifanya kazi ya kukabula watumwa wao, huyu askofu alimubeba mu kazi yake bwana arusi ya mkubwa ya Vandali na alimuwaambia kutumika ma shamba yake.

Askofu alianza kazi yake na mapendo mingi. Kila siku alileta pa meza ya mkubwa yake boka muzuri na matunda ya mbalimbali. Kwa ajili ya tabia nzuri yake na kazi wa mapendo yake mkubwa yake alianza kumusifu. Mara mengi alienda huyu mkubwa ma shamba na walisuburia pamoja. Huyu munyanganyi alishangaa hekima na akili ya mutumwa wake. Pole pole ilifanyika urafiki moja nguvu katikati ya mutumwa mugeni (askofu) na mkubwa wake.

Kisha wakati fulani mt. Pavlinos alisema kwa mkubwa yake na namna ya siri:

-Ni wakati kuwaza juu ya kutengeneza ku mbele ufalme wenu.

-Juu ya nini unasema hii sauti? Alimuuliza na musangao mkubwa yake.

Ku mwanzo alikataa kumwelejea, lakini kisha alimwaambia ya kama Mungu alimujulisha lufu ya mkubwa yake itakuwa karibu. Mkubwa yake hasikusadiki, lakini alisema hii sauti ya mutumwa wake (askofu) kwa mume mwake. Hule alitaka kumufamia huyu mutumwa wa ajabu, mwenye, alisema, ya kama anasuburia na Mungu wake.

-Kuja, kesho tutakula pamoja na mimi nitakuletea mutumwa yangu, alimwaambia bwana-arusi yake.

Siku ingine mfalme alenda nyumbani ya bwana-arusi yake. Mt. Pavlinos, sawa alizombelea kila siku, aliwaletea matunda wa sasa. Wakati mfalme alimuona alishituka.

-Huyu mtu anafuchama fumbo moja wa ajabu na wa siri! alisema pa risikio ya bwana-arusi wake.

Wakati askofu alichofa, mfalme alimuelejea ndoto moja aliiona usiku iliyepita.

-Niliona ya kama walinipeleka ya kufungwa mu nyumba ya uhukumu juu ya kuangalia na kuhukumu matendo yangu yote nilifanya mu uzima yangu. Katikati ya Waamuzi, waliyekuwa wingi, alikuwa na huyu mtu. Alionyesha ya kama alikuwa na kiti kinene na cheo urefu, kwa sababu alihamuru askari kutosha ya mikono yangu kitu ya mamlaka yangu na kisha kunipiga na hii kitu. Basi, umuulize, akuwaambia mutu gani ni huyu? Ni kweli, ya kama huyu si eko sawa watu wengine.

Bwana-arusi yake alishangaa juu ya hii sauti ya mume mwake. Alimuchofesha kidogo mutumwa mwake na alianza amuulize nani eko, inchi yake na mwanzo kizazi na kazi yake.

-Mimi ni mutumishi wa Mungu, alisema mt. Pavlinos, na weye ulinipokelea kunichunga pa fasi ya kijana moja ya mama balaka, aliyekuwa kwako na mimi juu ya kumuuhuru mwana wake wa pekee.

Mkubwa yake lakini, alikataa kusadiki ma sauti ya askofu. Tena alimulapa na malapo manene juu ya kusema kweli. Vile, askofu alimwaambia kweli ya kama alikuwa askofu ya katika mapenzi yake, alijitoa mutumwa kwa mapendo ya ndugu wake.

Wakati alisikia hii ma sauti ya askofu mkubwa wake, alimueshimu na alianguka chini, mbele yake, na alibusu miguu yake! Kisha hii jambo ya uzima yake aliijulisha kwa mume mwake. Na kisha wote wa wili pamoja, walimwaambia:

-Utuombee kila kitu unataka na sisi tutakutuma na zawadi wingi, kwani weye uko kweli mustahili, mu inchi yako. Kwa sababu haina muzuri kuchunga sisi hapa mutumwa moja, sawa weye.

Mt. Pavlinos aliwashukuru juu ya huruma na roho nzuri yao, lakini alikataa kubeba zawadi yao.

-Haina lazima kubeba zawadi, kwa sababu haitanilazimisha. Lakini, kama munapenda kweli kufanya kazi kimoja kizuri, muwapatie kwa wa ndugu wangu wote, wenye ni watumwa wenu, uhuru wao.

Wakubwa wa wili waliitika mara moja na furaha. Walitafuta mu ufalme wake pa fasi gani walikuwa na walitumika watumwa na wa ndugu ya mt. Pavlinos. Waliwasanyika wote, waliwaweka pa chombo na waliwatuma mu inchi yao pamoja na askofu mustahili yao. Tena waliwapatia na chakula ya kuachana na zawadi mengi.

Kisha saa kidogo ilitimizwa unabii ya askofu. Mfalme alikufa na alimufata mufwasi wake, bwana-aruri yake. Na huyu mu uzima yake yote alikumbuka hii sandaka wa mapendo alionyesha askofu Pavlinos juu ya watoto wa roho yake.

## Mapendo ya mbali-mbali

Muhubiri mkubwa padri Venediktos Petrakis (+1961) alikuwa na karibu yake musaidizi mwenye nguvu bwana Ilia Ksenos, aliyeishi kisha umri yake miaka 55 mu Mulima Takatifu na alifanyika padri muzee ya nyumba ya watawa «Mt. Spiridon» mu mukini Skiti Mupya. Huyu bwana Ilias, wakati alikuja mu Mulima Takatifu, alifanyika mutawa na padri na jina yake Spiridon. Huyu anatuelejea juu ya padri ya roho yake Venediktos:

«Padri Venediktos alitumika bila muchoko na ukimya juu ya watu wote na mambo yote.

Wakati mapadri ya njimbo Etolokarnania ya inchi Grekia (Hellas) walienda mu Athina kufata mafundisho juu ya kazi yao. padri Venediktos, aliwasalimia na aliwagusa pa mabeka yao, kama walivaa manguo wa nguvu. Kama hawakuvaa manguo wa nguvu, yeye aliwapatia manguo yake na mupila na ngochi na aliwaambia kuvaa muzuri mu muji Athina, kwani kule baridi inapita.

Lakini vile, huyu alibaki bila manguo yake na hile wakati ya baridi aliteswa huyu mumoja.

Siku ingine alinisema:

-Suburia na mama Eftikhia juu ya kunifanyishia gochi moja wa inje, kwa sababu ninasikia baridi.

-Ee padri, nilimujibu, tulikupatia mbele ya miezi wa wili gochi moja na nguo nguvi, iko wapi?

-Watoto (wapadri) wale wanaenda mu muji Athina kusikia mafundisho, hawakuvala muzuri na niliwapatia gochi yangu. Tutafanya nini? Tutaacha watoto wetu kupata malari?

Mapendo yake ilikuwa bila mpaka!

Siku moja aliniita na aliniambia:

-Tuna wanafunzi mu masomo wa juu mnane. Tunataka makuta filani juu ya kulipa mu masomo yao, tutapata wapi? Mpaka sasa mimi niliuzi watu watajiri filani kwa kutusaidia. Lakini na wale watatupatia mpaka wakati gani? Basi, omba weye ya wale watu na mimi nitaomba ya wanawake wengine.

Basi, tulilokota makuta 10. 500 na tulikuwa na lazima tena ya 1500 drakhma, nikusema malipo moja ya kila mwanafunzi ilikuwa 1500.

Tunapashwa kutafuta na ingine makuta, aliniambia. Kama hakuna namna nitauzisha msalaba yangu.

Aliniambia juu ya hii Msalaba moja ilibakia kwake na alivaa pa kilari yake ya kila ibada na sala yake mu Kanisa.

Nilimujibu na kisilani:

-Kama utauzisha msalaba wako, nitaondoka mbali yako. Sisi hatuweze kusaidia juu ya kufunda watoto wote ya dunia!

Ku mwisho, bila mimi kujua, hule aliuzisha msalaba wake. Nilimuona mu Juma moja na mu Juma wa wili alifanya Liturgia na kuhubiri, bila kuvaa msalaba.

-Ee padri, msalaba wako iko wapi?

-Mtoto wangu, usisikitike. Sauti na kuhubiri ya Mungu ninaweza kuisema na bila msalaba!

Kisha ma siku kidogo alipata malari kwa homa. Nilienda kumuona na yeye alinipatia kartasi moja mukusema:

-Hii ni nini?

-Uko na, ee padri, kibueta moja mu posta. Nitaenda mu posta kuibeba.

Nilienda, niliipeleka nyumbani yetu na kule tuliifungula. Tuliona nini ndani? Ilikuwa msalaba moja wa kilari ndani, zawadi moja toka askofu wa njimbo Triki na Stages jina lake Dorotheos. Huyu askofu alipata kilonda kwa ajili ya kuanguka na motogari, lakini aliokolewa. Padri Venediktos alimutuma barua kwa wokovu wake. Kisha huyu askofu alimutuma msalaba moja sawa zawadi kwa mapendo na heshima mbele yake.

-Unaona, weye usiyena imani nguvu? Aliniambia mimi p. Venediktos. Nilipatia msalaba wa zamani, nilibeba msalaba mupya.

Siku ingine, anasema bwana Ilias Ksenos, nilimupatia kwake mufuniko ya kitanda wa tano. Nilimwaambia:

-Ee padri, usipatie hii mufuniko ya kitanda kwa watu wengine, kwa sababu iko nguvu ya kutafuta ingine. Mutaichunga hii juu ya kusaidia wa ndugu na wapadri wenye wanakuja kwako.

Na tazama, kisha siku kidogo alikuja bwana Dimitrios Panayotopulos pamoja na wengine wa wili. Alinibeba ba sigo (telefon) na aliniambia:

-Musuburie na mama Eftikhia atuletee mifuniko ya kitanda juu ya usiku wetu.

-Ee Padri, mimi nilimil; etea mifuniko wa tano; iko wapi?

-Alipita mutu moja aliyeondoka ya kifungo (buloko). Nilimupatia hii mifuniko kuuzisha juu ya kununua chakula na vitu vingine ya jamaa yake.

Nilisirika, lakini misikuseme kitu.

Wakati ingine nilienda nyumbani yangu na nilipata mama moja muzee aliyeniongojea inje ya mulango yangu. Padri Venediktos alinichofa kidogo na aliniaambia:

-Hii zulia tuko na yo pa dari ya mbau ya kanisa yetu, uende kuitosha na uipatie kwa huyu mama.

-Lakini, padri, mbele ya nyakati kidogo tuliiuza juu ya dari ya kanisa. Bado kufurahi na yo. Na ndani ya kanisa chini baridi inapita. Utapata malari, bila zulia pa hile fasi unasimama ndani ya Altari Takatifu.

-Fanya hii sauti mimi ninakuwaambia, alinijibu.

Nilienda, niliitosha, niliifunga na kamba moja na niliishusha chini.

-Mama.. . . . .  mtoto wangu, beba hii zulia. Uiuzishe na makuta hile utabeba umupatie kwa binti yako, aliyefunda mu masomo juu ya kulipa deni yake.

Wakati hule mama aliondoka, mimi nilikamata mbau ya mulango na nilipaza sauti kupigana kwake:

-Weye, padri, usitaache hata kintu kimoja huku! Mambo gani unafanya hivi? Sisi tusiweze kutengeneza mateso yote ya watu wote!

-Kuja ndani, aliniambia.

Lakini hakuna namna kumukaribia, kwa sababu alisimama na bakora pa mukono yake.. .

Nilikimbia na haraka na mulango wa mukongo.. .

## Moto ya roho.. .

Mu uzima ya padri mkubwa Athanasios ya Monasteri ya mt. Grigorio ya Mulima Takatifu tunapata jambo wa ajabu kwa mapendo ya padri mbele ya nyama.

Siku moja alishuka toka fasi ya mashariki ya kilima kwa fasi ya Monasteri nyama moja  ya pori, aliyeitwa Kuro! Watumishi wengine, wakati waliona huu nyama walikamata ma bunduki yao na maibwa na walianza kumulubata. Huunyama alikaribia kikavu na, kwa sababu hakuna fasi ya kutembea pa inchi, aliingia na aliogolea ndani ya bahari.

Lakini na walubataji, bila kupotesha wakati yao, walifungula mutumbwi yao na waliingia ndani ya bahari. Walimubamba. Aliisha kuogolea ndani ya bahari kilometre wa wili. Na walianza kumuletea inje juu ya kumua na kukula huu nyama, ili ni utamu sana.

Padri mkubwa Athanasios alipata tangazo ya hii mambo na, aliacha kila ingine kazi yake, na alishuka pa kikavu na haraka. Juu ya nini? Juu ya kuokoa huu nyama ya pori. Aliwaongojea inje ya kikavu na watumishi katika amri yake, waliacha huu nyama arudie mu pori. Hivi alipenda dunia muzima padri Athanasios.

Tendo ingine pempeni na hii jambo ilikuwa na hii:

Ma shamba pahali monasteri ilikuwa na muzabibu alitumika mutawa moja, jina lake Yoanikios. Ndani ya muzabibu, hile wakati matunda yao iliisha kuivya, waliingia ma nyama ya pori, anaitwa mbweha na walikula na waliharabisha matunda.

Huyu mutawa aliweka matego, alibamba hii ma nyama na aliwaua. Tena alitosha na ngozi yao na alifanya vilato.

Hii yote hadisi padri mkubwa Athanasios hasikujue muzuri. Kwa hivi, siku moja alimuita hule mutawa na alimushauria hivi:

-Mtoto wangu, uwaza namna ingine juu ya huu nyama mbweha. Piga ma tuku wazi na mbau moja na hivi nyama watasikia makelele na watakimbia. Haipashwe kuwabamba na matego na kuwaua ma nyama ya Mungu.

Wakati ingine watumishi ya shamba ya hii monasteri ya mt. Grigorio walibamba ndani ya pori watoto wa wili ya imbwa ya pori.

-Ee Muzee (padri mkubwa), walimuwaambia, tuko na kukuonyesha ono moja wa ajabu.

Ni nini hii musagao wa ajabu?

-Tazama, tulipata ndani ya pori hawa watoto wa imbwa muke ya pori. Mbele ya kuwaua, tulimilitea kwako juu ya kuwaangalia na kufurahi.

Padri Athanasios aliwaangalia mara wa kwanza hawa watoto wa imbwa ya pori. Aliangalia miguu murefu yao, singo na pua na maiskio yao.. .  Hawa walisikia woga, kwani walikuwa katikati ya watu wageni. Padri alionyesha wema na huruma yake. Aliwaza umivu na huzuni ya roho ya mama wao.. .  na ku mwisho alisema kwa watumihsi wake hii ma sauti:

-Musikieni! Musiuzi hii watoto-nyama ya pori. Musiwauwa.. .  Mutawaacha warudie mu mama yao mu pori. Mama yao sasa atawatafuta na atakuwa na sikitiko mingi.. .

Watumishi wake, walishangaa na hii sauti ya Igumeni yao, lakini walimutii na waliacha ma nyama wahuru warudie kwa mama yao.

# Usafi

## Mushahidi mwanamuke Efrasia

Mu tarehe 19 mwezi ya Kwanza (Yanuario) Kanisa yetu inashangilia mt. Mushahidi Efrasia.

Huyu Mushahidi aliteswa mu muji Nikomidia ya inchi Turkia wa zamani mu karne (milele) wa tatu (3). Alikuwa toka jamaa kabaila na aliangaza uzima yake kwa uzima ubikira na heshima ya Mungu. Alibambwa kwa sababu alisadiki kwa Kristu na alipata hatari munene kumuharabisha uzima ubikira wake. Alitumia hile saa huyu Binti kijana namna moja wa akili.

Mkubwa ya hile njimbo alimutoa kwa askari moja mukali juu ya kufanya naye, bila mapenzi yake, zambi ya usharati. Hile saa huyu mutu mubaya alimukaribia, mtakatifu Efrasia alimwaambia:

-Kama utasimama mbali yangu, mimi nitakulipa! Nitakupatia dawa moja toka mulozi. Katika hii dawa utaishi na utakombana ma adui yako bila adui kukupiga na bila weye kukufa.

Mafaa ya hule askari ilikuwa sasa munene.

-Kama, tena unataka kusadiki, bila shaka, aliendelea amuwaambioe huyu binti bikira tutafanya moja kipimo. Tazama, hapa ni shingo yangu! Pima. Piga  nguvu na kisu yako na utaona ya kama mimi misitapata hata mambo moja. Nitabakia muzima.

Huyu askari alipima. Alimupiga pa shingo na nguvu yake yote. Kichwa ya mt. Efrasia ilipasukwa na huyu Binti alianguka chini ndani ya damu yake! Lakini sifa yake kwa uzima ubikira yake aliichunga, bila kumuharabisha na zambi hule askari mugeni na mukali.

## Ndege moja na miiba

Hile wakati ya kwanza mu uzima utawa yake padri mutawa Venediktos (480-547) alipima moja jaribu wa mwili matata kabisa.

Ku mwanzo alionekana shetani ya uzini na uso ya ndege moja meushi, aliyeluka pempeni ya uso yake. Aliluka karibu pempeni yake na ilikuwa namna padri kumubamba. Huyu padri alisikia tendo wa shetani; alifanya alama ya msalaba na mara moja ndege alikimbia!

Lakini ilianza bugonvi moja ndani ya roho na akili yake. Kwa sababu padri aliisha kuona zamani, wakati alikuwa kijana, mwanamuke moja, sasa shetani alimuletea uso ya hule mwanamuke mu akili yake juu ya kumulekesha. Padri alikuwa karibu kutoka ya jangwa aende mu dunia. Lakini Neema Takatifu hasikumuache! Alikuja neema ya Mungu. Alimusaidia, alimutosha kizingu-zingu na jaribu ya akili yake na shetani alikimbia. Padri Venediktos juu ya kutesa mwili yake, kwa sababu alipokelea mawazo ya usharati na uzini, alifanya nini?

Alipata shamba moja ya kujaza na miiba mirefu. Alitosha manguo ya mwili yake na hivi mutupu alitelemuka ndani ya miiba. Alijizungusha katikati ya miiba mara mengi mpaka miiba

walimupingilia na mwili yake ilijaza na damu yake. Alisikia maumivu mnene kabisa, lakini alivumilia na damu ilitoka ya vilonda wake.

Shetani ya usharati na uzini, mukuona hii namna kubwa ya padri, alikimbia ma siku zote na hasikumuuzi mara ingine.

## Nyasi ya kukauka na makala wa moto

Wakati moja mu muji Nursia ya inchi Italia aliishi padri moja wa heshima pamoja na bibi na watoto wake. Alifundisha waaminifu ya parokia yake katika woga ya Mungu. Tangu hile wakati alijipadirisha, alisimamisha kila ugano wa mwili na bibi (presvitera) yake. Alimupenda sawa muke yake, lakini aliepuka ya kwake. Hasikupokelee hata saidio moja yake.

Vile ilipita wakati ya miaka maku mi inne tangu upadirisho wake. Aligonjwa mubaya na kivukutu mingi na alikuja karibu ya lufu. Wakati presvitera yake alimuona kuwa pa kitanda sawa wa kupooza juu ya malari na uzee yake, alikaribia kusikia kama aliishi, ao alikufa. Alinamisha, basi, kichwa yake, pa pua ya padri.

Hule padri alipumuzi tena na alisema na sauti chini kwa bibi yake:

-Toka, bibi. Inaishi tena makala ya moto (matakio ya mwili). Chofesha nyasi ya kukauka (toka mbali na mwili yako).

Presvitera alitoka mbali. Kisha saa kidogo alimusikia padri kusema: :

-Wafu wako, wakubwa wangu, wafu wako! .. .  Namna gani mulikuja kwangu musiye stahili?.. .  Niko na kuja.. .  Niko na kuja.. .

Na paka hii ma sauti yake aliingia mu Paradizo.. .

## Jaribu ya mutawa moja wa jangwa

Mwanamuke moja wa zambi alisema kwa rafiki wanaume wake ya kama paka huyu ataweza kukokota mu zambi hule fulani mutawa wa jangwa, aliyeishi mbali ya muji yao na alikuwa na tangazo ya kama alikuwa mtakatifu.

Basi, alivaa nguo murefu na hivi alifuchika uzuri uso na mwili yake na alipanda pa kilima. Warafiki wake walimuongojea katikati ya njia. Ilifika magaribi na huyu mama alikaribia nyumba ya hule mutawa na alikokola mulango wake. Hule, wakati alimuona, alishituka na alitetemeka. Namna gani hii saa ya usiku alikuja mwanamuke moja mu jangwa?

-Ee Shetani, alisema, hii ni mutego yako.

Alimuuliza nani alikuwa na alitafuta nini sasa ndani ya jangwa. Hule alianza kuliya:

-Ma saa mengi ninazunguluka katikati ya hii jangwa, ee padri wangu.. .  Nilipotesha njia na kundi ya wa ndugu wangu na misikusikie na mimi namna gani nilifika huku mbele yako. Lakini kwa jina ya Mungu, usiniache, kwa sababu ni hatari nikula ma nyama ya pori huku.

Mutawa wa jangwa alisimama akili yake na asikuweze kukamata mpango. Ataweka mwanamuke moja ndani ya nyumba yake? Hii tendo haikukuwe wakati ingine kwake. Lakini ataacha kiumbe ya Mungu inje? Na, kama ma nyama ya pori watamukula? Hii itakuwa tendo kibaya, taskiri munene. Kwa ajili ya mapendo yake, alielekea akili yake na alimuweka ndani ya nyumba yake. Hule mama, alitosha kidogo manguo yake juu ya kumuonyesha uso na mwili yake muzuri. Majaribu ya uzini ilianza kumuuzi sana hule mutawa, kwa sababu kazi ya zambi ilikuwa teketeke sasa.

Alitupa chini mayani ya kukauka na alisema kwa mama kulala pale, na hule aliingia mu fasi kidogo mbali ya nyumba yake. Alipika magoti pale na alimuomba kwa Mungu.

-Hii usiku, alisema kwa Mungu, nikona bugomvi munene kupigana adui asiyeonekana (shetani) na adui aliyeonekana (mwanamuke). Ao nitashinda ao nitapotesha michoko yangu yote.

Usiku ilipita na moto ya usharati ilimubamba sana pa mwili na akili yake. Ushindani ndani yake ilianza kulekea. Mutawa aliogopa na alisema kwa akili yake:

-Hawa walifanya zambi ya mwili wataenda mu gehena, alisema na sauti nguvu. Pima moto, utaweza kuivumilia? Namna gani utavumilia moto ya gehena?

Basi, aliwaakisha moto ya kandili moja na aliweka kidole yake pa moto. Lakini moto ya zambi ile iliisha kumubamba ilikuwa kuliko munene. Ililungua kidole yake wa kwanza. Sasa alianza kulungua kidole yake wa pili. Kisha wa tatu.. .  Mpaka asubui aliisha kulungua bilole vyake wa tano ya mukono wake moja! .. .

Hule mwanamuke kahaba alimuangalia kwa siri na alishituka. Alitetemeka sana kwa sababu alisikia ya kama, kwa ajili yake huyu padri analungua mukono yake pa moto. Kwa ajili ya tetemeko yake alikufa. Warafiki ya huyu mwanamuke, wenye walisimama katikati ya njia, kidogo mbali ya nyumba ya mutawa, asubui walienda kwa nyumba yake juu ya kumuchekelea na kucheka kwa ajili yake. Lakini walimupata inje na aliomba kwa Mungu.

-Walimuuliza: Alipita jana huku mwanamuke moja?

-Ni ndani na analala, aliwajibu mutawa.

Waliingia ndani na walimupata kuwa mufu!

-Ee Ava, alikufa! walimwaambia na sauti nguvu.

Padri alifungula manguo juu ya kuona vilonda vyake na aliwaambia:

-Muangalieni huku, huyu mama alinifanyishia nini.. .  Lakini amri ya Mungu inanihamuru kufanya kazi kizuri pa hile fasi ninapata kazi mubaya.

Basi, alisimama yulu ya maiti yake na alifanya sala na alimufufusha!

Kisha huyu mama alitubu kweli. Alianguka mbele yake na aliomba hurumia yake. Tena alimwaambia ya kama alitubu kweli kwa hii zambi zake na asipende kurudia duniani. Anapenda kufata na yeye uzima utawa. Padri alimutuma mu Yerusalema, mu monasteri ya mutawa mwanamuke Pavla. Na kweli huyu mwanamuke alienda mu Yerusalema, alikuwa mutawa na aliishi na kitubio mpaka mwisho ya uzima zake. Tena alitakashwa na alifanya na miujiza.

## Sandaka ya mutawa moja mwanamuke

Mu muji takatifu Yerusalema aliishi wakati moja mutawa moja mwanamuke. Alikombana mu uzima takatifu na alimufurahi Mungu katika uzima usafi wake.

Lakini shetani alimuchukia na alituma kwa kijana moja mwanaume na mawazo mubaya  ya usharati juu ya kufanya zambi pamoja na hule mutawa mwanamuke. Huyu mutawa mukuona ya kama anaanza kumupenda huyu kijana mwanaume na ni hatari kupotesha tena na uzima yake, alifanya nini? Alibeba ndani ya kitambaa moja bego kidogo ya mahalaki na aliingia mu jangwa ya mutoni Yordani. Kule aliishi uzima utawa wake, bila kumuona mtu mwingine.

Siku moja, halafu, alimukuta mutawa moja wa jangwa, mtu ya mungu na mufazili mkubwa. Alimuuliza:

-Ee Ama, (mama mutawa) unafanya nini hapa mu jangwa?

Hule mutawa, kwani alitaka kufuchama uzima yake, alimujibu:

-Niko huku kwa sababu nilipotesha njia. Kwa jina ya mapendo ya Kristu, unisaidie kupata njia.

Mutawa huyu wa jangwa alimusema:

-Ninajua ya kama wala njia ulipotesha, wala njia unatafuta. Kwani unajua ya kama sauti ya uwongo inatokea ya shetani, uniseme kweli, ya mambo gani ulikuja huku?

Mutawa mwanamuke alimujibu:

-Unihurumie padri wangu, lakini kijana moja mwanaume alinipenda na mimi kwa hii mambo niliondoka na nilikuja jangwani. Ninapenda kufa huku na hapana kurudia duniani na nitazibiya wokovu ya hule kijana mwanaume.

-Wakati ngapi, unabaki huku?

-Katika neema ya Kristu niko huku miaka kumi na saba (17).

-Na unakula nini??

-Nilibeba hii kitambaa na ndani yake nilibeba mahalaki na katika mapendo ya Mungu, ninakula paka hii kila siku kidogo-kidogo, na bado kuisha!

Lakini na mambo ingine nikona yo: Wema ya Mungu ilinifunika mpaka sasa miaka 17 na hata mtu moja hasikunione, ila tu weye leo. Mimi niliwaona wote, lakini wale, wenye walipita ya huku, hakuna namna kuniona!

Mukusikia hii ma jambo hule mutawa wa jangwa, aliondoka mukutukuza Mungu kwa hii fazila ya hule mutawa mwanamuke.

## Malipo ya uzima usafi

Mtu moja mwenye biashara toka muji Askalona ya Palestini alisafiri na chombo na alipata musiba na alipotesha na bintu vyake na vitu vya wageni. Paka aliokolewa huyu wa pekee.

Halafu, wakati alirudia mu muji yake, walimubamba wale watu walipotesha vitu vyao kwa ajili yake na walimutupa ndani ya buloko. Tena walimubamba na mali na uriti yake yote. Walibakia huyu mwenye biashara paka na bibi yake, bila hata kitu kimoja.

Bibi yake alitafuta kazi na alianza kutumika. Na hii makuta kidogo alibeba, alinunua kidogo chakula, aliendа kwa buloko na alikula pamoja na bwana wake. Ma siku yao wa furaha iliisha kupoteshwa. Hakuna kitumaini moja kwa kubadilisha hali yao, haikuonekane.

Siku moja alikuja mkubwa moja mu buloko juu ya kusaidia wenye kifungo. Aliona kule na bibi yake na alishangaa kwa ajili ya uso na mwili yake muzuri.

Alimuita na askari moja. Hule mama aliendа wa furaha kwa sababu alitumainia kwa saidio na huruma wake. Huyu mutajiri alimuchofesha pa fasi ingine na alimwaambia:

-Juu ya nini uko huku? Mambo gani uko na yo?

Huyu mama alimuelejea uzima upotevu na sikitiko yake.

-Unataka kulala pamoja na mimi hii usiku? Mimi nitakuripa ma deni yako yote.

-Mkubwa wangu, alimujibu huyu mama, nilisikia Mtume Paulo, aliyesema ya kama kila mutu mwenye ndoa haina na mamlaka mu mwili yake, lakini paka mume (ao muke) yake. Basi, uniache kuuliza bwana wangu na kama yeye atanipatia ruhusa yake, nitakuja kwako. Mimi niko bibi yake na misina na mamlaka kufanya kila kazi bila yeye kuijua.

Alienda, basi, kwa bwana yake na alimwaambia hii jambo yote. Huyu bwana yake hasikufurahi, kwa sababu hule mutajiri alisema kwa bibi yake ya kama ataripa ma deni yao yote. Paka aliomboleza, aliwaza uzima usafi na utii ya bibi yake mupendwa na kutosha machozi ya ma macho yake, alimujibu:

Usipokelee sauti yake! Uende kumwaambia ya kama bwana yangu anakataa. Na ninatumainia kwa Bwana Yesu Kristu ya kama yeye hasitatuache ndani ya mateso yetu.

Alisimamama hule na alisema hii sauti kwa hule mutajiri, aliyemuongojea jibu yake.

-Nilisema kwa bwana yangu na hasikuitike.

Mkubwa mutajiri aliondoka, lakini hii zungumuzo ya mama na bwana wake alisikia munyanganyi moja, aliyekuwa mu chumba moja ya buloko. Aliomboleza na alisema ndani yake:

-Angalia pa hali gani weko hawa watu na walikataa kuharabisha sifa ya uzima yao! Waliweka uzima usafi yao kuliko yulu ya uhuru na mali yao. Walizarau furaha ya hii dunia, kwa ajili ya fazila ya Kristu. Nitafanya nini mimi mupotevu, misikuwaza ya kama eko Mungu na mpaka sasa niliua watu wingi?.. .

Basi, aliwaita karibu ya dirisha ya chumba yake na aliwaambia:

-Mimi ni munyanganyi na muuaji. Sasa ninaongojea akuje mkubwa juu ya kuhamuru lufu yangu.. . Nilisikia hii sauti yenu yote mulisuburia. Uzima usafi yenu ilinifurahi. Kwa hivi ninataka nimionyesha sauti yangu wa siri: Pa fasi hile fulani ya kibabashi ya muji hii nilizibiriya makuta yangu. Muchibule na mubebe yote. Hivi, mutaripa ma deni yenu yote na itabakia na ingine juu ya kuishi uzima moja wa furaha. Ninamiomba, musisahau na mimi kwa maombi yenu.

Kisha ma siku madogo alikuja mukubwa na amri yake walikata kichwa ya hule munyanganyi.

Bibi yake alibeba piki moja na alienda pa hile fasi aliisha kumwaambia hule munyanganyi. Na kweli, alipata jerekani moja ya kujaza makuta wa zawadi. Juu ya hapana kumuona watu, alienda pale na alibeba makuta usiku kidogo-kidogo. Vile pole-pole aliripa ma deni yao yote, alitosha bwana yake toka buloko na waliishi pamoja na furaha mpaka mwisho ya uzima yao katika baraka ya Mungu.

## Mutawa Musa wa inchi Ugaria

Mt. Mutawa Musa wa inchi Ugaria alivumilia bugomvo munene kwa zambi ya mwili. Lakini ku mwisho alishinda na utukufu na aliacha maungo yake mfano moja wa akili na usafi.

Huyu alikuwa mupendwa sana kwa mtoto ya mfalme ya Rusia, aliyeitwa Voris. Wakati Voris alijiuwa ku mwaka 1015 toka ndugu wake Zviatopolk karibu ya mutoni Alta pamoja na wakubwa ya ufalme wake, mwenye heri Musa paka yeye aliokolewa. Hile wakati alikimbilia kwa mwaaminifu mama Prentislava, dada ya mkubvwa ya inchiYaroslavos na huyu mama alimufuchama. Kwa sababu hasikuweze kwenda fasi ingine, alibaki kule na aliomba kwa Mungu kila siku sana.

Ndugu mkubwa Yaroslavos, kwa sababu alisikitika sana kwa lufu ya ndugu mudogo wake Voris, alienda na askari wake kupigana kwa Zviatopolk, ndugu wake mwingine na alimushinda.

Huyu muzulumu Zviatopolk alikimbia kwa inchi Polonia na aliungana na mufalme ya hile inchi, jina lake Boliaslavo na alitayarisha kundi ya askari kupigana muji Kievo, muji ya ndugu wake. Yaroslavos alishindwa na Zviatopolk alipanda pa kiti ya inchi.

Kisha ushindi ya Zviatopolk, musaidizi yake Mbolieslavos alirudia mu inchi yake, Polonia na alikamata karibu yake na watumwa wingi. Katikati yao walikuwa na wa dada wa wili ya Yaroslavos, watu wakubwa wake na mwenye heri Musa, aliyemufunga miguu na mikono yake na monyororo.

Mu inchi Polonia mt. Musa alibaki wakati ya miaka tano kwa kufungwa mu buloko, mukuvumilia utumwa na sala na shukrani kwa Mungu

Hile wakati mwanamuke moja muzuri sana na kijana, mkubwa ya inchi pPolonia na mutajiri sana, alimuona Musa, ya kama alikuwa mwanaume mkubwa, mwenye nguvu na uso muzuri na alimupenda katika mapendo ya shetani. Alilekea roho yake kwa hii mapendo ya mwili na siku moja alimukaribia na alimwaambia:

-Ee mtu wangu! Unavumilia isiyo haki hii mateso yako yote. Ninaona ya kama uko mwenye nguvu na mwenye akili. Basi, juu ya nini utabaki katikati ya monyororo na utapotesha uhuru yako?

-Vile Mungu alipenda kwa mimi, alimujibu Musa.

-Ndivyo, lakini mimi nitakuuhuru! Alimwaambia mwanamuke na sauti yake wa nguvu. Nitakusaidia juu ya kuwa mutajiri na mkubwa ya inchi yetu. Nitakuowa bwana wangu. Paka fanya mapenzi yangu! Zimisha moto ya nafsi yangu! Uniache kufurahi na weye pamoja! Misiweze kusadiki ya kama uso nzuri na mwili mwenye nguvu yako itakuwa kwa bure. Kama utapokelea sauti yangu, mimi nitatimiza matakio ya zambi yangu na weye utakuwa mkubwa wangu na mkubwa ya watu wingi. Basi, unasema nini?

-Jua mara moja kwa milele, alimujibu mwenye ajabu Musa, ya kama wala mapenzi yako nitafanya, wala mali na mamlaka yako ninapenda. Usafi ya roho na uzima wa akili ni kupita julu ya hile bintu weye unanilapa. Ninateswa katikati ya monyororo, lakini misi na mukosefu. tena nitatumainia ya kama hii monyororo itanitosha toka malipizi wa milele mu gehena.

Mukuona hule mama mkubwa ya kama atapotesha huyu mwanaume muzuri, aliwaza: «Kama nitamununua (yeye alikuwa mutumwa) na makuta yangu, kisha huyu atanifata, hata na bila mapenzi yake».

Basi, alituma mtu yake moja kwa mkubwa ya watumwa na alimwaambia amuuzishe huyu kijana Musa, bila mambo ya makuta. Hule alisikia ya kama ilikuwa muda moja muzuri juu ya kuwa mutajiri. Na, kweli, alimuuzisha na makuita 3000 feza wa zawadi!

Wakati alimununua, alihamuru amuletee mbele yake, amutoshe monyororo yake na manguo mabaya yake na amupatie kuvaa manguo mapya. Kisha alihamuru wasaidizi wake huyu mama amuletee chakula ya mbali-mbali na alimusukuma Musa na kila namna akule pamoja naye na alimusukuma tena afanye zambi pamoja naye.

Halafu hule, sawa zamani Yosefu mwenye muzuri wa Misiri, alikataa ma sauti yake na asipende kufanya zambi ya uzini pamoja naye. Alivaa manguo ya bule, alikula kidogo, alifanya sala siku na usiku. Alipenda kula mukate ya kukauka na maji na kuchunga akili na mwili yake safi na hapana chakula vizuri na zambi ya usharati.

Hii mfano nguvu ya kijana Musa ilileta kisilani kwa hule mama na mara moja alihamuru amuache kufa kwa njaa.

Lakini Mungu hasiache ninyi wote wanatumainia Kwake. Mutumishi moja ya hule mama mukali, alimuwema na alimuletea kwa siri kidogo chakula.

Lakini watumwa, wa ndugu wengine, walimushauria na walimusukuma kuitika na kufata ma sauti ya mama mukubwa wao. Walimwaambia hivi:

-Ee ndugu Musa, kizibiyo nini inakuzibiya juu ya kuowa? Uko tena kijana. Na huyu mama ni balaka (bila bwana) na aliishi na bwana yake paka mwaka moja. Uso na mwili yake ni nzuri kabisa, utajiri yake kubwa, nguvu yake munene. Kama, huyu alipenda kuowa mkubwa yake moja, nani atakataa? Na weye, uko mutumwa  na mutumihsi wake na usipende kuwa mkubwa na bwana wake? Juu ya nini unakataa ndoa? Kama, utakufa pa hii hali yako, nani atakutukuza? Mutu nani kutoka Adamu mpaka sasa alizarau mwanamuke? Walifanya nini Abrahamu, na Isaka na Yakobo? Lakini na huyu Yosefu wa Misri, alifanya nini? Ya kwanza alishinda jaribu ya zambi wa mwili na kisha aliowa bibi! Na weye, kama utaokowa uzima yako, bila shaka utabeba bibi moja. Lakini mutu gani hasitakuchekelea kwa hii upumbafu yako? Haina kupita nzuri kuowa huyu mama mkubwa, utauhuruwa ya uzima utumwa na utakuwa mkubwa yake?

Musa mubarikiwa aliwajibu:

-Wandugu na warafiki wazuri wangu, mweye munasema muzuri, lakini ninazania ya kama ma sauti ya nyoka (shetani) mu Paradizo kwa mama Eva, haina ingine mbele ya ma sauti yenu. Munanisukuma kuowa huyu mama. Hakuna namna kumisikia. Kama nitakufa ndani ya hii monyororo, ninatumainia ya kama nitapata huruma kwa Mungu. Kama wenye haki wote waliokolewa, lakini walikuwa wa ndoa, munapashwa kujua mweye ya kama mimi misi na mwenye haki. Mimi niko mwenye zambi na misiweze kuokolewa, kama nitaishi pamoja na mwanamuke. Kama Yosefu alijitoa kwa mikono ya hule bibi ya mkubwa Petefri, kisha hakuna namna kuwa mfalme ya Misri. Mungu aliona uvumilia yake na alimupatia ufalme ya Msiri. Na hivi anatukuzwa yeye kwa milele kwa uzima usafi wake, lakini alizala na watoto. Lakini mimi, misitake hata ufalme wa Misri, wala mamlaka wa dunia ninatafuta, wala ninatakia kubaki ndani ya hii inchi, wala ninakombana kujitukuza  mu inchi wa Rusia. Ninazarau vitu vyote vya hii dunia paka kwa ajili ya ufalme mbinguni. Kama nitatoka muzima toka mikono ya hule mama, mara moja nitafanyika mutawa.

Wakati alipata tangazo ya hii mazungumuzo yao yote hule mama mkubwa, alitengeneza kutimiza namna ingine sasa. Alihamuru kumupandisha huyu Kijana Musa pa nyama punda moja na watamuzunguluka katikati ya ma njia ya mukini na muji yake. Hule mama alitembea pempeni yake pa punda mwingine. Wakati alimuonyesha ufalme wake, alimusema:

-Hii inchi ni yako. Huyu taifa ni yako. Fanya kila kazi weye unataka.

Kisha aliangalia taifa yake na alipaza sauti kusema:

-Tazama mkubwa wenu na bwana wangu! Tangu leo mutamuheshimiwa na mutamusujudu!

Kijana Musa alicheka na hii upumbafu ya hule mama na alimuwaambia:

-Unachoka kwa bure. Usiweze kunilekea na kunikokota na vitu ya ufalme wako. Kamata mpango mu roho na akili yako ya kama unachoka kwa bure na hautaweze kulekesha akili yangu.

Hule mama alisirika sana.

-Unasahau ya kama mimi nilikununua? Nani ataweza kukutosha ya mikono yangu? Hautatoke muzima toka mikono yangu! Nitakupiga bila huruma na kisha nitakuua!

-Misiogope ma sauti yako, alimujibu mutukufu Musa. Kama Mungu anapenda nitafanyika mutawa na haraka.

Hii sauti ya Musa ilitimizwa na namna wa ajabu. Hile ma siku alipita pale padri moja toka Mulima Takatifu. Alimukuta na mapenzi ya Mungu huyu Musa. Alisikia mateso yake na matakio ya uzima utawa na alimuvaa nguo ya utawa na aliumufanyishia mutawa. Alimushauria kuchunga na kila sandaka mwili na nafsi yake usafi na hapana kutoa maungo yake kwa adui (shetani), alimutakia kuokolewa toka hule mama mwenye zambi na aliondoka.

Huyu padri walimutafuta, lakini hakuna namna kumupata. Aliondoka pasipo kujua wakubwa wa hule mama alienda wapi.

Huyu mama, kwa sababu alipotesha kila kitumaini ya kutimiza matakio mabaya yake, alimutoa kijana Musa kwa wa askari wake juu ya kumupiga. Walimuralisha pa meza moja na walimupigilia, bila taabu, na ma bakora wa chuma. Inchi chini ilijaza na damu yake. Hile saa walimupiga, walimwaambia:

-Fata sauti ya mama mkubwa wako na fanya mapenzi yake. Kama hautaitike, sisi tutakata mwili yako vipande-vipande. Hautaokolewa ku mikono yetu. Utatoa nafsi yako kwa lufu na namna uchungu. Basi, penda na taabu ujana wako. Tosha hii nguo kibaya na vaa nguo mupya na utaokolewa ku mateso yetu..

Lakini mwenye heri Musa aliwajibu na roho nguvu:

-Wa ndugu, mufanye kila amri walimipatia. Hakuna namna mimi kukataa malapo ya uzima utawa wangu. Wala maumivu, wala moto, wala vilonda wataweza kunichanisha toka Bwana wangu na uzima utawa wangu. Huyu mama mwenye ngiza anaonyesha uzima wake isiyo na haya. Hasiogope wala Mungu, wala watu na ananisukuma bila mapenzi yangu kwa zambi ya uzini. Lakini misitafanye mapenzi yake mubaya.

Huyu mama alisirika sana, kwa sababu aliona nguvu ya kijana Musa, bila hata kidogo kulekea ao kufata matakio yake. Iliisha kupita wakati ya miaka sita (6) na huyu mutumwa wake alisimama na roho nguvu. Sasa alitaka kumulipiza kwa sababu Musa alimupatia haya mbele ya taifa wake. Basi, alituma watu wake kwa mfalme Mbolieslavo:

«Ee Mfalme wangu, unajua muzuri, alimuandika, ya kama bwana wangu alikufa mu nvita. Kisha weye ulinipatia ruhusa yako kuchagua bwana yangu mupya. Basi, nilipenda mutumwa moja muzuri, nilimuuhuru, nilimuletea nyumbani yangu, nilimulaka uriti wangu wote, ma shamba, taifa na maungo yangu. Lakini yeye hii yote aliizarau. Mara mengi nilimupiga na nilimutesa katika njaa. Nilimutesa mpaka sasa miaka sita, lakini huyu eko na roho nguvu sana, anavumilia kila mateso yangu na anakataa kufata sauti na matakio yangu. Tena, sasa alikuwa kwa siri mutawa ku moja mutawa, aliyekuja toka Mulima Takatifu. Basi, unaamuru kufanya mini je?»

Mfalme Mbolieslavos alihamuru kusimama mbele yake wote wa wili. Wakati walikuja, alianza kushauria na kusukuma Musa kuitika na kufata ma sauti ya hule mama. Ku mwisho alimwaambia:

-Nani ni mumbafu sawa weye na utapotesha hii vitu vyote na unapenda kuliko mateso? Basi, unapashwa kujua ya kama unakamata pa mikono yako ao uzima ao lufu yako. Ao utafanya mapenzi ya mama mkubwa wako na utapata masifu na matukufu ao utapata lufu matata.

Kisha mfalme alipindula kwa hule mwanamuke:

-Hakuna namna huyu mutumwa yako, weye ulimununua, kufanya kila mapenzi yake. Weye uko mama mkubwa yake na huyu  ni mtumwa yako. Basi, kama atakataa kutii, utamupatia moja malipizo muzuri, juu ya kubeba na wengine mfano moja muzuri na kisha wote watafata ma sauti yako.

Musa Mubarikiwa alisema kisha kwa mfalme:

-Bwana wangu anasema: «Faida gani atapata mtu moja kama watamupatia dunia muzima, lakini atapotesha nafsi yake?» Namna gani, basi, unanilapa matukufu na masifu, kwani na weye, kisha wakati kidogo, utakufa na huyu mama atajiuwa?

Hii unabii ya mwenye mwangaza katika Mungu mutawa Musa ilitimizwa kisha wakati kidogo.

Mutawa Musa aliteswa tena na mateso ya kuachana ku hule mama. Tena aliteswa sasa kuliko mingi, kwa sababu alikuwa na ruhusa ya mfalme. Sasa alimukjokota kufanya zambi naye.

-Michoko yako ni kwa bure, alimujibu mwenye heri Musa. Usinizanie ya kama mimi ni bumbafu ao asiye na nguvu na misiweze kufanya hii tendo ya usharati. Ninakuzarau, lakini, kwani uko mtu asiye na woga ya Mungu na isiyo haya.

Hile saa hule mama alihamuru amupige kila siku mara miya moja (100) na fimbo moja na kisha watakata na vipadne ya mwili yake, moja-moja;

Mfalme Mbolieslavos, juu ya kuonyesha mapendo kwa hule mama mkubwa, alihamuru ufukuzo ya watawa wote ya ufalme wake. lakini Bwana yesu na haraka alimulipa kwa hii tendo yake. Kwa rafla usiku moja alikufa, wakati alilala. na mara moja ilianza bogomvi ndani ya ufalme wake. Taifa aliua wakubwa ya inchi na hule mama aliyemupiga mutumwa ya Mungu padti Musa.

Kisha lufu ya hule mama, Musa mwenye ajabu alijiuhuru na alienda mu Monasteri ya Kievo ya inchi Rusia. Pala alistahiliwa kuwa mtakatifu mkubwa na aliangaza katika mafazila na miujiza yake mu inchi muzima ya Rusia.

Mungu alimutukuza, na kisha kulala, wake, kwa sababu alimupatia zawadi kusaidia wale watu weko na majaribu yao kwa mwili na zambi ya usharati.

## Kipimo wa miaka tano

Mutawa moja aliyeishi mu Monasteri Stavrovunio ya Kisanga Kipros alikuwa  mutawa na padri Kiprianos.

Alizaliwa mu mwaka 1880 mu muji Idalion, karibu ya muji kubwa Lefkosia na wazazi wake walikuwa walimaji. Ku kipimo ya umri yake miaka 25 aliingia mu monasteri na alifanyika padri wa roho mkubwa. Waaminifu wingi walipata faida ya roho karibu yake.

Hile wakati alikuwa padri kijana ma shamba ya monasteri walitumika pempeni ya watawa na waaminifu. Mujenganji mkubwa aliisha kuleta pale na bibi yake. Huyu alimusaidia ya kumufanyishia chakula na kisha alituma ma shamba. Padri Kiprianos aliishi pamona na wao miaka tano mpaka monasteri alimuita kutumika mu Kanisa ya monasteri na sawa padri ya roho.

Siku moja alienda kuungama na bibi ya hule mujengaji. Padri Kiprianos alimuuliza alikuja toka fasi wapi na hule mama alicheka! Alishangaa, kwani aliishi pamoja naye miaka tano kwa kumusaidia bwana mujengaji wake na huyu padri alimuuliza hivi. Padri Kiprianos alimufamia huyu mama katika mucheko yake, kwa sababu ya miaka tano hasikuache ma macho yake kuona uso ya huyu mama! Hivi, waliishi pamoja miaka tano, lakini hasikumufamie nani alikuwa na aliikaa wapi!

## Kikuao mu shamba

Monasteri ya mt. Dionisios ya Mulima Takatifu ku mwaka 1919 alituma ma shamba yake, inje ya Mulima Takatifu, mutawa kijana moja, jina lake p. Lazaro. Huyu alipata mambo ya hatari munene sana. Anatuwaambia sawa alipata hii mambo mtu mwingine, lakini ni huyu wa pekee:

«Ku Mwezi wa sita (Yuni) ilifanyika mavuno ya ngano, katika zoezo ya hile fasi. Mukongo ya wale walivuna, waliwafata na wamaskini na walilokota hile mayani ya ngano ilibaki chini.

Hii kazi ya kulokota mayani ya ngano walikuja kila mwaka wanawake wa wili, wenye walibaki ma nyumba yetu ya hii shamba na walitusaidia na kwa pisi. Hile mwaka 1919 mwanamuke moja alikuwa binti kijana na uso na mwili yake ilikuwa muzuri sana. Mutawa aliyetumika pale alikuwa kijana na huyu binti ilikuwa mambo na kikuao munene mbele yake.. . Aliogopa sana hule mutawa, kwa sababu huyu binti kijana alimucheka na alimusaidia ya kuchoma mukate mu tanuru. Tena na shetani alimupandisha na bego-mawazo mabaya ya zambi ya usharati ndani ya akili yake. Woga wake ilikuwa munene kwa sababu ilikuwa namna kuanguka mu mutoni ya zambi.

Kwani alipata hii mambo, hasikujue ataenda wapi na namna gani ataokolewa. Alikimbilia kwa Mulinzi ya Monasteri yao, mt. Yoano Mutangulizi. Alipika magoti mbele ya Picha yake na machozi mingi alimwaambia hii hatari alipata kwa ajili ya hule binti.. .

Kisha ma siku wa wili hule binti kijana mara moja alipata malari na mwili yake ililekea sana. Waliita wazazi wake na wale walikuja na walimuweka pa punda na walimupeleka mu mukini yao.

Vile mutawa kijana p. Lazaro aliokolewa na alimushukuru mulinzi mkubwa mt. Yoano Mubatizaji kwa sababu alimusaidia mara moja.

# <u>UMASKINI</u>

## Makuta wa deni

Padri mutawa Yoano wa inchi Persia aliomba wakati moja, makuta fulani sawa deni na alinunua vitu vyake juu ya kutumika. Hile siku alikuja kwake mutawa moja na alimwaambia:

-Unipe, ava, nyushi kidogo, sawa deni kusudi kufanya na mimi nguo moja yangu.

Padri Yoano alimupatia na furaha mingi. Na hii namna alikuja kwake na mutawa mwingine na alimuomba hivi:

-Ee Ava, unipe na mimi nyushi kidogo kusudi kufanya kitambaa moja kwani ninailazimisha.

Padri Yoano alimupatia na kwake. Tena alipatia na furaha mingi na kwa wengine wenye walimuomba nyushi sawa deni. Lakini vile ilibakia kwake nyushi kidogo sana.

Kisha ma siku madogo alikuja hule mutawa, aliyemupatia makuta-deni kwake na sasa aliomba makuta-deni yake.

Ongojea kidogo, alimujibu mutawa Yoano na kisha saa kidogo nitakuiletea.

Kwa sababu hakuna namna kutafuta hii feza, alienda kwa ava Yakovo, aliyekuwa na kazi ya kutengeneza mambo ya watawa wote.

Kwa kutembea pa njia alipata chini feza. Ilikuwa hii feza alikluwa lazima ya kumupatia kwa hule mtu. Lakini alikataa kuibeba. Alirudia kwa hule mutawa na alimuwaambia:

-Usisikitike nitafanya nguvu na nitatafuta makuta yako.

Alienda mara ya mbili kwa padri yakovo na mara ya mbili alipata pa njia hii makuta, pa hile fasi umoja. Alirudia na alibeba sasa njia ingine juu ya kwenda kwa padri Yakovo. Lakini na pa hile njia alipata chini makuta, hile makuta alikuwa na lazima kuirudisha. Alifanya sasa alama ya msalaba na aliibeba na mikono yake. Alienda kwa padri Yakovo na alimusema:

-Wakati nilikuja kwako, ee padri, nilipata pa njia chini hii feza. Basi, fanya mapendo na onyesha kwa watawa wote, wenye wanaishi pa hile fasi, kama mtu moja alipotesha feza yake. Na kama ataonekena hule mutawa aliyepotesha makuta yake, weye utaimupatia.

Padri Yakovo alienda inje na alizunguluka mukini ya watawa wote na aliwajulisha juu ya hii feza, lakini hakuna namna kutafuta mtu moja aliyeipotesha hii makuta. Kisha alimusema padri Yoano:

-Kwa sababu hasikuonekane hule mtu aliipotesha, ninakuomba, umupatie kwa hule mutawa fulani, kwa sababu nikona deni kwake. Kwa sababu misikuwa na makuta nimurudishe, nilipata hii makuta mu njia.

Alishangaa padri Yakovo, kwa sababu padri Yoano alikuwa na deni, aliipata hii feza mu njia na alikataa kuibeba amupatie kwa hule mutawa.

Tena huyu mumoja p. Yoano, kama alikuja kwake mtu moja na aliomba kintu kimoja, p. Yoano alimwaambia: «Uende weye wa pekee na kamata hile kintu ukona yo lazima». Kama huyu ndugu alimurudisha hile kintu aliomba sawa deni, padri Yoano alimujibu: «Uiache pa fasi yake». Kama hule ndugu alikataa kuirudisha, padri Yoano, hasikumwaambie hata sauti kimoja.

## Kitumaini kwa mwenye busara

Mwaaminifu moja aliyependa watawa, aliwatembelea na alisikia ma sauti yao kwa faida ya roho yake. Siku moja alipata mutawa moja muzee na mugonjwa. Alimutaabu na alitaka amuache makuta juu ya mambo ya maisha yake.

-Ee padri, alimuwaambia, uko muzee na mugonjwa. Usiweze tena kutumika. Hii makuta itakulazimishwa.

-Ninatesha na hii ugonjwa mpaka sasa miaka 60, alimujibu na katika saidio ya Mungu, misina na kintu kimoja lazima. Hule aliyeangalia maisha yangu, ananituma kila kintu ninailazimishwa! Sasa, weye, ndugu wangu, unataka kumufukuza Huyu mwenye busara wangu?

Hivi, alikataa kupokelea makuta yake.

## Otoleo ya vitu wa zahabu

Hile wakati  mama mkubwa wa muji Roima jina lake Melani Muzee (349-410) alitembelea mikini ya watawa ya Misri, alienda na kwa mutawa mkubwa Pamvo, aliyekuwa mutukufu kwa umaskini wake.

Mama Melani, kwani alikuwa mutajiri, alimupatia kwake 300 litre wa zahabu! Mt. mutawa aliikaa hile saa na alitumika kufanya vituga na mayani ya kukauka. Alimubariki na alimwaambia:

-Mungu akubariki na akupatia malipo ya roho.

Kisha alisema kwa musaidizi wake, jina lake Origenis:

-Beba hii vitu vya zawadi na kabula kwa makundi wote ya Watawa ya inchi Livihi. Usikabule hii zahabu kwa ma kundi ya Msiri, kwa sababu watawa wanaishi pa inchi utajiri na bulongo ni nzuri na hawakuwa na lazima ya saidio.

Mwenye heri Melani, aliongoje Pamvo amusifu kwa hii zahabu alimupatia, halafu hasikusikie hata sauti yake moja. Hile saa Melani, kwa sababu hasikusikie sauti na shukrani ya Pamvo, alimuwaambia:

-Unapashwa kujua, muzee wangu, ya kama hii makuta ya zawadi ni uzito ya 300 litre.

Na mtakatifu alimujibu:

-Hule mutu weye ulimupatie, hana na lazima ya kipimo. Huyu aliyepima milima, (Mungu) anajua kuliko ya mimi ngapi ni vitu vya zahabu vyako. Kama uliipatia kwa mimi, ilikuwa lazima kunionyesha na uzito yao. Lakini, kwa sababu unaipatia hii mali yako kwa Mungu, haina lazima kuniambia sauti moja, ni kusema ngapi ni zawadi na uzito yao.

## Otoleo ya zahabu na Melani kijana

Mtakatifu Mutawa mwanamuke Melani wa kijana (383-439) mukana ya Melani Muzee, alikabura pamoja na bwana wake, jina lake Pinyano, mali yake yote ma kanisa na maskini.

Kisha walisafiri mu Msiri kusudi wafamie watawa wa jangwa na wapatie na kwao zawadi yao.

Hivi, walifika na mu pango ya mutawa Ifestionas. Walimusalimia na walimuomba kubeba na huyu kintu hata kimoja. Hule alimujibu:

-Hainilazimishwa kintu kimoja! Nitafanya nini hii mali ya zahabu huku mu jangwa?

Mtawa Melani alimusukuma aibebe, lakini na mutawa wa jangwa alikataa. Basi, aliwaza amupatie mali kidogo kwa siri! Aliingia ndani ya nyumba yake na alifanya sawa alitafuta maji. Hasikupate hata kintu kimoja ndani, ila tu vituga na mayani ya kukauka juu ya kazi yake na birika moja kidogo na chumvi ndani. Hile saa alisuburia bwana wake pamoja na mutawa, huyu mama aliweka ndani ya birika kifulusi moja na makuta wa zahabu. Kisha alitoka inje, alisimama mazungumuyzo yao na walijiepuka na haraka.

Mt. Mutawa Ifestionas hasikuchelewe kupata hii feza na alitembea mbio mukongo yao juu ya kuwaipatia. Alipaza sauti toka mbali kusema hivi:

-Mubebe hii makute. Misitafanye kintu na hii makuta yenu, hapa mu jangwa.

-Ee Muzee, chunga hii makuta, walimujibu wale. Na, kama hauna na lazima yao, uipatie kwa watu wengine.

-Hata mutawa moja hasitabebe, aliwajibu toka mbali. Na watu ya dunia hawapite ya huku.

Lakini, kwa sababu huu uwili alikataa kubeba hii makuta, mutawa alitupa hii makuta ndani ya mutoni, juu ya kuishi bila mawazo ya upenda feza.

## Mutawa wa jangwa na wanyanganyi

Mutawa wa jangwa alitembelea mt. Zosimas mu monasteri yake mu muji Tiros ya Palestini wa zamani. Waliikaa pamoja na walisoma Hadisi ya Watawa Watakatifu. Vile walibeba nguvu ya roho.

Katikati ya ma hadisi walipata na hii: Wanyanganyi waliiba vitu vyote toka nyumba ya mutawa moja wa jangwa. Katika hii hadisi, wanyanganyi waliiba vitu vyake vyote, lakini walisahabu kubeba na mufuko moja yake. Mutawa alitembea mukongo yao, hile saa wale waliondoka, na alipaza sauti kusema kwao:

-Watoto wangu, mulisahabu kubeba na hii!

Wale, roho yao ilikuwa ya kujaza na ugumu, lakini walishangaa kwa hii umaskini ya hule mutawa. Mara moja walimurudisha vile vitu waliiba mukusema na kitubio wa kweli:

-Kweli, huyu ni mutu wa Mungu!

Pa hile fasi ya hadisi mwenye kutembelea mutawa wa jangwa alisema kwa padri Zosimas:

-Unajua, Ava wangu, hii hadisi ilinapatia faida ya roho mingi.

-Na namna gani ilikusaidia? Alimuuliza mutawa.

-Niliisha kuisoma, hile wakati niliishi kama mutawa karibu ya mutoni Yorodani. Nilistaajabu huyu Muzee na nilimuomba kwa Mungu: «Ee Bwana, unistahili kufata mwendo yake, sawa vile Weye ulinistahili kuwa mutawa». Wakati nilikuwa hii matakio, kisha ma siku wa wili, walikuja kwangu wanyanganyi! Wakati walikokola mulango yangu na mimi nilisikia walikuwa wa nani, nilisema ndani ya roho yangu: «Utukufu kwa Mungu; ilikuja nyakati Mungu nipime uharibifu ya vitu vyangu». Mukufungula mulango, niliwapokelea na furaha. Niliwaakisha lampi, nliwaonyesha kila kitu niko nayo ndani ya nyumba yangu, mkukusema kwao: «Musishake, misitafuchika hata kitu kimoja». Wale waliniuliza: Ukona zahabu? Niliwajibu: «Ndivyo, nikona makuta tatu ya zahabu. Na mara moja nilifungula sanduku moja kidogo, pahali nilikuwa na hii feza ya zahabu. Hawa walibeba hii feza ya zahabu na waliondoka na amani.

Mtawa Zosimas alimuuliza wa furaha:

-Walirudisha hii makuta sawa walifanya na wale wanyanganyi katika hii hadisi tulisoma?

-Mungu hasipende wanirudishe, lakini na mimi misikuwa na lazima ya hii makuta, alimujibu mutawa wa jangwa, aliyepata faida ya roho kuishi bila makuta.

# UHODARI

## Mushahidi mwanamuke Potamiena

Hile wakati ya ufukuzo ya mfalme wa Roma Maksimianos (286-310) alibambwa mu muji Aleksandria wa Misri bintri moja muzuri na mwaminifu orthodokse, jina lake Potamiena.

Huyu alikuwa mutumwa ya mtu moja mupagano, mwenye zambi ya mwili. Huyu alikombana na namna ya kuachana kumusukuma huyu mutumwa wake binti Potamiena afanye zambi ya mwili. Ku mwisho alimutoa kwa mkubwa moja ya inchi, alimupatia na makuta mengi na alimuwaambia:

-Kama ataitika kufanya huyu binti zambi ya mwili, umuache muhuru, lakini, kama anakataa kumaliza zambi, umulipize na namna ugumu.

Huyu mkubwa ya inchi na namna mengi alipima kumuogopesha. Tena alihamuru kuwaakisha na chugu moja munene na ndani waliweka kaburibo na chini moto. Hile wakati kaburibo ilianza kuchemuka, mwamuzi alimusema:

-Ao uende na fata sauti ya mkubwa yako, ao nitakutupa ndani ya hii kaburibu!

Hule bin ti hasikuogope mbele ya hii teso na alimujibu na uhodari:

-Ole, ole, kama mwamuzi mumoja anatushauria kwa hii uzima ya usharati!

Mkubwa alisirika na alihamuru amutupe huu Binti ndani ya chugu. Hile saa Mushahidi kijana alipaza sauti kusema:

-Kama, hivi ulikamata mpango, sema wa askari wako niweke mimi ndani ya kaburibo pole-pole. Utaangalia nguvu ngapi Kristu anatatia kwa watoto wake wa roho!

Na hivi ilifanyika! Mtakatifu Potamiena alijilungua saa mingi pole-pole mpaka alitoa nafsi yake kwa Bwana wake Arusi Yesu Kristu.

## Askofu wa kweli

Ku mwaka 371, kisha uzalio ya Yesu Kristu, waaminifu ya njimbo Kapadokia wa Siria, walikuwa kundi moja kidogo, lakini watu wengine walifata kanisa ya uwongo. Mfalme Walis alikombana kunyosha fundisho ya uwongo ya padri Arios na fasi yote. Sasa alikombana pa hile fasi ya Kapadokia, pahali ilikuwa kiti ya askofu Basilios mkubwa.

Ma fasi iongine ya ufalme wake walifata mapenzi ya huu mfalme kwa mambo ya dini. Hii kazi yeye alifanya katika mafukuzo, mateso na kuiba uriti ya watu, tena na lufu!

Kapadokia ilibaki fasi wa mwisho, pahali walichunga imani Orthodokse waaminifu pamoja na askofu wao. Mfalme alituma pale mkubwa yake, jina lake Modestos.

Huyu Modestos alibeba na ma akida wengine, aliingia mu muji Kesaria na alihamuru kuja mbele yake askofu ya hii muji, Basilios mkubwa.

Huyu askofu, hile usiku alifanya sala mingi na asubui aliondoka.. .  Baridi ilipita, lakini roho yake ilijaza na moto ya mapendo ya Mungu. Walimufata na waaminifu kwa kuenea. Lakini nyumbani ya mkubwa waliacha kuingia paka askofu, lakini kundi ya waaminifu wake walisimama inje.

Mkubwa Modostos alimuongojea na tabia mubaya na ukali. Alimuuliza:

-Ee Basilie, juu ya nini weye unakataa kufata mapenzi ya mfalme wetu? Namna gani unamuzarau? Unazania ya kama uko nani?

Mt. askofu hasikukuwe na woga. Na upole na amani alimuuliza:

-Ya mambo gani unanishitake? Kosa yangu ni nini?

-Usifate imani ya mfalme. Paka weye unakataa kufata imani ya padri Arios.

-Mfalme hasifate imani wa kweli! Anaamini ya kama Yesu Kristu ni kiumbe. Lakini mi ninamusujudu Kristu kama Mungu muzima.

-Halafu sisi, wenye tunafata mfalme wetu, tuko watu wa nani?

-Mweye munafata fundisho ya uwongo!

Mkubwa alishituka. Hasikuongojea hii uhodari ya askofu moja.

-Lakini, kweli, usitake kufata imani yetu? Usipende kuwa rafiki yetu?

-Mimi ninakuwa mukristu na ninataka kuwa na warafiki katika imani na hapana katika ma cheo ya serkali.

-Usiogope mamlaka wangu?

-Juu ya nini nitaogopa? Weye utaweza kufanya nini?

-Nitaweza nini? alisema na kisilani. Nitakamata uriti, nitafukuza, nitapiga, nitaleta mateso na lufu!

-Hii yote, alimujibu askofu muhodari, misiiogope. Kintu ingine uko nayo?

-Usiiogope? Juu ya nini?

-Uriti wangu ni paka manguo mabayawa zamani na vitambu vidogo. Na misiogope kuiba mali yangu. Kama utanifukuza ya huku, misiopgope kwa sababu hii inchi ni ya Mungu na kila kintu ni juu yake. Mimi, huku nilikuja ya wakati kidogo sawa ndege na nitaenda mu fasi ingine. Juu ya hile mateso unase, a, misiogope kwa sababu mwili yangu ni ya kukonda na kujaza na malari mengi na mbio-mbio atakufa! Kama unasema ya kama utaniua, mimi misiogopa lufu, kwa sababu lufu itafayika mufazili yangu mkubwa! Na mimi huu lufu ninamupenda juu ya kuunganwa pamoja na Mungu wangu na haraka!

Mkubwa alisimama na aliwaza. Kisha alinyanyua kichwa yake yulu na alisema:

-Ee Basilios, hata askofu moja hasikunijibu na hii uhodari mpaka sasa.

-Ndivyo, kwa sababu weye usikukute askofu wa kweli!

Mkubwa Modestos alikuwa na fasi ugumu. Kisha aliondoka na alimwacha askofu muhuru. Kwa mfalme alimujibu: Ee Mkubwa, tulishindwa.. . . »!

## Askofu na mufalme

Mfalme ya Konstantinopoli Theodosios mkubwa alimushinda katika nvita mfalme jina lake Maksimos mu njimbo Italia wa kaskazini ku mwaka 388. Kisha mfalme Theodosios aliienda mu muji Mediolana, pahali pale alikuwa askofu Ambrosios (340-397). Mfalme alimuheshimiwa askofu na askofu alimusifu mfalme mutukufu na mwaaminifu.

Theodosios mkubwa alibakia mu muji Mediolana mpaka ku mwaka 389. Katikati ya hii nyakati ilifanyika jambo moja. Katika hii jambo askofu Amvrosios alionyesha utukufu ya Kanisa mbele ya mamlaka ya ufalme ya dunia.

Taifa ya muji Thesaloniki wa inchi Grekia (Hellas) aliomba ku wakubwa ya Thesaloniki kwa kumutosha ku buloko mtu moja, aliyeua mtu mwingine. Wakubwa ya muji walikataa hii matakio ya taifa na watu ya taifa walifanya funjo. Walimuua jemadari kubwa ya muji jina lake Vutherikos na wakubwa ya wa askari wengine. Tena maiti yao walikokota pa njia ya muji Thesaloniki!

Mfalme Theodosios alisikia hii tangazo na alisirika. Aliwaza kuwalipiza juu ya kufundisha na watu wengine. Askofu Amvrosios alimuwaambia haipashwe kuuwa watu wakosefu na wasiyokosa. Mfalme alimulaka ya kama haitahamuru kulipiza watu ya muji Thesaloniki. Lakini walimukaribia wakubwa ya hii muji na walisema kwa mfalme ya kama hii uwaji walifanya watu wingi ya muji yao na haipashwa kuchelewa ya kulipiza wale wakosefu.

Mfalme Theodosios aliitika na shauria yao na alihamuru kuua taifa ya muji Thesaloniki ndani ya kiwanja, pahali walicheza na ma punda yao.

Basi, wakubwa waliita watu ya taifa kufika siku na saa fulani mu kiwanja juu ya ushindani ya kutembea na punda na kuona hii ushindani. Wakati ilijaza kiwanja na watu waliingia ndani wa askari na visu vyao na waliua watu 7. 000.

Hii tangazo wa taabu ilifika na kwa askofu Amvrosios ya muji Mediolana na alitaabu sana. Askofu alimutuma kwa mfalme barua moja, alimuonyesha hii uwanji munene alifanya na alimushauria ya kutubu.

Mfalme alishituka. Mu Juma alipashwa aende mu Misa, lakini bila kutubu, kwa sababu alizania ya kama, kama aliacha taifa ya muji Thesaloniki muhuru, bila malipizo, ilikuwa namna kuharabika ungano ya inchi yake. Basi, aliingia mu Misa bila kitubio.

Wakati mfalme alikuwa karibu na inje ya kanisa, askofu alimusimamisha inje na alimukataza kuingia mu Misa, mukusema kwake hivi:

-Ee mfalme wangu, ninaona ya kama usikusikie kazi kibaya nini uliifanya.. . Ninazania ya kama mamlaka yako haikuache kuona kosa yako.. . Inapaswa kujua ya kama hii mamlaka ni kwa bure na ya nyakati kidogo.. . Moja ni Mkubwa na Rabi ya dunia, Muumba na Mujengaji ya dunia muzima! .. . Namna gani utafungula mikono yako na utapewa Mwili na Damu ya Kristu? Toka mbio na usifanye sasa zambi ingine munene.. .

Mfalme Theodosios alivumilia hii sauti na shauria ya askofu. Alisema paka kwa askofu ya kama na mfalme Daudi alianguka na alifanya zambi ya usharati na uuanji. Hile saa askofu mwenye akili alimujibu:

-Sawa vile, basi, ulimufata Daudi mu njia ya zambi, sasa umufate na mu njia ya toba!

Mfalme alisikia na aliondoka! Alitubu kweli na alistahiliwa kukomunika kisha mwaka moja, mu Siku Kuu ya Kuzaliwa Kristu.

### Mazimu na mfalme wa Rusia

Ku mwaka 1570 mfalme wa inchi Rusia jina lake Ivan (Yoano) wa Tromeros (Wa Matata) alikuja mu muji Novogorodi na alihamuru lufu ya wakaa ya hii mji, kwa maana alizania ya kama watu ya muji walijiungana na wa adui wake.

Kisha hii uuanji matata, alienda mu muji Pskofi, pahali aliishi mwaaminifu moja mazimu katika Kristu, jina lake Nikolaos. Wakaa ya hii muji waliongojea na wale hii bahati mubaya. Hile saa mutu ya Mungu Nikolaos na mkubwa jemadari ya hii muji walisuburia na walikamata mpango kuweka pa njia, hile atapita mfalme Ivan, mukate na chumvi, sawa kutim ya mapokeo na ukaribisho na watamupokelea mfalme na heshima mingi.

Kisha hii mapokeo yao, mfalme alikaribia padri Nikolaos kuomba baraka yake. Hile saa mazimu katika Kristu alimupatia pa sahani moja nyama muzima na wa sasa! Lakini hii wakati ilikuwa kwarezima ya Siku Kuu ya Ufufuo ya Kristu. Mfalme alikataa kuibeba.

-Niko mukristu! Misikule nyama hii wakati ya kwarezima! .

Na padri Nikolaos alimujibu:

-Usikule nyama.. . Lakini unakunywa damu wa watu!

Mfalme alisikia uuanji wake na asikufanye hii uuanji mu muji Pskofi.

## <u>ISIYO NA CHUKI</u>

### Jirani mwivi

Karibu ya mutawa moja mtakatifu wa jangwa aliishi na mutawa mwingine mubaya. Siku moja, wakati mutawa wa jangwa alilofa, jirani mubaya aliingia nyumbani yake na aliiba vitu vyake vyote. Wakati mutawa wa jangwa alirudia hasikupate vitu vyake na alienda, bila kuwaza nani alikuwa mwivi, kwa jirani yake. Basi, aliingia nyumbani ya hule jirani na aliona vitu vyake katikati ya nyumba, kwa sababu mwivi bado kuypata nyakati juu ya kuifuchika!

Muzee wa jangwa, wakati aliona vitu vyake ndani ya nyumba ya jirani mutawa, hasipende amupatie haya na alimwaambia sauti moja ya uwongo ya kama inamuuma tumbo yake na alitoka inje. Hule mutawa mwivi alipata saa na alifuchika bile bintu. Alirudia kisha saa kidogo hule mutawa wa jangwa na alisuburia naye mambo ingine, lakini mambo ya vitu vyake asikuseme kwake hata sauti moja.

Kisha ma siku madogo watawa wengine walifamia ya kama vintu vyake aliiba hule mutawa na walimubamba na walimupeleka mu buloko, bila kujua hii kazi yao huyu padri wa jangwa. Kisha ma siku ingine walimujulisha ya kama jirani yake ni ndani ya buloko, lakini hasikujue sababu gani walimufunga. Basi, alienda kwa padri mkubwa ya monasteri wa pempeni na alimuomba hivi:

-Ee padri wa roho wangu, fanya mapendo na unipe mayayi madogo na mukate kidogo meupe.

-Unataka kukaribisha mutu moja nyumbani yako? Alimuuliza padri mkubwa.

-Ndivyo, alimujibu mutawa muzee, bila amuwaambie sababu gani.

Lakini, kweli, aliomba mayayi na mukate juu ya kuipeleka mu buloko amupatie hule mutawa, aliyeiba vitu vyake. Alienda mu buloko. Wakati alimuona mutawa mwivi, alipika magoti mbele yake na alimwaambia:

-Ee padri wangu, kwa ajili yako mimi ni huku ndani, kwani mimi niliiba vitu vyako. Lakini kitabu fulani yako ni kwa mikono ya mtu fulani, raso (kanzo meushi) ni kwa mtu fulani.. .

-Mtoto wangu, unapashwa kujua ya kama mimi nilikuja huku hapana ya hii mambo. Misikujua hata ya kama weye uko ndani ya buloko kwa ajili yangu, lakini wakati nilisikia ya kama uko huku ndani, nilitaabu na nilikuja kukutulivu kidogo. Tazama sasa, nilikuletea kidogo mukate na mayayi. Sasa nilipata tangazo ya mambo gani uko huku ndani, lakini, usisikitike, nitafanya nguvu juu ya kukutosha ya huku.

Kweli alienda na aliliya mbele ya wakubwa wengine, wenye walimufamia na walimusifu kwa fazila yake na wale walimuuhuru.

## Uvumilia ya mtakatifu mutawa Dorotheos

Hile wakati mutawa Dorotheos alitumika mu obitalo ya wazee ya monasteri ya padri mkubwa Seridos ya muji Gaza, ndugu moja, alimuchabula p. Dorotheos, bila sababu. Huyu Dorotheos hasikuseme sauti hata moja mbele yake!

Padri mkubwa Seridos alijulishwa juu ya hii tabia ya ndugu na alitaka amulipiza.

Hile saa padri Dorotheos alianguka mbele ya miguu yake na alimusema:

-Hapana, padri mkubwa wangu.. .  Hapana, kwa jina ya mapendo ya Kristu.. .  Mimi nilikosa. Si eko mukosefu ndugu!

Wakati ingine watawa wengine walikuja kila siku na walipumputa manguo ya vitanda vyao mbele ya chumba ya mutawa Dorotheos, kwani walikuwa na chawa.

Usiku alirudia nyumbani yake padri Dorotheos na muchoko mingi juu ya kupumuzika na ma chawa wote walimulumiza na huyu alifanya nguvu juu ya kuwaua. Kwa ajili ya muchoko mingi, alilala, lakini asubui ma chawa waliisha kumulumiza sana.

Lakini, hasikuseme hata kwa ndugu moja: «Juu ya nini unafanya hivi»? ao «Usifanye tena» ao «Simama kuniuzi».

Hasikusema sauti moja mbele yao! Hata sauti moja hasikuseme juu ya kuleta huzuni ya roho kwa ndugu moja wake!

## Chemchem moja mu Pambluki

Mutawa mtakatifu Serafim wa Domboitis (1527-1602) katika amri na onekano ya Mzazi-Mungu Bikira Maria, alinunua shamba moja karibu ya mukini Dombos ya njimbo Viotia ya Grekia (Hellas) na alianza kujenga monasteri yake.

Lakini walimusitake kwa mkubwa ya muji Livadia ya kama alilanda watu wa hile mukini na alinunua shamba yao na bei kidogo sana. Mkubwa ya njimbo alituma wa askari tatu juu ya kumubamba na kumuongoza mbele yake.

Wale wa askari walifika mu mukini Dombo, pahali alitumika mutawa Serafim. Walimuchabula na walimupiga pa kichwa yake na padsri alianguka chini ya kutosha damu mingi na alikuwa sawa kufa. Kichwa yake ilifunguliwa! Kofi pa kichwa yake inaonekana mpaka sasa pa mufupa ya kichwa yake.

Wakati alisikia kidogo nzuri, walimufunga na ma kamba na waliondoka waende mu muji Livadia. Walitembea na miguu mpaka saa moja na wa askari walikuwa  na lazima ya kihu. Walitafuta mu njimbo Pamluki ya maji, lakini hakuna namna kuipata. Waliteswa sasa kwa ajili ya maji.. . .

Hile saa mutawa Serafim aliteswa kwa ajili ya pigilio na bilonda yake, lakini alifata mapendo na uvumilia ya Bwana Yesu Kristu. Aliwaambia wa askari wamufungule mikono yake na wasimame kidogo juu ya kufanya sala kwa kusaidia hawa!

Wa askari walimufungula ku monyororo yake. Hule mutawa alipika magoti na aliomba na machozi mingi. Kisha alipiga na bakora yake bulongo chini na mara moja ilitoka maji safi na wa baridi na walikunywa wa askari na wlaifurahi.

Hii maji, ni muujiza ya mapendo na uvumilia ya mutawa Serafim. Inatosha maji mpaka sasa na inafurahisha wale watu wanapita ya hile fasi.

## Muuaji wa ndugu wake

Wakati mtakatifu askofu wa Egina jina lake Dionisios (1547-1624) aliishi mu Monasteri ya Mzazi-Mungu wa Anafonitria ya Kisanga Zakinthos ya Grekia, usiku moja alikokola mulango ya monasteri yake mtu moja asiyemufamia.

Macho yake ilikuwa na makali, uso yake ilijaza na muchoko, sauti yake iliisha kuzimishwa. Alitetemeka. Alikuwa mukali sana. Mtakatifu Dionisios alimuuliza ya mambo gani alikuja kwake usiku na juu ya nini eko na sikitiko rohoni yake.

-Padri wangu, nilikosa, alimujibu na sauti yake wa taabu na alianza kuliya. Niliua! .. . Akili yangu ilijaza na ngiza na nilifanyika muuaji. Sasa kundi ya watu wingi wananitafuta na wanataka wanibambe. Unifuchame ndani ya monasteri yako na uniokoe.

-Unaua mutu gani, mtoto wangu?

-Niliua mtu mkubwa moja ya muji Zakinthos. Jina lake Konstantinos Siguros.

Mtakatifu Dionisios alishituka, kwa sababu huyu Konstantinos alikuwa ndugu yake katika mwili. Machozi kidogo ilianguka na ma macho yake, pasipo kusema kwa muuaji ya kama alikuwa ndugu yake.

Walikuwa wa ndugu wapenzi. Padri Dionisios aliisha amupatie uriti yake yote na ndugu yake alikuwa mutajiri, mwenye furaha na mkubwa ya Kisanga yao.

Mt. Dionisios alijulishwa hii jambo ku midomo ya muuaji ya ndugu yake. Tena mara moja huyu muuaji alimuomba amufuchika na amuokoe. Ilipaswa sasa mt. Dionisos kufanya nini? Ilipaswa amupatie muuaji ya ndugu yake kwa kundi ya wa askari, wenye walikuja kisha saa kidogo ao ilipaswa kusukumu huzuni ya roho yake na amufuchike muuaji ya ndugu yake?

Mungu alimutuma uwezo yake kwa roho ya mt. askofu Dionisios. Alizimisha ndani ya roho yake kila woga na kila mapendo ya ndugu yake na alifata mapendo ya Bwana Yesu Kristu, aliyesamehe wenye walimusulubisha.

Mukristu alishinda mtu. Mt. Dionisios aliona mbele yake paka moja muuaji mupotevu, aliyemuomba saidio na ulinzi yake. Na askofu alimupatia mapendo na ulinzi katika roho yake muzima. Na hivi alitukuza uzima yake na hii tendo kubwa!

Wakati kisha saa kidogo ilifika kundi ya wa askari na wandugu ya kizazi yake, mt. Dionisios alimubeba muuaji na mukono yake na alimufuchama ndani ya nyumba moja. Wa askari walikuja na kutosha jashu mingi na walimwaambia hii jambo wa matata. Askofu anaonyesha ya kama hasijue kintu na alianza kuliya pamoja nao. Juu ya kupata wakati aliwaambia:

-Muuaji ya ndugu yangu hasikupite huku, mwende mbio kutafuta kama aliingia ndani ya hile pori ni ngambo ingine, kwani pale ni miti marefu na iko namna alienda pale kufuchamwa.

Wakati kundi ya wa askari waliondoka, alishuka askofu chini pa hile chumba aliisha kufuchama muuaji ya ndugu yake na alimuita na sauti wa chini:

-Hule mutu ulimuua, alikuwa ndugu mudogo wangu! Niliweza kukuhukumu na kukutoa kwa hakli ya inchi.. . Lakini misikufanye hivi. Basi, uende sasa.. . Nilitayarisha mutubwi moja na vitu vya chakula yako juu ya kuenda mu fasi ingine jina lake Peloponisos. Pale, wakati utafika fanya nguvu kutubu na kuungama zambi yako. Kristu pa Msalaba alihurumia zambi ya hule munyanganyi, aliyetubu ku mwisho ya uzima yake. Basi, na weye kombana kutubu na kupata usamehe ya zambi zako!

Alipika magoti yake mbele ya askofu huyu muuaji na alilobana mikono yake katika machozi yake.

Ilikuja usiku na inje muda ilikuwa na ukimya na utulivu. Katika amri ya askofu watawa wa tatu walimubeba huyu muuaji na mutubwi ya monasteri yao walimupeleka mu inchi ingine Peloponisos pamoja na vitu vya chakula vyake.

## Wanyanganyi walimupiga mt. Serafim wa Sarofi

Mu tarehe 12 Septembrie (Mwezi ya Tisa) ya mwaka 1804 mtawa mt. Serafim wa Sarofi walikuja mu pango ya jangwa yake wanyanganyi na walimupiga sana..

Watu tatu wa mukini moja walimukaribia na walimwaambia:

-Tunataka kutupatia hii makuta waaminifu wanakupatia.

-Misibebe makuta ya watu, aliwajibu padri Serafim.

Wale walikataa kumusadiki. Tena munyanganyi moja alimupika na kofi yake ku mukongo juu ya kumutupa chini. Lakini alianguka huyu wa pekee. Wanyanganyi wengine walisirika. Mt. Serafim alikuwa na nguvu yake na shoka pa mukono yake na aliweza kuchunga maungo yake, lakini alikumbuka sauti ya Yesu Kristu ya kama ninyi wote walikamata kisu, watakufa na kisu. Basi, aliacha shoka chini, alifunga na alama ya msalaba mikono yake pa kilari yake na alisema na unyenyekevu:

-Mufanye kila tendo munataka.

Alikuwa asiye na kosa, lakini aliisha kukamata mpango kuvumilia kila mambo kwa ajili ya mapendo ya Kristu.

Hile saa munyanganyi moja alikamata shoka na alimupiga mt. Serafim pa kichwa yake. Mt. Serafim alianguka chini. Wanyanganyi walimubamba na walimukokota mu nyumba yake. Kwa kutembea pa njia, walikuwa makali na walimupiga na miguu yao. Mara moja waliwaza kumutupa ndani ya mutoni, lakini, kwa sababu walizania ya kama aliisha kufa, walimufunga mikono na miguu yake na walimuacha inje ya nyumba yake. Kisha waliingia ndani juu ya kutafuta makuta sawa vile walizania.

Walianza kutafuta na haraka: Walibomoa hile fasi ilikuwa moto, waliharabisha dari ya mbau na walichanga vitu vyote. walipata paka picha (ikone) moja na bilashi kidogo. Hile saa walisikia kosa yao, kwa sababu walimupiga mt. Serafim mpaka karibu yakufa juu ya kubeba makuta yake, lakini sasa hawakupate kitu. Waliogopa na walikimbia na haraka.

Mt. Serafim, wakati alisikia kidogo nzuri na alifungula monyororo yake. Alimushukuru Mungu, kwani alimustahili kuvumilia kwa ajili Yake na alimuomba amusamehe wanyanganyi.

Hile usiku alipita katikati ya maumivu na maombolezo yake. Asubui aliondoka aende mu monasteri yake. Alifika pale pa hile saa wapadri walifanya Ibada ya Liturgia kimungu. Uso yake ilikuwa na vumbi na damu. Tena vilonda ilikuwa pa mikono na meno yake iliisha kupasuka. Toka kinywa na masikio yake ilitoka damu, lakini manguo yake iliisha kujaza na damu ya kukauka.

-Mambo gani ukona yo? Walimuuliza watawa wengine.

-Mwende kumuita padri mkubwa  na padri wa roho ya monasteri.

Wakati walikuja wale, aliwaelejea hii jambo yake. Kwa ajili ya vilonda vyake alibaki mu monasteri yake.

Ma siku mnane wa kwanza hali yake ilikuwa mbaya. Hasikuweze kubeba hata chakula, hata maji, hata musingizi kidogo kwa ajili ya maumivu yake. Watawa wote walisadiki ya kama atakufa.. .

Lakini, katika saidio ya Mzazi-Mungu aliponyeshwa. Hile wakati alionyesha uvumilia na mapendo yake.

Wanyanganyi waliwabamba! Walikuwa watumishi ya mkubwa moja ku mukini Kremenoki. Padri Serafim na padri mkubwa ya monasteri Isaya waliwasamehe na walisema na kwa mkubwa yao hapana kuwalipiza!

Lakini Uhaki kimungu uliwalipiza! Ma nyumba yao ililungua na wale walikuja kwa mutawa mt. Serafim na machozi pa ma macho yao na waliomba usamehe na maombezi yake.

## Usiku moja ndani ya nyumba ya nguruwe

Askofu mkubwa ya Rumania mu milele 19, alikuwa Grigorio Mikulesku (1765-1834). Aliishi sawa mutawa mu monasteri Neamchu na mu mwaka 1823 alipokelea ndani ya chumba yake kundi moja ya watu wakubwa, wenye walimusema:

-Mkubwa ya inchi yetu anakuita kufanyika askofu mkubwa na anakuita kufika mu muji kubwa ya inchi yetu.

-Kwa sababu ananiita mkubwa ya inchi yetu nitakuja, alisema mutawa wa jangwa Grigorio. Lakini juu ya kuongoza waaminifu mu njia ya wokovu misina mustahili. Paka hii uwazo inanitetemesha.

Vile, kisha ma siku wa wili aliondoka aende mu Bukuresti, muji kubwa ya Rumania.

Wakati alipita mu mukini Tunari, padri alimuona ya kama huyu mugeni alivaa manguo mazuri na alizania ya kama alikuwa mwivi moja na mutawa wa uwonga. Basi, alimubamba na alimufunga ndani ya nyumba ya nguruwe. Siku ingine asubui musaidizi ya padri moja alimuuhuru mutawa Grigorio kwa siri.

Kisha wakati kidogo huyu padri alimuona mutawa Grigorio Askofu mkubwa ya inchi Rumania na alishituka. Lakini askofu Grigorios alimuwaambia na mucheko:

-Usitaabu, ee padri, kwa sababu na ma nguruwe yako walinionyesha mapendo na uvumilia na tabia yao ilikuwa nzuri mbele yangu!

## Uzaifu ya mkubwa wa askari

Padri mkubwa Yoano wa Kronstandis ya inchi Rusia (1829-1908)  pampeni ya kazi ya waaminifu juu ya wokovu wao, alijenga na nyumba mnene moja juu ya kusaidia wale waliishi bila kazi.

Alifanya nguvu ya kutafuta makuta juu ya hii majengo miaka tisa. Hii nyuumba iliisha mu mwaka 1881.

Wakati iliisha majengo yake, ilifanyika teso moja matata: Usiku moja ndani ya magazine moja kidogo mbali ya hii nyumba mupya ilipata moto na ililungua! Moto ilizambala ma fasi ingine pempeni na ilikaribia hii nyumba ya padri Yoano. Padri aliangalia hii hatari iliyekuja na alimwaambia kwa mukubwa ya police kufanya nguvu ya kusaidia hii mambo. Maombi ya padri ilikuwa ya bure, kwa sababu huyu mkubwa ya wa askari hasikufanye kitu na nyumba mupya yake ililungua yote!

Padri Yoano alipata uchungu mingi ndani ya roho yake na alimuhamakia huyu mkubwa, bila kusema sauti yake.

Waaminifu na inchi walisaidia na hii nyumba ya kusaidia  watumishi walijenga mara ingine.

Huyu mkubwa ya wa askari (police) walimupeleka nyumbani ya uhukumu juu ya matendo mabaya yake na padri Yoano walimuita kusema sauti yake na kumusitake. Padri Yoano alijua uzima na mfano ya hule mkubwa mbele ya mambo yake, lakini alifanya na alisema nini? Hasikuseme kintu juu ya makosa ya hule mkubwa! Pahali pa kosa yake, alikobana kumuokoa kwa kusema matendo vizuri na namna ya tabia yake muzuri. Mankagamano yake ilikuwa munene juu ya kumutosha ya uhukumu, lakini alijua ya kama kwa ajili ya uzaifu ya huyu mkubwa ililugua nyumba mupya yake. Mkubwa ya uhukumu Mwamuzi alisikia ya kama padri Yoano alikombana kumusaidia na kumutosha ya nyumba ya uhukumu na alisema kwa padri:

-Sema paka kweli na usifuchike matendo yake m, abaya.

-Mimi ninasema kama padri ya Mungu, alimujibu na nguvu padri Yoano mukungamana kufanya tendo kizuri pahali yeye alipata tendo kibaya.

# UKAMILIFU

## Wivi ya Madiko Takatifu

Mutawa Gelasios alikuwa na kitabu moja muzuri sana «Madiko Takatifu» na bei yake ilikuwa karibu makuta kumi na tano ya zahabu. Kitabu yake ilikuwa na bei mingi, lakini padri aliiacha mu kanisa ya mukini wa Watawa kuitumika naye watawa wote.

Lakini siku moja mutawa mugeni moja, aliyepita ya mukini yao aliiona hii Kitabu na aliiba. Padri Gelasios mara moja alisikia ya kama huyu mutawa aliiba Kitabu yake, lakini hasikupende kumubamba huyu mutawa mugeni. Hule mugeni, wakati alienda mu muji, mu soko, alipata mutu moja juu ya kumuuzisha. Aliomba makuta kumi na sita. Hule aliyependa kuinunua alimwaambia ya kama anaomba makuta mengi. Ku mwisho mutawa alimupatia hii Kitabu kwa hule mtu juu ya kuionyesha kwa mtu moja mwingine aliyejua bei ya hii Kitabu.

Hivi hule mutu mugeni alibeba Kitabu na aliipeleka kwa padri Gelasios aliyekuwa rafiki yake. Alimuuliza:

-Nitanunua hii Kitabu na makuta kumi na sita? Bei yake haina mingi?

Mt. Mutawa Gelasios mara moja alifamia Kitabu yake, lakini hasikuseme ya kama ilikuwa yake. Aliichukua pa mikono yake, aliipapasa sawa aliiona mara ya kwanza.

-Muzuri. Bei yake ni muzuri, Uinunua, alisema kwa rafiki yake.

Wakati alirudia huyu mtu alienda kwa hule mutawa mwivi na alimwaambia:

-Nilipeleka Kitabu yako kwa padri Gelasios na aliniambia ya kama unaomba makuta mengi. Hii bei unasema ni mingi.

-Hasikukuulize padri Gelasios kitu ingine? Alimuuliza na ushituko na tetemeko hule mutawa mwivi.

-Hapana, alimujibu huyu mtu aliyetaka kuinunua hii Kitabu.

-Ninatubu! Misitake kuiuzisha, alisema huyu mutawa.

Ndani yake ilianza bugomvi moja munene. Pa ngambo moja alishangaa ukamilifu na mapendo ya padri Gelasios na pa ngambo ingine nafsi yake ilimuhamakia (condrol) juu ya hii

tendo yake kibaya. Basi, alibeba kitabu na alipanda mu mukini ya watawa. Wakati alipata padri Gelasios, alipika magoti mbele yake na alimuomba hurumia na alimurudisha hii Kitabu yake. Hule padri alimuhurumia mara moja na nafsi yake yote na tena alitaka amupatie Kitabu yake sawa zawadi. Lakini, namna gani ataipokelea huyu mutawa?

-Beba Kitabu yako, ee padri wangu, kwa sababu roho hangu paka vile itapata ukimya.

-Kama ni vile, uende mu kanisa na uiache pa hile fasi uliiba, alimuwaambia na mapendo mt. Gelasios.

Tangu hile wakati alifata muzuri njia wa kweli huyu mutawa na asikufanye hii tendo ya kuiba vitu vya watu vingine.

## Vitunga ya mutawa wa jangwa

Mutawa moja wa jangwa aliondoka siku moja aende kuuzisha vituga yake mu muji wa karibu yake. Mu njia, alimupata shetani na kwa ajili ya mfano na tabia mubaya yake, alikamata vituga ku mikono ya mutawa na alikimbia bila kuonekana.

Hile saa mutawa muzee, bila kusikitika hata kidogo, alinyanyua ma macho yake mbinguni na alisema:

Ee Mungu wangu, ninakushukuru, kwani ulinibeba uzito ya vituga yangu na misitachoke kuenda kwa muji ya hii kazi.

Hile saa shetani, kwa sababu, hasikuvumilie ukimya ya roho ya mutawa, alirudia na alimutupa pa uso yake vituga vyake na sauti nguvu kusema kwake:

-Kamata mukongo, muzee mubaya.

Mutawa wa jangwa alilokota vituga vyake na aliendelea njia yake aende mu mukini ya kuiuzisha.

## Saidio ya mt. Yoano Mubatizaji

Mu monasteri ya Pentukla, karibu ya mutoni Yordani aliishi mutawa wa jangwa mtakatifu Konon. Kwa ajili ya uzima takatifu yake walimupatia wapadri wakubwa baraka kubatiza wale walitaka kubatizwa. Kisha aliwapakala na Mafuta Takatifu (Krisma).

Lakini kila mara alibatiza mwanamuke moja, alijikuaza na kwa hii mambo alitaka kusimamisha hii kazi ya ubatizo ya watu na kutoka ya monasteri yake. Lakini kila mara aliisha kukamata mpango atoke, alionekana kwake mt. Yoano Mubatizaji na alimwaambia:

-Fanya uvumilia na mimi nitakushushia bugomvi yako pa mwili yako.

Lakini bado kupata hata kidogo saidio.

Siku moja alikuja kubatizwa binti moja toka inchi Persia, aliyekuwa muzuri sana pa uso na mwili yake. Kwa sababu alichelewa padri Konon kufanya kazi yake, walimusitake kwa askofu mkubwa yake, ya muji Yerusalema, jina lake Petro. Arkiaskofu aliwaza ya kuenea na kisha alisema hii yeyuko: Alikamata mpango kuweka mwanamuke moja juu ya kupakaa wanawake na hivi atasaidia padri Konon.

Hii yeyuko ya arkiaskofu walikataa watawa ya Monasteri. Wahakutake kuikaa karibu yao mwanamuke moja. Mukuona hii mambo padri Konon alisimama, alivaa nguo-mupila yake na aliondoka atoke.

Hile saa, basi, alikimbia pa milima, alionekana kwake mt. Yoano Mubatizaji na alimusema:

-Rudia mu monasteri yako na mimi nitatosha bugomvi ya mwili yako.

Mt. Konon alimujibu na sikitiko:

-Misitakusikie mara ingine! Mara mengi tangu zamani uliniambia ya kama utanisaidia, lakini usikufanye kintu.

Mubatizaji ya Kristu alimukaribia, alimufanyishia alama ya msalaba mara tatu pa uso yake na alimusema:

-Misikusaidie mpaka sasa, kwa sababu nilitaka kupata weye malipo ya roho kwa ajili ya ushindani yako kupigana ya majaribu ya mwili yako. Lakini, kwa sababu weye usitake malipo, tazama, tangu leo hautakuwa na bogomvi ku mwili yako, lakini hata malipo ya roho. Basi, rudia mu monasteri yako.

Alirudia mu monasteri yake mt. Konon na siku inmgine alibatiza na alipakaa hule binti wa Persia, bila kuwaza ya kama mbele yake alikuwa mwanamuke! Aliendelea tangu hile siku kubatiza waKatikumeno ya wakati miaka kumi na mbili (12), ni kusema mpaka mwisho ya uzima yake, bila kufanya uchanisho moja katikati ya wanaume na wanawake.

### Wanawake wasiyo heshima

Siku moja alipita mt. mutawa Andreas mazimu katika Kristu, mbele ya ma nyumba ya wale wanawake wenye zambi na alifanya sawa alicheza. Alimuona mwanamuke moja mwenye zambi namna gani alicheza na alimukokota nyumbani yake. Hule alimufuata. Wakati aliingia ndani, walikuja pempeni yake na wanawake wengine wenye zambi.

-Walimuuliza na muchekeleo: Namna gani ulipata hii malari?

Mt. Andreas alicheka, lakini hasikujibu hata sauti moja. Wanawake wengine walimupiga, lakini wengine walimubebelesha na walimubusu juu ya kumukokota mu zambi. Wakati walisikia ya kama alikuwa mukamilifu na asiye kuwa matakio ya zambi ya mwili walisema:

-Huyu ni ao mufu ao wa mbau ao wa njiwe!

Mtakatifu mutawa Andreas aliona katikati yao shetani ya usharati! Huyu shetani alikuwa mueushi na mukali. Pa kichwa yake hasikukuwa na ma nywele. Alikuwa pa kichwa yake maivi na buchafu. Ma macho yake ilifanana sawa ma macho ya nyama mbweha na pa ribeka yake alikuwa na kilako moja. Yulu yake ilitoka harufu mubaya tatu ya kuachana. Hii harufu ilikuwa hata nguvu na mtawa Andreas hasikuweze kuvumilia na alifunga pua yake. Mukuona shetani kumuzarahu hivi mt. Andreas alimusema:

-Watu weko na mimi ndani ya roho yao sawa sali utamu na weye unanizarahu na unatosha tema juu yangu?

Mt. Andreas, alimuchekelea shetani kwa hii harufu mubaya yake na aliondoka ku hii nyumba ya zambi.

## <u>KUKATAA MAPENDO YA MAUNGO</u>

### Kimbiyo ya mwenye kufunga

Taifa moja iliyeitwa Logovardi wakati moja waliiba na waliharabika kipande wa kaskazini ya inchi Italia.

Walibamba sawa mutumwa shemasi moja na walikamata mpango kumuua na mateso ya mbali-mbali. Mukristu moja, ku taifa ya Logovardi, aliyekuwa mukristu na wandugu wake waliheshimiwa sawa mtakatifu alifanya nguvu na alizungumuza pamoja na wakubwa juu ya kumuokoa hule shemasi mutumwa. Lakini hasikutenda hata, paka walimupatia ruhusa yao kusimama huyu mukristu karibu ya shemasi hile usiku ya mwisho yake, mbele ya kumuua.

-Mbakia karibu yake, alimwaambia mkubwa ya taifa, lakini kama atakimbia, unapashwa kujua ya kama sisi tutakupiga weye.

Huyu mukristu, jina lake Sagktulos, aliitika na aliikaa zamu ya shelami hile usiku yake wa mwisho. Basi, katikati ya usiku, hile saa kundi ya askari walilala wote, alilamusha shemasi na alimuwaambia asimame na atoke na haraka. Inje aliisha kutayarisha na punda ya kutembea mbio.

-Ndugu wangu, hakuna namna kukimbia mimi, alimujibu mwenye kufunga. Kama mimi nitaokoa, weye hakuna namna kuokolewa ku mikono yao. Namna gani mimi nitakuwa sababu kukufa weye na lufu matata?

-Usisikitike juu ya mimi, alimujibu Sagktulos. Mungu atanifunika.

Vile alikamata mpango kukimbia huyu mutumwa shemasi.

Siku ingine asubui wakubwa ya taifa Logovardi, walitafuta mutumwa.

-Alikimbia, aliwasema na upole zamu yake.

-Sasa utajua wewe namna gani huyu alikimbia.

-Ndivyo, aliwajibu nguvu mukristu Sagktulos.

-Kwani uko mtu muzuri, misitake kukupiga, alimujibu mkubwa, mwenye alimustaajabu, bila kuonyesha hii musagao yake. Chagua sasa namna juu ya kukufa!

-Niko pa mikono ya Mungu, alimujibu Sagktulos bila kuogopa. Hii lufu Mungu anapenda, mimi nitaipokelea na shukrani katika mapenzi ya Mungu.

Ku mwisho walikamata mpango kumukata kichwa yake na shoka! Walipatia ya kumaliza hii uwanji kwa askari moja mkubwa katika mwili yake.

Sagkulos alipika magoti, alifanya sala yake na alinamisha na uvumilia kichwa yake juu ya kupokelea pingilio na shoka. Nafsi yake ilijaza na shangilio, kwa sababu kisha saa kidogo ataenda katikati ya mikono ya Bwana Yesu Kristu.

Huyu askari alinyanyua shoka na alikuwa tayari kumupiga, lakini mikono yake walibakia pa pepo bila kutengwa, sawa nguvu moja ingine iliwafunga. Alisikia maumivu mengi, alianza kuliya sawa nyama ya pori kwa kilonda yake. Wa askari wengine waliogopa.

-Walisema katikati yao: Tunataka kufanya nini? Tunataka kupiga mtakatifu moja, aliyeishi pamoja na Mungu?

Basi, walianza kumuomba hule mukristu amuponyeshe huyu askari, aliyekuwa na mikono yake pa pepo.

-Misiweze kuomba hii saidio toka Bwana Mungu wangu, paka, kama huyu atanilapa ya kama hasitanyanyua shoka mara ingine kupiga mukristu mwingine, alisema Sagktulos.

-Ninalaka, alipaza sauti nguvu huyu askari na alitetemeka kwa woga wake.

-Mutumishi ya Mungu alimuhamuru: Basi, shusha sasa mikono yako.

Mikono yake ilitengwa na wa kwanza walitupa shoka.

Watu ya taifa Logovardi walishangaa mbele ya hii matendo wa ajabu waliona, walimuacha hule mukristu aishi na tangi hile siku alikuwa mutume katikati yao mu imani ya Bwana Yesu Kristu.

## Uchinjo ya watoto wa mfalme ya inchi Rusia

Mtakatifu Vladimiros, mfalme wa kwanza ya inchi Rusia, alikuwa na watoto wake, wanaume, kumi na moja. Kisha lufu yake (1015) mtoto mkubwa wa kwanza, jina lake Zviatopolk, alikombana kuepuka wandugu wadogo wake juu ya kuwa paka huyu mkubwa ya inchi Rusia. Ya kwanza alikombana kuua mudogo yake Voris, aliyekuwa na kipimo yake umri miaka makumi mbili (20).

Voris, wakati alipata ujulisho ya mkubwa ndugu wake, alikuwa mkubwa ya kundi moja ya askari. Wanaume wake, askari, walimupenda, kwa sababu walimufamia sawa mkubwa mwenye nguvu juu ya kuchunga na kulinzi inchi yao mbele ya adui yao. Lakini, bila kusimama na nvita mbele ya mkubwa ndugu yake, alijitoa na askari ya mkubwa ndugu yake walimuua, pasipo wema.

Alikuwa kijana na alipenda kuishi katika imani ya Kristu, lakini hasikupende kwa ajili ya ulinzi yake kukufa wa askari wake. Alikuwa tayari kuongoza mu njia ya nvita kundi ya wa askari yake juu ya kuchunga wazazi na ma jamaa na watoto wao, lakini pa hii fasi, adui alikuwa mwingine; alitaka paka kiti yake ya ufalme wake. Voris alikamata mpango akufe na kutoa uzima yake juu ya kuchunga wa askari wake wazima, wenye walimufata hamuri yake.

Ndugu mudogo yake, jina lake Gklebi alifata mfano ya ndugu yake Voris na alijitoa na yeye na namna umoja, kisha ma siku ingine.

Taifa wa Rusia alishangaa na aliliya kwa hii ucjinjo ya wa ndugu wa wili. Tabia yao ilifanyika mu Hadisi yao mara ya kwanza. Wa askofu walisema ya kama hii sandaka yao ilikuwa kwa bure, lakini waaminifu wa Rusia waliwaza na namna ingine. Walifamia ya kama lufu wao ilifanyika katika mapenzi yao, ilikuwa utimizo ya amri ya Kristu juu ya kupenda ndugu yako sawa maungo yako. Ku mwisho waaskofu waliitika na walifata uwazo ya taifa wa Rusia na ku mwaka 1020 waliwafamia wote wa wili watakatifu mu Kanisa yao Orthodokse.

Ma jina yao wanabakia mpaka sasa na mapendo mingi katikati ya ma jamaa ya inchi Rusia na mfano yao inawaongeza musagao yao, kwa sababu walikufa katika mapenzi yao juu ya kuchunga wa askari wa ndugu wao. Voris na Gklempi hawakuitwa washahidi, kwa sababu hawakukufe kwa imani. Waliitwa «wabebaji wa mateso», kwani waliteswa na walikufa kwa ajili ya mapendo.

## Wa askari wa inchi Germanie mu monasteri Logovarda

Usiku ya tarehe 14 ku 15 mwezi ya tano ya mwaka 1944 chombo moja na wa askari ya inchi Aglia, ilikaribia mu kikavu ya Kisanga Paros ya inchi Grekia (Hellas). Hawa wa askari walipanda mu mukini Chipido na walibamba wa askari wa Germanie pa musingizi yao. Waliuawa askari wa wili, walipiga jemadari yao na walimuacha na vilonda, jina lake Tambe na walikimbia pamoja na wa askari watumwa saba.

Asubui wa askari wa Germanie walibamba sawa mukosefu mtu mwingine, wa inchi Grekia, jina lake Nikolaos Stelas na walimutundika pa fasi moja urefu juu ya kuogopa na wakaa watu ya mikini wa pempeni.

Kisha mkubwa ya Kisanga Paros, aliomba toka wakubwa ya mukini yao wamupatie 125 wanaume vijana juu ya kuwaua! wakubwa ya mukini walifanya makusanyo pamoja na wapadri ya Kisanga yao na padri mkubwa ya monasteri ile ni mu Kisanga yao na inaitwa Logovarda, jina lake padri Filotheos.

Huyu padri aliisha kukamata mpango hapana kuomba saidio ya watu wengine. Mpango yake ilikuwa paka moja, bila kitengo!

Kundi moja na watu wa tatu: Padri Filotheos, munganga Alipranti na mkubwa ya mukini moja, jina yake Kavalis walienda kwa mukubwa wa Germanie, aliyekuwa mkubwa ya wa askari wa Germanie (Hile wakati Grekia ilikuwa pa utumwa ya mamlaka wa inchi Germania) kusema kwa mukubwa yake hapana kuuwa vijana 125, bila kosa yao.

Huyu mkubwa, jina lake Zase, aliwajibu:

Niliisha kumuomba hapana kuua hawa vijana, kwani wasikuwa wakosefu, lakini yeye anakataa. Paka padri mkubwa iko namna kumuita kumubebelehsa na kisha atamwaambia hii mambo ya 125 vijana. Niliisha kumusema ma sauti mengi mazuri juu ya hii monasteri yenu na yeye alisikia na furaha.

Padri Filotheos hasikupoteshe wakati yake. Mara moja alimuita mkubwa jemadari. Huyu alimujulisha ya kama atakuja mu monasteri mu juma ingine pamoja na kundi ya wa askari wake sita.

Hile siku alisema, alikuja na wafwasi wake. Mfano yake ilikuwa ukali na ugumu, lakini ma macho yake pole-pole kwa ajili ya ukaribisho muzuri ya padri na watawa wengine, mfano yake

ilikuwa sasa kupita nzuri. Alikuwa ndani ya Ibada ya Magaribi na pasipo kusikia, alifanya padri na maombi juu ya wokovu ya wale 125 vijana!

Kisha Ibada wale wakubwa walikuwa tayari kuondoka. Padri Filotheos aliwaza namna gani ataleta mambo yao katikati ya hule mkubwa juu ya kuzungumuza. Mzazi-Mungu alimuangaza akili yake!

Mbele ya kufungula kinywa yake padri Filotheos, huyu mkubwa alimuwaambia: Kama anataka kuomba tendo moja, sasa iko namna amuombe ya kwake.

Padri Filotheos alibeba nguvu aliomba kubakia ya zungumuzo paka huyu pamoja na jemadari mkubwa na mufasiri yake juu ya kumufafanusha ma sauti yake.

Alisema kwa mufasiri: Sema kwa mkubwa yako ya kama ninataka anifanyishie sawa zawadi tendo kimoja.

Jemadari alimupatia mukono wa kuume na alimulaka ya kama atamutimiza kila maombi atamuomba..

-Ninataka, alimuwaambia padri mkubwa (Igumeni) kuacha wauhuru wale vijana aliwabamba kwa sababu uhukumu yao ni isiyo na haki.

Lakini jemadari alimujibu:

-Omba kintu ingine! Hii amri haina yangu; ni ya wakubwa yangu, wenye wanasema, kama anauwa askari moja wa Germania, pa hile fasi tunapaswa sisi kuua watu wa Grekia 50. Kama misitamaliza hii amri, hata kama ni isiyo na haki, wataniua mimi. Basi, omba ombi ingine.

Padri mkubwa alimwaambia na nguvu ya roho yake:

-Ulinilaka ya kama utanifanyishia hii ombi nitakuomba. Sasa unapashwa kutimiza sauti-malako yako.

Lakini, kwa sababu jemadari mkubwa alikataa, padri Filotheos alitembea pa njia ya sandaka ya maungo yake. Alimujibu:

-Kama unakataa kutimiza hii ombi yangu, utaniua na mimi pamoja na vijana!

Jemadari alishituka. Kisha alimujibu:

-Nitakupatia wale vijana wako wazima! Lakini utasema kwa watu wote ya Kisanga yenu, hapana kufanya hii tendo kibaya mara ingine, kwa sababu nitakuwa mukali sana.

Padri mkubwa alimulaka hivi na wa askari wa Germania waliondoka ya Kisanga Paros. Hivi Paros kwa ajili ya sandaka ya padri mkubwa aliokolewa.

# **<u>KIASI</u>**

## Fundisho moja kwa wakaa ya Tavenisos

Mtakatifu mutawa Makarios wa muji Aleksandria alipenda sana ushindani ya roho. Kama kwa m, fano alisikia ya kama mutawa mwingine alitenda ushindani moja fulani, alikombana na huyu kuimaliza! Hapana juu ya majivuno, lakini juu ya mapendo yake mbele ya ushindani ya roho, inaye iko mama ya utakaso.

Hivi, kwani alisikia siku moja ya kama mutaw amoja alikula kila siku paka 320 gram. mukate, alikata mukate ya kukauka na vipande-vipande, aliiweka ndani ya birika moja na alikula na yeye paka 320 gram. kila siku.

Huyu mkubwa mutawa wa jangwa, wakati alisikia juu ya uzima takatifu ya wanafunzi ya mt. Antonio, alivaa manguo sawa mutumishi wa dunia, alienda mu monasteri ya watawa wa fasi Tavenisos ya Misri. Pale alipata padri mkubwa na alimuomba:

-Unipokee mu monasteri yako, ninataka kuwa mutawa. Mtakatifu mutawa Pakhomios alimuangalia na alimuwaambia:

-Sasa weye uko muzee na usiweze kufanya ushindani ya roho. Wandugu wangu huku weko washindani ya roho na hautaweze weye kufata michoko yao. Utajikuaza na utaondoka katika haya na utatusimanga. Padri mkubwa Pakhomios alikataa kumupokelea ya juma moja. Padri Makarios aliyeonekana sawa mutumishi wa dunia, alisimama inje ya mulango ya monasteri na alimuomba mara ingine:

-Ee Ava, unipokee, na kama mimi misitafate desturi ya kifungu na ya kazi sawa wa ndugu wako, utanifukuza.

Katika hii sikilizano alimupokea. Alimuuweka ndani ya monasteri pahali waliishi 1400 watawa.

Kisha saa kidogo ilifika na wakati ya Kwarezima. Mtakatifu Makarios aliona hile wakati wa ndugu wake kutumika katika roho kila mtu na namna ya mbali-mbali. Mutawa moja, kwa mfano alikula paka kila magaribi, mwingine mara moja kila ma siku wa wili, mtawa mwingine mara moja kila ma siku tano na mwingine alifanya sala kila usiku muzima.. .

Huyu alilobana mayani ya palme na aliikaa pa fasi moja alifanya vitunga. Alikula paka mayani mumpichi mara moja kila juma lakini mukate hasikukule tangu mwanzo ya Kwarezima mpaka siku Kuu ya Paska. Alitumika kila siku, bila kusimama na bila kusuburia na mutawa mwingine. Alitumika na mikono yake na roho yake alisema sala ya Bwana Yesu Kristu. Paka hii kazi wa pili alifanya: Kazi moja ya mwili na kazi moja ya roho.

Wakati walimuona watawa wengine, walishituka na walisema kwa mkubwa wao padri Pakhomios:

-Ulituletea ya fasi wapi huyu mutu, aliyeishi sawa asiye na mwili na anatuhukumu katika ushindani wake? Ao utamufukuza ao, unapashwa kujua sisi wote tutaondoka!

Padri Pakhomios alifanya sala kwa Mungu kusudi amujulishe huyu mtu mupya ushindani ya roho nini anafanya na nani eko. Mungu alimujulisha na kisha padri Pakhomios alimubeba padri makarios na mikono alimupeleka mbele ya Altari takatifu na alimuwaambia:

-Kuja basi, ee mutawa. Weye uko padri Makarios na ulikuja huku kwa siri. Nilipenda kukuona miaka mengi. Ninakukushukuru kwa sababu ulibomoa majivuno ya watoto wa roho yangu na uliwafundisha ya kama haipashwe kujivuna katika ushindani ya roho yao. Basi, uende mu fasi yako. Ulitusaidia ya kuenea katika ushindani yako na umuombe kwa Mungu juu ya sisi.

## Safari wa jangwa

Wakati nilikuwa mu Monasteri ya Pirgi, karibu ya mutoni Yordani, anatuelejea, askofu wa Rosu jina lake Theodoros, alikuja siku moja mutawa muzee Petros aliyekuwa toka fasi ya Pontos na aliniomba:

-Fanyua, ee ndugu Theodoros, mapendo na unisidikize niende mimi mu mulima Sinaya, kwani nilimulaka kwa Mungu.

Mimi, kwani misikupende kumutaabu, niliitika. Lakini, wakati tulitambuka mutoni Yordani, ananiaambia:

-Unapenda kulaka kwa Mungu ya kama tutatembea mpaka kufika mu mulima Sinaya pasipo kula hata kitu kimoja?

-Nilimujibu: Ee padri, hii ni ugumu kwa mimi! Misiweze kufanya hii malako.

Hule alipika magoti mbele ya Munmgu na alifanya na hii malako. Vile hasikukule hata kidogo mpaka alifika mu monasteri ya Mulima Sinaya! Pale, alipewa Vitu Vitakatifu (Mwili na Damu ya Kristu) na kisha alikula.

Kisha tuliondoka pamoja tuende mu muji Aleksandria. Na pa hii safari katika miguu, hasikukule hata kidogo! Wakati tulifika mu muji tulienda mu Kanisa ya Mt. Mushahidi Minas. Pale alikomunika mara ingine na kisha alikula.

Kisha tulibeba njia ya kurudia kwetu. na mara ingine muzee mutawa Petros hasikukule mu njia hata kidogo mukate mpaka tulifika mu muji Yerusalema. Na, wakati alipewa Mwili na Damu ya kristu mu Kanisa ya Kaburi ya Yesu Kristu, alikula chakula!

Vile kwa hii safari murefu muzee Petros alikula paka mara tatu. Moja mu Sinaya, moja mu muji Aleksandria na moja mu muji Yerusalema!

### Nguvu ya kifungo

Wakati moja walipeleka mu Skiti (mukini ya watawa) kijana moja mwanamume aliyekuwa na pepo buchafu ndani yake, kusudu wamuponyesha wapadri katika sala yao. Lakini wale kwa ajili ya unyenyekevu walikataa kufanya sala. Hivi huyu kijana aliteswa ya wakati mingi mpaka muzee mutawa moja alimutaabu, alimuweka pa kichwa yake alama ya msalaba na alifukuza huu pepo wa shetani.

-Kwa sababu unanitosha ya makao (chumba) yangu, alimuwaambia shetani, sasa nitaingia ndani yako.

-Kuja, alimujibu bila kuogopa huyu muzee padri.

Vile shetani aliingia ndani ya hule mutawa na alimutesa miaka kumi na mbili (12)! Alivumilia bugomvi ya shetani na padri alimukombanisha paka katika kifungo ya chakula na sala bila usimamisho. Hii miaka 12, hasikukule hata mara moja chakula ya kuipika pa chugu!

Shetani alishindwa kwa ajili ya hii bugomvi ya roho ya hule mutawa na alikimbia.

-Juu ya nini unakimbia? Alimuuliza padri muzee. Lakini, mimi misikufukuze.

-Kifungo yako iliniharabisha! Misiweze kuvumilia! Alisema shetani na alikimbia mbio.

## Huruma

### Mtakatifu Martinos na msikini moja

Wakati ya baridi ilikuwa ugumu kabisa mu fasi ya kaskazini ya Franza mu mwaka 334. Siku moja wa baridi nguvu sana mt. Martinos (316-397) alikuta mskini moja mutupa inje ya mulango ya muji yake.

Lakini atafanya nini sasa? Alivaa paka manguo yake. Alikata nguo yake wa inje na kipande alimupatia kwa hule mskini. Pa njia watu wenginer walimuchekela na hii mavazi yake.

Lakini usiku aliona mu ndoto yake Yesu Kristu, aliyeonekana na kuvaa na hii kipande alimupatia mt. Martinos kwa hule mskini. Na alisemaka kwa malaika wake:

-Martinos leo alinivaa na hii nguo!

### Mavazi nzuri sana

Padri mtakatifu ya muji Konstantinopoli, jina lake Markianos, alipambwa na ma fazila mengi, lakini kabisa na fazila ya huruma na umaskini. Hii ma fazila wa wili ni wa ajabu! Nikusema alikuwa maskini na alisaidia na watu wengine. Namna gani?.. .

Mt. Markianos alikuwa yulu ya kila kitu ya hii dunia na hasikupate vitu vya hii dunia hata manguo ya pili! Kama wale warafiki wake walimufamia na walimupatia kitu kimoja-zawadi moja, huyu mara moja aliipatia kwa maskini  wa kwanza atamukuta pa njia.

Hile siku ya kufanya siku Kuu ya mwanzo ya Kanisa ya Mtakatifu Anastasia, aliondoka ya nyumba yake asubui mapema na alienda mu Misa kutayarisha Altari Takatifu. Ilikuwa desturi akuje na patriarki na wa askofu wengine wingi! Tena atakuja na mfalme na wakubwa wake!

Wakati alifika karibu ya kanisa, hile yeye aliish akuijenga na muchoko mingi, alimukaribia mtu moja maskini mutupu na mwili yake ilikuwa na ragi meushi juu ya baridi mingi. Aliteswa sana. Alifungula mukono yake na alimuomba huruma. Mt. Markianos alitafuta mifuko ya gochi yake, lakini hakuna kintu. Lakini ilipaswa amupatia kwa hule mutupu kintu kimoja. Roho yake ilijaza na sikitiko kwa sababu hakuna kintu ya kumusaidia na mskini alitetemeka kwa baridi.

Padri mupenda wanadamu alikamata mpango wake. Atamupatia manguo yake! Lakini hakuna manguo yake ingine mu nyumba yake! Aliwaza: Hakuna mambo, kwa sababu ndani ya kanisa atavaa manguo takatifu ya upadri. Basi, aliingia mu Misa, alitosha manguo yake na alivaa manguo ya upadri. Alitoka inje na alimupatia kwa hule maskini manguo yake yote. Alishangaa mskini na alisikia haya kubeba manguo ya hule padri na yeye alivaa manguo ya upadri, lakini alifanya utii na alibeba manguo ya padri Markianos na aliondoka.

Hile saa walikuja na wapadri wengine pamoja na patriarki na ilianza Ibada ya Liturgia takatifu. Lakini hile siku ilifanyika jambo moja wa ajabu. Ma macho ya waaminifu wote kutoka mfalme mpaka mwaaminifu wa mwisho walimungalia padri Markianos. Hivi na wapadri wale walikuwa ndani ya Altari Takatifu. Tena wapadri wa wili walianza kusuburia na sauti chini:

-Alipata wapi hii mavazi wa zahabu huyu padri Markianos? Huyu hana na makuta hata siku moja mu mfuko yake. Vile alionyesha mbele yetu.. .

-Angalia manguo ya upadri wake ni kuliko muzuri ya mavazi yetu.. . namna gani? Alipata wapi makuta na alinunua hii manguo takatifu?\

Wakati ku mwisho ya Liturgia alitoka inje pa mulango Bora padri Markianos juu ya kukomunika waaminifu, watu wote walishangaa na walisimanga na sauti chini na musagao juu ya mavazi yake, iliijaza na mwangaza. Na kanisa ilijaza kwa ajili ya mwangaza ya manguo yake.

Padri moja mkubwa alimukaribia patriarki na alimuuliza na kisilani:

-Ee Rabi, unapashwa kusema kwa huyu padri Markianos, mwenye ni padri wa bure, ya kama iko kuazo kuvaa hii manguo wa mwangaza na utukufu. Hii mavazi anaweza kuvaa paka mfalme.

Patriarkis alikuwa mtu mwema na alianza kusikitika kwa hii kisilani ya wapadri wakubwa wake. Na huyu kweli aliisha kushangaa kwa hii manguo matukufu ya padri Markianos, lakini alizania alivaa hivi kwa ajili ya Siku Kuu. Ku mwisho alikamata mpango amuulize:

-Hii mavazi ya upadri ulipata wapi, padri Markianos? Hii mavazi anapashw akuvaa paka mfalme. Padri moja anapashwa kuvaa manguo hapana kabisa matukufu kwa sababu itakuwa kuazo mbele ya wamaskini wa ndugu wetu.

Padri Markianos aliangalia na richo moja mbio-mbio pa manguo yake ile alivaa na aliona ya kama ilikuwa ya bure na hakuna ingine ya kufanya Liturgia, na kisha alimuangalia patriarki na alimuuliza:

Ee Rabi, unaniuliza ya mavazi gani? Hii manguo ninavaa mu hii Liturgia weye ulinipatia mbele ya miaka makumi mbili na tano (25) wakati ulinipatia upadirisho na mikono yako!

Patriarkis alishituka. Aliwaza ya kama ilikuwa muchekeleo mbele yake kumulanda mbele ya ma macho yake padri moja wa bure.. .

-Na hii mavazi unavaa? Na alikamata na mikono yake Felonion (nguo wa inje yake) ni nini?

Lakini aliangalia muzuri na ndani ya manguo yake alikuwa mutupu na hii mavazi ilionekana mbele ya watu ya kama ilikuwa na utukufu ilikuwa mavazi ile alikuwa na yo mbele ya miaka mengi na alifanya Liturgia kila siku.

-Ee padri Markianos, nani alitosha manguo yako na sadasa weye uko mutupu? Alimuuliza na musagao patriarkis.

Mt. Markianos alikamata pa mikono yake Evangelio na alienda mbele ya askofu mkubwa yake na alimuwaambia:

-Huu Kitabu alitosha manguo yangu, ee Rabi!

Patriarkis alifurahi sana, alimubatia na alimubusu sawa baba wake wa roho na alimujibu:

-O, kama wapadri wote watakufata, hatuna na lazima ya wahibiri. Mfano yao itakuwa na kuhubiri yao!

## Kulanda ya patriarki

Patriarkis wa muji Aleksandria wa Misiri jina lake Apolianrios (551-569) alikuwa murahimu sana.

Kijana mwanaume moja ya muji Aleksandria aliriti ya wazazi wake uriti moja munene ku chombo na zahabu. Lakini alishindwa kuichunga na kutumina nao muzuri na alipotesha hii uriti yake yote na alikuwa mskini.

Mtakatifu patriarkis alimuona na hii bahati mubaya na alitaka amusaidie, lakini aliogopa ya kama, kama atamupatia huruma, huyu kijana atasikia haya. Lakini kila mara alimuona kutembea huyu kijana na kichwa yake chini na alikuwa na mavazi mabaya, alipata huzuni ya roho na aliwaza namna gani atamusaidia:

Aliita karibu yake musaidizi moja ya patriarkhie yake na alimuwaambia:

-Unaweza kuchunga sauti yangu moja wa siri?

-Ninatumainia, ee Rabi, alimujibu hule ya kama katika saidio ya Mungu, nitafanya nguvu na nitachunga sauti yako.

-Basi, uende na tayarisha kartasi moja. Utaandika ya kama patriarkhie yetu eko na deni moja kwa baba ya kijana, jina lake bwana Makarios, na makuta makumi tano (50) litre ya zahabu. Tayarisha hii kartasi na uniiletee huku.

Musaidizi (mwandishi) yake alimaliza amri ya mt. Apolinarios na alileta hii barua kwake. Kwa sababu baba ya kijana aliisha kufa mbele ya miaka kumi na barua ilikuwa wa sasa, patriarkis alisema kwa mwandishi wake:

-Uende na fuchika hii barua ndani ya ngano yetu, juu ya kubeba ragi ya kimajano na itaonekana sawa barua wa zamani.

Musaidizi yake kisha ma siku madogo alileta hii barua kwa patriarki, kuwa sawa wa zamani.

-Sasa uende kwa hule kijana mskini na umuwaambie: «Unanipatia nini na mimi nitakupatia barua moja?» Utamuomba lakaini hapana makuta mengi. Inenea paka makuta ya zahabu tatu. Utaomba hii makuta kidogo juu hapana yeye kuwaza mubaya.

Basi, musaidizi ya patriarki alienda kwa hule kijana na alimuwaambia:

-Mbele ya ma siku tano nilitafuta kartasi yangu ndani ya nyumba yangu na nilipata hii barua na nilikumbuka ya kama baba wako, bwana Makarios, kwani alikuwa na imani kwa mimi aliniacha hii barua ya wakati kidogo. Lakini alikufa na mimi niliisahabu. Sasa, kisha miaka kumi, niliipata na niliwaza kukupatia. Utanipatia malipo nini?

-Weye unataka nini?

-Inenea kwa mimi makuta tatu wa zahabu. Hii barua yako inaandika ya kama hii makuta unapashwa kubeba ni 3000 makuta wa zahabu!

-Muzuri, nitakupatia. Lakini huyu mtu, mwenye eko na deni kwa baba yangu ni mutu wa kweli ao hapana?

-Ni patriarkis mumoja!

Huyu kijana alibeba hii barua, alienda nyumbani ya patriarki, aliomba kuzungumuza naye, alibusu mukono yake na alimutoa hii barua ya baba yake. Hule aliisoma na alianza kuonekana ya kama alishituka na alikuwa na kisilani.

-Na ulikuwa wapi mpaka sasa? Alimuuliza. Baba yako alikufa mbele ya miaka kumi na ni ndani ya kaburi yake! Misitakuripa hii deni. Toka.

-Ee Rabi, alimujibu hule kijana, hii barua misikukuwa na mimi pa mikono yangu, lakini mutu moja aliniipatia. Aliipata katikati ya ma kartasi yake na aliniipatia.

Patriarkis alionekana ya kama hasiitike. Alikamata hii barua, lakini hule kijana alimufukuza mukusema kwake:

-Nitawaza hii mambo yako.

Kisha juma moja huyu kijana alikuja kwa patriarki. Askofu alimuchabula huyu kijana, kwani alikuja kisha miaka kumi toka lufu ya baba yake na aliomba makuta katika hii barua. Ku

mwisho alionekana patriarkis ya kama anaitika, halafu huyu kijana alimuomba hata kipande ya hii deni alikuwa na patriarkis kwa baba yake.

-Ee Rabi, ninakuwaambia kweli ya kama misina na hata kidogo makuta kununua mukate ya jamaa yangu. Kama munaweza munisaidie.

-Nitakupatia makuta yako yote, lakini ninakuomba hapana kuuzi Kanisa yetu na utaomba makuta ingine.

Huyu kijana alifurahi sana, alimubusu mukono yake na alimusema:

-Nitafanya kila sauti muliniambia. Tena, kama munataka kutosha kipande moja ya hii makuta mutaweza kuikamata.

-Hapan, hapana, alimwaambia mt. Apolinarios.

Mara moja alitosha ya sanduku ya Patriarkie yake na alimupatia makumi tano (50) litre feza wa zahabu. Kijana alifurahi sana na aliondoka.

## Patriarkis murahimu

Mu Kanisa Orthodokse kama tunataka kutafuta mtakatifu moja aliyefanya mu uzima yake yote paka matendo wa huruma alikuwa mt. Yoano Murahimu, askofu mkubwa ya muji Aleksandria ya Msri (+619). Huyu alizaliwa mu Kisanga Kipros. Alikuwa mutajiri sana. kwa ajili alimupenda Mungu, alisaidia sana wa ndugu wamasikini. Na Mungu alimupatia mali kuliko mingi, kwa sababu aliomuona mutumishi wake kusaidia wandugu maskini.

Matendo yake ile alifanya mu inchi yake ilikuwa mengi. Huruma yake ilifika mpaka mu muji kubwa ya Konstantinopoli. Na wakati alikufa askofu mkubwa ya Aleksandria, wakubwa ya Kanisa wote walimuita padri Yoano. Lakini huyu alikataa kupanda pa kiti ya Aleksandria. Mufalme ya Konstantinopoli jina lake Iraklios alimuwamabia nguvu kumutii. Vile alimupenda na taifa muzima. Hivi padri Yoano aliitii na alipanda pa Kiti na alikuwa patriarkis mkubwa ya muji Aleksadria ya Msiri.

Wakati alikuwa patriarkis, aliita karibu yake wapadri yake, wenye walisaidia wamaskini ya muji yao na aliwaambia:

-Mwende mu muji kutafuta na kuhesabu wamaskini wetu wa ngapi ni wakubwa wangu.

Wale walimuangalia na musagao! Hawakusikie aliwaambia nini. Kisha aliwaelejea hivi:

-Ninasema juu ya wale watu wanawaita wamaskini. Hawa weko wakubwa wangu!

Kisha ma siku madogo wapadri wake walimuletea ma jina ya wamaskini 7. 500, wenye walikuwa na lazima kabisa ya kuwasaidia. Hawa watu alifanya nguvu patriarkis mupya kuwasaidia.

Hata mingi alipenda watu wengine na alisahabu maungo yake. Aliishi na yeye na namna umaskini. Hasikuweze kulala na ukimya kama aliwaza ya kama yeye alikula na alilala muzuri na wa ndugu wake hawakuwana hata kipande moja ya mukate. Kwa hivi aliwapatia vitu vyake vyote na makuta yake. Raso yake ilikuwa na yo paka moja na wa zamani na chumba yake ilikuwa karibu wazi.

Wakati moja mukubwa moja ya muji aliona hile fasi ubaya alilala patriarkis. Basi, alinunua nguo ya kitanda moja ya muzuri na munene na alimupatia kufunika mwili yake usiku. Patriarkis aliibeba. Usiku alijifunika na hii nguo ya kitanda upya. Lakini hakuna namna kufunga ma macho yake. Mu akili yake ilikuja mfano na uzima ya wenye maskini, waliishi bila chakula, bila mufuniko usiku na walitetemeka kwa ajili ya baridi. Siku ingine asubui mapema alituma shemasi yake na aliuzisha hii mufuniko. na hii makuta alibeba alinunua ma nguo na alisaidia wamaskini. Lakini, hule mutajiri alimupatia hii mufuniko ya kitanda aliiona mu soko pa mikono ya mtu mwingine. Aliinunua mara ya pili na aliituma mara ingine kwa askofu mkubwa. Lakini mt. Yoano aliiuzisha mara ingine na alisaidia na manguo wa maskini wengine! Hii tendo ilifanyika na mara ingine na ingine na ku mwisho walikutana askofu na hule mutajiri.

Mtakatifu alicheka na alimuuliza mutajiri:

-Tutaangalia nani atachoka katikati yetu mimi ya kwanza, mwenye ninauzisha mufuniko ya kitanda ao weye, unayeinunua mara ingine na unaniirudisha?

Hile saa mutajiri alimujibu:

-Ni hatari kupata mweye homa na baridi na kisha wamaskini wenu watafanya nini?

-Ninakushukura sana juu ya mapendo wa roho ya kweli yako, alimujibu patriarkis, lakini namna gani mimi nitaweza kupumzika pa kitanda na hii mufuniko, kama ninawaza wamaskini wa ngapi pempeni yangu wanateswwa na wanasikia njala? Iko namna baba moja kuishi muzuri na watoto wake watateswa na wataishi bila bitu ya chakula na manguo yao?

Mutajiri alisikia ya kama mt. Yoano alikuwa na haki na hasikuseme kwake sauti ingine.

Wakati moja mt. Yoano walimujulisha ya kama maskini moja alikuwa na sikitiko moja munene, lakini alisikia haya aombe makuta mbele ya watu. Basi, usiku aliendа patriarkis kwa siri nyumbani yake na alimupatia makuta mengi. Huyu maskini alipika magoti mbele yake, alibusu miguu yake na aliliya kwa furaha na shukrani.

-Simama machozi yako, alimujibu askofu mkubwa. Misikusulubiwe tena kwa ajili yako, wala nilimwanga damu yangu kwa ajili yako, sawa vile alifanya Kristu kwa sisi wote!

# UTUME ORTHODOKSE

## Mtakatifu mutawa na watenzi

Mtakatifu mutawa Serapioni alikuwa wa Misri, maskini kamili na murahimu kabisa. Mara mengi walimuona watu kutembea na sanda moja (nguo teketeke ya kitanda) pempeni ya mwili utupu yake, kwa sababu manguo yake yote aliisha kupatia kwa maskini. Joo vile ilibakia kwake na jina ile inatoka ya hii nguo: Sindonios. Mu lugha kigreki sindonio ni hii nguo inaitwa mu kiswahili sanda.

Wakati ingine aliuzishwa sawa mutumwa kwa mutenzi moja (mtu mwenye kucheza) mupagano na makuta makumi mbili. Basi, alinza na mapendo mingi kutumika kwa mkubwa wake na jamaa yake. Alitumika, bila kusimama na bila kuomba saidio hata moja. Aliishi paka na mukate na maji. Mikono yake walitumika, lakini akili yake ilikuwa kwa sala mbele ya Mungu. Mapenzi na uwazo nzuri yake ilikuwa kufundisha imani ya Kristu kwa mkubwa mupagano na jamaa yake. Na aliweza kufanya hii tendo! Aliwakokota ya kwanza na katika mfano ya uzima yake takatifu na kisha katika sheria ya Evangelio.

Wakati mutenzi (mwenye kucheza) alibatizwa pamoja na bibi na watoto wake, waliacha hii kazi yao, kwani haikukuwe katika sheria ya uzima mupya yao na walifata kazi ingine katika amri ya Kristu.

Siku moja mukubwa alimuita Sindonios (mt. Serapioni) na alimusema:

-Ee ndugu ilikuja wakati, na sisi tutakurudisha ufazili yako, hile ulifanya kwa sisi, kwani ulituuhuru toka ngiza ya dini upagano. Beba na weye sasa sawa malipo yako, uhuru yako na uende.

Hile sasa aliwaza mt. Serapion ya kama ilikuja saa amufafanusha mfano na uzima yake. Basi, alimuwaambia ya kama hana mutumwa, lakini na mapenzi yake aliuzishwa juu ya kumuongoza huyu na jamaa yake kwa imani ya Kristu!

Alirudisha hii makuta makumi mbili, mukubwa yake alimupatia na litoka mu inchi ingine. Kule aliuzishwa mu jamaa moja, wenye walifata fundisho ya uwongo ya imani ya Kristu. Na hii namna alileta na hii jamaa ndani ya Kanisa ya Kristu!

## Kuhubiri ku nguzo (colone)

Mtakatifu mutawa Simeoni wa Nguzo (+459) alikuwa toka Azia (Turkie) Kidogo. Ku mwanzo aliishi mu monasteri moja. Halafu tangazo ya utakaso yake ilizambalala mbio- mbio na walikuja kwake watu wingi. Juu ya kuishi bila kumuuzi watu aliwaza kupanda pa nguzo moja urefu, karibu metre 15. Yulu pa nguzo alipita kuliko kipande ya kila muchana na usiku alifanya sala ao metanies (kupika magoti).

Sala yake alisimamisha mara mbili kila siku, juu ya kuhubiri kwa wale waaminifu ao wapagano walikuja chini yake juu ya kusikia ma sauti yake. Alipona wagonjwa, alisaidia watu kusikilizana katikati yao na alifundisha wapagano kufata imnai ukweli.

Watu wingi toka Arabia, Persia, Armenia, Iviria (Georgia) toka Italia, Hispania na Anglia walipata karidu yake nuru ya fundisho ya kweli. Wati wingi wapagano waliacha kila siku mafundisho yao ya shetani na mafumu, ma sanamu na ma dini ya shetani yao na waliamini kwa Kristu.

Tena na wakristu wenye zambi waligeuza mgano na uzima yao na walifata sheria ya Evangelio ya Kristu. Watu wingi, wenye zamani waliishi ndani ya zambi, walifata uzima ya fazila. Wenye zambi walifata uzima ya kiasi. Wanawake wenye zambi walivaa mavazi ya haya na walivaa nguo ya kitubio.

Na hii yote matendo wa ajabu, kwa sababu walisiskia kuhubiri yake, waliona uso wa mwangaza wake na uzima takatifu yake.

Utakaso na tangazo ya uzima yake ilikuwa munene sana na walikuja tena na waskofu. Siku moja alikuwa askofu moja na mt. Simeoni alisema kwa wale waaminifu walikuwa chini yake ya kama katikati yao ni na moja askofu na inapashwa kubeba baraka na kubusu mukono yake. Waaminifu ilikuwa hatari munene kumuuwa huyu askofu kwa sababu walienda mbio karibu yake kuomba baraka yake na askofu alipata mambo ya pumuzi yake. Hivi munene na nguvu ilikuwa utii yao mbele ya sauti ya padri ya roho yao, mt. Simeoni.

Wakati ingine ma kabila wa wili walikuwa karibu kufanya bukomvi katikati yao kwa sababu walisema moja kwa ingine ya kama aliisha kubeba baraka ya padri Simeoni ya mambo moja yao, lakini na mkubwa ya kabila ingine alisemaka na yeye ya kama alibeba baraka ya padri Simeoni. Walikombana katikati yao, kwani walisadiki ya kama baraka ya padri ni kitu kimoja takatifu na kimungu!

Hakuna namna kuhesabu (kubalulula) hawa wakubwa na watawala, wenye walibatizwa ku mikono ya mt. Simeoni na walifata imani orthodokse, Waliomba sala yake na baraka yake juu ya mafalme wao. Wengine walimuomba kusali juu ya kuwasaidia mbele ya mambo magumu yao.

Wakubwa ya inchi wenyezi walipokelea ma shauria yake na walimuita Baba na Mwalimu yao! Na hule mtakatifu aliwashauria katika mapenzi ya Bwana Yesu. Alikamata mpango kwa utukufu ya Mungu na wokovu ya watu. Kabisa alikombana kutengeneza hali ya maskini na aliwasaidia mbele ya tabia mubaya ya wakubwa wao.

HIle wakati maisha ya ma taifa wa Arabia na wa Konstantinopoli ilikuwa nzuri na katika ukimya, mkubwa moja ya kabila moja wa Arabia, jina lake Namani, alimuuliza jemadari ya muji Damasko, jina lake Antiokho:

-Uniseme, huyu mutawa aliyekaa pa nguzo, jina lake Simeoni, ni mungu?

-Hapana, alimujibu hyule, paka ni moja mwaminifu mutumishi ya Mungu.

-Namani alimwaambia: Wakati watu ya kabila yangu walijulishwa juu yake, walianza kumutembelea. Wengine walirudia wakristu na wengine hawakurudie. Walifata uzima utawa wake. Wakubwa ya ma inchi yetu waliogopa juu ya hii mambo na waliniambia kutakaza watu wangu waende kwa hule mutawa, kwa sababu pole-pole wote watafanyika wakristu, watakimbia ya kazi yao na watafata imani Orthodokse. Mimi, alisema mkubwa ya kabila Namani, nilisanyika watu ya kabila yangu na niliwaambia ya kama haipashwe waende mara ingine kwa mutawa Simeoni, kwa sababu watapotesha kila huruma yake na huruma ya jamaa yake. Nitakata na kisu yangu kila mtu ataenda kwa padri Simeoni! .. .

Hii usiku, hile saa nililala ndani ya hema yangu, niliona ku ndoto yangu mwanaume moja wa mwangaza aliyeingia ndani ya hema yangu pamoja na wafwasi wengine tano. Misikumuona mara ingine na nilishituka! Nilitetemaka sana, nilipika magoti mbele yake na nilimusujudu. Aliniaambia: «Nani uko weye na unazibiya taifa ya Mungu akuje kwangu, mutumishi ya Mungu?» Mara moja walinibamba wafwasi wake na walinipiga sana mpaka huyu mutawa mukubwa yao alinitaabu na aliwahamuru kusimama ya kunipiga. Kisha alitosha kisu yake na aliniambia: «Kama utataka kuzibiya hata mtu moja, mwenye anataka aende kwa padri Simeoni, nitakata na kisu yangu kichwa yako». Nililamuka na kutosha jashu mingi. Asubui mapema niliita wanaume wangu na niliwapatia ruhusa, kama wanataka waende kwa padri Simeoni pamoja na ma jamaa yao na kuwa wakristu, bila woga hata kidogo. Nilitaka na mimi kumukuta na kusikia fundisho ya hule mtu ya Mungu, lakini ninaogopa mfalme ya inchi Persia, kwani atawaza ya kama itakuwa haya mbele yake. Lakini pempeni ya mukini ya kabila yangu watu wangu walijenga ma kanisa ya Kristu, pahali wapadri walifanya ibada yoyote. Tena eko huku na askofu moja orthodokse, mwenye anabatiza kila mutu anataka kubatizwa na kufata imani ya Kristu.

Ninyi wote walisikia hii neno ya Namani walishangaa na walimutukuza Mungu juu ya hii neema anataka kwa watumishi wa roho wake.

## Otoleo ya padri moja wa kwanza

Padri Yoano wa Kronstandi ya inchi Rusia (1829-1908), wakati alikuwa mwanafunji ya masomo ya theologia aliacha uwazo yake juu ya kuwa mutume katikati ya wapagano. Lakini alisikia ya kama ni lazima kutumika kabisa katikati ya wakristu wa inchi Rusia.

Mpango yake iliivya ndani ya akili yake kwa kutumika sawa mutume katikati ya wakristu, wakati walimupatia kiti kutumika sawa padri wa kwanza mu kanisa ya mt. Andrea. Juu ya kufata hii uchuguo alimusaidia na hii alama: Aliona mu ndoto yake ya kama alikuwa ndani ya kanisa moja munene. Alitembea ndani ya Altari Takatifu ku mulango wa kaskazini na alitoka inje ku mulango wa kusini.. . Wakati kisha muda ingine alienda mara ya kwanza ndani ya hii kanisa ya mt. Andrea wa muji Kronstandi, mara moja alimifamia. Ilikuwa sawa vile aliiona hii kanisa mu ndoto yake. Alisikia ya kama Bwana Yesu mumoja aliisha kumuwaambia atatumika wapi.

Mu tarehe 11 ya mwaka 1855 ilifanyika upadirisho yake kwa kuwa shemasi na siku ingine alikuwa padri. Alipadirishwa mu muji Petrupolis ku askofu Khristoforos mu kanisa ya Mitume Petro na Paulo.

Padri Yoano ya kwanza alitengeneza mambo ya waaminifu ya parokie yake na kisha alijenga ma nyumba wa wili juu ya kusaidia waaminifu wake. Moja ilikuwa nyumba juu ya kuwapatia kazi kwa waaminifu wake na nyumba ingine ilitumika juu ya kusaidia wamaskni na bintu ya kuachana.

Hii nyumba ya kupatia kazi iliitwa Ergatiki Estia (Nyumba ya watumishi) na ku mwanzo watu walitumika ya kutengeneza mbau na kartasi.

Ndani ya hii ma nyumba ya kazi walitumika mu mwaka 1902, watumishi 7. 281. Ndani ya hii Ergatiki Estia walikuwa na wlaitumika masomo wa kwanza (premier) masomo ya kufunda fundi moja, masomo ya kufatula, masomo na wanawake, nikusema ya kusona, kutengeneza vilato, nyumba ya vitabu na nyumba ya kuuzisha vitabu.

Karibu ya Ergatiki Estia walitumika tena na:

a) Masomo ya mu Juma. Ku mwaka 1897 walifata hii masomo 133 wanaume na 34 wanawake, wingi walikuwa chini ya umri miaka 20.
b) Nyumba ingine murefu, pahali waaminifu walisikia maneno juu ya dini, hadisi na maneno ingine. Mu mwaka 1898 wale watu walifata hii mafundisho walikuwa 264.
c) Nyumba ingine pahali watu waliingia na walisoma sawa deni vitabu ya mbali-mbali.

Nyumba ingine ile ilitumika juu ya kusaidia wamaskini iliitwa Enoriaki Pronia, nikusema Maaguzi wa parokie. Pale walifanya vitabu na kuhubiri ya padri Yoano. tena pale waliishi watoto

wasiyo wazazi na watoto wadogo karibu 50, tena ilikuwa sehemu ingine ya wanawake maskini 22-25 na nyumba ingine ya wale wanaume na wanawake walikuja mu muji Kronstandi na hasikukuwe fasi ingine ya kulala na kula.

Pempeni hii kazi tunapashwa kuongeza na saidio ya wagonjwa na wamaskini. Kwa mfano, mu mwaka 1896 walipita ndani ya obitalo wagonjwa 2721. Hawa wagonjwa walikula ndani na kila siku walikula 400 mpaka 800 watu.

Ya hii kazi yote alikuwa mkubwa padri Yoano, aliyechoka sana, lakini alipata na wakati juu ya kufanya na kupashwa ya kazi yake sawa padri ya roho.

Alisimama kusikia zambi ya wale walitubu. Hii kazi yake alifanya na mapendo mingi. Kila mwaka hesabu ya wale walipenda kungama ilinenepa na padri Yoano kila siku aliungama watu mpaka 200-300 na yulu.

Hile wakati ya kwarezima aliungama tangu kati ya muchana, saa ya pili (2) mpaka saa ya pili kisha kati ya usiku. Alisimama paka kidogo minuta mu saa kumi na moja (11) juu ya kupuzi kidogo pepo safi ao ya kutembea kidogo.

Aliungama mbele ya mulango Bora ya kusimama ndani ya kanisa kubwa ao ma kanisa madogo. Kwa hile saa ya maungamo hasikuikaa hata kidogo!

Kitabu moja na maisha yake inatuelejea ya kama hesabu ya waaminifu wale walienda ya maungamo kila siku ilikuwa 150-300 watu. Lakini hesabu ya waaminifu wale waliungama mu wakati ya Kwarezima ilifika mpaka 6000 watu!

Miaka yake ilipita na huyu aliungama watu kuliko wingi. mara mengi aliungama mpaka asubui! Hile wakati alikamata mpango kungama waaminifu wote pamoja. Nikusema aliwauliza zambi fulani fulani kama walifanya na aliwaambia kutubu. Kisha alisoma pa vichwa vyao sala ya usamehe.

Mbele ya kufanya maungamo mbele ya waaminifu wote, alisoma ma sala ya maungamo, kisha alisema mbele ya watu ma zambi ya wafalme Daudi na Manasi, tena kitubio na usamehe yao ku Mungu, katika sauti ya Agano la Kale na kisha aliwafundisha hivi: «Mungu alitupatia vitu vyote! Kila siku Mungu anaonyesha mapendo yake na anatusaidia. Lakini sisi tunafanya nini? Sisi ma zawadi wake tunaitimia paka ya kufanya zambi zetu. Tunaharabisha Picha ya utukufu yake. Tunachekelea mapendo na wema Wake. Ee wa ndugu wenye zambi, mutubuni.. . » Waaminifu wanasikia zambi na makosa yao na wanaanza kuomboleza na kuliya. Padri anawauliza kama watu walifanya fulani na fulani zambi. Wanamujibu na wanaliya!

Fundisho yake ilikuwa upole. Tena aliwafundisha hivi: Toba ni zawadi ya Mungu. Sisi tunapashwa kukamata mpango kuacha uzima yetu wa zamani, tunapashw akumupenda Mungu na roho yetu muzima. Kisha alianza kuwauliza waaminifu: «Pa hile saa ya sala yenu mulikuwa nas uzaifu?.. . Mulikunywa vinyo mingi na mulilewa?.. . na maulizo ingine.

Kisha ulizo ya zambi ya watu aliisha hivi: «Wa ndugu wangu, mukona zambi mengi. Ma zambi zenu hakuna namna kuihesabu weko wa ngapi». Kisha aliwashauria na sauti yake wa nguvu: «Mutubuni! Mutubuni ya kila zambi na kosa mulifanya mbele ya Mungu! » Hapa waaminifu walianza kuomboleza na kuliya sana. Wengine waaminifu waliliya, wengine waliomboleza, wengine walisema zambi zao mbele ya watu wote. Padri Yoano alisimama ya kushituka na musagao. Midomo yake walisema maombi kwa Mungu. Richo yake ilikuwa kwa mbingu. Alisimama na mikono yake alikuwa nayo pa kilari yake sawa alama ya msalaba. Toka macho yake ilitosha machozi mnene».

Wakati watu wote walifanya ukimya, padri aliwaambia: Mufanya kimya na mimi sasa nitamisoma sala ya usamehe. Munamicheni vichwa vyenu chini. Nitaweka juu yenu epitrakhilio yangu. Nitamibariki na mutabeba toka Bwana Yesu maondoleo ya zambi zenu». Kisha sala ya usamehe alifanya Ibada ya Liturgia Takatifu.

Mu uzima yake padri Yoano, kama hasikusafiri, alifanya Liturgia kila siku. Alianza ibada ya Liturgia asubui mu saa wa sita (6).

Hiule wakati alikuwa padri wa kwanza mu kanisa ya mt. Andrea, kwa sababu alikuwa na muzee alienda mu kanisa na motogari moja hile waliikokota ma punda. Tena alitembea na motogari, kwa sababu waaminifu wingi tangu asubui mapema walimuongojea inje ya nyumba yake juu ya kuomba baraka yake na walimusukuma na walimuzibiya aende mbio mu kanisa.

Tena mu kanisa ilikuwa watu wingine sana na hakua namna kuingia ku mulango wa mbele juu ya watu walimuzibiya. Walifunga fasi moja pale juu ya kuingia mu kanisa bila kumuuzi waaminifu wake.

Lakini na ndani ya Altari takatifu hasikuingie na ukimya. Walikuja watu wingi na walimuwambia ma mambo yao. Na huyu padri aliwaakaribia na mapendo. Mwingine alimubebelesha, mwingine alimupiga na urafiki pa ribeka yake.

Kila siku alibeba toka posta sanduku moja na barua mengi, bile walituma waaminifu ya ma fasi ya mbali-mbali na waliandika ma jina yao na wa ndugu wao juu ya kukumbuka mu Proskomidi padri Yoano.

Tena hile matoleo (Prosforo) walimutuma walifika kila wakati mpaka 6000 vipande kila siku! Lakini padri hakuna namna kutosha Amnos ya kila prosforo, na tena hakuna namna kusoma ma jina mengi ya waaminifu wote.

Juu ya kufanya Fumbo ya Komonyo Takatifu padri Yoano alichoka sana. Mu wakati ya Kwarezima waaminifu wale walitaka kukomunika walifika mpaka 3000 kila siku! Pa Meza Takatifu ya kanisa yake walikuwa Vikombe Vitakatifu kumi na mbili (12)!

Kisha Liturgia, ile alifanya na muchoko mingi, alikwenda nyumbani yake paka ya 15 minute (dakika) na kisha aliondoka kutembelea wamaskini, watumishi wake, wagonjwa na kutengeneza kila mambo yao, pahali waliishi karibu watu 8000.

Magaribi alirudia nyumbani yake juu ya kutengeneza mambo ya kutuma mbarua kwa waaminifu filani na filani. Kisha alipashwa kusoma na kutayareisha kuhubiri yake ya kesho, kuandika ma jambo yote ya hile siku ndani ya kartasi moja.. .

Huyu padri alitumika ndani na katikati ya watu wingi, lakini alikombana kusema na katika akili yake na sala ya Bwana Yesu Kristu! Alifata uzima ya wapadri wakubwa ya Kanisa yetu. Alitumika sawa mutume moja mukubwa ndani ya dunia juu ya wokovu ya watu.

## Sandaka ya p. Kosmas mu kazi ya utume

Mutawa ya monasteri mt. Grigorio ya Mulima Takatifu jina lake padri Kosmas (jina lake ya ubatizo Yoano Aslanidis) eko mutume wa mbili, mwenye anapumzika ndani ya bulongo mu inchi Afrika, kisha padri mutume wa kwanza mu Afrika Khrisostomo Papasarantopulos.

Katika lufu yake, padri mkubwa yake, Igumeni ya hii monasteri arkhim. Georgio Kapsanis alisema hivi: «Mu Kazi Tano, ya tarehe 27 Mwezi ya kwanza ya mwaka 1989, kisha kushuka jua, alishuka ku hii uzima na mtume wa ndugu wa Afrika, padri na mutawa Kosmas juu ya kushariki mu siku isiyo magaribi ya ufalme mbinguni.

Safari yake kutoka muji Lumbumbashi aende mu Kolwezi iliisha kwa rafla kwa ajili ya musiba moja. Mara moja ilianza safari yake kwa milele, mu inchi iliyependa sana!

Fundisho yake alifunda ya kwanza toka wazazi wake, jina yao Dimitrios na Despina. Tangu kipimo kidogo yake alikuwa mwanafunzi ya masomo ya Katikhitiko mu parokie yake. Kisha yeye alikuwa mwalimu ya watoto juu ya fundisho ya Mungu na kisha alikuwa musaidizi ya askofu wa njimbo Florina, jina lake Avgustinos Kantiotis. Tena alifata na fundisho ya kuingia mu masomo ya Theologia.

Ku mwezi ya mnane ya mwaka 1975 na umri yake miaka 33 aliondoka mu Kongo (Zair), pahali na baraka ya padri mtume Alfilokhios Tsukos alijenga ma kanisa 10 ndani ya miezi 14!

Ku mwezi Dekembrie (kumi na mbili) ya mwaka 1977 alikuja mu monasteri yetu, kwa shauria ya wapadri wengine wakubwa juu ya kuwa mutawa na kisha katika baraka yetu arudie mu kazi yake mu Afrika. Kisha mwaka moja alikuwa mutawa na nilimupatia jina ya mt. Kosmas wa Etolos, kama mulinzi na muongozai mu uzima yake.

Kisha alipadirishwa shemasi na padri, ku askofu wa Rodostolou jina lake Khrisostomo, na alirudia mara ingine mu Kongo.

Pale walimuongojea mashindani mengi na mnene.

Majengo ya kanisa, fundishso, kuhubiri, ubatizo ya watu (alibatiza ndani ya miaka kumi 15. 000 waaminifu), tengenezo ya shamba na nyumba ya ma nyama: (Nguruwe, ngombe, ma kalulu, wa kuku, mbuzi na kondoo, ma bata na ingine.. . ) juu ya kusaidia wapadri na waaminifu wake na wagonjwa ya muji Kolwezi.

Nani ataweza kuelejea na stahili michoko yake na mashindani juu ya kuendelesha hii kazi ya utume wake?

Wakati alikuja mara ya mwisho mu monasteri yake, Mwezi ya sita (Yuni) alionekana ya kama aliisha kuchoka sana. Mara moja kila miaka wa wili ao wa tatu alikuja mu Mulima Takatifu juu ya maungamo, sala na kusikia ma shauria ya padri mkubwa yake juu ya kuendelesha kazi yake.

Mu mwaka 1980 alikuwa padri ya roho na kisha arkhimandriti ku askofu ya Afrika katikati jina lake Timotheo.

Padri hasikupende ma cheo ya utukufu. Mafaa yake ilikuwa wokovu ya watu na usabitisho ya Kanisa Orthodokse mu Afrika.

Alifunda watu wa Afrika sala ya Bwana Yesu na aliwaambia ya kama hii sala ni bunduki munene kupingana malozi na mafumu ya Afrika.

Kupasua yake wa kwanza ilikuwa juu ya kuzombelea waaminifu wake kufata ma Ibada ya kanisa yetu na kufunda kuimba katika muzike (Mwimbo) Vizantina (wa Konstantinopoli). Aliisha kujua muzuri na lugha ya wakaa ya Kongo inayeitwa Kiswahili na hii ilimusaidia mu kazi yake sana.

Tena tunapashwa kusema na hii jambo: Alipita ku mikono yake makuta mengi, lakini yeye alikufa maskini, kwani alikuwa mutawa wa kweli.

Alikuja mu monasteri yake mara ya mwisho mu mwaka 1988 na aliandika kitabu moja pahali aliandika namna gani iko namna mtume moja ya Kristu kufanya kazi utume yake bila mambo mengi.

Kwa moja makusanyo ya watawa wetu wote alikuja na padri Kosmas na alitwaambia ya kama hata mtu moja hasitaweze kutoa kazi kizuri na munene mu Afrika, kama atakataa kuacha mwili yake katikati ya wandugu wake wa Afrika.

Mu Siku Kuu kubwa ya Epiphani ya Bwana Yesu Kristu ya mwaka 1989 alibatiza mu muji Kolwezi 350 watu wa Kongo na alifanya na ndoa yao ya uwili 22. Ku mwisho ya kazi p. Kosmas alisema ya kama anatumainia ya kama hii kazi ya ubatizo wake atamusaidia kwa wokovu wake.

Kiliyo yake ilifanyika mu Kolwezi ya Kongo ku mkubwa askofu wake Timotheo, mwenye ni mutumishi asiye kuchoka mu kazi utume ya Kristu. Tena walikuja na Wakubwa ya inchi, kwa sababu walimusifu sawa mtu wa Mungu. Mweshimiwa askofu, Bwana Timotheo na taabu na huzuni ya roho mingi alizika maiti takaitfu yake mu bulonmgo ya hile inchi aliipenda na alitumika mpaka lufu yake.. .

# <u>UVUMILIA</u>

## Mkubwa Isidoros

Bwana Isidoros alikuwa mkubwa wa inchi moja toka muji Aleksandria wa Misri na alikamata mpango kufata uzima utawa mu monasteri moja wa Misri. Padri mkubwa aliyemupokelea, aliona roho na akili yake na alisikia ya kama huyu mtu alikuwa na majivuno mingi na alikuwa mugumu. Basi, alimwaambia juu ya kumusaidia:

-Kama kweli ulikamata mpango kufata msalaba uzito ya Kristu, mbele ya sauti yangu ingine ninakuomba kufanya uvumilia.

-Sawa chuma ni pa mikono ya mwenye kutumika na chuma, vile na mimi, ee padri mtakatifu, ninajitoa kwa utii yako, alimujibu hule kijana.

Padri mkubwa alifurahi na hii jibu yake na alimupatia kwake kazi yake ugumu:

-Ninataka, ee ndugu, kusimama weye inje ya mulango ya monasteri yetu na kwa kila mtu aliyeingia ndani ao anatoka inje utapika magoti yako mbele yake na utamuwaambia: «Omba kwa mimi, ee padri, kwa sababu mimi niko na epilipsie (mazimu)».

Kijana Isidoros alimusikia  kwa padri mkubwa wake, sawa malaika moja alisikia kwa Mungu!

Pa hii tendo ya kupata uvumilia alitumika miaka saba (7) na alifika mu unyenyekevu mingi ya roho yake. Kisha padri mkubwa juu ya kumulipa uvumilia hile alifanya miaka mengi, alikamata mpango kumuhesabu katikati ya kundi ya watawa wengine na tena amupadirisha shemasi na padri.

Lakini hule Isidoros alimuwaambia amuache kuisha uzima yake paka pa hii tendo alifanya mpaka hile siku. Ndani ya hii maombi yake alifuchama kusema ya kama mwisho yake ilikuwa karibu na Mungu atamuita Kwake!

Na vile ilifanyika. Padri mkubwa alimuacha pa hile kazi kusimama inje ya mulango na kisha ma siku kumi aliende kwa Mungu kwa kutembea njia ya utukufu toka njia isiyo na utukufu.

Ma siku saba kisha lufu yake alichukua karibu yake na mutumishi mwenye kuchunga mulango ya monasteri. Aliisha amuwaambie:

-Kama nitapata uwezo mbele ya Mungu, na haraka nitakubeba kwangu na tutakuwa pamoja, bila uchanisho.

Vile Mungu alionyesha ya kama lifurahi kwa hii uvumilia ya mutawa Isidoros.

Mbele ya kuka huyu mushahidi ya roho mkubwa mt. mutawa Yoano wa Sinaitis alimuuliza, alisikia nini, hile wakati alikuwa inje ya mulango na aliweka metania mbele ya kila mtu?

-Ku mwanzo, alimujibu hule, niliwaza ya kama niliuzishwa kwa zambi wangu. Kwa hivi na uchungu na sikitiko na bila mapenzi yangu nilioweka metania (kupika magoti) mbele ya watu, waliyepita mbele yangu. Lakini kisha mwaka moja, misikusikie taabu, lakini niliongolea toka Mungu malipo ua uvumilia yangu. Wakati ilipita na mwaka ingine nilisikia  ndani yangu, ya kama misikukuwe stahili kusimama ndani ya hii monasteri, ao kuona ao kukutana na watawa wengine ao kupewa Mwili na Damu ya Kristu ao kuona mtu mwingine. Hivi nilitupa chini ma macho yangu na kuliko mingi niliachusha sifa ya maungo yangu, niliwaomba kwa watawa na watu waliyepita mbele yangu kuomba kwa Mungu juu ya wokovu wangu.

## Usingi ya jangwa

Ndani ya pango moja (nyumba ya jangwa)mu jangwa ya muji Aleksandria aliishi mutawa moja kijana, bila ndevu. Pango yake ilikuwa mbali ya Skiti (mukini ya watawa) karibu 25 kilometre na aliifamia paka padri mt. Daniel na mwanafunzi wake.

Padri Daniel aliisha kumwaambia kwa mtoto wa roho yake aende mara moja kila juma mu jangwa juu ya kupeleka kwa hule mutawa wa jangwa chakula na maji. Hii bintu ataweka kila mara inje ya pango yake na atatoka bila kusuburia na ye.

-Kama utapata, alimwaambia, matafari moja iliyoandikwa pa mulango ya pango yake utaniiletea.

Hii kazi alifanya mtoto wa roho yake miaka makumi mbili na mnane (28)!

Basi, siku moja alipata kitafari moja pahali iliandikwa: «Leta bitu ya kuchibula kaburi ya kumuzika mtoto yako, Anastasios». Wakati ndugu alimupatia kwa padri ya roho yake hii tangazo, hule aliliya sana na alisema:

-Ole mu jangwa! Leo jangwa inapotea usingi moja munene.. .

Walibeba Kikombe Takatifu na bitu ya kuchibula kaburi na waliondoka mu jangwa.

Wakati walifika, walipata mutawa wa jangwa, jina lake Anastasios, aliyeteswa pa kitanda chini ya kivukutu mingi. Padri Daniel alipika magoti mbele yake na alimusema:

-Weye uko mwenye heri, kwa sababu ulitumika mu uzima yako katika sheria ya Mungu na ulizarau ufalme ya hii dunia.. . Fanya sala na kwa sisi.

-Mimi nikona lazima ya ma sala yako, alimujibu hule.

Kisha aliikaa chini, alifungula mikono yake, alimbatia kichwa ya padri mt. Daniel, aliibusu na alisema:

-Mungu aliyeniongoza pa hii fasi, ninatakia kubariki na miaka yako, sawa vile alibariki Abrahamu!

Mt. padri Daniel alipokelea baraka, alilamuka na alikaribisha mtoto wa roho yake juu ya kumubariki, mukusema:

-Bariki na mtoto wangu.

Huyu mutawa wa jangwa alimumbatia na huyu mtoto na alimuomba kwa Mungu hivi:

-Ee Mungu wangu, weye unayejua mwendo wa ngapi alifanya huyu ndugu afike mpaka huku kwa Jina Lako, umupatia uwezo wa roho ya wapadri wake, sawa vile ulimupatia na kwa Nabii Eliseo, uwezo ya roho ya Nabii Ilie.

Kisha alimuangalia padri Daniel na alimwaambia:

-Kwa jina ya Mungu musinitosha hii manguo mimi sasa ninavaa, lakini sawa vile niko vile, mutanituma kwa Bwana Yesu. Na tena haipashwa hata mtu mwingine kujua matendo ya uzima yangu na kila tendo munaona huku.. .

Kisha alipewa Mwili na Damu ya Kristu, aliomba kuomba kwa Mungu juu ya wokovu wake, alidanya alama ya Msalaba na alisema:

-Ee Bwana, pa mikono Yako, ninatoa roho yangu.

Uso yake ilijaza na mwangaza na mara moja alilala musingizi wa milele! .. .

Padri Daniel pamoja na mtoto wake walianza kuliya. Kisha walikamata nguvu na walianza kuchibula kaburi yake, mbele ya pango (chumba) yake. Kisha mt. Daniel alitosha ngochi yake na alisema kwa ndugu wake:

-Umuvaa na hii ngochi, maiti yake yulu ya manguo yake.

Huyu mufu alivaa kanzo moja iliyepasuka sana na mupila moja ndani yake. Wakati alimuvaa mtoto wa roho yake, alisopoka muzuri kilari yake na aliona ya kama huyu mtu alikuwa mwanamuke! .. . Lakini hasikusema sauti moja.

Wakati iliisha maziko, waliomba na waliondoka mu mukini (skiti) yao.

Kwa kutembea pa njia mtoto alisema kwa padri ya roho yake:

-Ee Muzee, huyu mutawa wa jangwa sisi tulimuzika alikuwa mwanamuke!

-Ndivyo, alikuwa mwanamuke na aliitwa Anastasia. Unataka kujua mambo ya uzima yake?

-Ndivyo, ninataka.

-Huyu mama alikuwa mama mkubwa wa kwanza mu nyumba ya mfalme Yustinianos ya Konstantinopoli (527-567). Wazazi wake walikuwa waaminifu na walimukomesha katika fundisho na woga ya Mungu. Ma fazila yake na tabia yake walimufurahisha mufalme na alipenda kumubeba nyumbani wake! Lakini bibi ya mfalme, jina lake Theodora, alimuchukia na alimufukuza mu muji Aleksandria. Huyu mama Anastasia kwa ajili ya chuki ya bibi ya mfalme, alikataa mafuraha ya hii dunia. Alijitoa kwa mapendo ya Mufalme wa mbinguni na alijenga monasteri moja. Lakini, wakati alisikia ya kama alikufa Theodora na mfalme Yustianianos alimutafuta ma fasi yote ya njimbo yake, huyu mama Anastasia alitoka usiku ku muji Aleksandria na alikuja mu mukini (Skiti) yetu. Aliniomba kumufuchama na nimupatie chumba moja kuiingia. Basi, nilimuvaa na manguo wa wanaume na nilimwaambia hii pango kuishi pale. Na huyu aliishi mpaka mwisho ya uzima yake, miaka makumi mbili na mnane (28)! Hata mtu mwingine hasikumufamie mpaka sasa, paka weye. Mfalme alituma wakubwa wake wingi juu ya kumutafuta.. . Lakini hata moja hasikuweze kumupata. Alimutafuta hapana paka mfalme, lakini na askofu mkubwa ya Aleksandria na wakubwa ya hii muji wote!

Hule, lakini alimufurahisha Mungu, kwani aliishi ndani ya unyamasha na unyenyekevu. Ninatakia na sisi kustahili kutembea hii njia umoja wake juu ya kupata rehema hile siku ya uhukumu pamoja naye na pamoja na watakatifu Wapadri wetu. Amina.

## Mfalme mwanamuke mushahidi mkubwa

Mfalme mwanamuke wa inchi Georgia Katevan (+1624) alimubamba mfalme wa inchi Persia, jina lake Ambasi, na alimufunga mu buloko ya miaka kumi (10)!

Ndani ya hii wakati alivumilia mateso mewngi, matusi, machekeleo na matendo mabaya ya wakubwa wa Persia. Huyu mama alikataa sauti ya mfalme wa Persia juu ya kumuondowa na amufanyishia mfalme bibi yake ya inchi yake! Tena alikataa ma sauti ya watu wengine, wenye walimuwaambia kusema paka sautri moja-matusi kupigana ya Yesu Kristu na ataokolewa. Alibakia pamoja na Bwana-Arusi wake Yesu Kristu mpaka saa yake wa mwisho. Alihubiri imani yake Orthodokse na alimwanga damu yake kwa mapendo Yake, sawa tutaangalia hapa sasa.

Ndani ya buloko alitesa mwili yake na kifungo, sala, sala ya usiku, alilala vhini pa mbau, alipika magoti. Na hivi alitayarisha nafsi yake kwa kufata mateso ya mbali-mbali kwa jina ya Kristu.

Kweli, siku moja alikuja mutu moja aliyemutuma mfalme wa Persia na alimuwaambia:

-Mkubwa wangu anakuhamuru: Ao utakataa Kristu na utakuwa musulmani ao utakufa na mateso wa matata.

Na hule mama mweye heri, kwani alijua ya kama hii mateso ni ya bure mbele ya hile utukufu itamufata mu uzima wa milele, alimujibu na ma sauti ya Mtume Paulo:

-Haitaweze hata kintu kimoja ya kunichanisha ya mapendo ya Kristu! Wala taabu, wala sikitiko, wala ufukuzo, wala kifungo ya chakula, wala utupu, wala hatari wala lufu wa mateso mengi.

-Penda uzima yako, alimujibu mtu ya mfalme. Kumbuka kizazi ukubwa wako na kataa Kristu, kwa sababu mfalme alihamuru kukata mwili yako.

Hule mama alifanya alama ya Msalaba na alimujibu:

-Hakuna namna mimi kukataa imani yangu. Ninapenda kufa kwa ajili ya imani ya Kristu wangu.

Kisha huyu mama aliomba saa kidogo uhuru na mkubwa alimuacha wa pekee. Hule mama kisha alipika magoti na alianza kuomba na machozi mengi:

-Ee Mungu Mwenyezi, weye unayetenga milima na unatetemeka masingi ya ulimwengu, unisaidia hii saa.. .  Fungula, kwa mimi mutumishi wako, mulango ya ufalme wa mbingu na unihesabu mu kiviringo ya Watakatifu Washahidi wako. Ee Bwana, ma zambi yangu hakuna namna kuihesabu! Hasikufanye zambi mingi mtu mwingine sawa mimi. Samehe ma zambi zangu.. .  Hile saa nafsi yangu itapanda kufika karibu ya Kiti yako, tuma malaika Wako niokoe toka ma kundi mabaya ya ma shetani.. .  ee Bwana uniokoe.. .

Wakati aliisha sala yake takatifu, alipewa Mwili na Damu ya Kristu na alikamata nguvu juu ya kufata mateso ya Kristu.

-Ee Kristu wangu, alipaza sauti, usiniache kukataa mimi mutumishi wako Jina na imani yako. Usiniache kuanguka pa mikono ya shetani.

Kisha alifanya mara ingine alama ya Msalaba na alisema bila woga kwa wa askari:

-Mufanye  kila tendo munataka. Niko tayari ya kila kitu.

Wale wa askari walimufunika pempeni yake na walimukokota mu  kiwanja ya muji yao. Waliwaakisha moto na walitupa ndani bintu ya chuma. Hii ilikuwa bintu ya mateso yake. Ono ilileta woga. Jemadari ya muji hasikuweze kuvumilia na aliondoka mukutaabu.

Wa askari walimubamba na haraka, walimutosha manguo yake yote, walimutundika pa muti moja na walifunga mikono yake katika alama ya msalaba. Kisha walitosha ku moto chuma moja. Mbele ya hii ono wa ajabu, mushahidi mama alipaza sauti kusema:

-Kwa jina ya Baba, na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu!

wa askari wakali walianza kumukata maziwa wake na hii chuma wa moto. Na hii chuma wa moto walikata nyama ya mikono yake

Kisha walichukua ku moto sahani ya kukalanga na walilungua na hile mabeka yake na mwili yake karibu muzima. Wakati waligusa ma sahani wa moto pa mwili yake, ilitoka simoko mingi. Kisha walimushusha ku muti na walimularisha ma kitanda moja, juu yake waliweka misumari wa moto. Kisha walibeba posholo wa chuma ile ilijaza na moto na walitupa pa mwili yake misumari na bintu ingine kuijaza na moto. Misumari wa moto waliingia ndani ya mwili yake na mwili yake yote inafanya kilonda moja muzima, lakini damu ilitoka sawa mutoni. Umivu yake hakuna namna kuivumilia.

Wa askari, lakini waliendelea kazi kibaya yao. Walitosha misumari ingine ku moto na walianza kupasula mwili yake sawa kisu. Pa hile mistari ilipita misumari walilugusha mwili yake na fasi ya mwili yake ilijaza na vilonda na damu!

Mtakatifu alitesa sana, lakini alikaribia kutoa nafsi yake kwa mikono ya Mungu. Mateso yake bado kuisha huku. Wenye kumupiga walitosha ku moto monyororo moja. Hii monyororo waliifunga pempeni ya kifuno yake. Umivu ilikuwa munene, lakini wa askari wanafanya mbio juu ya kuisha kazi yao. Kisha walikamata posholo moja wa moto na waliiweka pa uso na singo yake. Simoko mingi ilitoka ku kinywa, pua na masikio yake. Sasa anaanza kupuzi ya mwisho, lakini wa askari walimaliza na mateso yao wa mwisho.

Walikamata sahani moja wa chuma, waliiweka ndani ya moto na waliongojea kubeba ragi nyekunda. Kisha waliikaribisha hii sahani mu Mushahidi mkubwa. Mwenye heri Mushahidi, mwili yake iliisha kulungua ma fasi yake yote, alisema sauti yake ya mwisho:

-Kwa jina ya Baba, na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu.

Walimuvaa pa kichwa yake hii sahani wa moto na ilifunika kichwa yake yote mpaka mabeka yake. Hii dakika simoko ilitoka kwa ajili ya ma nywele wake na Mt. Katavani alitoa nafsi yake kwa Yesu Kristu mu tarehe 13 Mwezi ya Tisa (Septembrie) ya mwaka 1624. Hivi alichukua na alivaa taji ya milele!

Vile aliisha uzima yake mfalme mwanamuke katevani, Mushahidi mkubwa na alifika mu kikavu wa mbingu, pahali anaomba kwa Mungu juu ya watoto wa inchi yake Georgia.

Wakati huyu Mushahidi alitoa nafsi yake kwa Kristu, mbingu alionyesha ushindani wake mbele ya shetani na hii namna wa ajabu: Ma nguzo (Colone) tatu walianguka pa mwili yake na waliiangaza, na watu wingi walitembea mbio pa hile fasi ya lufu yake katika mateso. Mfalme wa Persia Ambasi alihamuru kutupa maiti yake ndani ya mtoni moja. Lakini nuru wa mbingu ilimufata mwili yake. Usiku kabisa waaminifu wengine walitosha toka hile fasi waliitupa mwili takatifu wake na waliiweka ndani ya sanduku moja na walimuzika na heshima na sala.

## Mutawa mwanamuke asiye kuchoka

Mtakatifu mutawa wa inchi Pantani alizaliwa mu mwaka 1819 mu njimbo Kharkofi ya Rusia. Jina ya ubatizo zake ilikuwa Anna. Tangu ujana wake alipenda sana uzima utawa na wa jangwa. Lakini aliogopa kufata mapenzi wake na alikimbilia mu sala mbele ya Mzazi-Mungu. Alimuoba amuwaambie kama matakio yake inamufurahi Kristu. Jimu yake ilikuwa hii ndoto yake:

Aliona mu ndoto yake ya kama alichunga pa mikono wake Picha (Ikone) moja ya Mzazi-Mungu. Toka hii Picha ilitoka sauti moja utamu na upole. Tena mara moja alisikia na kivukutu wa furaha. Hii kivukutu ilipita ndani yake, lakini iligeuza na haikukuwe wa furaha, lakini uchungu.

Ku hii ndoto alisikia ya kama matakio yake ilikuwa katika mapenzi ya Mungu, lakini ushindani na maisha yake ku mwanzo itakuwa wa furaha, lakini kisha itageuza na itakuwa mugumu na matata!

Kisha wakati kidogo alikuta binti moja, aliyekuwa na huyu hii matakio umoja, jina lake Maria. Wote wa wili waliondoka mu fasi wa kaskazini, mu njimbo ya Olonechi, pahali waliishi uzima moja wa jangwa na walitii moja kwa mwingine karibu ya mukini ya Maria.

Ku mwisho walimukuta na padri muzee moja, jina lake Ignatio, toka Nyumba wa jangwa ya mt. Nikiforos mu Kiziwa Vaza, na huyu alikuwa muyomba ya binti Maria. Huyuy mtakatifu padri ku mwanzo aliwashauria wa wili waishi wa pekee mu jangwa. Kisha wakati kidogo, aliangalia usabitisho ya tabia na uzima utawa wao na aliwapatia nyumba moja mu njimbo ya monasteri yake.

Kisha lufu yake watawa waliwafukuza ya hii nyumba. Vile watawa wanawake walianza kuchibula bulongo juu ya kutengeneza nyumba yao mupya. Walikata miti, wlaipeleka bintu ya kazi ya ma fasi wa mbali. Hii kazi yao ilikuwa ugumu kwani na hawa walikuwa ma binti ya teketeke. Waliendelesha kazi yao katika sala na kutosha machozi.

Ku mwisho walijenga chumba kimoja na mbau na mayani ya kukauka, lakini nvula ilipita ndanbi. Kisha, wale wanawake kila siku walitosha maji inje ya chumba yao. Pa fasi ya mulango, kwa sababu hakuna mbau muzuri ya kufunga mulango, waliweka ma nguo yao!

Kisha walijenga tanuru moja juu ya kuchoma mukate. Wakati waliiwakisha tanuru mara ya kwanza, ililungua na iliharabika. Chakula yao kila siku ilikuwa paka buyoka, lakini na ingine buyoka walikuwa na bilulu.

Ilipita wakati kidogo na mutu wa mukini moja aliwaletea shoka, kisu na bunga. Aliwafanyishi mulango wa mbau moja. Simoko na baridi ilijaza chumba yao udongo. Ndani yake waliishi mwaka moja wa baridi mukufanya sala kwa Mungu na muvumilia magumu wote.

Kisha wakati kidogo pa fasi ya mufuniko, pahali waliisha kuweka mayani na mbau. Huyu mutu wa mukini aliweka mufuniko moja nzuri wa mbau. Kisha ugumu wao ilikuwa hii: Miti hile ilikuwa pa mufuniko na pempeni ya nyumba yao, kwa ajili ya baridi, walitosha mayani mapya wa sasa na kisha mwaka moja nyumba yao, ilianguka chini muzima! .. .

Wale watawa wanawake wa jangwa walivumilia hii mateso, bila kupotesha kitumaini yao. Roho yao ilipenda kabisa uzima ukimya mu jangwa na walikuwa tayari kuvumilia kila mateso. Ndani ya hii ukimya usiku walipata ndani ya roho Bwana Arusi Yesu Kristu!

Wakati moja Anastasia aliemnda kulokota buyoka. Alijipotea mu pori na alilala usiku chini ya miti marefu, lakini aliteswa kwa ajili ya pepo wa baridi na nvula!

Mu fasi waliishi walikuwa na ma nyoka mengi wa sumo. Walitoka toka muti moja, iliyekuwa karibu ya nyumba yao. Siku moja Anastasia alirudia ya kulokota buyoka, alipata nyoka moja munene pa hile fasi alilala!

Wakati ingine alienda kubeba mukate ku mufuko yao, na ndani alipata nyoka moja munene.

Wakati ingine alienda kulokota buyoka; alipata fasi moja na aliwaza kufanya pale shamba yake. Alileta mayani ya kukauka juu ya kulungua mayani ingine kusafisha hii fasi. Muda, lakini ilikuwa kukauka na moto ilikuwa munene ndani ya pori! Anastasia, hile saa alianguka chini na alimuomba Mungu amusaidie. Mara moja ilionekana mawingu moja mbinguni na ilileta nvula na moto ilizimishwa.

Wakati ingine wanyanganyi wa wili waliwabamba, waliwafunga mikono yao mukongo na waliwaomba makuta. Kwani hawakupate makuta, waliiba hile buyoka kidogo walipata, bunga kidogo na waliona ya kama hawa watawa wanawake walikuwa maskini sana. Kwa hivi, waliwafungula, waliomba hurumia na walikimbia.

Mateso ya Anastasia hawakuishi mpaka sasa. Magumu ya maisha yake hapana kumuepuka ya hile jangwa, lakini adui ya kizazi ubinadamu, ni kusema shetani, alianza sasa kumuuzi na uzaifu, ma sauti mabaya, woga na ingine.. . Lakini Bwana Yesu hasikuwaache. Aliwasaidia na maono wa ajabu.

Wakati moja aliona ndoto moja. Aliona shetani moja, aliyeandika ndani ya kitabu moja ya kama atabomoa monasteri yote. Anastasia alianza kusema ya kama Monasteri inafanya sala juu ya kusaidia dunia muzima. Hile saa shetani alianguka yulu yake.

-Tena watawa wanaomba juu ya mweye, alisema mutawa Anastasia kwa shetani.

Shetani alisirika, lakini nguvu moja isiyoonekana ilimuokoa ku kisilani ya shetani.

Tena aliona na maono ingine ya wanawake wabikira, wenye walikamata mishumaa na waliimba wimbo ya utamu sana. Aliungana na sauti yake na aliimba pamoja nao mpaka alilamuka na alisikia furaha mingi.

Mateso na ma taabu yake yote alivumilia na uvumilia munene. Vile alikomea katika ma fazila ya Kristu na watu wengine walikuja kwake kufata mafundisho yake.

Mtakatifu askofu Ignatio Mbriachaninofi alimutafuta na alimukuta. Aliona aliisha wapi na namna gani aliishi. Hasikuweze kusadiki ya kama mwanamuke moja aliishi na ugumu mingi kwa ajili ya Bwana Arusi wa mbingu na alitosha machozi.. .

Pole-pole karibu yake walikuja na wengine wanawake na walifanya kundi moja na watawa na walijenga moja Monasteri.

Huyu mutawa Anastasia alilala katika Kristu (alikufa) mu tarehe 11 Yuni (Mwezi ya sita) ya mwaka 1901 na mpaka mwisho yake aliishi ndani ya tundu munene ya muti moja.

# KUTOSHA MACHOZI

## Shukrani ya wenye wanakuwa wakali

Hile wakati mtakatifu mutawa Savvas aliishi mu jangwa ya Ruva ya inchi Palestini, alikutana na wa inne musulmani, waliyekwa na njaa na waliisha kulekea.

Aliwahuruma na aliwaambia kuikaa karibu yake. Alibeba mufuko yake na alitosha inje bile bintu ilikuwa ndani. Lakini haikukuwe kintu kimoja ndani, paka mizizi na roho ya simbala ya mumbichi. Wale wa misulmani walikamata na walikula na waliziba. Kisha waliangalia pango ya hule mutawa ilikuwa fasi wapi.

Kisha ma siku madogo walikuja na walimuletea mukate, maziba ya kulamata na matunda. Mtakatifu Savvas alishituka kwa hii shukrani walimuonyesha na alitosha machozi na alisema:

-Ole wangu, nafsi yangu.. . Hawa watu wanyanganyi walikuja mbio kabisa juu ya kunionyesha shukrani yao kwa sababu mimi nilifungula mufuko yangu mbele yao ya kupata chakula ya kula! Nitafanya nini mimi mutu mupotevu, kwa sababu kila siku Mungu ananipatia zawadi wake wote, lakini ninapita maisha yangu na uzaifu kubwa na uvivu, bila kumushukuru kwa hii zawadi wake?

Ya wakati mingi alikumbuka hii tendo ya wenye watu wakali na alitosha machozi kwa shukrani wao.

Watawa wa jangwa wa wili waliishi pamoja, walisoma vitabu na ma Ibada yao kila siku. Mutawa moja alikuwa na zawadi ya kutosha machozi kila siku! Kwa ajili ya hii zawadi, aliacha kitabu kuanguka chini ku mikono yake.

-Lakini unawaza nini na unaria hivi na umivu mingi, wakati unafanya sala yako? Alimuuliza mutawa mwingine.

-Ninazania, ndugu wangu, ya kama hii saa ninasimama mbele ya Kiti ya hukumu ya Kristu na Yeye atanihukumu. Na kwa sababu, misina na sauti ya kumujibu, kwa ajili ya zambi zangu zote, kinywa yangu inafunga kwa woga na ninapotea maendeleo ya somo ya hii kitabu. Lakini, kama ninakuuzi, kila moja atasoma kitabu na ibada yake mu fasi ya kuachana.

-Hapana, ndugu wangu, alisema mutawa mwingine, usiniuzi. Lakini unanipatia faida ya roho munene. Kwa sababu mimi, kwani misi na zawadi ya machozi yako, mukuona weye ninataabu juu ya ugumu ya roho yangu na ninafanya nguvu kukumbuka na mimi zambi zangu.

## Mwenye desturi mutawa Gerontios

Padri mkubwa ya Monasteri ya mt. Dionisios ya Mulima Takatifu, jina lake padri Gabriel, wakati alikuwa mutawa kijana, ku mwaka 1911, alisafiri na alienda mu Monasterei ya mt. Panteleimon, pahali wanaishi watawa wa inchi Rusia, juu ya kuwa mu Ibada ya Kanuni kubwa ya Mt. Andrea wa Kreta (Mu Kazi Inne ya Juma wa tano ya Kwarezima). Mwenye desturi mu Monasteri hii alikuwa Mutawa Gerontios, walimufamia kwa ajili ya ma fazila yake. Padri mkubwa Gabrieli ya monasteri ya mt. Dionisios aliandika hivi, kisha miaka filani:

«Ilianza Ibada kitakatifu! Ilikuwa kimya na tengenezo muzuri ndani ya kanisa.

Kisha somo ya zaburi ya Eksapsalmos na wimbo ya Utatu Mtakatifu padri Gerontios alianza kuomba wimbo wa kwanza ya Kanuni ya mt. Andrea: «Nitanzia wapi, wakati ninapashwa kulilia matendo yote ya uzima wangu? Kwa kipindi gani yafaa kuimbia kiliyo changu? Lakini mu wema wako, ee Kristu, uniupe maondoleo ya zambi zangu». Roho yangu ilishangilia kwa hii wimbo na sauti utamu yake. Mara moja nilimuona kupaguza machozi zake, hile saa aliimba hii wimbo ya kutubu. Ku mwisho ya wimbo wa kwanza, hata mingi ilijaza roho yake na toba, na, wakati aliimba wimbo ya Mzazi-Mungu, alinyanyua mikono yake mbele ya Picha (Ikone) ya Mzazi-Mungu na heshima mingi na machozi mingi aliimba hii wimbo: «Ee Mzazi-Mungu, matumaini na ulinzi wa hawa wanaokuimba, punguza uzito, mzigo wa zambi zangu; Bibi mtakatifu kamili, unipokeye mwenyi kugeuzwa kwa toba».

Katikati ya Kanuni ya Mt. Andrea inafanyika somo ya Uzima ya mt. Mutawa mwanamuke Maria wa Misri.

Mu Monasteri ya Mulima Takatifu hii Uzima ya mt. Maria anasoma padri mkubwa ya kila monasteri. Mu Monasteri ya mt. Panteleimon, kwa sababu padri mkubwa eko toka inchi wa Rusia na asijue lugha kigreki, alisoma hii kitabu na uzima ya mt. Maria, padri muzee Gerontios. Huyu alikuwa wa kwanza katikati ya watawa waliyekuwa toka Grekia. Alianza kusoma hii kitabu, lakini pole-pole roho yake ilijaza na moto ya kitubio. Alisimama kwa sababu machozi yake hakuna namna kumuacha kuendelesha somo. Wakati alifika pa hile fasi walisuburia mt. Maria pamoja na padri Zosimas, muzee Gerontios hakuna namna kusimamisha machozi yake. Hii mambo waliifata na watawa wengine ndani ya Kanisa na walianza kuliya. Kisha mara moja alikuja kwake padri mkubwa ya monasteri aliye kuwa tuka inchi Rusia, alimukamata na mukono na alumupeleka mu kiti yake.. .

Kisha wakati ingine nilijulishwa ya kama huyu muzee mutawa Gerontios aliikaa pa fasi wa kwanza ya kanisa. Na mukono moja alichunga komboskini na alifanya sala ya Kristu na mukono ingine yake alichunga kitambaa na alipaguza machozi yake. Kama kitambaa yake ilijaza na machozi alienda mu bahari na aliisafisha.

# <u>T O B A</u>

## Utakaso ya mwenye zambi mwanamuke

Hile wakati uzima ya watawa ilikuwa munerne mu jangwa wa Misri, aliishi mu muji Aleksandria binti moja yatima, aliyeitwa Taisia. Wakati walikufa wazazi wake wazuri, walimupatia sawa uriti ya kwanza heshima na mapendo mbele ya wamaskini na wageni na kisha nyumba moja munene na makuta mengi.

Huyu binti kwa ajili ya heshima mingi mbele ya watawa wa jangwa aliwapokelea nyumbani yake, aliwapatia chakula na nyumba yake ilikuwa sawa hoteli. waakti walikwenda mu muji Aleksandria kuuzisha bintu yao na kununua bintu ya chakula yao, aliwapokelea na mapendo mingi huyu binti Taisia. Mwaka kwa mwaka mali yake ilikuja ku mwisho na huyu alikuwa sasa

maskini. Hile waakti wlaiingia katikati watu wabaya na wenye zambi na walimukokota mu zambi ya usharati na uzini. Ksiah binti muzuri Taisia alikuwa moja ndumba mkubwa!

Wakati Watawa wa jangwa walisikia ya kama huyu Binti alianguka mu zambi ya mwili, walikamata mpango kwa kumusaidia na kila namna juu ya kumuokoa.

-HUyu binti, wakati alikuwa na mali yake, alituonyesha mapendo na saidio yake, walisuburia katikati yao watawa. Lakini sasa, kwani nafsi yake ilipata hatari ya wokovu, sisi tunapashwa kumusaidia.

Basi, walipatia hii kazi nguvu kwa mutawa Yoano wa Kolovos. Yeye aliwaza ya kama hasitaweze kufanya kintu. Ku mwisho, juu ya kufanya utii mbele ya Watawa wakubwa wake, alikamata mpangu ashuke mu muji na atakuja nyumbani ya huyu mwenye zambi mwanamuke. Alimuomba kwa hule binti alikuwa pa mulango sawa zamu juu ya kumupeleka kwa mama mkubwa wake.

-Toka ya huku, ee mutawa mubaya, alimufokea huyu binti na kisilani. Mulikula mweye uriti ya mama mkubwa yangu na sasa hamusimame kumuuzi.

Ava Yoano, hasikupoteshe kitumaini yake. Alimwaambia mara ingine juu ya kuona mama Taisia. Kwani padri alimuomba bila kutoka, huyu zamu, alienda kumujulisha mkubwa mama wake.

-Hawa watawa, alisema mama Taisia, wanalopola mu bahari Nyekundu na wanapata vitu vizuri ya bahari. Umuita kufika mbele yangu.

mama Taisia aliona uso yake pa rikalashi. Alitengeneza ma nywele yake, ma nguo yake, alimimiya na manukato mwili yake juu ya kupokelea mutawa moja muzee.

Muzee Yoano aliingia mu chumba yake na alisimama mbele yake na taabu. Alimuangalia saa ya kuenea na wema bila kusuburia naye. Kisha alimusema na sauti wa chini:

-Ee Taisia, ni gani kosa ya Bwana Yesu Kristu na unamuzarau sasa weye mingi na bila wema?

Alisimama. Hasikuweze kuendelesha sauti zake. Alianza kuliya. Machozi ilianguka toka macho yake. Huyu mama alisikia haya. Aliacha tabia mubaya yake na alimuuliza na sikitiko:

-Juu ya nini, ee padri, unaliya?

-Binti wangu, namna gani minisitaliya, kama ninaona shetani na anacheza pa uso yako?

Binti alishituka. Tetemeko ilipita mwili yake muzima.

-Ee Muzee, sasa ulikuja wakati ilipita.. . Ndani yangu kila kintu ilianguka. Nilijaza roho na mwili yangu ndani ya zambi ya uzini (zambi ya mwili).

Padri muzee alimusikia na mikono yake ya kufunga pa kilari yake sawa alama ya msalaba. Ndani yake aliomba kwa Mungu juu ya toba wake.

-Iko tena kitumaini ya wokovu kwa mimi, ee Muzee: Alimuwaambia na sauti chini binti Taisia.

-Ndivyo, iko binti wangu, alimujibu na furaha padri Yoano. Kitubio inaongoza mu wokovu.

Muujiza iliisha kufanyika.

Taisia alianguka chini mbele yake, alitosha machozi na alimuomba:

-Unitoshe ya huku mbio, ee padri wangu. Unionyeshe njia ya wokovu.

-Unifate.

Bila sauti ingine huyu binti alilamuka na alimufata muzee Yoano. Hule alishangaa, kwa sababu Taisia hasikuangalia mukongo mambo ya nyumba na wasaidizi wake. Wote wa wili walichukua njia mu jangwa. Walikuwa na njia murefu ya kutembea na hile usiku walimama ndani ya jangwa. Muzee Yoano alikata mayani ya kukauka na alilala juu yao binti Taisia.

-Weye pumzika huku mpaka asubui na mimi nitaenda fasi ingine kidogo mbali.

Padri alifanya sala yake na alilala pa bulongo kupumzika kidogo na chini ya kichwa yake aliweka njiwe (mwamba) moja. Alipumzika kidogo na usiku alilamuka kuendelesha sala yake.

Hile saa ilionekana mbele ya ma macho yake jambo moja wa ajabu. Kutoka hile fasi aliisha kumuacha binti ya kupumzika ilianza njia moja wa nuru murefu iliyefika mbinguni! Malaika na mabawa na haraka walipeleka nafsi ya Taisia mbinguni, pa Kiti ya Mungu! Mt. Yoano alisimama saa mingi na aliangalia hii jambo wa ajabu.

Kisha alienda kumukuta Taisia. Alimuita juu ya kumulamusha. Hasikubebe jibu. Alimutenga kidogo. Hasikusikie kintu. Nafsi yake iliisha kuruka mbinguni.

Mt. Yoano alipika magoti na uso yake chini ya bulongo alifanya sala kwa Mungu. Hile saa sauti kimungu ilimujulisha ya kama toba ya wakati kidogo ya huyu binti Taisia ilimufurahisha Mungu, kupita mingi ya toba ya watu wengine, kwa ajili ya kivukutu wa roho kwa toba yake.

## Shemasi mufungwa

Mu monasteri moja ya Misri aliishi shemasi moja mufazili. Wakati moja alikuja kule mkubwa moja wa inchi pamoja na jamaa yake na aliomba ulinzi. Shetani alifanya tendo uovu wake, kwa sababu shemasi alianguka mu zambi ya uzini pamoja na binti moja ya hule baba mkubwa. Hii tendo kibaya ilijizambala mbio na walikuaza watu wingi.

Mukosefu alitubu mara moja. Alienda bila kuchelewa kwa mutawa padri wa roho mwingine na aliungama zambi zake. Huyu padri ya roho alikuwa na pango moja, ndani ya nyumba yake. Shemasi alimuomba amupatie baraka yake juu ya kuingia ndani ya hii pango na kuishi mpaka mwisho ya uzima yake. Alitaka kujizika ndani ya kaburi moja muzima na kuliya zambi yake mpaka lufu yake!

Vile na alifanya. Huyu mwenye zambi aliingia ndani ya kaburi (pango) yake. Padri ya roho kila magaribi alimutupa kidogo mukate ku tundu moja.

Miaka mingi ilipita. Watu walipotesha mwendo ya shemasi. Walisimama kusimanga zambi zake. Ku mwisho waliisahabu.

Mwaka moja mutoni Nilos alikuwa na maji kidogo. Ma shamba ya Misri hakuna namna kumwangisha na maji. Ma ngano waliharabika na watu bila kitumaini walikimbilia mu Monasteri na ma kanisa juu ya kuomba sala na kufanya Litania (Kuziuguluka). Lakini kwa bure, kwa sababu maji hakuna namna kupanda yulu.

Ku mwishi askofu ya njimbo pale moja, alikuwa mtu mtakatifu, alifanya sala mingi juu ya hii mateso ilifika kwao. Mu musingisi yake alisikia sauti moja ilimuwaambie: «Kama atafanya sala huyu shemasi, anayekuwa ndani ya nyumba ya padri fulani, maji ya mutoni itapanda yulu». \Siku ingine asubui huyu askofu mweshimiwa pamoja na wapadri wake wote na taifa mengi walienda mu nyumba ya hule mutawa padri ya roho na walitosha inje shemasi. Walimusukuma na haraka afanye sala kwa Mungu.

Wakati huyu shemasi alinyanyua mikono yake mbinguni nas alisema sala kidogo, mara moja mutoni Nilos ilipandisha maji zake na ma shamba walikunywa maji mingi.

Watu, wenye zamani walikumbuka zambi zake na waliisha kukuaza, mukuona sasa uwezo yake kwa ajili ya kitubio nzuri yake, walimuheshimiwa na walimutukuza Mungu.

## Huu (ndege) mueupe

Mutawa moja alikwenda mu muji juu ya kuuzisha vitu vya kazi vyake. Mu njia alikuta kwa bahati binti moja muzuri, aliyekuwa mtoto ya padri moja mupagano. Aliacha mwungo yake na alijibamba na mawazo ya zambi wa mwili. Alisahabu malako lake mbele ya Kristu juu ya kuchunga utakaso na ubikira na alimuomba ku baba wake kusudu amubebe bibi yake.

-Misiweze kukupatia mtoto wangu, kwani mbele ninapashw akuuliza mungu wangu.

Kweli alienda hekaluni yake juu ya kumuuliza mungu (shetani) yake.

-Mkubwa ya hekalu (mulozi) alimwaambia: Umuombe kukataa yeye uzima utawa wake na ubatizo yake.

-Ninakataa yote wa wili, alimujibu huyu mutawa mupotevu, kwa sababu aliisha kujaza akili yake na ngiza ya zambi.

Mukusema hivi aliona kutoka ku kinywa wake huu (ndege) moja mueupe na alitoka mbali.

Baba ya hule kijana mwanamuke hasikufurahi mara moja. Aliomba jibu ingine toka mkubwa ya hekalu yake.

-Usimupatie mtoto wako, kwa sababu Mungu wake bado kumukataa na kumuacha.

Wakati alisikia jibu ya mutumishi ya shetani huyu mutawa alishituka. Roho yake ilipasuka.

-Mimi mwenye zambi na mupotevu! alipaza sauti. Nilikataa Mungu wangu, lakini Huyu asipende nikatale, mimi kiumba wake?

Aliomboleza kwa hii zambi zake, sawa zamani mtume Petro na alirudia mu jangwa. Alienda mara moja kwa padri mkubwa moja na aliungama zambi zake na kitubio mnene.

Hule alimusikia na mapendo, alimusaidia, alimutulivu, lakini alimupatia na malipizo moja munene:

-Ingia na funga maungo yako ndani ya hile pango, na alimuonyesha ilikuwa wapi mu jangwa. Utakula mukate kidogo mara moja ya ma siku tatu na usisimama kumuomba kwa Mungu juu ya kukuhurumia. Vile nitafanya na mimi kwa ajili ya hurumia na wokovu yako. Ninatumainia ya kama Mungu atatupatia alama moja ya kama alipokelea toba yako.

Ndugu alisikia na utii shauria ya padri mkubwa wake. Pamoja naye alifunga chakula na padri ya roho yake na alichoka naye.

-Ee Bwana wangu, ninakuomba, alisema mu sala yake huyu Muzee, pokea toba ya huyu ndugu na okoa nafsi yake.

Mungu Mwema alisikia maombolezo wale watu wa wili! Kisha juma moja alienda padri muzee kuona anafanya nini ndugu wake. Hule ndugu alimuwaambia ya kama aliona mbinguni kufika huyu Huu (ndege) mueupe.

-Endelea ushindani wako, ee ndugu wangu, na tumainia kwa rehema kubwa ya Mungu, alimusema padri muzee.

Ilipita tena juma moja na ndugu aliungama kwa padri ya roho yake ya kama huyu ndege mueupe alikuja na alisimama karibu yake.

-Endelea, mtoto wangu, toba na sala yako, alimuwaambia na furaha padri ya roho yake.

Wakati ilipita na juma wa tatu alienda kumutembelea ndugu wake alitembea namna gani. Alimupata na aliliya na furaha.

-Ee Ava, ndege alikuja na aliikaa pa kichwa yangu. Mimi nilifungula mukono yangu juu ya kumubamba, lakini huyu aliluka na aliingia ndani ya kinywa yangu.

-Ava (padri ya roho) alifuraha na alisema: Utukufu kwa Mungu, aliyetujulisha ya kama alipokelea kitubio yako. Sasa uende nyumbani yako na sopoka muzuri maungo yako na usifukuze mara ingine Neema ya Roho Mtakatifu, hile ulichukua wakati ulibatizwa mu Kanisa Orthodokse.

Huyu ndugu alibakia mpoaka mwisho ya uzima yake pamoja na huyu padri muzee. Alimutii na alimufata ma shauri na sauti yake na hivi alikufa na aliokolewa.

## Maungamo ya munyanganyi

Munyanganyi moja alikamata mpango kutubu na alienda mu monasteri moja wa Misri. Padri mkubwa, mwenye hekima na mtakatifu ku mwanzo alimuhamuru ya wakati miaka saba hasitatumike, paka ataangalia desturi na uzima ya monasteri yake.

Siku wa mnane alimuita na alimuuliza kama inamupendeza monasteri ambakie pale. Wakati alisema ya kama anapenda kuikaa daima ndani ya hii monasteri yake, alimuuliza mara

ingine zambi gani alifanya duniani. Munyanganyi aliungama zambi zake zote! Kisha padri mkubwa juu ya kumupima alimuwaambia:

-Ninataka hii zambi zako zote kusema na mbele na watawa wote.

Na hule, kwani aliisha kuchukia zambi zake na alizarau kila haya, alimujibu bila shaka:

-Kama unataka, nitasema zambi zangu na katikati ya muji Aleksandria!

Kisha sauti yake, padri mkubwa alisanyika watawa wote ndani na katikati ya kanisa, walikuwa wote miya mbili na makumi tano (250). Kisha somo ya Evangelio, alimuita huyu munyanganyi kusimama katikati ya kanisa.

Watawa wengine walimukokota ya kufungwa mikono wake mukongo. Pa kichwa yake aliisha kuweka maivi ya makala na alivaa mufuko moja. Watawa, wakati walimuona walishangaa, kwa sababu hawakujue ya mambo gani walimuleta katikati yao. Watawa wengine waliliya.

Wakati kundi ya wale watawa walimupeleka ndani ya kanisa walifika ku mulango wa kwanza, padri mkubwa alimuita kusema hivi:

-Simama! Usiwe stahili kuingia hapa.. .

Hule munyanganyi alishituka! Alizania ya kama alisikia kogoloma na hapana sauti ya mutu. Alianguka mara moja na uso yake chini na alitetemeka kwa woga. Huyu padri mkuwa, mwenye alitaka kumusaidia huyu ndugu juu ya kunyenyekevu na kupatia mfano nzuri na kwa watawa wengine, alimuhamuru kuungama zambi zake moja-moja, mbele ya kundi ya watawa wote.

Kweli huyu munyanganyi alianza na woga maungamo yake. Alisemaka matendo hile watawa walisikia mara ya kwanza. Aliisha kufanya zambi hapana katika mwili, lakini na alikwenda kwa mulozi, aliua watu na ingine zambi, hakuna namna kuiandika.

Kisha maungamo yake huyu padri mwenye hekima alimupatia na amri ingine: Mara moja alimuita padri moja juu ya kusoma ibada ya kuwa mutawa. Toba na maungamo ukweli yake ilikuwa ya kuenea juu ya kuwa mutawa.

Mtakatifu Yoano wa Sinaitis, aliyekuwa katikati ya hii kundi ya watawa aliangalia hii yote jambo, alimuuliza padri mkubwa juu ya nini alitimia hii namna juu ya kumutubu huyu munyanganyi, na padri mkubwa alimujibu:

-Juu ya sababu wa wili: Ya kwanza nilitaka huyu ndugu kusikia haya juu ya zambi zake juu ya kuokolewa toka haya wa milele. Na hii jambo ilimalizwa. Ndugu wangu Yoano, huyu munyanganyi hasikusimame ya chini mpaka aliungama zambi zake zote. Mutawa moja aliniambia ya kama aliona hile saa muhu mutu aliungama moja-moja zambi zake, aliona mwanaume moja mwenye matata, aliyekamata pa mukono kartasi na nguo moja. Kila mara huyu mtu alisema moja zambi zake, huyu mwanaume aliizimisha ku kartasi yake!

Ya mbili nilitimia hii namna kwa sababu nikona huku watawa wengine, wenye mpaka sasa bado wafanye maungamo ya kweli. Na katika hii mfano niliwasukuma kufata mfano yake, kwa sababu bila maungamo hata moja hasitaweze kupata maondoleo ya zambi zake.

# Uzima isiyokufamia

## Mugeni katikati ya wa ndugu wa nyumba

Mtakatifu Aleksios, «mutu wa Mungu», alikuwa mtoto ya wazazi wakubwa ya muji Roma wa Italia zamani. Baba yake, jina lake Efimianos, alikuwa mkubwa moja mu makutano ya wakubwa ya Roma, wakati mfalme alikuwa Onorios (395-423). Alikuwa baba yake mkubwa, lakini alikuwa rafiki na wamaskini na aliwasaidia sana.

Mtoto wake Aleksios alikuwa mwenye hekima na murafiki ya mafundisho yote. Na haraka alipata mafundisho ya hekima ya hii dunia na ilimusaidia hii hekima kumufamia Mungu.

Basi, alikamata mpango kumutoa maungo yake kwa Mungu mukuishi uzima ubikira. Wazazi wake, lakini walikataa na walimusukuma kuondowa. Ndoa ilifanyika, lakini usiku wa kwanza Aleksios alitosha pete na musipi yake aliitoa kwa bibi-arusi wake na alikimbia kwa siri mu kikavu ya bahari. Pale alipata chombo na alifika mu muji Laodikia ya inchi Siria na kisha na miguu alifika mu muji Edesa ya Siria.

Mu muji Edesa alibaki ndani ya kanisa moja na aliishi katika huruma ya waaminifu. Desturi yake ilikuwa sawa kuishi yeye mu jangwa; Nikusema alifanya kifungo ya chakula, sala ya usiku na sala ya muchana. Watu walimusifu sawa mtakatifu! Kwa hii neno alikimbia ku muji Edesa na alitembea kwenda mu muji Tarsos. Lakini pepo ingine ilisukuma chombo na alienda mara ingine mu muji Roma ya Italia.

Mtakatifu Aleksios alisadiki ya kama hii tendo, ni kusema ya kurudia mu mukini yake, ilikuwa katika mapenzi ya Mungu! Basi, aliwaza kuishi uzima wa utawa na namna nguvu kabisa: Nikusema alikamata mpango kuishi ndani ya lupango ya nyumba yake, pasipo wale amufamie na pasipo yeye aliwaambia nani alikuwa. Na sula na mwili yake iliisha kugeuza kwa ajili ya kifungo ya chakula na kipimo yake.

Ya kwanza alitembelea ma kanisa ya muji yote na alibusu ma Ikone ya Watakatifu wote na aliomba saidio wao. Kisha alirudia nyumbani yake, pa hile fasi alizaliwa. Mu njia kwa bahati alimukuta baba yake:

-Mkubwa wangu, alimwaambia, niko mskini na mugeni. Ninakuomba unipokee mu fasi moja ya kona ya nyumba kubwa yako.

Hule baba wake, hasikumufamie ya kama alikuwa mtoto wake na, kwani alikuwa mukaribishaji, alimupokelea na alimupatia chumba moja mu lupango yake. Mtakatifu Aleksios alianza ushindani ya roho yake.

Shetani sasa alianza kumuuzi sana. Chum, ba ya mutawa ilikuwa karibu ya chumba ya mama yake na ngambo ingine ya bibi wake. Mara mengi kila siku aliwasikia kuomboleza na kuliya kwa sababu walipotesha mama mtoto wake na bibi bwana wake.

-Olo kwangu mwenye mateso, alisemaka bibi yake. Eko wapi sasa bwana mupendwa wangu? Juu ya nini alionyesha hii ugumu mbele yangu? Juu ya nini aliniacha mimi wa pekee?

Lakini na mama wake aliliya na aliombopla kwani alipotesha mtoto mupendwa wake:

-Mtoto mupendwa wangu, juu ya nini ulionyesha hii tabia yako mubaya mbele yangu? Juu ya nini ulinipatia umivu na huzuni ya roho munene?

Roho ya mt. Aleksios ilipasuka kila siku, lakini alivumilia na uvumilia wa ajabu. Alileta mu akili yake ma sauti ya Madiko Takatifu: «Yeye anayependa baba ao mama kupita mimi hanistahili.. . » (Matayo 10, 37). Alipenda sana watu wa nyumba wake. Lakini aliweka kupita yulu mapendo kimungu mbele ya mapendo ya wa ndugu wake.

Pempeni ya hii mateso yake alikuwa na mateso ingine: Watumwa ya baba wake, wenye walitumika pale walimuchekelea na walimuchabula na walimutesa sana. Walimupiga na walimutupa maji na buchafu pamoja. Lakini mutu ya Mungu alivumilia bila kusema sauti mubaya mbele yao. Juu ya wazazi ya bibi yake alimuomba kwa Mungu sana juu awapatie uvumilia mu taabu na sikitiko yao.

Hivi alipita miaka kumi na saba (17) ndani ya hii uzima wa mateso. Hile mwaka ya mwisho Bwana Yesu alimufunua ya kama siku ingine, mu Kazi Tano, atapumzika toka mateso ya hii uzima. Basi, mt. Aleksios alibeba kartasi na stilo na aliandika hadisi ya uzima yake. Ku mwisho aliandika hivi: «Wazazi wapenzi na bibi wangu, musinichukieni kwa hii taabu mimi nilimipatia. Mimi niliuma mu roho yangu, lakini nilimuomba kwa Mungu amipatie Bwana Yesu ufalme wake wa mbingu! Ninasadiki ya kama Yesu atanisikia kwa sababu na mimi kwa ajili ya mapendo yake nilikuwa na tabia ugumu mbele yenu, tena nilikuwa mugumu kupita mbele ya maungo yangu.. . Katika hii umivu mutasikia, mutapata na malipo ya roho yenu.. . »

Wakati alifunga barua yake, alisimama kufanya sala yake mpaka mwisho ya uzima yake.

Ma siku madogo, mbele ya lufu yake, patriarki wa Roma jina lake Inokentios, alisikia, hile saa alifanya Liturgia, sauti moja:

-Mu Kazi Tano asubui mtu ya Mungu anatoka ya mwili yake. Mutamupata nyumbani ya mkubwa bwana Efimianos.

Patriarkis alishjituka na alishangaa sana.. .  Ni nini ilikuwa hii tangazo? Basi, aliondoka hile siku pamoja na mfalme, wakubwa na waaminifu wingi kwa kutembea nyumbani ya mkubwa Efimianos. Pale walipata pa lupango yake ndani ya chumba moja hule mugeno mutawa, aliyekuwa mufu. Mtakatifu Aleksios aliisha kufunika uso yake na pa mikono yake alikamata hii barua aliisha kuiandika. Patriarkis alitosha hii nguo ilikuwa yulu ya uso yake na uso yake ilijaza na mwangaza. Wakati walisoma barua yake na walisikia ya kama huyu alikuwa Aleksios, ilianza maombolezo munene ku wazazi na bibi wake. Lakini na wale walikuwa pale karibu walianza kuliya!

Mfalme na patriarkis walihamuru kupeleka maiti takaitfu yake katikati ya muji juu ya kumubusu waaminifu wote ya muji. Heshima hile walimuonyesha na wakati ya kumubusu waaminifu ilikuwa na juma muzima. Kwa hile wakati ya kumubusu mwili takatifu yake ilifanyikwa miujiza na wagonjwa wingi waliponyeshwa! Kisha walimuweka ndani ya sanduku wa argint na walimuzika mu kanisa ya mt. Petros.

Ukumbusho ya mt. Aleksios, «Mutu ya Mungu», Kanisa yetu inashangilia mu tarehe 17 Mwezi ya tatu, siku ya kulala (lufu) yake. Alilala katika Kristu mu mwaka 410. Kifupa ya kichwa takatifu yake ni mu Monasteri ya Lavra takatifu, karibu ya muji Kalavrita ya Grekia.

## Mutawa mwanamuke Efrosini

Uzima ya Watakatifu wanawake, wenye waliingia mu monasteri ya wanaume  ni wa ajabu. Hii tendo yao haiko zoezo mu uzima ya utawa. Lakini Neema  takatifu aliwafunika na aliwaongoza yulu kabisa kwa utakaso yao. Katikati yao eko na mutawa mwanamuke Efrosini.

Alizaliwa mu muji Aleksandria, mu mwaka 410 mu wakati ya mfalme ya Konstantinopoli Theodosios wa Mudogo. Aliitwa Efrosini, kwa sababu na uzalio yake alileta furaha na shangilio kwa wazazi wake, wenye mpaka hile wakati walivumilia hii taabu yao, kwa sababu hawakuweze kuzala mtoto. Baba wake, jina lake Pafnutios, aliisha kuomba ku watawa wingi  na wafazili juu ya kuomba kwa Mungu na, kama Mungu atawapatia mtoto, huyu atakuwa tunda ya sala ya watawa.

Wakati binti Efrosini alikuwa na umri miaka kumi na mbili (12), alikufa mama yake na baba yake Pafnutios alikamata huyu wa pekee mambo ya kumukomesha muzuri. Alimuongoza kabisa mu njia ya Mungu na alimusoma vitabu vya Mungu. Hivi pempeni ya umri yake ilikomea na tabia ubikira na ufazili wake.

Wajirani na wale walimufamia mukuona ma fazila yake, mwili nzuri yake na kizazi kitakatifu yake, walianza wamushauria kuowa mwanaume  fulani, ndugu wao. Lakini huyu alipenda kujitoa kwa Kristu na alikataa kila shauria yao juu ya kuowa bwana ya hii dunia.

Baba mupendwa wake, kwani alikombana kumufurahisha mtoto wake, aliisha kuchangua mwanaume kijana juu ya bwana ya mtoto wake. Binti yake Efrosini alikataa daima. Hasikupende hata kidogo kufata ma shauria ya baba wake.

Wakati mtoto wake alikuwa na umri miaka kumi na mnane (18) alimupeleka mbele ya hile monasteri, watawa na padri mkubwa waliomba kwa Mungu juu ya uzalio wake.

-Ee Muzee (padri wa roho mkubwa) ninakuletea mbele yako binti yangu, tunda ya sala yako. Umushaurie na umuombe kwa Mungu juu ya kuowa na kufanya jamaa moja na vile atamufurahi Mungu.

Padri mkubwa aliwachunga mu monasteri yake ma siku tatu. Ndani ya hii ma siku binti Efrosini alishangaa uzima takatifu ya watawa, desturi ya ma Ibada yao, heshima na woga ya wimbo na maombi yao na uzima yao ufazili.. .  Alisema ndani yake: «Kweli hawa wa ndugu

weko wenye heri! Wanaishi ndani ya hii uzima kwa mapendo ya Mungu; Wanafanya uzima wa malaika na wataenda mu paradizo na watasikia kwa milele karibu ya Kristu».

Alibeba baraka ya padri mkubwa na alirudia nyumbani yake na alianza na mapendo mingi uzima ya roho. Vitu vyake vyote wa zahabu na ingine aliikabula kwa maskini. Kisha alivaa manguo mapole. Alikataa mazungumuzo na watu wa hii dunia na wanawake wenye zambi na hivi alichunga mapendo yake ndani ya roho yake kwa Mungu. Alikomesha roho yake katika maosmo ya vitabu vitaaktifu na alisali sana.

Wakati moja, baba yake alilofa ku nyumba yake na binti yake Efrosini, alipata wakati juu ya kutoka ya nyumba na dunia na alikimbilia mu monasteri moja, pahali ataweza kuishi uzima takaitfu ya roho. Kama alikwenda mu monasteri ya wanawake ilikuwa namna na haraka baba yake amupate na amurudishe kwake. Basi, alivaa manguo ya mwanaume na alikimbilia mu monasteri ya wanaume.

Padri mkubwa alimuuliza nani alikuwa na alitaka nini.

-Ninaitwa Smaragdos, alimujibu na niko musaidizi mu nyumba ya mfalme Theodosios. Lakini niliacha makelele ya dunia na, kwani nilisikia ma fazila yenu, nilikuja kwenu juu ya munipokee mu makutano ya watawa wenu.

Hule Igumeni alifurahi mukuona kijana moja mweshimiwa na alimujibu:

-Ee Ndugu, tuko karibu yako kusaidia mu matakio yako. Kama monasteri yetu inakupendeza bakia huku. Lakini, kwa sababu uko kijana kabisa na haujue desturi ya uzima yetu, nitakupatia padri moja mufazili na yeye atakufundisha namna gani unapashwa kuishi katika uzima ya roho. Kwake utamutii bila kukataa.

Mt. mutawa Efrosini alinamisha na unyenyekevu kichwa yake na alimulaka ya kama atafanya utii hapana paka kwa hule muzee padri ya roho yake, lakini atatii mbele ya kila mutawa ya hii monasteri.

Padri mkubwa alimupatia kwa mutawa muzee moja wa zamani, jina lake Agapios.

-Ee Padri, kamata huyu kijana, aliyemutuma kwa sisi Mungu na umusaidie kuwa mufwasi muzuri mu uzima yetu. Umusaidie kuwa mutawa kupita mkubwa ya weye.

Tangu hile siku padri muzee Agapios alikombana kumunyolosha huyu kijana mu uzima kitakatifu. Lakini na mt. Efrosini na jina mupya, sawa mwanaume, alimufata ma shauria yake na alikomea kila siku mu zima wa utawa.

Kisha wakati fulani shetani alianza kumukombana kwa kumukumbusha mapendo ya baba yake, ao matakio ya bwana wake, aliyependa amupatie baba wake, ao masifu na mafuraha ya dunia. Lakini hii majaribu yote walikimbia kwa mapendo ya Mungu, ile ilikuwa ndani ya roho yake.

Adui shetani alipata na namna ingine: Alipanda bego ya zambi ya uzini (zambi ya mwili) ndani ya akili ya watawa wanaume vijana, kwani huyu binti Efrosini alikuwa na uso na mwili muzuri. Padri mkubwa alisikia maungamo yao na aliwaza atafanya nini? Hakuna namna kufukuza kijana moja aliyekuwa mufazili na mutilifu. Aliwaza na ku mwisho alimuhamuru mutawa Smaragdos (Efrosini) atoke mu nyumba moja inje na kidogo mbali ya monasteri na pale atasoma ma ibada yake na atatumika. Tena hasitakuja mu meza hata mu kanisa ya kula ao ya sala pamoja na watawa wengine. Muzee padri ya roho yake atamupatia chakula, bintu ya kazi yake na kila kintu atailazimishwa. Mt. Efrosini alifurahi na hii sauti ya padri mkubwa ya monasteri. Sasa alikankamana nguvu juu ya kufuchika ukoo (Uzazi) wake. Tangu hile siku alikuwa kupita muhuru. Kwa sababu alikuwa inje ya watawa wengine na ma kazi yao yote, ataweza kuongeza kifungo ya chakula na sala yake kila usiku. Mashindani ya roho yake walimustaajabu padri muzee Agapios na yeye alijulisha matendo ya roho yake kwa watawa wengine.

Wakati baba yake, Pafnutios, alirudia nyumbani yake na alijulishwa kutokuwa kwapo ya binti yake, alishituka na alianza kumutafuta ma fasi yote. Alituma watu wake kumutafuta ndani ya monasteri ya wanawake na ma nyumba ya jangwa mu inchi ya Misri, Livii na Palestina.

Kwani hakuna namna kumutafuta, uchungu yake mu roho ilikomea na ilimupatia huzuni munene na umivu mingi.

Kisha miaka mengi, aliwaza kuomba saidio ku hule padri mkubwa aliyemufamia ya zamani. Alitumainia kwa maombi yake na maombi ya watawa wake ya kama watamupata.

Alienda mu monasteri, alianguka mbele ya miguu yake na aliomboleza toka chini ya roho yake:

-Ole wangu, Muzee wangu, nilipotesha tunda ya sala yako! Efrosini, mtoto wangu alikimbia ku nyumba na hata mutu moja hasijue eko wapi. Nilipotesha nuru ya ma macho yangu! Lakini, ninakuomba fanya mapendo juu yangu: Mufanye mweye pamoja na watawa wote sala juu ya hii mambo yangu. Mufanye sala na ninatumainia ya kama Mungu atanifunua furaha ya uzima yangu, mtoto wangu!

Padri mkubwa aliliya kwa ajili ya umivu ya baba yake. Alisanyika watawa wote wake na aliwalejea taabu ya rafiki yake na aliwaambia watawa wote kuchunga chakula juma moja na watamuomba kwa Mungu juu ya kuonekana binti yake Efrosini. Huyu Efrosini aliisha kujua hii mambo ya baba yake. Alimuelejea muzee Agapios. Sasa Efrosini alifanya sala kwa Mungu juu hapana kumuonekana Mungu kwa baba wake. Na mungu mwenye hekima kamili alitengeneza hii mambo yao wa wili na namna wa ajabu!

Ilipita juma moja hile walifanya sala na kifungo padri mkubwa pamoja na watawa wake. Walisikia ya kama hakuna ufunuo ao ono moja kimungu ao ujulisho moja fasi wapi alikuwa mtoto ya bwana Pafnutios. Hile saa Igumeni alisema kwa bwana Pafnutios:

-Usitaabu mtoto wangu. Usipotee kitumaini yako na usiliye, sawa vile wanafanya wasiyoimani, wenye hawakuwa na kitumaini mu uzima wa milele na kila kitumaini yao weko nayo paka pa vitu vya hii uzima yao. Unisadiki, ya kama, kwa sababu Mungu anakataa kutwaambia eko wapi binti yako, ninasadiki ya kama binti yako ni mu njia muzuri. Anakataa Mungu atuonyeshe eko wapi, kwa sababu atazibiya wokovu wake.

Bwana Pafnutios alijitulivu na ma sauti yake. Aliendelea aende mu hii monasteri na kila mara alirudia na amani kuliko mingi.

Pa mutembeleo moja padri mkubwa alimuaambia:

-Unataka kufamia mutawa moja wa ajabu, anayeishi yeye wa pekee inje ya monasteri yetu? Anaitwa Smaragdos na alizaliwa toka jamaa kubwa. Halafu, kwa ajili ya mapendo ya Kristu, alikataa vitu vyote vya hii dunia na alikuja huku mu monasteri yetu. Huyu ni mfano ya mafazila yote!

Pafnutios alipokelea na furaha na alienda kwa hule mutawa Smaragdos pamoja na muzee padri Agapios.

Wakati mutawa Smaragdos (mtoto wake Efrosini) alimuangalia, alianza kuliya. Baba wake Pafnutios hakuna namna kumufamia, kwa sababu uso na mwili ya Efrosini aliisha kukauka kwa uzima nguvu ya roho na kifungo yake. Tena na manguo yake ilikuwa manguo ya mutawa mwanaume. Wakati alimuona mtoto wake Pafnutios, hasikumufamie na alizania ya kama aliliya kwa ajili ya mateso yake. Mt. Efrosini alifanya nguvu ya kusimamisha machozi yake na alimwamabia:

-Mkubwa wangu, ninajua mambo yako. Lakini usipotee kitumaini yako. Nikona kitumaini ya kama binti yako ni mu njia nzuri kabisa. Tena ninasadiki ya kama Mungu atasikia ma sala ya wapadri wetu na atakusaidia na utamupata mtoto wako. Basi, usitaabu na fanya uvumilia kidogo. Kumbuka ya kama na patriarkis Abrahamu aliliya miaka mengi mtoto wake Yosefu na aliwaza ya kama aliisha kufa. Lakini alistahiliwa kumuona mkubwa mutukufu mu inchi Misri! Ninakuwaambia na mimi mara ingine: Utaona na weye binti wako, mbele ya kufunga ma macho yako (mbele ya lufu yako).

Kisha hii mapatano na mazungumuzo yao bwana Pafnutios hasikuweze kumushukuru padri mkubwa kwa hii ufamio na hule ndugu Smaragdos, aliyemutulivu sana.

Wakati ingine mt. Efrosini aligonjwa sana na alikuwa karibu ya lufu. katikati ya wale walikuja kumuangalia pa kitanda yake, alikuwa na baba yake Pafnutios. Vile alipata hii muda mt. Efrosini amuonyeshe ya kama huyu alikuwa binti wake na ya kama alimukana hapana kwa uzarau yake, lakini kwa mapendo ya Bwana Arusi wa mbingu.

Kisha hii onekano na ufafanusho yake mt. Efrosini alilala (alikufa). Uso yake mu Kiliyo yake iliangazwa sawa jua! Mutawa wa jangwa moja aliyekuwa kipofu pa richo yake moja, wakati alibusu maiti kitakatifu yake, aliponyeshwa! Padri mkubwa na watawa wote walishangaa kabisa. Watu wote walikikishwa ya kama mt. Efrosini alipata uwezo mnene mbele ya Mungu.

Baba wake Pafnutios hasikupende kutoka ya hile chumba ya mtoto wake. Alikabula uriti wake wote kwa maskini na alikuja ndani ya hii chumba ya binti yake! Aliishi miaka kumi na alilala (alikufa) sawa mutawa mtakatifu. Kanisa yetu inashangilia makumbusho yao mu tarehe 25 Mwezi ya Tisa, kila mwaka.

## Muzee Antimos mwenye kutwanga

Mujengaji ya Monasteri ya Utatu Mutakatifu mu njimbo Oropos ya Atiki, inje ya muji kubwa Athina ya Grekia, alikuwa padri mkubwa Kheruvim. Huyu ndani ya kitabu yake «Makumbusho ya Mulima Takatifu) anaandika mapatano na kizungumuzo yake pamoja na mutawa moja, jina lake Antimos, aliyekuwa toka umoja mukini yake.

«Wakati moja niliondoka niende mu muji Karies ya Mulima Takatifu juu ya ma kazi ya kuachana. Niliomba baraka ku padri mkubwa wangu nitembee mutawa Antimos, aliyekuwa mu nyumba moja, karibu ya monasteri Stavronikita, pahali alitumika ya kutwanga bunga.

-Uko toka fasi wapi, mutawa kijana?

-Niko toka Skiti (Mukini ya watawa) Mtakatifu Anna. Toka Nyumba ya Uzalio ya Mzazi-Mungu.

-A, uko mutoto ya roho ya muzee Grigorios. Na namna gani ulikuja huku mu jangwa? Uko na baraka ya padri ya roho yako?

-Ndivyo, nikona baraka yake. Tangu zamani nilitakia kumiona na kwa hii mambo nilikuja kwenu.

-Wafwako, basi. Ikaa.

Alinionyesha kuikaa pa kiti kifupi moja na alienda mbio niletee matunda na maji baridi. Kisha tulianza mazungumuzo.

-Weye uko kijana, mtoto wangu. Sasa unaanza hii uzima utawa. Mbele yako uko na kutembea njia urefu na njia ya mutawa ni ugumu sana. Mara mengi utaumivu. Mara mengi utasema ya kama watu wanakuzarau. Wakati ingine padri mkubwa yako aomutawa mwingine watakata mapenzi yako na ndani yako utasikia uchungu na ugumu. Lakini juu ya kulamuka usiku haina tendo ugumu? Inazimishwa ushindani munene juu ya kulamuka usiku, kisha utafanya sala yako mu chumba yako na kisha utasimama mu kanisa paka asubui. Na matendo ingine na ingine.. . Paka kitu kimoja itakusaidia ya kila ugumu yako: Kama utaweza kuweka Yesu Kristu-neema Yake-ndani yako, Huyu atakusaidia ya kila ugumu yako.

-Ee Muzee, muko ya fasi wapi?

-Juu ya nini unaniuliza? Mimi niko toka mbali, toka Peloponisos. (Njimbo moja ya Grekia).

Na mimi nilikuwa toka mukini yake umoja, lakini nilimuacha kusikia ma shauria yake.

Wakati nilimwaambia ya kama watawa ya nyumba yangu waliendelesha sana sala ya Bwana Yesu Kristru, uso yake ilijaza na wangaza.

-Basi, utaweza na weye kuendelea pa hii tendo ya kusema sala ya Yesu Kristu. Uniambie na mambo ingine: Ulizaliwa wapi? Uko toka muji munene Athina?

-hapana. Niliisha miaka mengi karibu ya Athina, lakini fasi ya kuzaliwa yangu ni njimbo Mesinia ya Peloponisos.

-Toka muji Kalamata?

-Hapana. Mimi ni toka Mesinia wa kaskazini, toka mukini Konstantini.

Nilijua ya kama na huyu alikuwa toka hii mukini umoja. Sasa nilimuona atasema na atafanya nini. Lakini alifuchama na yeye hii jambo. Lakini mimi nilitaka kusuburia hii mambo ya mukini umoja yetu mara ingine.

-Ee Muzee, kwani muko toka Peloponisos, munafamia njimbo Mesinia. Iko vile?

-Ndivyo, ninaifamia, alinijibu bila furaha.

-Muliisha kwenda hata mara moja mu mukini Konstantini?

-Wakati moja nilikuwa na mimi ndani ya hii mukini.

-Nikusema mulizaliwa na mweye ndani ya hii mukini?

-Ndivyo, lakini niliondoka mbele ya miaka makumi inne.

-Mweye muko mtoto ya mama muzee-Marina?

-Ndivyo, nilikuwa na mimi zamani mtoto wake.

Hasikuniulize hata sauti moja juu ya mama yake, wala ya mukini wala ya jirani na wa ndugu wake. Nilimuwaambia;

-Ee Muzee, mbele ya kutoka ya mukini nifike huku mu Mulima Takatifu, nilikua mama yenu na uzee kabisa na tulisuburia naye kidogo. Tena nilimuwaambia ya kama hile saa ya lufu yake Mungu atatuma malaika wake juu ya kupelekea nafsi yake kwa Yesu Kristu, kwa sababu alitoa mtoto wake kwa Muingu. Na huyu alinijibu: «Amina, mtoto wangu». Lakini baba wenu aliisha kufa zamani.

-Ninajua ya kama alikufa.

Aliniangalia mara ingine, bila kuendelesha zungumuzo juu ya wa ndugu na wazazi wake. Kisha aliniuliza paka matendo ya uzima ya roho na alinipatia mafundisho ya roho.

Mimi misikujue kushangaa nini toka mafazila ya tabia yake: Upole, tabia utamu yake ao ya kama alisahau na mapenzi yake kila kifungo na dunia, na wandugu na wazazi wake?

Huyu mutawa aliisha kukataa kila mapendo na ufamio na wa ndugu wake na akili yake alinyanyua paka kwa Mungu.

# I M A N I

## Kihu ya mtoto wa roho

Mfano wa ajabu juu ya imani ya mtu moja kwa mapendo ya Mungu ni hii jambo inafwata:

Ava Visarioni pamoja na mtoto wa roho yake mutawa Dulas walitembea ya saa mengi karibu ya kikavu. Mufwasi yake alisikia kihu na aliisema kwa padri ya roho yake. Hule alisimama, alifanya sala na alimuhamuru:

-Tazama, kunywa maji toka bahari!

Mutawa Dulas alipika magoti chini na alikunywa. Kweli maji iliisha kuwa utamu! Wakati alikunywa, alijaza na chupa moja juu ya kunywa mu njia. Hii tendo yake aliiona padri Visarioni na alimwaambia:

-Juu ya nini unabeba hii maji?

-Unibariki ee Muzee, lakini niliibeba hii maji juu ya kunywa mu njia.

-Haina lazima! Huyu aliyekupatia kunywa maji huku, Huyu ataweza kukusaidia na ma fasi ingine.

## Nvula iliyetoka ya Mungu

Ava Musa alikamata mpango kuikaa ndani ya pango moja, iliyekuwa chini ya njiwe moja munene ya mulima moja. Alipanda mu pango na aliwaza hivi:

hakuna mambo ya maisha yangu pa hii pango, lakini nitapata wapi nikunywe maji?

Aliwaza hii mambo mara mengi na alianza roho yake kulekea. Hile saa alisikia sauti moja:

-Tembea ku mbele na acha kila mambo ya maisha yako kwa Mimi!

Padri alikamata nguvu na aliikaa ndani ya hile pango. Kisha wakati kidogo walienda wamutembelea watawa wa wili wengine wa jangwa. Mu pango yake ilikuwa paka birika moja na maji na hii maji alipika malalaki kwa kuwapatia chakula yao. Hile saa alianza kusikitika. Alitoka inje ya pango, aliingia ndani na aliomba kwa Mungu juu ya maji.

Kwa rafla, pasipo kuongojea hii jambo wa ajabu, ilikuja yulu yao mawingu moja na ilisimama pa pango yake na ilinesha nvula, ile ilaizimishwa ya kujaza ma birika yake yote!

Wazee, walimuona ya kama alikuwa na sikitiko na walimuuliza:

-Asubui juu ya nini ulikuwa na sikitiko na ulikwenda saa ingine ndani na saa ingine inje ya pango?

-Nilikuwa na uhukumu pamoja na Mungu! Aliwajibu na upole. Nilimukumbusha ya kama Huyu aliisha kusubuka mambo ya maisha yangu na alipashwa kunituma maji juu ya kunywa watumwa Wake. Na tazama, Rabi Mwema wetu alikamata mpango nitume maji.

## Paska mu monasteri moja

Hile wakati ilijengwa monasteri ya mtakatifu Theodosios (423-529) mu Palestini, ilikuwa umaskini na mara mengi haikukuwe hata vitu wa lazima kabisa juu ya maisha ya watawa.

Mwaka moja, wakati waliongojea kushanglia Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu, wa ndugu, bila kitumaini walitafuta monasteri yao muzima kutafuta vitu vya kula. Walitafuta hapana vitu vingi. Walitafuta kabiosa prosforo moja (mukate ya Liturgia), kwani walitaka kesho kukomunika. Lakini hakuna namna kuipata! Walisema hii sikitiko yao kwa padri mkubwa yao mt. Theodosios. Aliwasikia bila kushituka. Alisema kwao kutayarisha bintu ya kufanya Liturgia ya Paska usiku, tena kutayariosha na meza ya chakula yao! Lakini bila bintu?

Watawa wake walishangaa kwa hii imani nguvu ya padri mkubwa wao, lakini hakuna namna kuifata.

Jua ilianguka magaribi na mugeni moja alikokola mulango ya monasteri yao. Pamoja naye alikuwa na ngamia wa wili na vitu vingi yulu yao na uzito sana!

-Huyu mugeni aliwaambia watawa: Nilipeleka hii vitu mu mukini ya watawa ingine, kidogo mbali ya huku. Lakini, wakati nilifika huku ma nyama yangu walisimama na wanakataa kutembea fasi ingine! Ninawaza, basi, Mungu anataka kushusha bile bintu huku?

Katikati ya bile bintu ya chakula ilikuwa na prosforo ya Liturgia. Na walifika kula mpaka Pentikoste na kupita mbali.

-Imani ya padri wetu ni kubwa kabisa, walisema katikati yao watawa wake. Na tangu hile siku walimueshimiwa kuliko padri mkubwa wao.

## Omoforio ya patriarki

Patriarki wa muji Antiokhia, jina lake Efremios (527-546) alikuwa na mapendo mingi juu ya imani Orthodokse. Basi, wakati alisikia ya kama mu njimbo ya Ierapolis aliishi mutawa moja mu jangwa, lakini alifata fundisho ya imani ya uwongo, alienda karibu yake juu ya kumurudisha mu imani ya kweli.

Walisuburia saa mengi na huyu mutawa alisimama pa fundisho yake na aliomba maonyesho.

-Ni kusema unataka nini? Na namna gani nitakuonyesha ya kama fundisho yetu ni ukweli?

Tazama, Patriarki mkubwa, alimujibu huyu mukosefu ya imani. Tutawakisha moto moja na tutaingia sisi wa wili ndani ya hii moto! Huyu mwenye ataishi bila kulungua, atakuwa orthodokse wa kweli.

Hile saa Patriarkis alimwaambia:

-Ilipashwa mtoto wangu, unisikie mimi sawa baba wa roho yako na haipashwe kuomba vitu vingine. Lakini, kwa sababu uliomba onyesho, hile ni kuliko yulu ya nguvu yangu, nitasadiki kwa Bwana wangu Yesu Kristu na nitafanya hii tendo uliniambia juu ya wokovu ya nafsi yako!

Aliita kisha wapadri wafwasi wake na aliwaambia: Ahimidiwa ni Mungu. Muniletee huku kuni.

Walimuleta kuni na patriarkis aliwaaka moto na alisema kwa mutawa mukosefa kwa imani:

-Basi, kuja na weye kuingia ndani ya moto, katika matakio yako.

Hule mutawa alishituka mbele ya imani ya patriarki na anakataa kukaribia.

-Weye uliniambia hii sauti, alimujibu patriarkis. Namna gani sasa unakataa?

Hile saa patriarkis, alitosha Omoforion yake, alikaribia moto na aliomba kwa Mungu:

-Ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, uliyekuja dunia na ulifanyika mtu kwa wokovu wetu katika Mzazi-Mungu Malkia wetu Bikira daima Maria, utuonyeshe imani wa kweli.

Wakati aliisha sala hii yake alitupa Omoforion yake (nguo pa mabeka yake-alama ya upadirisho yake) ndani ya moto. Hii moto aliaaka ma ra mengi na aliharabisha ma kuni yote. Wakari alizimisha moto, wapadri wengine walikaribia na wlaibeba Omoforion ya patriarki kuwa muzima, bila kulungua hata kidogo.

Hule mutawa mukosefu kwa imani alishituka na alikataa fundisho ya uwongo wake. Alisadiki mu Kanisa Orthodokse, alibatizwa na mara moja alipewa Mwili na Damu ya Kristu ku mikono ya patriarki.

## Feza wa zahabu

Usiku moja mt. Theodosios wa Kievo, monasteri ya Rusia (1029-1074) alitumika na alikuja kwake musaidizi yake, jina lake Anastasios, na alimwaambia ya kama makuta ya munasteri iliisha na hakuna namna kununua mukate ya siku wa kesho!

-Sawa vile unaona, alimujibu bila kushituka mutawa mtakatifu, sasa ni usiku na mpaka asubui tukona wakati. Basi, uende sasa kuomba kwa Mungu. Fanya uvumilia kidogo na Mungu atasubuka kwa sisi.

Alitoka musaidizi yake na padri Theodosios aliingia ndani ya chumba yake juu ya kufanya sala yake. Kisha sala yake, musaidizi alirudia kwake na alimuuzi paka na hii mambo.

-Nilikuwaambia fanya paka sala, alimujibu padri mkubwa wake. Fanya ukimya na kesho asubui utaenda mu soko na utanunua kila kitu tukona yo lazima na tutaripa wakati ingine, wakati Mungu atatutuma makuta. Anasema na imani bila shaka Huyu aliyesema kwa sisi: «Basi musisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe» (Matayo 6, 34). Mungu atatutuma neema Yake.

Kisha ondoko ya musaidizi yake, alikuja mu chumba ya mtakatifu kijana moja na manguo ya askari. Alinamisha kichwa yake, aliacha feza wa zahabu moja pa meza na bila kusema hata sauti moja, alikimbia. Mtakatifu alisimama, alibeba hii feza pa mikono yake na alimutukuza Mungu. Asubui alimuita mujukumu ya mulango, nani aliingia usiku ndani ya monasteri. Hule alimukikisha ya kama mulango iko ya kufungwa tena toka magaribi ya jua na hata mtu moja hasikuingie ndani.

Kisha aliita musaidizi yake padri Anastasios.

-Juu ya nini unasema ndugu Anastasios, ya kama hatuna na makuta? Beba hii feza wa zahabu na uende kununua kila kitu tunailazimishwa.

Huyu mutawa Anastasios hasikuweze kusikia hii baraka munene ya Mungu. Alizania ya kama hasikutafute nzuri na kwa hii mambo alimuomba hurumia ya padri mkubwa yake.

-Ee ndugu, alimushauria mt. Theodosios, usipoteshe kitumaini yako kwa Mungu. Chunga imani yako kwa Mungu na kila sikitiko yako uiache mbele Yake. Huyu anasubuka ya kila kintu yetu! Basi, tayarisha leo meza ya vitu vingi, kwa sababu leo hii siku ni siku ya matembeleo

kimungu. Na, kama tutapata mambo ya kulazimisha vitu vingine, Mungu atasubuka juu ya watumwa Wake.

## Mushahidi moja mupya asiye kumufamia

Mutu moja toka Chekhia, jina lake Mitrovichi ku mwaka 1591 alienda mu muji Konstantinopoli juu ya kzi fulani ya inchi yake. Kule aliona na macho yake namna gani walikufa vijana wa wili, mwanaume moja na muchumba yake, wenye walipenda kuowa.

Siku moja huyu kijana alienda safari mu Kisanga Kreta. Hila wakati huyu alilofa musulmani moja mkubwa ya nyumba ya mfalme ya Konstantinopoli alishangaa kwa uso na mwili nzuri ya muchumba yake na alienda kwa baba yake amumuombe juu ya bibi yake. Ku mwanzo baba yake alikataa, lakini ku mwisho aliitika, kwani huyu musulmani alimusuka nguvu. Aliharabisha uchumba na hule mwanaume wa Grekia na aliruhusa binti yake afanye ndoa na huyu musulmani wa turkie.

Wakati muchumba yake alirudia ya Kreta, alipata nyumbani yake barua moja ya muchumba mwanamuke yake na alimuelejea namna gani alimuacha kwa ajili ya kumusukuma nguvu huyu musulmani baba yake. Walizungumuza kukutana kila wakati. Lakini waliwapata na waliwahukumu kwa lufu wote wa wili, kwa sababu huyu kigana wa Grekia alikataa kugeuza imani yake na kufata imani ya umusulmani.

Hile siku ya kumaliza mpango ya nyumba ya uhukumu yao walimutosha huyu kijana ya buloko kwa kumufunga mikono yake mukongo na walimuweka pempeni ya singo yake na monyororo moja.

Wakati watu wingi walimuona huyu kijana mwanaume aende mu fasi ya kumuua, walisema ya kama ni zambi kupotea huyu kijana. Watu wote walimushauria kufata imani ya dini ya umusulmani. Lakini yeye aliwajibu:

-Hapana, misitageuze imani yangu!

Tena na huyu mukubwa musulmani, aliyebeba na ndoa muchumba ya hule kijana wa Grekia, alimuwaambia ya kama, kama atafata dini yake umusulmani, atamuacha kuishi na atamurudisha na muchumba yake juu ya kumubeba biba yake.

Lakini huyu kijana bila kuogopa, alimujibu ya kama alizaliwa ku wazazi waortodoksi, alibatizwa na alikomea mukristu na atakufa paka mukristu.

Hile saa walimutosha ku buloko na muchumba yake kijana mwanamuke na alitembea pa punda moja. Huyu alivaa mupila nyekunda, bila kitambaa pa kichwa yake, aliisha kutengeneza ma nywele yake, sawa namna ya wanawake wa musulmani, alivaa kolie pa sibgo na bintu ya masikio.

Aliliya sana. Aliomba kusuburia na muchumba wake. Alisimama mbele yake na aliliya sana. Kisha alimuomba kukana imani orthodokse na kwa mikono yake ni furaha mu uzima yao. Alimuomba saa mingi, lakini muchumba-mwanaume yake alimujibu:

-Hapana! Misitafanye hii tendo. Misitaache imani yangu. Nitakufa katika neema ya Mungu paka muorthodoksi. Ma sauti yako ni wa bure!

Walisikia ma sauti yake wanaume wa misulmani na walisirika na walimuchabula hivi:

-Weye uko mwenye mafigwa! Mutoaji! Walimufokea na kisilani. Imbwa! Juu ya nini unakana huyu mwanamuke muzuri?

katika ma sauti mabaya na matusi waliwapeleka pa hile fasi ya lufu yao.

Muchumba mwanamuke yake alimufata pa punda moja na aliliya. Pempeni yake wanawake wa misulmani walimubebelesha na walimutulivu.

Wakati walifika pa hile fasi ilipashwa kuteswa na kumutundika, walitosha manguo ya hule mwanaume mukristu na walimuacha paka na kapitula yake.

Kisha saa kidogo alimukaribisha na muchumba-mwanamuke yake. Aliomba kusuburia mara ingine naye. Alisuburia, lakini mwanaume-muchumba yake alikataa kumujibu. Kisha huyu muchumba yake alisirika na alianza kumufokea na kumulaana hivi:

-Imbwa! Mutoaji! Wa ebranie! Kufa, kwa sababu unataka kukufa! Nilitaka kuokolewa ku lufu, hiyo itakuja kwa ajili yako!

Wa askri ya misulmani, mukuona ya kama huyu kijana mukristu alikataa kufata dini yao, walipaza sauti kusema juu ya kumupigilia pa msalaba yake.. . .

Kisha ilikuja na mustari ya muchumba yake:

Mujukumu ya punda alimushusha ku nyama huu na alimufunga mukongo mikono yake. Na kamba ingine alimufunga kifuno yake na kamba ingine alimufunga miguu yake. Alimukokota ndani ya mutumbwi moja na alimupeleka ndani ya bahari. Alimusukuma ndani ya maji ya bahari na huyu binti alikufa..

Muchumba mwanaume wake alibakia pa msalaba wake ma siku tatu. Aliomba maji ya kunywa, lakini hata mtu moja hasikumupatia maji. Usiku wa tatu musulmani moja alimuwema pa hile fasi ya mateso yake na alimupika na bunduki yake na alikufa huyu mushahidi mupya. Vile iliisha mateso yake na alipanda nafsi yake mu Paradizo.

## Samaki ya Siku Kuu

Padri mkubwa ya monasteri ya Mt. Grigorio ya Mulima Takatifu, jina lake Simeoni, alikuwa na kitumaini kwa ulinzi na saidio ya mt. Nikolaos. Alisadiki ya kama Mtakatifu Nikolaos anasubuka juu ya mambo yote ya Monasteri yake, kuliko ya mwingine.

Mwaka moja ilikuwa karibu Siku Kuu yake, mu tarehe 6, Mwezi ya Kumi na mbili (Dekembrie) na wapadri wote walikuwa na sikitiko mingi. Matayarisho yote ya Siku Kuu yake ilikuwa nzuri. Lakini mupisi alikuwa na sikitiko kwa sababu hawakuweze kupata samaki ya kula.

Magaribi ya siku moja mbele ya Siku Kuu ya mt. Nikolaos walikuja kwa padri mkubwa wao:

-Ee Muzee, walimwaambia, tutafanya nini juu ya samaki? Hakuna samaki wa sasa, ya mubichi. Tutaweka pa maji samaki wa chumvi?

-Hapana! hapana! Musiwaze hii sauti. Tutapata ma samaki wa sasa. Mt. Nikolaos atasubuka juu ya Siku Kuu yake.

Usiku ilianza sala ya usiku: Apodipno, sala ya magaribi, sala ya Mikate wa tano, Somo ya ma zaburi wa sita (Eksapsalmos) na kisha wimbo moja ilifwata ingine.. . Wapisi walisuburia mara ingine na padri mkuwa yao, kwa sababu saa inatembea mbio. Itaanza Liturgia na kisha watu watakula nini? Tutaweka pa moto malaki?

-Hapana! hapana! Watakuja ma samaki.

Hii sauti ya padri mkubwa yao, hakuna namna kuisikia. Namna gani watakuja samaki? Na watakuja saa gani? Tazama, sala ya asubui ni katikati! Namna gani padri yao alikuwa na hii ukikisho?

Waimbaji waliimba wimbo ya Masifu ndani ya kanisa. Hile saa walisikia ma sauti wa furaha inje ya lupango ya monasteri. Alikuwa mutawa mujukumu ya kikavu. Alipaza sauti kusema kwa watu na watawa wengine:

-Wapadri, mushukeni mbio! Mubebe vituga na mushukeni! Mt. Nikolaos alifanya muujiza yake!

Mambo nini ilifanyika? Tufani moja ya bahari ilitupa inje samaki ningi munene! Ilikuwa zawadi ya Mungu! Watu wote walishangaa. Kabisa walishangaa wapisi, wenye hawakuweze kustaajabu nini: Muujiza ya mt. Nikolaos ao imani isiyona tengwa ya padri mkubwa wao?

## Kifungo ya chakula

Mwaka moja hali ya afya ya padri na mutawa Yoakim wa Ayananitis (toka mukini ya Mt. Anna ya Mulima Takatifu) haikukuwe nzuri. Padri mkubwa wake alimuita munganga.

Ufamio ya afya yake ilikuwa kibaya! Lufu yake ilipashwa kuja kisha miezi madogo. Huyu mugonjwa alipashwa kula nyama, samaki na mayayi.. . na, kama hii chakula, haikukuwe ndani ya Mulima Takatifu, alipashwa aende mu muji Thesaloniki ya kutafuta hii chakula. Tena munganga wake alimuwaambia kupumzika pa kitanda wake.

Padri Yoakimu alisikia ma sauti ya munganga bila woga. Wakati aliondoka munganga, aliita padri ya roho yake na alimwaambia:

-Ee Muzee wangu, unipe baraka yako nibakie ndani ya kanisa hii usiku. Ninataka kuomba kwa Mzazi-Munguna asubui tutasuburia tutafanya nini juu ya afya wangu.

Hule alijua kintu ingine na alimupatia baraka yake. Alifanya sala hile usiku padri Yoakim, na asubui alimuomba kwa padri wake:

Ninakuomba tusifate sauti ya munganga! Tutaacha mambo ya afya yangu kwa mikono ya Mzazi-Mungu, Mama wetu. Huyu atatengeneza hii mambo. Na, juu ya kusadiki sisi kwa saidio ya Mzazi-Mungu, katika baraka yako, nitaendelea kula hii chakula tuko nayo na hapana nyama, samaki na mayayi katika sauti ya munganga. Tena misitaweka ndani ya kinywa yangu kintu kimoja ya utamu. Vile atatukuzwa Mama wetu wa mbinguni.

Padri wa roho yake alishangaa mbele ya imani na nguvu ya roho ya mtoto wa roho wake. Alimupatia, basi, baraka yake, kwa sababu alijua wa zamani ma fazila na imani na nguvu ya p. Yoakimu.

Ilipita muda ya mwaka moja na kipande. Munganga alipenda kujua kama padri Yoakimu eko mu uzima ao alikufa.

-Anaishi na afya nzuri, alimujibu padri ya roho yake.

Munganga alitake kumuhamakia mwili na ugonjwa wake.

-Misione hata kintu kibaya kimoja, alisema na ushituko. Uko muzuri sana mu afya yako. Ninazania ya kama, kwa sababu ulikula nzuri, katika ma shauria yangu, sasa uliponyeshwa!

Padri mkubwa na p. Yoakimu walionana katikati yao na hawakuweze kusimama, bila kucheka. Wakati p. Yoakimu alijiepuka, padri ya roho yake alimuelejea kwa munganga namna ya uponyesho ya mtoto wake. Munganga alishangaa sana! Alisimama ya kufunga kinywa yake. Alistaajabu uwezo ya imani ya padri Yoakimu.

# U P O L E

## Muzee mupole

Wakati moja aliishi muzee moja mupole. Hii fazila yake ilikuwa hata munene na watu wote walimusifu sawa malaika ya Mungu!

Siku moja alienda mtu moja, katika shauria ya shetani, na alimuchabula mbele ya watu wote! Muzee alimuangalia na pasopo mingi na alimwaambia:

-Ee ndugu, ninakutakia neema ya Mungu aingie kinyuwani yako.

-Ndivyo, ee muzee mupotevu na mubaya na mwenye kula sawa nyama! .. . Aliendelea kumuchabula hule mtu. Hii sauti unasema juu ya kuonekana mbele ya watu ya kama uko mupole. Mudanganyifu!

-Kweli, ndugu wangu, aliitika padri muzee. Hii sauti unasema ni ya kweli!

Kisha ii tendo alimuuliza mtu mwingine:

-Ee Muzee, usitetemeke hata kidogo ndani ya akili na roho yako?

-Hapana! Alimujibu Avas. Nilisikia ya kama nafsi yangu aliifunika Mungu.

## Toba ya mulimaji

Kundi moja na watawa, wlaitembea na walipotesha njia yao na waliingia ndani ya shamba moja. Basi, watawa, bila mapenzi yao, walikanyanga mayani ya ngano.

Wakati aliwaona mulimaji, aliyetumika hile saa pale karibu, alianza kuwachabula na aliwaambia:

-Mweye muko watawa? Hamuogope Mungu? Kama mulikuana woga ya Mungu juu ya nini mulikanyanga shamba yangu?

Padri mkubwa ya hii kundi yao aliwashauria hivi:

-Musimujibu hata mtu moja, kwa jina ya Bwana.

Kisha alimujibu huyu padri vile:

-Uko na haki, mtoto wangu. Kama kweli tulimuogopa Mungu hatutaweze kufanya hii tendo kibaya.

Mulimaji aliendelea kusema matusi mengi mbele yao.

Kisha padri mkubwa alimujibu:

-Unasema kweli! Kama tulikuwa watawa wa kweli, hatukufanye hii kazi kibaya. Lakini, kwa mapendo ya Mungu, utuhurumie.. . .

Mulimaji alishangaa kwa upole na unyenyekevu ya hule padri, alianguka mbele ya miguu yake na aliomba hurumia.

## Asiye na shukrani mwenye kuomba saidio

Mwenye kuomba saidio moja alimukaribia patriarki wa muji Aleksandria, jina lake Yoano Murahimu (+619) na alimuomba saidio;

Hule alimuwaambia shemasi yake amupatie saidio mara moja. lakini hii makuta aliibeba haikumufurahisha. Ilikuwa kidogo. Alifungula hile saa kinywa yake isiyo na mulango na alimuchabula patriarki mbele ya uso yake.

Uzarau mbele yake ilikuwa munene! Watu wake walisirika na walikuwa wakali sana. Wanataka kumupiga huyu mwenye matusi. Wanataka kumukamata kwa kumutupa mara moja inje ya nyumba.

Lakini patriarki munyenyekevu alisimama na tabia ingine mbele ya hule mutu mubaya, aliyemuchabula sana! Alimuangalia na upole na utamu. Hasisirike hata kidogo. Hasisikie haya na uzarau. Na katika upole tabia yake alisema:

-Mumuache na ukimya huyu ndugu wetu. Mimi mpaka sasa niko na umri miaka 60 na ninazarau katika matendo yangu Yesu Kristu, lakini Yeye ananivumilia! Na sasa mimi, misipenda kuvumilia hii uzarau na matusi kidogo ya ndugu wangu?

Mtakatifu munyenyekevu na mwenye kuwa roho munene hasijue jivuno hata chuki ndani ya roho yake. Anajua kusaidia tena na wale watu wanamuchabula na wanamuchukia.

-Mumupatie, alisema kwa watu wake, na makuta ingine na mumuache kutoka na ukimya.

# M A O M B I

## Watawa wageni

Wakati nilibakia mu Skiti (mukini ya watawa), alitusimulia mt. mutawa Makarios wa Misri, niliona wakuje kwangu watawa wa wili wageni vijana. Moja alikuwa na ndevu, na pa uso yake ya mtawa mwingine sasa ilianza kuonekana ndevu. Basi walikuja kwangu na waliniuliza:

-Iko wapi chumba ya ava Makarios?

-Munamutafuta juu ya nini?

-Tulisikia matendo makubwa ya hule mutu na tulikuja tumuone.

-Mimi niko.

Waliweka metania na waliomba baraka yake.

-Tunataka na sisi tubakie huku, ee Ava.

Mimi, kwani niliona ya kama hawa watawa wageni waliisha kuzombelea na namna ingine ya teketeke maisha yao, niliwaambia:

-Hamutaweze mweye kubakia karibu yangu.

Kisha alinijibu hule mkubwa na namna nzuri:

-Kwani tusiweze kubakia huku, tutaondoka tuende mu fasi ingine.

Hile saa niliwaza na nilisema katikati ya roho yangu: «Juu ya nini nitawafukuza na hawa wataondoka na kuazo mbele yangu? Muchoko mingi ya uzima utawa wao karibu yangu itawafukuza. Basi, niliwaambia:

-Mukujeni na mujengani chumba yenu na mubakieni, kama munataka.

-Utuonyeshe fasi ya kujenga chumba yetu, walimwaambia.

Niliwapatia piki moja, mufuko moja na mukate na chumvi kidogo na niliwaonyesha jiwe moja mukusema:

-Mwanze kutumika huku. Mupeleke mbau. Mujengani ma chumba yenu na muifunike na muikaa ndani.

Mimi nilizania ya kama, wakati wataona hii muchoko mingi, wataondoka. Lakini wale waliniuliza mara ingine:

-Hapa watawa wenu kazi gani wanafanya na mikono yao?

-Wanafanya vituga na mayani ya palme ya kukauka, niliwajibu.

Nilibeba mayani ya kukauka na niliwafundisha namna gani watafanya kituga moja ao mufuko ao kintu ingine. Ku mwisho niliwauliza:

-Mufanye vitunga na mutaipatia kwa zamu na wale wataiuzisha na watamiletea makuta ao mukate na vitu vingine kwa mweye.

Vile niliwashauria na niliondoka.

Wale walifata ma shauria yangu yote. Lakini ya wakati miaka tatu hawakufike nitembelee hata mara moja. Basi, niliwaza na nilisema ndani ya mawazo yangu: «Namna gani wanatembea kwa mambo ya uzima yao ya roho? Juu ya nini, ilipita wakati urefu na bado kufika kwangu kuniuliza mambo yao? Watawa wengine wanakuja toka ma fasi mbali kabisa na hawa, wenye wanaikaa huku karibu hawakufike hata mara moja! Lakini na kwa muzee padri mwingine hawakufike. Wanakuja paka mu kanisa, wanasimama na unyamasha, wanakomunika na wanarudia nyumbani yao».

Nilifunga chakula ya juma moja na nilimuomba kwa Mungu anifunue kazi yao katika roho. Kisha nilisimama na nilienda mimi mwenyewe kuangalia wanaishi namna gani. Nilikokola mulango. Walinifungula na walinisalimia na unyamasha. Kisha sala tulifanya pamoja, niliikaa.

Mutawa mkubwa alimwaambia kwa mutawa mudogo kutoka inje na huyu aliikaa kuendelesha kazi yake na unyamasha. Wakati ilikuja saa ya kusoma Saa wa Tisa, alipika kengele na alikuja na ndugo mudogo. Alifanya chakula kidogo, alitayarisha meza ya kuweka mukate ya kukauka na alisimama na unyamasha. Hile saa mimi nilisema:

-Musimame tukule.

Tulisimama. Tulifanya sala. Alileta na chupa ya maji na tulikunywa. Karibu ya usiku, aliniuliza:

-Utaondoka?

-Hapana, nilimujibu. Nitalala huku.

Waliweka nguo moja ya kitanda toka mayani ya kukauka juu ya mimi na wale walilaria mu fasi ingine yulu ya mayani ya kukauka. Walitosha misipi na nguo ya Utawa wao (Skhima) na walilaria mu ngambo ingine.

Mimi nilimuomba kwa Mungu anifunua kazi yao wa roho na ma fazila yao. Na hile saa ilifunguliwa ufuniko ya nyumba yao na ilifanyika nuru sawa ilikuwa muchana! lakini wale hawakuione hii nuru. Wakati walizania ya kama mimi nililala, mutawa mkubwa alimusukuma

mwingine mudogo. Walivaa misipi na Skima ya Utawa wao, walifungula mikono yao kwa mbingu na walianza kuomba kwa Mungu. Mimi niliwaona, lakini hawa hawakunione. Hile saa niliona ma shetani wenye walikuja sawa ma inzi mengi pempeni ya mutawa mudogo: Ma shetani pempeni ya kinywa yake, beingine pempeni ya ma macho yake. Niliona na malaika wa Mungu aliyekuwa na kisu wa moto, aliyemuchunga huyu mutawa na alifukuza ku kwake ma shetani. lakini hule mutawa mkubwa ma shetani hawakuweze kumukaribia.

Wakati ilikuja asubui mapema, walilaria kupumzika.

Mimi nilifanya ya kama nililamuka na hawa walifanya hivi ya kama walilamuka. Mutawa mkubwa alifungula kinywa yake na aliniambia paka hii sauti:

-Unataka kuimba pamoja ma zaburi kumi na mbili?

-Ndivyo, nilimujibu.

Alianza hule mutawa mudogo kuimba ma zaburi tano pamoja na mistari na «Alliluya» moja. Kisha ya kila shairi (mustari ya zaburi) niliona ya kama ilitoka na taa wa moto moja ku kinywa yake na ilipanda mbinguni! Hii jambo umoja niliona na kwa mutawa mkubwa. Wakati alifungula kinywa yake aimbe, sawa kamba moja wa moto ilitoka ya kinywa yake na ilipanda mbinguni! Nilisema na mimi ma zaburi ingine. Wakati ilikuja saa ya kuondoka, niliwaambia:

-Muombeni na kwa wokovu wangu, ninamiomba.

Wale walinifanyishi metania na unyamasha.

Vile niliona ya kama huyu mutawa mkubwa alifika mu kipimo ya ukamilifu, lakini mutawa mudogo alimukombana tena adui-shetani.

## Mafundisho ya mutawa Evagrios

Mu Kitabu hile aliandika mutawa Evagrios wa Pontikos na inaitwa «Sura 153 juu ya sala» tunafata na hii ma jambo mazuri:

Wakati mutawa moja alinyanyua mikono yake yulu juu ya kumuomba kwa Mungu, shetani alimukombanisha sana na alionekana mbele yake sawa simba! Alisimama pa miguu yake wa mukongo na aliweka makucha ya miguu yake wa mbele ndani ya mwili ya hule mutawa wa jangwa juu ya kumusimamisha kwa woga na umivu sala yake.

Lakini mushindani ya Kristu, hasikusimamishe mikono yake, mbele ya kuisha hile sala alipenda kuifanya.

Jambo moja umoja ilifanyika na kwa mutawa Yoano aliyeitwa Kolovos.

Shetani alionekana na mfano ya nyoka murefu na aliikaa pempeni yake, alilumiza nyama ya mwili yake na alipepula hile saa ya sala yake.

Lakini huyu mutawa alikuwa hodari na hasikutoke ku hii ungano utamu pamoja na Yesu Kristu.

Mutawa mwingine tena, hile saa aliomba kwa Mungu, alimulumiza nyoka mwingine aliyekuwa na sumo! Lakini hasikushushe mikono yake mpaka aliisha hile sala alipenda kuifanya.

Na sumo ya huu nyoka katika saidio ya Mungu, haikuweze kufanya kintu kwa hule ndugu, aliyependa Kristu kuliko ya maungo yake.

Ma shetani wingi walionekana kwa mutawa wa jangwa moja aliyefanya sala kwa Mungu. Walimubamba na walimutupa pa pepo kama muviringo (futball), lakini ma shetani wengine walimupokelea mu ngambo ingine. Na hivi walicheza.

Hii mateso ya hule mutawa ilifanyika ya wakati ma juma wa wili! Lakini ma shetani hawakuweze kumutosha akili yake toka ono ya Mungu, kwani alimuungana naye katika sala wa moto.

Jambo ingine tunapata ndani ya hii Kitabu ya Mutawa Evagrios. Malaika wa wili walionekana kwa mutawa wa jangwa moja, aliyetembea mu jangwa na alisema na sala ya Yesu.

Huyu mutawa, aliona malaika wa wili mu fasi ya kuume na kushoto wake, lakini alikataa kusuburia na wao, kwa sababu hasitake kusimamisha ungano wa siri pamoja na Yesu Kristu. Ni kweli ya kama aliwaza ma sauti ya Mtume Paulo aliyesema: «.. . wala malaika, wala mamlaka, wala wenye uwezo, wala maneno ya sasa.. . hakitaweza kututenga na mapendo ya Mungu yaliyo ndani ya Kristu Yesu Bwana yetu» (Wa Roma 8, 38-39).

## Chumba iliyo lungua muzima!

Wakati moja walimuuliza padri Paladios, aliyekuwa toka muji Thesaloniki:

-Utuelejee, ee padri, sababu gani ulikuwa mutawa?

-Mu mukini yangu, aliwajibu huyu, kipande kilometre mbali ya kibabashi ya mji aliishi mutawa moja, jina lake Daudi. Aliisha kuja toka Mesopotamia (Iraki). Alikuwa mufazili sana, murahimu na mwenye kiasi. Alibakia ndani ya chumba yake na aliomba kwa Mungu karibu miaka makumi saba (70)! Hile wakati kibabashi ya mji Thesaloniki waliichunga wa askari kwa ajili ya ma adui mabaya.

Usiku moja wa askari wale walichunga kibabashi, hile ilikuwa karibu ya chumba ya hule mutawa, waliona ya kama toka ma didrisha ya chumba yake ilitoka ulimi wa moto. Waliwaza ya kama wa adui walikaribia na wlaiweka moto pempeni ya chumba yake. Asubui mapema, huler mutawa muzee alitoka inje ya nyumba yake muzima na chumba yake ilikuwa muzima! Wale wa askari walishangaa. Usiku ingine waliona mara ingine ulimi ya moto mu chumba yake. Hii mambo umoja ilifanyika na ma usiku ingine. Hii jambo wa ajabu waliijulishwa na watu wengine na kila usiku walikuja pale karibu kuona chumba ya padri namna gani ililungua. Hii jambo iliendeleshwa mpaka mufu ya mutawa muzee.

## Mpadri mupole

Askofu moja wakati fulani alitembelea mikini ya njimbo yake na alifika na kwa mukini moja wa mbali kabisa. Alitafuta kuona padri. Kisha saa ya kuenea alikuja mbele yake mtu moja wa mukini mupole, aliye hile saa aliisha kurudia ku shamba yake na alikuwa na manguo ya kazi yake. Huyu alikuwa padri ya mukini! Askofu hasikufurahi, wakati alimuona. Alitaka mutumishi ya Mungu kuwa na mavazi mazuri na ono nzuri.

Siku ingine ilikuwa siku ya Mungu. Padri alitayarishwa juu ya kufanya Liturgia. Askofu alikuwa pa kiti yake katikati ya kanisa na alimuangalia huyu padri namna gani atafanya Liturgia yake. Alitumainia ya kama atapata makosa filani yake.

Lakini hakuna kosa! Tangu mwanzo ya Liturgia Kimungu pempeni ya mwili ya padri ilikuja mawingu moja wa moto na alimujaza na mwangaza, pasipo kumulungua! Na hii tendo wa ajabu ilikuwa mpaka mwisho ya Liturgia yake!

Wakati alikabula antidoro kwa waaminifu waka huyu padri, alimuita askofu wake ingie mu Altari Takatifu. Askofu alipika magoti mbele ya mpadri mupole wake na alimuomba amubariki. Padri mupole alishituka:

-Namna gani iko namna mpadri mkubwa atabarikiwa ku padri mudogo yake? Ee Rabi, weye unibariki.

-Hakuna namna kubariki mimi huyu anayeikaa katikati ya moto kimungu na anatoa Sadaka isiyo na damu, alimujibu askofu wake.

-Ee Rabi mtakatifu, eko padri ao askofu ao tena na shemasi, mwenye anakaribia Altari Takatifu na hasikuje pempeni yake hii nuru kitakatifu? Alimuuliza na ushituko huyu padri mupole.

Sasa askofu atajibu nini kwa hule mpadri aliyeona hii nuru kimungu ya kila mu Juma? Alisthaajabu usafisho na utakaso ya roho yake na aliondoka ku mukini yake na faida munene ya roho yake.

## Miti marefu wa wili

Mama mkubwa (IGumeni) ya monasteri Khrisovalantu ya muji Konstantinopoli, jina lake mt. Irini (milele (karne) wa tisa) aliendelesha sana kazi ya sala. Mara mengi alifanya sala mpaka ma saa 20-24! Mikono yake aliinyanyua mbinguni ma saa mengi na kisha mutawa mwingine alienda kuishusha kwa sababu walikuwa nguvu na mt. Irini hasikuweze kuitengesha.

Mara mengi alitembea usiku mu lupango ya monasteri yake na aliomba kwa Mungu kwa siri. Aliona ma nyota, hali nzuri ya ulimwengu na alifurahi na alimutukuza Muumba.

Usiku moja alikuwa mu lupango mutawa mwingine mwanamuke na aliona ono moja wa ajabu: Mama mkuwa wake, mt. Irini aliomba, lakini miguu yake walikuwa yulu ya inchi! Ni kusema alikuwa pa pepo karibu metre wa wili! Miti wa wili marefu waliisha kuinamisha chongo yao mpaka chini, mbele ya mt. Irini na walibakia hivi mpaka aliisha sala yake mt. Irini! Hile saa mt. Irini aliigusa, aliibariki ya kufanya alama ya msalaba pa chongo yao na kisha hii ma miti walirudia pa fasi yao wa zamani.

Hule mutawa mwanamuke aliyeona hii ono wa ajabu alianza kutetemeka. Kwa sababu hii tendo wa ajabu ilionekana saa ya kuenea, alienda mbio mu chumba ya mama mkubwa wake. Na, wakati aliona ya kama ilikuwa wazi, alisadiki ya kama huyu mutawa mu lupango alikuwa mama mukubwa wake!

Na hile saa hasikuseme kintu. Lakini usiku ingine mt. Irini alifungu pa kila chongo ya kila muti na moja kitambaa. Siku ingine asubui watawa wanawake wengine waliiona ma kitambaa pa chongo na walishangaa, nani alipanda yulu na alifunga hii kitambaa? Hile saa huyu Dada aliyeona hii tendo wa ajabu, aliwaelejea namna gani ilifanyika hii tendo kitakatifu. Mt. Irini, wakati alisikia ya kama watawa wake walisuburia hii jambo wa ajabu aliwaambia hapana kuendelesha kuisuburia.

Mutawa mt. Parthenios

Mtakatifu mutawa Parthenios wa Kisanga Khios (1815-1883), wakati alikuwa mutawa kijana, alipenda kuishi mu jangwa inayeitwa Penthodo ya monasteri Mupya ya Khios. Padri mkubwa, jina lake Meletios Fluras alikataa amupatie baraka na tena alifanya na tendo ingine. Alimuita mtu wa police, aliyekuwa na dini musulmani, aende kumubamba hule mutawa kijana na atamurudisha ndani ya Monasteri yake.

Huyu mtu wa police, alikuwa mtu mupole. Alienda na ma silaha yake yote na alimukuta mutawa kijana.

-Weye uko mutawa fulani? Weye unafanya hii tendo mubaya na unakataa kuikaa ndani ya monasteri yako? Monasteri yako iko wapi?

Mutawa alimuonyesha pango moja mu kilima moja na ndani ilikuwa na kanisa moja kidogo.

-Ole, ole. Maneno hapa unaishi na umaskini hii?

Mutawa alisikia kikomo ya hule jemadari ya inchi. Hasikupende majaribu ndani ya usiku. Jemadari aliitika na alimuuliza:

-Na mimi nitabakia wapi hii usiku?

-Pale, ndani ya pango.

-Hapana pale. Pango ya mulima inasukuma roho yangu.

-Unataka hapa ndani ya kanisa kidogo?

-Ninataka. Lakini nitalala inje. Ndani iko zambi. Ndani utalala weye. kanisa iko yako.

Walikula chakula kidogo na jemadari alitosha ya ngochi yake na alimupatia kwa mutawa kidogo kinywaji, inaitwa raki.

-Mimi misikunywe, alisema mutawa.

-Mimi iko namna nikunywe, kwa sababu hapa ni na Mzazi-Mungu?

-Ndivyo, unaweza kunywa.

Alikunywa kidogo na alilala. Katikati ya usiku alilamuka. Alisikia makelele kidogo. Alikaribia kanisa, aliona na tundu moja na alishituka. Mbele ya moto ya mishumaa mutawa alimuomba kwa Mungu. Lakini hasikukuwe chini ya inchi na uso yake ilijaza na nuru upole! .. . Aliisha kunyanyua mikono yake na hii nuru kimungu iliangaza pempeni yake. Kisha saa kidogo alinamisha mikono yake. Nuru ilikimbia. Huyu mutawa aliomba juu ya maungo yake na aliliya, aliria sana.. . Na huyu mutu wa askari alisikia hii maombolezo yake, iliyetoka pamoja na ma sauti ya sala yake.

Asubui mapema, alitoka huyu mutu wa askari mwenye kushituka sana, wa pekee, pasipo kumubeba na mutawa. Hakuna namna wakati ingine kwa kumuuzi.

Askofu alishituka:

-Eko wapi mutawa? Alimuuliza.

-Ee Rabi mkubwa wangu, huyu mutawa ni mtu wa Mungu, alimujibu huyu mkubwa wa askari na alimuelejea hii matendo yote aliona mu pango yake.

Askofu alisikia. Alisikia hii jambo alitaka kujua. Sasa alituma mtu mwingine amuletee mutawa mu muji.

Alienda na alimuletea mu muji. Askofu alimuuliza:

-Weye uko mutawa Parthenios?

-Mimi, alimujibu hule mutawa na alipika magoti na alibusu mukono yake.

-Wanakushitaki.. .

-Wekona haki. Hii njimbo ni yao.

-Unafanya nini pa mulima?

-Ninaomba.

-Kwa nani mtakatifu unamuomba?

-Kwa mt. mutawa Simeoni wa Theologo mupya.

Jina ya mtakatifu Simeoni alimutetemesha askofu na alimujibu:

-Hule aliona nuru kimungu na weye unaiona huu nuru?

-Mimi ni mutu wa zambi, alimujibu padri Parthenios na alikuwa karibu ya kuliya.

Askofu alimuangalia na pasopo mingi. Aliona ya kama huyu mutawa eko ndani ya roho yake nguvu moja wa Mungu. Aliona mwanagza pa uso yake. Alisimama, alimubusu na alimujibu:

-Muzuri, mtoto wangu. Uende muzuri.. . Tembea sawa vile unajua kutembea na unikumbuke na mimi mu sala yako.. .

## Mama moja wa mukini ya inchi Rumania

Asubui moja ya siku ya Mungu padri wa jangwa Kleopas Ilie alikuwa ndani ya Altari Takatifu ya kanisa ya monasteri yake, na alisoma Ibada ya Komonyo Takatifu. Kisha saa kidogo aliingia ndani ya kanisa na mama moja toka mukini moja ya inchi Rumania, aliyekuwa ku usiku mu Monasteri. Aliingia kufanya sala.

«Alibusu ma Picha (Ikone) wote na aliweka metanies mbele ya kila picha, alituelejea padri Kleopas. Huyu mama hasikujue ya kama alikuwa mtu moja ndani ya kanisa. Nilimuangalia ya kuendelea ku Mulango Bora, tangu hile saa aliingia ndani. Wakati huyu mama alibusu ma picha yote, alisimama kati ya Kanisa, alinyanyua mikono yake na alisema na roho yake hii ma sauti:

-Ee Bwana, usiniache! Ee Bwana wangu, mupendwa Bwana wangu, usiniache!

Hile saa niliona nuru moja kimungu na niliogopa! Huyu mama alianguka na uso yake chini na aliomba kwa siri. Hii mawingu aliyemufunika ilinenepa na kisha pole-pole ilikimbia. Wakati huu nuru kimungu ilizimisha, alisimama hule mama na alitoka inje ya Kanisa. Alikuwa mama moja toka wa mukini wetu.

Tazama, basi, neni eko na zawadi ya sala wa Mungu! Waaminifu wanapitisha kwa sala yao sisi watawa! Mimi kisha, alisema p. Kleopas, nilifanya Matayarisho ya Matoleo (Proskomidi) na kwa ajili ya furaha hile nilisikia nilianza kuliya na nilitetemeka. Paka Mungu anajua watu wa ngapi wanamutukuza katika ma fazila na sala yao! »

# **A K I L I**

## Ndugu muzaifu

Mu Juma moja mt. Mutawa Makarios alikuja mu Skiti ya watawa juu ya kusikia Liturgia. Kule, inje ya nyumba moja ya mutawa moja aliona kundi moja munene ya ma shetani. Wengine walikuwa sawa wanawake na walisuburia mubaya, wengine walikuwa sawa vijana, wenye walisema matusi ya mbali-mbali na wengine ma shetani walikuwa na mifano na ma tabia ya kuachana. Mt. Makarios aliyejua hii ma jambo yote, aliomboleza mukusema:

-Bila shaka huyu ndugu, mwenye anaikaa ndani ya hii chumba, anaishi bila kusopoka uzima ya roho yake joo vile ma shetani walikuja inje yake na wanafanya matendo mabaya!

Kisha Ibada ya Liturgia alienda nyumbani yake hule mutawa na alimusema:

-Niko na sikitiko mingi, ndugu wangu, kwa sababu ninaishi na uzaifu. Lakini nikona kitumaini kwa weye na ninajua nzuri ya kama, kama weye utaomba juu yangu, Mungu atakusikia na atanitosha majaribu na mawazo yangu mabaya.

Hule mutawa alimuweka metania na alimujibu:

-Ee Muzee, mimi misi na stahili kuomba juu ya weye.

Lakini mt. Makarios alimuomba afanye sala juu yake na alimusema:

-Misitoke ku huku, kama weye utakataa nipatie malako yako ya kama kila usiku utafanya sala juu yangu.

Huyu ndugu aliitii mu amri yake. Na hii amri mt. Makarios alimupatia sawa mwanzo juu ya kuanza yeye afanye sala na ya uzima na wokovu wake.

Basi, huyu mutawa usiku alilamuka na alifanya sala juu ya kusaidia mtakatifu Makarios. Wakati aliisha hii sala, alisikia furaha munene na haya pamoja. Alisema kwake:

--Nafsi yangu upotevu! Uliomba kwa Mungu juu ya hule mtakatifu mkubwa na unakataa kusali juu ya uzima na wokovu wako?

Vile, alifanya juu ya maungo yake sala mingi. Na hii namna alipita juma moja. Ni kusema kila usiku alilamuka alifanya sala juu ya mt. Makarios na kisha juu yake.

Mu Juma mukutembea Kanisani mt. Makarios aliona ma shetani waliikaa inje ya chumba ya hule mutawa, lakini walikuwa na sikitiko mingi! Alifurahi, kwa sababu alijua ya kama ma shetani walisikitika kwa ajili ya hile sala alifanya huyu mutawa. Alienda mu chumba yake mara ingine na alimwaambia:

-Fanya mapendo, ndugu wangu na ongeza na sala ingine kila usiku juu ya saidio yangu.

Usiku, wakati alifanya sala ingine juu ya Mtakatifu huyu mutawa alisikia furaha mingi ndani yake na alisema na akili yake:

-Ole wako, nafsi yangu upotevu! Usipende kuongeza na sala moja juu yako, kwani na weye uko na lazima munene?

Na hii namna, nikusema kila usiku alifanya ma sala wa wili ya Mtakatifu na sala wa wili ya nafsi yake; vile ilipita na juma ingine.

Mu Juma mukutembea kule mt. makarios aliona ma shetani ya kama walikuwa na sikitiko na unyamasha! Alimushukuru Mungu. Alienda nyumbani ya hule mutawa na alimuomba

aongeze kila usiku na sala ingine juu yake. Nas huyu ndugu aliongeza sala moja ya Mtakatifu na sala ingine ya maungo yake na hivi alifanya ma sala sita kila usiku.

Wakati mu Juma ingine alikuja Mtakatifu kuona huyu mutawa, ma shetani walisirika juu yake na walianza kumuchabula, kwa sababu waliona na sikitiko mingi wokovu ya hule mutawa. Mt. Makarios alimutukuza Mungu juu ya endeleo na wokovu ya hule mutawa. Tena alimushauria hapana kusimamisha sala na kisha aliondoka.

Hile saa ma shetani mukuona mapendo ya sala ya hule mutawa, walikimbia ya chumba yake.

## Ndugu mwenye kufanya amani

Watawa wa wili walikuwa na katikati yao chuki kimoja kidogo. Wakati moja, mutawa moja aligonjwa na aliita mutawa mwingine juu ya kusaidia masikilizano na mutawa mwingine, kwani aliogopa ya kama itakuja lufu.

Alirudia huyu mutawa mu chumba yake na aliomba kwa Mungu amuangazie atafanya nini, pasipo kuharabisha hii makankamano ya masikilizano yao. Kisha sala yake, ndugu mwingine alimuleta kitunga moja na matunda. Alibeba hii matunda na alipeleka kwa hule mutawa, ndugu ya mutawa mwingine mugonjwa.

-Ee padri, alimusema, hii matunda anakutuma mutawa fulani.

Huyu padri alishituka:

-Kwangu alituma hii matunda?

-Ndivyo, alimujibu ndugu.

Hule alipokelea matunda na alimushukuru huyu ndugu aliyemuletea. Alifurahi huyu mutawa, mwenye kufanya amani na matunda, kwa sababu aliona ya kama hii namna ilienda nzuri. Kisha alibeba ingine matunda na alipeleka kwa mutawa mwingine mugonjwa.

-Hii matunda, anakutuma mutawa fulani, alimusema:

-Unasema nini? Basi, tulisikilizana? Alimuuliza na furaha huyu mutawa mugonjwa.

-Ndivyo, ava, na baraka yako, alimujibu ndugu.

-Utukufu kwa Mungu, alisema na furaha hule mugonjwa.

Vile, paka ya matunda kidogo, akili na mapendo ya hule ndugu mwenye kufanya amani, ilifanyika masikilizano ya wale watawa wa wili.

## Mutawa moja aliomba kufanya miujiza

Mutawa moja wa kwanza mu uzima ya utawa toka jangwa Thivaida ya Misri, bila kubeba baraka, alifanya ushindani ya roho mingi. Lakini mbio akili yake ilijaza na mawazo ya majivuno. Shetani alimuwaambia ndani ya akili yake:

-Ulifika mu kipimo murefu ya utakaso na watu wengine hawataweze kufika pa hii kipimo yako! Uko sasa stahili kubeba zawadi ya kufanya miujiza na hivi Mungu atatukuzwa kwa ajili ya miujiza yako.

Basi, huyu mutawa alimuomba kwa Mungu amupatie hii zawadi. Siku moja aliwaza kuomba shauria ku mutawa moja wa jangwa mufazili. Ilikuwa mapendo ya Mungu, juu hapana kupotesha michoko yake! Mutawa kijana alimufunua mawazo na sala yake juu ya kumustahili Mungu afanye miujiza. Kisha alimuomba amushaurie. Padri ya roho alimusikia bila kusema sauti. Alisikia ugonjwa ya roho yake, lakini alinyamasha. Hule mutawa kijana alimuomba amupatie sauti na shauria yake. Alibakia saa mingi na unyamasha ku mwisho hivi huyu padri ya roho:

-Mtoto wangu, ninaogopa kukushauria, kwa sababu niko na ukikisho ya kama hautanisikie.

Ndugu alimulaka ya kama atachunga sauti yake, sawa atamwaambia Mungu.

-Beba hii makuta, alimusema padri ya roho, hile aliitosha ku kazi yake. Uenda mu muji na nunua kumi kilograme nyama, mukate kumi na vinyo kumi litre.

Ndugu alishituka. Alitaka nini hii bintu ya chakula huyu padri wa roho? Lakini hasikuweze kukataa, kwa sababu aliisha kulaka ya kama atamutii kila shauria yake. Aliondoka na sikitiko. Namna gani yeye mutawa ataenda mu magazine kununua nyama na vitu vingine? Watasema nini watu wengine, wenye watamuona?

na haya mingi alinunua hii bintu na alirudia kwa padri ya roho.

-Ulinilaka, alimusema padri ya roho, ya kama utafanya kila tendo mimi nitakuwaambia.

Huyu mutawa kijana aliisha kutubu juu ya malako yake, lakini hasikuweze kufanya kintu ingine.

-Beba hii bintu mu chumba yako, alimuhamuru padri ya roho, na kula kila siku mukate moja, nyama litre moja na utakunywa na vinyo litre moja. Kama itaisha hii yote rudia kwangu nione.

Ndugu alirudia bila utulivu mu nyumba yake.. . Aliisha kufanya kifungo ya chakula mingi na sasa atakula nyama na atakunywa vinyo?.. . . Aliwaza na aliuliza akili yake: «Juu ya nini alinifanyishia hii mambo padri ya roho? Alikuwa na matakio ya kukanyanga malako yake, lakini alikumbuka ya kama atachunga malako yake mbele ya padri ya roho. Hile wakati ilikuja saa ya kula, alilobana mukate na machozi yake! Alisema kwa maungo yake ya kama ni mutu mupotevu na mwenye zambi na aliwaza ya kama Mungu alimuacha! Mukuona Mungu unyenyekevu wake, alimuangaza akili yake ya kusikia ku wapi ilikuja malipizo. Kisha ma siku kumi alirudia kwa padri ya roho na roho yake iliisha kuvunjika. Alishituka padri ya roho, wakati alimuona ya kama alikonda sana, lakini alikula chakula nzuri kila siku!

-Mtoto wangu, alimuwaambia na wema na mapendo, umushukuru Mungu, kwani hasikuache roho ya jivuno kukamata akili nha roho yako. Shetani eko nayo hii fundi juu ya kuharabisha wokovu wako. Kama shetani hasitaweze kumutupa mutawa kwa uzaifu na uvivu, atamutupa mu ngambo ingine na atamupatia mutumwa kwa majivuno. Na sasa nitakufunua niliona nini, wakati ulikuja huku mara ya kwanza. Ma shetani wa wili na uso ya makaka walikufata na kila moja alikombana akukokote mu ngambo yake. Walikuwa ma roho ya jivuno na utukufu wa bure. Sasa wamekimbia. Pahali pa hile fasi, basi, utaomba toka Mungu kufanya miujiza, kuliko nzuri iko kumushukuru, kwani alikuokoa ku matego ya shetani. Hii ni muujiza kupita kubwa na wa faida munene.

Ndugu alimushukuru hule padri ya roho juu ya hii ma shauria yake na alirudia nyumbani yake na unyenyekevu.

## Makutano ya muji Tiros

Mu uzima yake yote patriarkis wa muji Aleksandria, jina lake mtakatifu Athanasios (295-373) alikombana kupigana wale watu walifata mafundisho ya uwongo kwa imani ya Kristu. Kwa hivi aliitwa «Nguzo ya Orthodoksia».

Miaka kumi kisha Makutano wa Kwanza, wakubwa ya mafundisho ya uwongo ya kama Yesu Kristu hana Mungu; ni paka kiumba ya Mungu, walikombana na walimusukuma mfalme ya Konstantinopoli kufata fundisho yao ya uwongo na walimushauria afanye makutano ingine mu muji Tiros ya Palestina, juu ya kufamia mafundisho yao.

Makutano mu muji Tiros ilifanyika mu mwaka 335. Mu mazungumuzo wa pili, ilifanyika jambo moja wa ajabu ili inatuonyesha hekima na akili ya mt. Athanasios.

Pa hile saa walizungumuza, ilifunguliwa mulango na aliingia ndani mwanamuke moja na maombolezo na machozi mingi.

Aliomboleza na alipaza sauti kusema ya kama, aliisha kumulaka kwa Mungu aishi uzima ubikira, lakini mt. Athanasios aliingia nyumbani yake juu ya kumukaribisha na alimubamba na alifanya zambi ya mwili pamoja naye! .. .

Musangao munene na umivu mingi ilijaza roho ya askofu wote mbele ya huyu mwanamuke kijana. Ma macho yao walipigiliwa kwa mt. Athanasios, aliyeangalia chini, bila kutaka kusikia ma sauti ya hule binti. Hile saa mpadri Timotheos aliyekuwa pempeni ya mt. Athanasios, alimuuliza huyu mwanamuke:

-Mimi nilikuja nyumbani yako? Mimi nilifanya zambi ya usharati na weye?

-Ndivyo, weye! Alipaza sauti nguvu. Weye uliharabisha uzima ubikira yangu. Weye ulitosha uzima safi yangu! .. .

Tena huyu mama, alitenga na kilole kwa mpadri Timotheos, kwa sababu alisadiki ya kama huyu alikuwa mt. Athanasios! .. .  Kwa sababu patriarki hasikumuona mara ingine.. .

Mambo ndani ya makutano ilikuwa munene. Wa adui ya mt. Athanasios walimuripa huyu mama mwenye zambi juu ya kusema sauti ya uwongo kupigana yake, kwa ajili ya chuki yao. Mt. Athanasios aliisha kujua hii mutego ya wa adui yake na aliita rafiki yake padri Timotheos juu ya kutengeneza namna ya kuharabisha hii mutego yao.

Wakati huyu mwanamuke alisikia kosa yake, ilikuwa ya kuchelewa.. .  Alianza kupotesha akili yake, alianza kusema ma sauti ingine na ingine, hasikuweze kujibu. Wa adui kwa imani ya mt. Athanasios, walimutosha huyu mama inje ya makutano. Mt. Athanasios alisema mbele ya wa askofu wote kumuchunga huyu mama juu ya kumuhukumu na kusema nani alimutuma huku. Lakini wa adui wake walikataa na walimutosha inje. Tena walisema ya kama watafunua na matendo ingine mabaya kabisa hile alifanya mt. Athanasios na wa askofu wote watasadiki ya kama huyu (mt. Athanasios) ni mtu mwenye zambi.

Hile usiku mtu moja mugeni, aliyekuwa musafiri, aliingia mu muji Tiros. Mara moja alienda nyumbani ya patriarki wa Misri.

Nani alikuwa huyu? Alikuwa mutu aliyemutuma Maaguzi ya Mungu hile saa ya muzuri. Ushindi ingine munene ilikuwa tayari ya mt. Athanasios.

Siku ingine makutano ilifanyika mara ingine. Wakati wa askofu wote waliikaa pa kiti yao, sanduku moja walileta ndani ya hii nyumba ya makutano. Ukimya ilikuwa ndani ya hii chumba.. .  Ma macho yao ilikuwa pa hile sanduku.

walifungula sanduku na ndani ilikuwa mukono moja muzima ya mtu fulani.

-Ee Athanasios, walimusema wa adui wake kwa imani. Hii mukono inakushitaki sana! Ni mukono ya askofu Arsenios. Utujibu sasa safi juu ya nini uliikata:

Wa adui wake walianza kufokea na kusema matusi na ma sauti mabaya kupingana ya mt. Athanasios. Huyu mtakatifu aliikaa na unyamasha pa kiti ya mukosefu. Kisha saa kidogo alisimama, aliwaambia kufanya wote ukimya na aliwauliza:

-Eko huku mutu moja, mwenye anajua askofu Arsenios?

Wa askofu wingi walimukikisha ya kama walimufamia tangu zamani.

Mt. Athanasios aliita mtu mwake moja aende kuleta kwake hule mutu mugeni jana usiku alikuwa nyumbani yake. Na tazama, iliingia ndani huyu mtu mugeni. Kichwa yake aliinamisha chini na uso yake haionekane. Mwili yake aliifunika na ngochi moja murefu. Huyu mugeni anaikaa kati ya makutano. Mt. Athanasios alikuja karibu yake, alipandisha kichwa yake yulu. Sauti moja ya ushituko ilijaza nyumba ya makutano yao.

-Huyu eko mutu mimi nilikata mukono yake? Huyu eko askofu Arsenios na mimi nilikata mukono yake?

Ndivyo, huyu alikuwa askofu Arsenios! Hasikuweze hata mutu moja kuishaka. Funjo munene ilianza ndani ya hile fasi. Wa adui ya Mt. Athanasios hawakuweze kusimama pale hata dakika moja. Walikimbia. Lakini patriarkis hasipende kuisha hii jambo na haraka. Alitembea ku askofu Arsenios. Alifungula kanzo yake na alitosha mikono yake wa  wili inje. Alionyesha mbele ya wa askofu wote mikono wa kuume na kushoto, na alisema:

-Ninazania ya kama hakuna hata mtu moja, mwenye anataka kuona mukono na wa tatu.. . Ninazania ya kama Mungu alitupatia mikono wa wili! .. .

Ufunuo hii ilikuwa munene kabisa! Fundisho ya kweli ya imani ya Kristu ulitukuzwa mara ingine.

### Uponyesho ya upenzi ya maungo yetu

Askofu ya Kiru, jina lake Theodoritos (393-460) anatusimulia hivi: «Wakati moja mama yangu aligonjwa mu richo yake moja na waganga hawakuweze kumusaidia.

Hile wakati alimutembelea rafiki yake mwanamuke moja na alimwaambia juu ya mt. mutawa Petros mwenye kimya. Alimujulisha ya kama na bibi ya mkubwa ya sehemu ya inchi wa Mashariki alikuwa na hii malari na hule padri alimufanyishia muzuri katika sala yake.

Mama yangu alimusikia sauti ya rafiki yake na mara moja alienda kwa mtu ya Mungu. Kwani alikuwa mwanamuke wa hii dunia, alivaa bintu ya mikono na singo na masikio wa zahabu. Mpaka hile wakati hasikujue uzima wa roho. Alikuwa mu kipimo uzana na alifata ma zoezo ya hile wakati.

Mt. Mutawa Petros, wakati alimuona, aliponmyesha ya kwanza malari ya utukufu wa bure yake, mukusema kwake:

-Kama mutu moja mwenye kufatula atafanya kibao moja nzuri na kisha atakuja mtu mwingine na ataweka ragi ingine na watu wengine pa hii kibao, hule mutu mwenye kufatula wa kwanza atasikitika ao hapana, kwa sababu mtu wa pili aliharabisha kibao yake?

-Ndivyo, atasikitika, alisema mama yangu.

Vile na Mungu wetu, mwenye eko Muumba wetu. Anasikitika, kama mweye wanawake munaweka ragi meushi ao nyekunda ao ragi ingine pa gozi na pa uso yenu. Vile munachabula hekima na nguvu ya Mungu-Muumba wetu. Lakini munapashw akujua ya kama Mungu eko na hekima na nguvu afanye kila kintu muzuri sana. Basi, musiharabikeni mweye sura ya Mungu, wala kuongeza bile bintu Muumba wetu hasikuweke kwa sisi.

Alisikia hii sauti yake mama wangu na alishangaa hekima ya mt. Petros. Kisha alipika magoti mbele yake na alimuomba kuponyesha na richo yake.

Hule, hile saa alimwaambia ya kama na huyu eko mtu sawa huyu mama, ya kama eko uzito mingi pa ribeka yake juu ya zambi zake na hakuna uwezo wake mbele ya Mungu. Lakini, kwa sababu mama yangu aliliya na alikataa kuondoka, muzee alisema ya kama paka Mungu ataweza amupatie uponyesho yake na paka Huyu anatimiza maombi ya wale wanamuamini na wanakimbilia Kwake.

-Basi, atakupatia afya yake, alimujibu, hapana kwa sababu atasikia Mungu sauti yangu, lakini, kwani anaona imani yako.

Aliweka, kisha mukono yake pa richo yake na mukufanya alama ya msalaba, mara moja alimutunza!

Wakati mama yangu alirudia nyumbani yetu, alitosha bile bintu aliisha kuweka pa uso na singo yake na kisha alivaa manguo katika shauria ya mt. Petros. Na alifanya hivi, wakati mama yangu alikuwa na kipimo miaka 23. Hata mingi alipata faida mu roho yake ku mt. Petros na alichunga ma shauria yake mpaka mwisho ya uzima yake.

Aliomba uponyesha ya mwili na Mungu alimupatia na uponyesha ya roho yake, kwani alikuwa na roho wazi na unyenyekevu na utii.

## Hekima ya kuchunga watoto wa roho

Padri mkubwa na mtakatifu Yoano wa muji Kronstandi, alianza kazi mu ushirika ya muji Kronstandi na watoto wamaskini. Kisha walimufata watu wakubwa. Pole-pole watu walimukaribia juu ya kuzungumuza mambo yao.

Mwaaminifu moja anasimulia hii jambo yake: Siku moja nilirudia nyumbasni yangu na nilikuwa mulevi kidogo. Niliona ndani padri moja, aliyekamata mtoto wangu pa mikono yake na alisuburia naye. Mara moja nilitaka kumuchabula.. . Ma macho ya hule mpadri (alikuwa padri Yoano) ilikuwa ya kujaza na mapendo na upole na wema. Nilisikia haya. Nilinamisha uso yangu chini, lakini huyu aliangalia ya kunyolola ndani roho yangu. Alianza kusema. Misitaweze kusema alinishauria nini. Alinisema ya kama ndani ya nyumba yangi ni paradizo, kwa sababu pahali popote ni watoto, pale ni paradizo na haipashwe hii paradizo kuikombola na simoko ya magazine. Huyu padri hasikunishitaki juu ya hii uzima mbaya nilifanya. Huyu aliondoka na mimi nilibakia wa pekee na unyamasha. Misikuliya. Halafu nafsi yangu ilikuwa sawa aliliya.. . Bibi yangu aliniangalia na ushituko. Na tazama tangu hile siku mimi nilifanyika mtu ya Mungu».

Jambo ingine: Mtu moja mwenye biashara alikuwa balaka, (bibi yake aliisha kufa) na aliishi paka na mtoto moja mudogo mwanaume. Kwa ajili ya sikitiko yake alianza kunywa kinywaji. Ilimufwata hasara mu kazi ya biashara yake na bila kuwaza muzuri alifika kuwa mulevi. Siku moja alimukuta padri Yoano, alimusema ya kama alikuja paka kwake na alianza amushaurie ya kusimamisha kinywaji:

-Inenee mpaka sasa kuzuguluka ma njia bika kutumika. Zamani ulikuwa mutu muzuri. Unapashwa kufanyika mara ingine mutu muzuri.

Kisha alisimama, alivaa epitrakhilion yake na alimusema:

-Juu ya kuwa mwanzo moja nzuri mu uzima yako tunapashw asisi kuomba kwa Mungu.. .

Na alianza kuomba.. .

«Huyu padri, alisema huyu mtu mwenye biashara, alimuomba kwa Mungu na machozi juu ya mimi mwenye zambi. Kisha alibariki mimi na mwanaume wangu. Alitulaka ya kama atatutembelea mu nyumba yetu na ataomba kwa mungu juu ya sisi.. Nilisikia ya kama nililamuka ku musingizi moja yenye uzito sana. Nyumba yetu niliipenda sana sasa. Na machozi ya toba nilimumbatia mtoto wangu.. . Kazi ya biashara ilitembea sasa nzuri na mimi nilikuwa mutu mupya.. . ».

Binti moja alizania maungo yake upotevu, kwa ajili ya ma sababu mengi toka miaka ujana wake. Tangu hile wakati alipotesha mama yake, alisikia maungo yake yenye taabu na isiyokitumaini na alianza kutundikwa. Siku moja alikuwa mu muji Kronstandi na mawazo mabaya ilijaza akili yake na aliikaa mu fasi moja ya kiwanja ya hile muji. Hile saa padri moja mugeni, asiyemufamie alimukaribia na aliikaa mu ngambo ingine ya hile kiti urefu.

«Mimi nilisimama na nilitaka niondoke, anasimulia huyu binti, lakini padri mugeni alinisimamisha na alisema:

-Munihurumie.. . . Misikuweze kuvumilia hali kibaya ya nafsi yenu na kwani niko padri, nilikamata mpangu kumikaribia.. . Muniambie taabu yenu. Iko namna Bwana Yesu katika mimi mwenye zambi, amisaidie na amitulivu.. .

Mimi nililiya mingi, lakini misikuweze kusema sauti moja, paka sauti moja:

-Niko mwenye taabu na asiye kuishi ndani ya hii dunia.

-Akili kubwa ya Muumba wetu hakuna namna kuumba kintu hata kimoja mu dunia, bila kuwa lazima na bila kutumika, alinijibu huyu padri».

Kisha hii jibu huyu binti alianza kusuburia. Huyu padri katika mapendo wa kweli alimupatia nguvu.

## Mutumishi wa kanisa mugonjwa

Padri mkubwa ya monasteri ya mt. Grigorio mu Kilima Takatifu, jina lake Athanasios, alikuwa mkubwa juu ya akili na hekima yake.

Usiku moja shetani alimwaambia pa masikio ya mutawa moja aliyekuwa mujukumu ya kanisa ya monasteri yake:

-Mara ingine utalamuka usiku na utapiga kengele na mbau? Utaharabisha musingizi utamu yako? Kila usiku utapata hii mateso? Ulichoka tu! Umuache kupiga kengele mutawa-musaidizi yako. Sema weye ya kama uko mugonjwa. Pumuzisha tena mwili yako.

Kisha saa kidogo alikuja musaidizi yake-mutawa mwingine na alimuuliza:

-Ee Padri I. mambo gani iko? Juu ya nini unachelewa? Saa ilipita.

-Ndugu wangu, misiweze! Misisikie muzuri. Niko mugonjwa. Piga weye kengele na mbau (kopanos).

Wakati alipiga na mbau wa tatu (talanto) watawa wote walishuka mu kanisa, walikamata kila moja kiti yake na Ibada ya asubui ilianza. Padri I. alishindwa ku shetani ya uzaifu na sawa mwenye kupooza alikuwa ndani ya kitanda yake. Hii usiku aliwaza ya kama «atazimba» musingizi!

Mutawa-musaidizi yake alimuelejea kwa padri mkubwa juu ya nini analofa padri I. Padri mkubwa, kwani alikuwa na akili safi, alisikia ya kama sababu yake ilikuwa ingine. Alitengenza namna ya kumuponyesha hule mutawa «mugonjwa».

Watawai wingi walishangaa, wakati waliona ya kama walitoka inje wapadri wengine ya kuvaa manguo matakatifu wao. Lakini walienda wapi? walienda mu chumba ya mutawa «mugonjwa».

-Tulikuja sisi wote juu ya kufanya Sala Maji ya Baraka na Fumbo ya Mafuta Takatifu, alimwaambia padri mkubwa.

Hule mutawa «mugonjwa», alishituka; ao alitaka ao asikutake alilaria pa kitanda na alisikia ma Ibada ya malari yake. Alisikia mubaya kwa hii jambo. Ibada iliendelea na huyu mwenye «malari» zamiri yake ilimulumiza. Sikitiko na huzuni ya roho ilijaza mu nafsi yake. Aliogopa ya kama kwa ajili yake inachekelewa ma Fumbo Matakatifu. Hii uwazo ilimuletea bikelele mingi mu roho yake.

Kisha saa kidogo iliisha sala ya maji ya Baraka na itaanza Fumbo ya Mafuta Takatifu! Hile saa, hasikuweze kuvumilia. Alilamuka na alisimama ku kitanda yake.

-Hapana! hapana, ewe wa padri! Musifanye Fumbo ya Mafuta Takatifu. Inenea. Nilitunzwa. Niko muzuri sana! Ninashuka mara moja sasa mu Kanisa. Misi na kitu.

Hii ilikuwa mambo yake. Iliisha. Hakuna namna huyu mutawa kusikia ma sauti ya shetani ya kama alichoka na anapashwa kupumzika tena! Tangu hile siku hakuna namna kusema uwongo ya kama eko mugonjwa!

## Ma jibu yenye nuru

Mu mukini  Mathia (Draga) ya Mesinia ya inchi Grekia alizaliwa padri arkim. Yoil Yanakopulos (1901-1966). Tangu kipimo yake ujana alifamia mwenye jangwa Ilia Panagulakis, aliyemusaidia kijana Yoil afate uzima ya Kristu na uzima utawa.

Mu mwaka 1925 alibeba kartasi ya masomo wa Thaologia. Mu mwaka 1929 alipadirishwa mpadri na mara moja alikuwa na mwalimu ya masomo ya inchi yetu.

Kisha miaka kidogo alirudia mu muji Kalamata na alianza kuandika vitabu-ufafanusho ya Madiko Takatifu. Mu uzima yetu tunapata ma jambo ya mbali-mbali, hile inatuonyesha hekima ya akili yake.

Wakati fulani mtu moja wa mukini alimuelejea kwa padri Yoil ya kama hasikuweze kusikilizana na ndugu yake:

-Misiweze, padri wangu, kusuburia mimi wa kwanza. Nduvu wangu, huyu anapashwa nisuburie na mimi ya kwanza! Huyu eko mukosefu. Misi na mimi! Tena huyu eko mudogo lakini mimi ni mkubwa wake.

-Uniseme sasa, alimuuliza padri Yoil, nani eko mkubwa: Sisi ao Mungu?

-Iko lazima kuniuliza? Mungu eko mkubwa.

Na nani eko mukosefu: Sisi tuko wakosefu mbele ya Mungu ao Mungu eko mukosefu mbele ya sisi?

-Sisi tuko wakosefu mbele yake.

-Na nani alifanya mwanzo ya sikilizano? Sisi tulienda kwa Mungu ao Mungu alikuja kwa sisi?

-Mungu alikuja kwa sisi.

-Basi?

Basi.. . Aksanti mingi! Mukona haki. Mimi nitaenda wa kwanza kwa ndugu mudogo wangu!

Mtu mwingine asikuweze kusamehe ndugu mwingine. pasdri Yoil alimushauria:

-Unapashwa kufunda muzuri sala: «Baba yetu uliye mbinguni.. . ».

-Padri, hii sala: «Baba yetu uliye mbinguni.. . » ninaijua tangu hile wakati nilikuwa mtoto mudogo.

-Unajua ya kuisema, lakini hauijue ya kuisikie maana yake.

-Nikusema:

-Haujue ni gani maana yake! Unaisema kwa bure, bila kusikia unasema nini. Kama ulisikia na maana yake, ilikuwa teketeke kuhurumia na ndugu yako. Kama unataka Mungu akuhurumie makosa yako, mbele unapashwa weye kuhurumia ma kosa ya ndugu wako. Hii neno: «utusamehe ndeni zetu, kama sisi vile vile tunavyosamehe wa deni wetu» inatuonyeshe hii maana. Basi, fanya nguvu ya kusikia maana ya hii sala.

Mwanamuke moja muzee, umaskini na mugonjwa, alimuuliza:

-Ni zambi, padri, kama mimi ninatakia ifike lufu kwa mimi?

-Kama unatakia lufu, alimujibu p. Yoil, kwa sababu unataka kuokolewa ku mateso na magumu ya hii uzima, hii ni zambi! Kwa sababu unaliya kupigana ya Mungu, anayeturuhusa hii mateso mu uzima yetu. Lakini, kama unatakia lufu juu hapana kufanya ma zambi ingine na hapana kumutaabu Mungu, hii haina zambi. Tena, kama unatakia lufu, kwa sababu usiweze kuvumilia uchanisho ku Mungu na unataka kuenda mbio karibu Yake, hii matakio yako ni ubarikiwa!

Baba moja alimuuliza padri Yoil:

-Juu ya nini, ee padri, unashauria ma binti wetu wafate uzima utawa?

-Mimi misishaurie, alimujibu hule padri. Lakini tena misizibiye. Matakio ya uzima utawa mimi misiwaka na misizima. Misiwaka, kwa sababu misiweze. Paka Roho Mtakatifu anaweza kuwaakisha matakio ya hii uzima. Lakini, misiweze hata kuzimisha matakio ya hii uzima, kwa sbababu haipashwe. Nani niko mimi juu ya kuzimisha hii moto anawaakisha Mungu?

-Kama weye usiwasukume ma binti wetu wafanyike watawa, namna gani unafafanusha hii mambo ya kama ma binti mengi wanaungama kwako na kisha wanataka kufanyika watawa?

-Ulizo yako itakuwa kupita nzuri kama utaniuliza hivi: «Juu ya nini ma binti mengi, wenye wanataka kufanyika watawa, wanakuja na wanaungama kwako?». Mimi hivi nitaweza kukujibu: «Kwa sababu mimi, sawa yote mweye munajua, misizibiye mtu moja anayependa hii uzima». Wanakuja, basi, kwangu, kwa sababu wanajua ya kama mimi misitawafukuze na misitazimishe matakio yao. Unasikia?

Wakati ingine padri Yoil alisafiri na mashua. Mu usimamisho moja ya mashua, alisikia ya kama mu hile mukini fulani ndani ya kanisa ilifanyika muujiza moja: Ikone moja alitosha machozi! Mara moja watu wasafiri wote walitoka inje ya mashua na walienda mbio kuona hii muujiza. Paka padri Yoil alibakia ndnai ya mashua, aliyesoma kitabu moja!

Wakati wasafiri walirudia, hule mtu aliyeikaa mu ngambo ingine ya padri, alimuuliza:

-Weye padri usisadiki kwa miujiza?

-Mimi ninasadiki, alimujibu padri na kwa hivi haina lazima kuona ya kusadiki muujiza moja. Weye usisadiki! Na ulienda kuona muujiza moja kusudi kusadiki. haina vile? Uniseme sasa, kwani uliona muujiza moja, ulisadiki sasa?

Mtu moja aliyefata kundi ya politiki hile watu wanakana Mungu (Komunist) alimuwambia kwa padri:

-Na Kristianisme, padsri wangu, ni system sawa Komunisme. Mu sehemu ya ushirika hakuna uchanisho. Wote wa wili wanataka uzima umoja, mapendo katikati ya wa ndugu wote na uhaki wa ushirika.

-Lakini iko uchanisho moja, alimujibu padri Yoil:

-Ni nani uchanisho?

-Kristianisme anasema kwa ndugu wake: Juu ya nini inapashwa kuana weye bintu na hapana huyu mtu mwinmgine? Basi, umupatie! Lakini Komunisme anasema kwa ndugu wake: Juu ya nini inapashwa kuwa na bintu huyu na hapana weye? Basi, beba bintu yake! Ulisikia uchanisho?

Mwalimu moja ya masomo wa pili alisema kwa padri Yoil:

-Padri wangu, ninazania ya kama haina muzuri sisi ya kama tunapashwa kufanya tendo nzuri juu ya kuingia mu Paradizo na kuokolewa toka mateso ya gehena. Tendo moja kizuri tunapashwa kuifanya paka kwa ajili ya mapendo ya Mungu.

-Weye, alimuuliza, padri Yoil, wakati uliweka daraja kwa wanafunzi wako, unatimia paka na 0 na 20? Usitimie na ma daraja ingine?

-Kweli nikona yo na ma daraja ingine. Ninatimia na ma daraja yote kutoka zero mpaka 20. Hawa wanabeba daraja yulu ya hesabu 10 wanaenda mu daraja ingine. lakini wengine wanabakia pa hii daraja mwaka wa pili.

Na Kristianisme eko na mugazi ya ma daraja yake. Wale wanatumika kila kazi, kwa sababu wanapenda kumaliza mapenzi ya Mungu, watapanda pa fasi ya kwanza mu Paradizo. Wale wanafanya kazi kizuri juu ya kuingia mu Paradizo wataikaa pa fasi kidogo chini ya wengine wenye yulu. Na wale wanafanya kazi kizuri juu hapana kuingia mu gehena watabeba fasi ingine kidogo chini. lakini hii ma cheo yao wa tatu ni yulu ya daraja 10, nikusema hawa watu watakuwa ndani ya Paradizo na ma fasi ya kuachana! Weye, kama unataka, kombana kuikaa mu fasi ya kwanza ya paradizo. Hakuna mutu moja ya kukuzibiya. Lakini, angalia na mapendo wale wa ndugu, wenye wanakombana hata kuikaa mu fasi wa tatu ndani ya paradizo!

# UNYENYEKEVU

## Mwenye zambi «wa pekee»

Mu akili ya mt. Mutawa Antonio Mkubwa ilipita uwazo moja, hile wakati aliishi mu jangwa ya Misri, alifika mu kipimo ngapi ya mtakatifu moja. Mungu, mwenye alitaka kunyenyekesha uwazo ya jivuno yake, alimuonyesha mu ndoto yake usiku moja ya kama mtakatifu mkubwa kupita yeye alikuwa mtu moja, mushoni ya vilato, aliyetumika mu magazine moja, ku mwisho ya muji Aleksandria!

Wakati ilikuja asubui mapema, mt. Antonio alibeba bakora yake na aliondoka aende mu muji. Alitaka kumufamia huyu mushoni ya vilato na kuona ma fazila yake. Na ugumu mingi aliingia mu magazine yake. Aliingia ndani na alianza amuulize juu ya uzima wake.

Huyu mutu mupole hasikuweze kujua nani alikuwa huyu mutawa, aliyekuja kwa rafla amutembelee. Bila kuchofesha ma macho ya hii kazi yake, alimujibu na namna upole na pole-pole:

-Misijue, ava wangu, ya kama mimi nilifanya tendo kimoja kizuri mu uzima yangu. Kila asubui ninalamuka, ninafanya sala yangu na ninaanza kazi yangu. Lakini ninasema ya kwanza ndani ya akili yangu ya kama hawa watu wa muji hii wataokolewa na paka mimi nitahukumiwa kwa zambi zangu zote. Na wakati usiku ninaenda kularia pa kitanda, paka hii sala umoja ninafanya.

Mt. Antonio alisimama na musagao, alimumbatia, alimubusu na alimwaambia na furaha:

-Weye, ndugu wangu, sawa mwenye biashara muzuri, ulipata zahazu kubwa, biula muchoko. Mimi nilizeka mu jangwa. Nilitosha jashu na nilichoka, lakini misikufike pa hii kipimo ya unyenyekevu yako.

## Mtakatifu mutawa mwanamuke Isidora

Mu monasteri ya Taveni ya inchi Misri waliishi watawa wanawake kupita ya 400 na katikati yao aliangaza kwa fazila wake mutawa Isidora. Huyu mwenye heri alidanganya ya kama alikuwa mazimu kwa mapendo ya Kristu. Alichabula na alichekeza kila siku maungo yake. Alivaa manguo wa bure. Alifanya ma kazi wa bura ya monasteri. Alisaidia sawa mutumwa wa dada wengine, bila kukataa kwa dada moja fulani.

Wale watawa wengine, sawa walitaka kumulipa ya hii saidio na mfano yao, walimuzarau na toka kanisa tena walimufukuza. Vile Isidora alikula hii chakula iliisha kubaki ku mwisho ya kila meza, karibu ya moto ya upisi. Na ma Ibada ya Kanisa aliisikia kwa kuikaa pa mugazi ya kupanda mu kanisa.

Hakna namna kupitisha siku moja, bila kumuchekela na kumuuzi. Na huyu aliipokelea kila uzarau na ufukuo na mucheko yao. Hasikuseme sauti ingine hata siku moja. Hasikufanye funjo ao makelele katikati yao. Alifanya uvumilia munene.

Na mungu alifufunua fazila yake!

Mu Mulima ya hile ngambo ingine aliishi mutawa moja wa jangwa, jina lake Pitiruni. Aliishi na mateso mengi na alichokesha mwili yake. Siku moja ilikuja kwake hii uwazo: Eko mtu mwingine duniani, anayefanya fazila kuliko mingi ya mimi?

Usiku alikuja mu ndoto yake malaika ya Mungu na alimujibu:

-Lamuka na uende mu monasteri ya wanawake fulani. Kule utapata dada moja bikira na taji pa kichwa yake! Huyu mutawa ni kupita mkubwa ku weye.

Avas Pitiruni hasikupoteshe wakati. Asubui mapema aliondoka aende mu monasteri hii. Watawa wanawake walimupokelea, kwani huyu alikuwana tangazo ya kama alikuwa mtakatifu pa hile inchi. Avas alienda mu kanisa na alisema kwa mama mkubwa awaite watawa wanawake wote juu ya kuwafamia moja-moja. Mama mkubwa alumutimiza matakio yake. Basi, watawa wote walipita mbele yake, waliweka metania, wlaibeba baraka yake na walienda mu kiti yao. Hule aliwaangalia muzuri, lakini bado kuona hule alikuwa na taji pa kichwa yake, sawa vile malaika ya Mungu aliisha kumwaambia.

Wakati alipita mbele yake na dada wa mwisho, aliuliza padri hakuna dada mwingine?

-Hapana, walimujibu, sisi wote tuko huku.

-Hakuna namna, aliwajibu padri. Inapashwa tena kuwa na mwingine dada. Mimi kwa ajili yake nilikuja huku.

-Tukona tena na dada moja, lakini yeye ni mazimu.

-Umuita akuje na yeye.

Walimusukuma afike mbele yake na huyu dada Isidora. Alikuja bila bilato, manguo yake ya kuharabika sana, na simoko ilijaza uso yake, kwani alisaidia ndani ya upisi. Wakati padri alimuona, alishangaa. Hii kitambaa ilikuwa pa kichwa ya huyu dada Isidora, ilijaza mbele ya ma macho ya padri sawa zahabu! Alinamishwa mbele yake na alimusema na sauti wa heshima:

-Unibariki, mutawa mtakatifu.

Lakini Isidora munyenyekevu alipika magoti na alibusu miguu yake.

-Weye unibariki, padri mtakatifu.

Watawa wanawake wengine walishangaa kwa hii zungumuzo yao na walimwaambia kwa padri Pitiruni:

-Usizarau hivi maungo yako. Huyu ni mazimu!

Lakini padri aliwaangalia na macho makali:

-Mweye muko mazimu na wapumbafu! Huyu dada hapa ni kupita mkubwa mbele yenu na mbele yangu. Ninatakia Mungu atustahili sisi kusimama pempeni yake mu hile siku ya Uhukumu ya Mungu.

Kisha aliwaalejea alimufunua nini Mungu juu ya huyu mwenye heri Isidora.

Wakati walisikia hii ma sauti yake watawa wengine, walipika magoti, waliomba hurumia ku dada yao na waliungamwa kwa padri juu ya hii matendo yao mabaya walimufanyishia mpaka hile siku.

Mt. Mutawa alifanya sala Mungu awasamehe matendo yao mabaya hile walifanya kwa dada yao isidora. Kisha alimuita Isidora juu ya kumuomba kusamehe na huyu ma dada wake. Walimutafuta, lakini hakuna namna kumupata. Alipata wakati na alikimbia ku monasteri yake juu ya kufukuza sifa ubinadamu na hata mtu mwingine hasikujue fasi wapi aliisha uzima wake.

## Kumukanyanga na miguu askofu moja

Askofu ya njimbo moja, wakati moja alianguka mu zambi moja munene. Siku ingine ilipaswa kufanya Ibada ya Liturgia Kimungu, pahali ilikuwa siku Kuu ya kanisa na pale watakwenda waaminifu wingi.

Wakati aliingia mu kanisa askofu alipanda pa Kiti ya kuhubiri. Toka hile kiti alijiungama mbele ya waaminifu wake yote. Alitosha Omoforion yake (Nguo ya upadirisho ya uaskofu), aliipatia kwa shemasi yake na taabu mingi alisema hivi mbele ya watu wote:

-Kisha hile zambi nilifanya, misiweze sasa mimi kuwa askofu wenu! Mweye munapashwa kuchagua askofu wenu mupya.

Alipima ya kuondoka. Lakini watu walimupenda na walimuzibiya.

-Bakia mu kiti yako na zambi zako, tunatakia ikuje yulu ya vichwa vyetu, walipaza sauti na walimwaambia wote.

Askofu alivunjika roho yake kwa hii mapendo ya taifa wake. Alipanda mara ingine pa kiti ya kuhubiri na alipaza sauti aseme:

-Kama munataka nibakie pa hii cheo yangu, mutafanya hii kazi mimi sasa nitamiaambia:

Alihamuru kufunga mara moja milango ya kanisa na itabakia wazi paka mulango moja mudogo. Alianguka chini katikati ya mulango hii na alisema nguvu mbele wa waaminifu wake wote:

-Mutapita yote mweye yulu yangu. Mutanikanyanga, kama munataka kuokolewa. Kama munakataa, hamutapate fasi ya furaha mu paradizo!

Wakristu walishituka. Lakini, kwa sababu walitaka kumuchunga karibu yao askofu yao, waliitika. Moja-moja mukristu alitoka inje na alikanyanga yulu yake. Wakati alipita na mukristu wa mwisho, ilisikiwa sauti toka mbingu kusema:

-Kwa ajili ya unyenyekevu yake munene, zambi zake ilisamehewa.

## Uwazo uwovu isiyona haki

Shemasi moja toka Monasteri ya mt. Gerasimos ya Palestina, alianza kuonyesha tabia wa baridi mbele ya ndugu yake mwingine. Hule, wakati aliona hii tabia yake, alienda mbio amuulize ya mambo gani. Shemasi alimujibu ya kama aliisha kumufanya tendo kimoja kibaya zamani.

Ndugu alisikitika na alimukikisha ya kama hasikumufanyishie kazi kibaya zamani. Tena, siku moja, wakati shemasi alisimama na Kikombe kitakatifu pa mikono yake, inhe ya Mulango Bora, alimukaribia huyu ndugu na alimulaka ya kama zamiri yake ilikuwa safi. Shemasi, lakini, alikataa kusadiki.

Hile saa mutawa, kufatana maneno ya Watakatifu wapadri, alianza kuwaza:

-Shemasi ananipenda na kwa hii mapendo yake kubwa, alikuwa na nguvu anionyeshe alifuchika nini ndani yake juu ya mimi. Alifanya hivi juu ya kusopoka mimi ku mbele hapana kufanya kazi ingine kibaya. Lakini, nafsi yangu upotevu, unakataa ya kama ulifanya hii matendo mabaya, lakini ulifanya ingine matendo mabaya mingi na uliisahabu! Zambi hile ulifanya jana ao mbele ya miaka kumi iko wapi? Unaikumbuka? Hapana, kweli. Basi, iko namna kuwa na hii kazi kibaya, lakini uliisahabu, sawa ulisahabu na matendo yako ingine wa zamani.

Vile huyu mutawa munyenyekevu alitengeneza roho yake sawa kweli aliisha kumushitaki shemasi na alisahabu uzulumu. Tena, alianza kumushukuru Mungu na ndugu yake, kwa sababu alistahiliwa kujua kosa ya tendo yake na alitubu.

Na hii mawazo yake alisimama na alienda kwake amuombe hurumia na amushukuru. Lkini, wakati alikokola mulango ya nyumba ya shemasi, alimufungula hule na alimuweka metania (kupika magoti) mukusema:

-Ndugu wangu, unihurumie, kwa sababu nilijilanda ku shetani na nilichunga ndani ya akili yangu uwazo uwovu kupigana yako. Mungu alinijulisha ya kama weye usiwe hata ujukumu moja.

## Kosa ya mtu moja wa mukini

Mtakatifu Sergios wa Rantonezi (1314-1342) alijivaa ma siku zote na manguo mabaya. Kwa hivi na wale watu walikuja mu monasteri, hakuna namna kumufamia. Mtu moja wa mukini toka mukini moja wa mbali, alisikia sauti mingi kwa hii mtakatifu. Basi, alitakia kumuona. Alikuja mu Monasteri yake na alianza kuuliza eko fasi wapi juu ya kumukuta. Walimwaambia ya kama alikuwa mu shamba. Alienda ma shamba na aliona kule mutawa moja mupole, aliyevaa manguo mabaya ya kujaza na kilako mengi na alichibula bulongo. Aliongojea kuona padri mkubwa moja ndani ya utukufu na sifa yake. Basi, alirudia mu monasteri na alianza kuomba:

-Muniseme, eko wapi padri muzee ya monasteri yenu? Nilikua ku mukini wa mbali kabisa na ninataka kubeba baraka yake.

Wa ndugu walimujibu:

-Huyu aliyekuwa mu shamba, huyu eko padri mkubwa wetu.

Mtu wa mukini alisikitika sana. Wakati padri mkubwa yao alirudia ku shamba, huyu mutu wa mukini alikataa, hapana kubeba baraka yake, lakini hata kumuona. Aliwaza hivi: «Nilichoka nifike huku juu ya kuona nabii moja mutukufu na sasa ninaona mutawa moja mskini na kuvaa manguo mabaya sana.. . »

Mtakatifu mwenye nuru alisoma mawazo yake na alimushukuru Mungu, kwa sababu, kama mtu mutukufu wa bure anafurahi juu ya ma sifa na masauti ya utukufu, mtu munyenyekevu anafuraha paka mbele ya ma taabu na mazarau. Lakini, kwa sababu alimupenda hule mtu wa mukini, alimuita karibu yake, alimutoa chakula na alimwaambia wa furaha:

-Ee ndugu, usitaabu. Kisha saa kidogo utaangalia huyu mtu, kwa ajili yake ulikuja huku.

Wakati mtakatifu Sergios alisema hii ma sauti yake, alikuja mtu moja, mwenye tangazo na alimwaambia ufikisho ya mkubwa ya inchi mu monasteri yake. Mtakatifu alisimama na alitoka inje amupokelee mkubwa ya inchi yake, aliyekuja na kundi ya wakubwa wake. Mutawala mukuona mtakatifu Sergios, aliweka metania mbele yake ku mbali na aliomba baraka yake. Mtakatifu alimubariki na alimuongoza ndani ya monasteri na sifa. Waliikaa moja karibu na mwingine na walisuburia, lakini kundi ya wakubwa wake walisimama inje!

Huyu mtu wa mukini hasikuweze kusadiki pa ma macho yake. Huyu aliyemubusu na heshima alikuwa mutawala ya inchi yake, lakini huyu (mtu wa mukini)mumoja wa pekee alimuzarau na alikataa kuomba baraka yake. Na woga kidogo aliuliza mutawa moja:

-Ee Ndugu wangu, nani eko huyu anayeikaa karibu ya mutawala?

-Usimufamie? Huyu eko Igumeni Sergios, mkubwa padri wetu.

-Kweli nilipotesha nuru ya ma macho yangu na misikumufamie Muzee! Alihukumu maungo yake huyu mtu wa mukini.

Alikaribia kisha na haya mingi mu roho yake, alimubusu, aliomba hurumia juu ya hii mfano mubaya yake. Hule mtakatifu alimushauria:

-Usitaabu! Unapashwea kufurahi kwa sababu paka weye uliwaza muzuri juu ya mimi. Wengine watu wanajilanda, kwa sababu wanasandiki ya kama mimi niko mtu moja mkubwa.

Mtakatifu Sergios alifurahi kabisa kwa hii uzarau ya hule mtu wa mukini na hapana kwa ma sifu ya mutawala. Huyu mtu wa mukini, hata mingi alishangaa kwa hii unyenyekevu tabia ya mt. Segios na kisha wakati fulani alikuja mara ingine na alifanyika mutawa.

## Patriarkis moja muchungaji ya ma punda

Mtakatifu askofu mkubwa Nifoni wa Pili alikuwa patriarki mu muji Konstantinopoli mara pili (1486-1489) na (1497-1498).

Kisha wakati wa pili yake sawa patriarkis alienda mu Rumania na alikuwa padri na muchangaji ya ma roho yao, kwani aliisha kumuita mkubwa ya inchi jina lake Radulos. Lakini kule alivumilia mafukuzo, kwa sababu alihamakia zambi ya usharati ya mkubwa moja.

Basi, aliacha Rumania na alikuja mu monasteri yake ya mt. Dionisios ya Mulima Takatifu, pahali zamani alikuwa pale mutawa. Alivaa manguo wa zamani na wa maskini. Alionekana mbele ya watawa na unyenyekevu sawa mutawa wa kwanza na aliomba kuwapokelea mu Kundi ya watawa wao. Alisema ya kama jina lake ilikuwa Nikolaos.

Katika desturi ya hii monasteri, ilipashwa huyu mtu wa kwanza kutumika ya miaka tatu mu kazi ya kuchunga ma punda na kupeleka bintu yote ya ma nyama! Huyu patriarkis wa Konstantinopoli aliitika na mapendo mingi afanye hii kazi na ma nyama ya Monasteri.

Lakini haikupite wakati mingi na mt. Yoano Mutangulizi na Mubatizaji, mulinzi ya hii monasteri, alikuja kwa ndoto ya padri mkubwa na alimwaambia na mfano mukali:

-Mpaka wakati gani mutakuwa na patriarki wa Konstantinopoli muchungaji ya ma punda? Mpaka wakati gani atatumika na ma nyama wasiyoakili, huyu aliyeokoa watu wingi na aliwapeleka mu Ufalme mbinguni? Lamuka mbio, sanyika watawa wote na mwende kumupokelea sawa vile ni desturi mu upadirisho ya uaskofu wake. Padri mkubwa (Igumeni) alishituka na aliogopa sana. Alimuuliza mt. Yoano nani eko patriarkis?

Kisha mt. Yoano Mubatizaji alimujibu:

-Huyu anayetumika ma nyama na jina Nikolaos, haina mutawa wa kwanza. Huyu eko patriarkis mkubwa ya Konstantinopoli na ulimwengu ya Orthodoksia muzima. Inenea, basi, unyenyekevu yake na malaika walishangaa sana!

Padri mkubwa, wakati alilamuka, alisanyika kundi ya watawa wote na ma mishumaa na ma taa ya kuwaakisha walimupokelea mtakatifu Nifon, hile saa yeye alirudia ku mulima na kuni pa ma nyama yake. Walimupokelea na sifa mingi na waliomba baraka yake.

Pa hile fasi walimupokelea, walijenga wakati ingine na moja Proskinitari (sawa kanisa kidogo na kandili moja), sawa ukumbusho ya unyenyekevu kubwa ya mtakatifu Nifon.

# U t i i

## Mtoto wa roho asiye kusema

Kijana moja mwamuzi toka muji Antiokhia aliendа mu mutawea moja wa jangwa na alimuomba amuchunge na amufanyishie mutawa. Basi, Muzee alimusema:

Kama unataka mimi nipokelee, uende na uuzisha bintu yako yote ao uwakabula kwa maskini katika amri ya Bwana Yesu.

Ndugu aliondoka na alifanya katika satui ya padri muzee. Kisha muzee alimusema:

-Unapashwa kuchunga tena na amri ingine: Usiseme hata sauti moja.

Na hule aliitika! Vile ilipita wakati na miaka tano, bila kutosha sauti ya kinywa yake! Hile wakati walianza kumusifu watu wengine. Kwa hivi alimuwaambia Muzee, padri ya roho yake:

-Hapa usiweze kupata faida ya roho. Nitakutuma mu monasteri, mu inchi Misri.

Na alimutuma kule. Lakini alimuhamuru kuchunga amri ya kunyamasha.

Padri mkubwa, aliyemupokelea, alitaka kumupima kama kweli ni bubu ao hapana. Basi, alimutuma afanya kazi kimoja. Juu ya kufika kule alipashwa kutambuka mutoni moja ya kujaza na maji. Vile, ilipaswa wakati atarudia, ya kama hasikutambuke mutoni kwa ajili ya kuijaza na maji.

Tena alituma na mutawa mwingine mukongo na kidogo mbali ya kumuona atafanya nini. Huyu ndugu, asiyekusema sauti moja, wakati alifika mu mutoni, kwani hasikuweze kutambuka, alipika magoti yake. Alikaribia hile saa mamba moja na alimupeleka mu ngambo ingine ya mutoni!

Hule mutawa aliyemufata ku mukongo, wakati aliona hii muujiza, alikimbia mbio kwa padri mkuwa wake na alimwaambia hii jambo wa ajabu; Waliisikia hii jambo watawa wote na walishangaa!

Kisha wakati fulani alikufa huyu mutawa asiye nakusema sauti na padri ya hii monasteri alimutangaza padri wake wa roho wa kwanza: «Ulitutuma weye mutawa-bubu, lakini huyu ni malaika ya Mungu».

Na padri wa roho yake alimuwaambia ya kama hasikukuwe bubu, lakini alichunga amri yake, hile aliisha amupatie tangu mwanzo ya uzima utawa wake.

## Maombi ya Muzee (padri wa roho)

Muzee moja wa jangwa alikuwa na musaidizi yake moja ku mukini wa karibu pale na huyu alimusaidia ya kila mambo yake. Lakini siku moja huyu musaidizi alichelewa akuje kwa padri na hivi vitu vya chakula ya hule padri iliisha kuisha. Ilimubamba lakini taabu, kwa sababu hakuna namna kuishi mu jangwa, bila bitu ya kula. Basi alisema kwa mtoto wa roho yake:

-Unataka kwenda mu mukini fulani juu ya kumutangaza musaidizi yetu atuletee chakula?

-Muzee wangu, nitafanya katika sauti yako, alimujibu hule mtoto, bila kuwaza majaribu gani atapata mu hile mukini kule.

Alichelewa kidogo ya ma siku kumi karibu huyu muzee, kwani alitumainia ya kama atakuja musaidizi yake. Kisha hii wakati alimuwambia mara ingine kwa mtoto wa roho wake:

-Unataka kwenda mu mukini?

-Nitafata sauti yako, muzee wangu.

-Uende, alimuhamuru p[adri ya roho yake. Ninasadiki ya Mungu wa Padri wangu atakufunika na atakuchunga ku kila majaribu.

Na, alimuomba kwa Mungu, alimubariki na alimutuma mu mukini.

Wakati alifika mu mukini, aliuliza kujua anaikaa wapi musaidizi ya muzee fulani wa jangwa na alipata nyumba yake. Lakini, kwa bahati mbaya, hile saa alilofa na huyu na watu wa nyumba yake kwani walienda mu Kiliyo moja. Alibakia paka binti yake nyumbani yake, na huyu alisikia pigilio ya mulango aliendа mbio na alimufungula. Mutawa alimuuliza eko wapi baba yake, huyu binti alimukokota kuingia ndani. Ndugu alikataa na hasikupende kuingia. Kisha hii bugomvi binti alimukokota na nguvu ndani. Hule mutawa, kwani aliona ya kama mawazo

mabaya ya zambi ya usharati walimubamba akili yake, aliomboleza na alipaza sauti kusema kwa Mungu:

-Ee Bwana, na maombi ya muzee padri wangu, uniokoe!

Wakati alisema hii maombi kwa Mungu, kwa rafla alijipata mu nia ya kurudia nyumbani yake mu jangwa. Alifika kwa muzee padri wa roho yake na alimuelejea hii mambo.

## Watawa wa jangwa Ori na Athre

Nilitembelea wakati moja, anatusimulia mtakatifu mutawa Sisois, watawa wa wili: Mutawa Ori alikuwa mugonjwa na alimusaidia mutawa Athre. Nilibakia karibu yao masiku madogo juu ya kufunda ma fazila yao.

Siku moja mtu moja aliwaletea samaki kidogo na avas Athre alitaka kuipika juu ya kula mugonjwa mutawa Ori. Alikamata kisu na alikata samaki na hile saa padri ya roho yake Ori alimuita.

Hule aliacha mara moja kisu, ndani ya samaki, bila kuikata katikati na alikimbia mbio karibu yake! Niliona na nilishangaa utii wake kubwa, kwa sababu hasikuseme: «uniache kukata mbele samaki». Hile saa mimi nilimuuliza ava Ethre.

-Namna gani ulipata hii fazila ya utii?

-haina yangu, alinijubu, Ni ya Muzee wangu.

Alinichofesha kidogo mbali na alinisema:

-Kuja kuona na weye wa pekee utii yake kubwa.

Alibeba kipande moja ya samaki, aliiweka pa moto na aliiacha kidogo kuchoma. Kisha aliipatia hii samaki kwa Muzee yake na huyu, bila kusema sauti kimoja, aliikula. Ku mwisho alimuuliza:

-Ee Muzee, samaki ilikuwa utamu?

-Muzuri sana, alijibu.

Kisha alimuletea na samaki ingine, lakini aliichoma muzuri sana na alimusema:

-Hii samaki, Muzee, niliichomesha kidogo.

-Ndivyo, uliichoma kidogo, alisema hule.

Kisha avas Athre alinisema:

-Uliona ya kama utii inatokea ya muzee wangu?

Niliondoka. Na kila fazila niliona karibu yao nilifanya nguvu ya kuichunga mu uzima yangu yote.

## Mtoto wa roho ku mutoni

Mtoto wa roho ya muzee moja mkubwa alikuja mu Monasteri ya mtakatifu mutawa Seridos, ku muji Gaza. Alikuwa na amri yake arudie nyumbani yake magaribi. Lakini mpaka hile wakati alitaka kuondoka ilianza kunesha nvula na umeme na makelele mingi pa mbingu. Na hile mutoni ilikuwa pale karibu ilijaza na maji.

Muda ilikuwa kweli kibaya, lakini hule mutawa, katika amri ya padri wa roho yake, alitaka arudie kwake. Wa ndugu ya monasteri wlaimuomba ambakie kwao, kwani hakuna namna kutambuka hile mutoni. Lakini hule aliwaambia ya kama alipashwa kutimiza amri ya muzee wake.

Wa ndugu mukuona ya kama hawakuweze kumwaambia abakie kwao, walimusidikiza mpaka mutoni na uwazo ya kama hule mutawa ataogopa mutoni na atasikia ya kama hakuna namna kuitambuka.

Lakini, hule mutawa, bila kuogopa alianguka ndani ya mutoni. Wa ndugu walimuangalia na ushituko mingi. Walimuona kuogolea na kisha saa kidogo alifika mu ngambo ingine! Aliomba baraka yao na aliendelea njia yake.

Hawa wa ndugu walirudia na musangao yao kwa ajili ya utii ya hule mutawa.

# U V U M I L I A

## Jamaa moja ya Washahidi

Mu tarehe 20 Mwezi ya Tisa kanisa yetu inashagngilia ukumbusho ya Jamaa takatifu moja. Hii jamaa ya Washahidi walikuwa mt. Efstathios, bibi yake, jina lake Theopisti na watoto wao wa wili, Watakatifu Agapios na Theopistos.

Mu mwaka 98, kisha uzalio ya Kristu, mwanaume Plakidas, hii ilikuwa jina wa kwanza ya mt. Efstathios, anatukuzwa sawa jamadari mkubwa na mutukufu mu ufalme wa Roma. Huyu anaachana hapana paka kwa ajili ya kizazi kitukufu yake, lakini kwa ajili ya mashindi makubwa na matendo ya ushindi yake kupigana ya adui ya ufalme wa Roma. Tena ilikuwa na ma fazila ya roho yake. Huyu alikuwa tena mwenye akili, mwenye kiasi, mwenye haki na murahimu. Alikuwa roho moja nzuri, lakini alikuwa tena mupagano. Hii ma fazila umoja alikuwa na bibi na watoto wake.

Mungu aliona ma fazila na mali ya roho yake na alimukokota na hii namna. Siku moja huu jemadari Plakidas alifanya kipimo ya nvita kwa askari wake na walienda mu pori kuwapima ya kulumbata ma nyama ya pori. Swala moja alikimbia, alisimama na alimuona pa macho yake. Alienda mbio Plakidas kumubamba, lakini huu nyama aliluka mu ngambo ingine ya shimo moja. kwa rafla aliona huyu jemadari katikati ya ma sego ya nyama msalaba moja wa mwangaza na juu yake Yesu Kristu. Alisikia sauti moja iliyemuwaambia ya kama Huyu ni Yesu Kristu, Mungu wa kweli wa pekee na anamuita kusadiki na kubatizwa.

Swala alikimbia na Plakidas alirudia nyumbani yake. Mbele ya kumufafanusha kwa bibi hii jambo wa ajabu, na bibi yake alimufunua ndoto yake moja ya kama Mungu ya Wakristu alimuita kumusadiki pamoja na jamaa yake yote. Hile usiku umoja huu jamaa ilipokelea Ubatizo Orthodokse ku mikono ya askofu ya muji Roma.

Asubui Plakidas alienda mara ingine pa hile fasi aliona jana hii ono wa ajabu. Na pale alisikia na ufunuo ingine wa ajabu:

-Utateswa sawa alitesa na Yovu zamani sawa anasema Agano la kale, lakini ku mwisho utamushinda shetani.. . Kuwa muhodari, ee Efstathios, na shindani mu njia ya fazila.

-Mapenzi ya Bwana ninatakia kufanyika, alimujibu Efstathios.

Vile alisema na bibi yake Theopisti, wakati, bweana yake alimusimulia hii zungumuzu yake na Bwana Yesu Kristu.

Kisha ma siku kidogo ilianza ushindani ya hule jemadari. kwa ajili ya ugonjwa moja wlaikufa wasaidi na watumwa wa nyumba wake. Kisha waligonjwa na walikufa ma nyama na ma punda yake yote. Siku moja hile walilofa ku nyumba yao, waliingia ndani wivi na waliiba bintu yao vyote. Walibaki paka na hii manguo waliivaa. Hawa walikuwa watajiri na watukufu waklubwa ya muji Roma sawa weko wa maskini na wenye stahili ya taabu. Hile walikamata mpango watoke ya Roma mu fasi isiyokuifamia. Fasi nzuri walipata muji Yerusalema na waliondoka waende kule.

Ku mwisho ya safari yao wa bahari, mkubwa ya chombo, mtu mubaya na mwenye zambi, aliomba makuta mingi juu ya safari yake, lakini wale walikuwa wamaksini na mkubwa ya chombo alikamata bibi yake Theopisti.

Bwana wake Efstathios aliendelesha njia yake na taabu mingi rohoni yake na alifika karibu ya mutoni moja. Pale aliacha mtoto mkubwa chini juu ya kumutambusha mtoto wake modogo. Wakati alirudia kubeba na mtoto wake mudogo, aliona ya kama aliisha kumubamba simba moja.

Alipindula ma macho yake mu ngambo ingine ya mutoni na aliona ya kama na mtoto mudogo yake aliisha kumubamba imbwa wa pori moja.

Katikati ya machozi yake alikumbuka mt. Efstathios ma sauti ya Bwana Yesu Kristu na atapita mateso sawa Yovu mu Agano la kale.

Huyu mwanaume na uvumilia mingi alienda mu fasi ya Mashariki na alitumika ma shamba ya miaka kumi na sita (16).

Bwana Yesu aliwaza ya kama ilikuja wakati ya mwisho ya mateso yake. Mutawala ya ufalme wa Roma, jina lake Trayanos alituma watu wake ma fasi yote ya ufalme wake juu ya kutafuta jemadari mkubwa wake wa zamani Plakidas. Paka huyu jemadari ni mustahili kuokoa ufalme wake kwa ajili ya adui wanataka kuibamba. Mutawala alimupata na alim, upatia ma cheo yake wa zamani.

Mt. Efstathios juu ya kusaidia ufalme wa roma aliita na wa askari wapya. katika ya wale wa askari walikuwa na watoto wake wa wili, bila yeye kujua hii jambo. Wote wa wili pa hile fasi ma nyama ya pori waliwabamba, waliokolewa na saidio ya walimanji.

Hasikuwajue, lakini aliwaona ya kama walikuwa na tabia na mfano muzuri, aliwachunga karibu yake juu ya kumusaidia mu meza ya chakula yake.

Nvita ilianza na ilifika mpaka hile muji aliishi Theopisti, bibi yake. Mungu alimuchunga na huyu muzima na asiye uharibifu na hule mkuwa wa chombo alimulipiza na ugonjwa wa haraka.

Jemadari, bila kujua, aliweka hema ya musingizi yake, mu lupango ya nyumba ya bibi yake.

Siku moja watoto wake wa wili waliingia nyumbani ya mama yao, pasipoo kumufamia ya kama alikuwa mama yao na walimupatia bintu ya kufanya chakula ya mkubwa jemadari. Mpaka chakula kuwa tayari watoto walisuburia na hule mwanamuke Theopisti. Ndugu mkubwa alisimulia kwa mudogo wake, pasipo kujua ya kama alikuwa ndugu mudogo wake, juu ya wazazi na ndugu mudodgo yake, juu ya safari yao mu Yerusalema na chombo, juu ya hile jambo pa mutoni na ma nyamna ya pori.. .

Ndugu mudogo wake alishituka.

-Weey uko ndugu mkubwa wangu, alimuwaambia na sauti nguvu na alianguka ndani ya mikono yake.

Mama Theopisti alikuwa mu pisi na aliskia mazungumuzo ya wale vijana na alianza kutosha machozi kwa sababu alifamia ya kama hawa walikuwa watoto wake. Lakini alisimama kidogo na hasikuseme sauti kwao. Kisha saa kidogo alienda kwa hema ya jem, adari juu ya kutafuta hawa vijana, wasaidizi wake. Wale walilofa hile saa. Lakini alipata jemadari aliyeikaa chini ya kimvuli ya muti moja. Alimuangalia muzuri na alianza kufamia mfano ya bwana wake. Alimukaribia na alimusimulia hadisi ya uzima wake. Wazazi walifamiana. Furaha yao hakuna namna ya kuisema. Walianguka moja ndani ya mikono ya mwingine. Waliliya na walimutukuza Mungu.

-Watoto wetu weko wapi? aliuliza mama Theopisti?

-Watoto wetu waliwakula ma nyama ya pori, alijibu bwana wake, na alimusimulia hadisi ya uzima wake.

-Tunapashwa sasa kumutukuza Mungu mara ingine, alimusema mt. Theopisti. watoto wetu wanaishi na weko katikati yetu! Nilisikia wakati walizungumuza kila mumoja juu ya uzima ya jamaa yake na nilisikia ya kama hawa weko watoto wetu. Jemadari mwenye ajabu aliwaita vijana wa wili na alikikishwa ya kama hawa weko watoto wake.

Furaha yao hakuna mupaka. Kisha miaka kumi na sita walijiungana. Pamoja na jamaa ya jemadari inashangilia na kundi ya askari wake.

Mungu alimulipa huu jamaa takatifu kwa hii uvumilia aliifanya, lakini sasa anamutayarisha na taji ingine munene na wa milele.

Mushindi na mutukufu sasa alirudia mu muji Roma jemadari Efstathios. Mutawala ya ufalme sasa alikuwa mufwasi ya Trayanos, jina lake Adrianos. Alitayarisha taifa wake juu ya

kutoa sandaka mbele ya ma sanamu yao kwa ajili ya ushindi wao. Lakini mt. Efstathios na nguvu mingi alimuwaambia:

-Ee mfalme, mimi ninaabudu Yesu Kristu. Huyu ninamutukuza na ninamushukuru ya ma tendo mazuri yake. Kwa Huyu ninaparia uzima na nafsi yangu. Huyu alinipatia uwezo na nilishinda wa adui ya ufalme wako. Huyu alinistahili na niliona na nilijiungana pamoja na bibi na wtoto wangu. Mungu mwingine misijue, wala nisadiki paka Huyu aliyeumba mbingu na inchi yetu.

Hii onyesho ya imani yake alifanya alimushitusha mfalme Adrianos. Wapadri wa pagano na wakubwa ya wa askri wapagano walisikitika na ma uso yao ilijaza na kisilani.

Mfalme alisirika na alimuhamuru mtakatifu Efstathios kutosha musipi yake (alama ya cheo yake) na kusimama mbele yake sawa mukosefu na mwenye kuhukumiwa. Alifanya nguvu juu ya kugeuza mufano na imani na roho yake, lakini hakuna namna. Na huyu mutukufu jemadari mwokozi ya ufalme wake walimuhukumu pamoja na jamaa yake wakufe.

Waliwapeleka pa kiwanja moja na waliacha simba mukali moja juu ya kuwakula. Lakini simba aliwakaribisha, aliwasujudu na lirudia mukongo. Kisha walifanya mfano moja ya ngoimbe toka chuma na waliweka ndani ya tumbo yake huu jamaa kitakatifu. Chini ya hii mfanmo ya ngombe waliwaakisha moto.

Kisha ma siku tatu, walifungula hii mufano ya ngombe ku chuma na ma nafsi yao waliisha kutoka mbinguni, lakini miili yao walikuwa mzima, na hata manyonya moja ya ma nywele yao haikuharabike, katika mapenzi ya Bwana Yesu Kristu.

## Mutawa wa kwanza muzee

Wakati mt. mutawa Paulo wa mupole alikamata mpango kufanyika mutawa, kisha safari mu jangwa ya ma siku mengi alifika pa hile mulima aliishi mt. Antonio. Alitafuta na alipata na pango yake. Alikokola na heshima mulango ya pango yake. Mtawa alifungula. Mt. Paulo alimuelejea na ma sauti kidogo sababu gani alifika kwake.

-Ninataka kuwa mutawa, ee Ava.

Mt. Antonios alishituka kidogo na alimujibu:

-Ulikamata mpango ya kuchelewa sana.. . Mtu wangu pa hii kipimo ya umri yako, usiweze kuwa mutawa ndani ya hii jangwa ugumu. Rudia mu fasi yako, tumika tena miaka kidogo na kisha utaishi uzima yako na utamushukuru Mungu.

-Unibebe, Ava wangu, alimuomba mt. Paulo. Ninakulaka ya kama nitafata sauti yako ya kila mambo.

-NInakuwaambia na mara ingine. Uko muzee sasa, usiwe nguvu ya kutumika kazi ya roho mu jangwa. Kama unataka kuwa mutawa, uende mu monasteri moja, pale uzima ya watawa haina ugumu sawa hapa mu jangwa. Mimi, sawa na weye unaniona, ninaishi huku wa pekee. Ninakula mara moja kila ma siku tano, bila kuzimba.

Lakini mt. Paulo alimuuzi mara ingine kumuchunga kwake. Wakati mt. Antonios aliona ya kama huyu muzee asisikie sauti yake, alifunga mulango ya pango yake na alimuacha huyu muzee inje. «Vile ataondoka», aliwaza.

Mt. Antonios alibakia ndani ya pango yake, bila kutoka inje ma siku tatu. Kisha alifungula mulango yake. Alishangaa kwa sababu alipata kuikaa inje na mt. muzee Paulo! Alimuheshimiwa, lakini alikataa kumuonyesha ya kama anaitika na anamupokelela.

-Toka, ee mtu wangu mubarikiwa na usinisikitishe. Misiweze kukubeba kwangu.

Lakini na mt. Paulo sasa alikuwa kupita mwenye imara mu mpango wake.

-Misienda hata fasi ingine, alimujibu. Ao utanipokea ao nitaikaa huku inje na watanikula ma nyama makali ya pori!

Mt. Antonios hasikuongojee mpango moja wa nguvu sawa hii mpango ya huyu muzee. Tena alisikia ya kama hii ma siku tatu alikuwa inje mt. Paulo bila chakula na maji. Basi, aliogopa

ya kama, kama atabakia inje ao atakufa kwa njaa, ao watamukula ma nyama ya jangwa na atakuwa na ujukumu mu nafsi yake.

Basi, alimwaambia kuingia ndani ya pango yake. Alimuweka kuikaa mu fasi moja ya pango yake na alimufundisha namna gani atafanya na nyusi ya mayani ya kukauka vituga.

Hule muzee mwenye njaa na mwenye muchoko na asiyekulala alifanya kazi na mikono yake ya kusimama na ugumu mingi. Hasikuwa na zoezo kwa hii uzima ugumu! Lakini alifanya nyusi na hii mayani metre kumi na tano (15). Aliendelea kazi yake pasipo kuonyesha ya kama alichoka.

-Mt. Antonio alimufokea, juu ya kumupima uvumilia na utii wake: Hii kazio ulifanya iko kibaya sana. Nilikuwaambia ya kama uko muzee, bila nguvu na akili ya kuishi huku na kutumika. Unaikaa? Rabisha mara ingine hii kazi ulifanya; iko mubaya; usisikie?

Mt. Paulo hasikuseme sauti moja ku kinywa yake juu ya kusema: «Hapana kazi yangu ni muzuri; ao nilikuja sasa na pole-pole nitafunda kupita muzuri.. .  ». Aliharabisha hii mustari aliisha kufanya na alianza kufanya ingine mupya. Sasa kazi yake ilikuwa kuliko kibaya kwa sababu mayani iliisha kufumbala.

Mt. Antonios alitaka kumupima na alijikikisha juu ya ma fazila yake manene. Wala alisikitika, wala alionyesha pa uso yake ya kama alipotesha uvumilia yake!

Wakati jua ilianguka chini mu fasi ya magaribi, alikamata mpango mt. Antonio amuulize:

-Unataka tukule kidogo mukate, ee muzee?

-Sawa vile weye unataka, ee Ava.

Aliwaza na musangao mt. Antonios: «alibakia huyu mutu ma siku mengi bila kula na hasikuseme ya kama anaikaa na njaa.!

-Tayarisha meza, alimuhamuru.

Mt. paulo alitayarisha meza. Mt. Antonios alileta vipande inee ya mukate ya kukauka; moja juu ya maungo yake na tatu juu ya mtoto wa roho mupya yake. Ku mwanzo alisema na ma zaburi kumi na mbili, katika zoezo yao wa zamani. Alimuona na huyu mutawa mupya ya kama aliomba na yeye, bila kusema mbio, kwani alisikia njaa.

Iliisha kuwa usiku na waliikaa kula pamoja. Mt. Antonios alikula mukate yake mbio na alimuongojea. Na huyu mutawa mupya alikula mukate moja na alisimama.

-Ee muzee, kula na mikate ingine.

Kkama utabeba weye mukate ingine, nitabeba na mimi.

-Kwa mimi mukate moja inenea. Mimi niko mutawa.

-Basi inenea na kwa mimi, kwani na mimi ninataka kufanyika mutawa!

Kisha chakula yao ya usiku mt. Antonios alisema ma zaburi yake katika zoezo yake na walienda kupumuzika kidogo. Walilamuka katikati ya usiku juu ya kuendelesha sala yao mpaka asubui.

Wakati aliona mt. Antonios ya kama huyu mutawa wa kwanza alimufata kabisa sawa alikuwa kijana, kisha ma juma madogo alimusema:

-Ee Ndugu wnagu, ninasadiki ya kama weye uliona namna gani mimi ninaishi mu jangwa. Kama unazania ya kama utaweza kufanya na weye hii uzima umoja, bakia karibu yangu.

-Misijue kama ukona matendo wa roho ingine nionyeshe mpaka sasa, alimujibu mutawa mupya. Hii yote matendo yako nitaifata na nitaifanya bila mambo na mbio-mbio.

Hivi mt. Antonios alimufanyishia mutawa na alimusaidia kujenga na chumba yake na simbala na bulongo, kidogo mbali ya pango yake.

-Sasa, na saidio ya Mungu ulifanyika mutawa, alimusema. Basi, mbakia weye wa pekee mu chumba yako juu ya kupima na ma jaribu yote ya ma shetani. Hivi utafanyika mwenye akili mbele ya mashindani wa roho yako.

Huyu muzee mupole alishindani na namna ugumu. Katika uvumilia na unyenyekevu yake aliweza kupanda pa kipimo murefu ya ma fazila matakatifu na Mungu alimupatia ma zawadi mengi!

## Mateso wa miaka mengi

Wakati mt. Mutawa mwanamuke Sigklitiki alifika mu kipimo ya umri yake miaka 80 aligonjwa na malari matata na aliivumilia sana.

Ku mwanzo iliharabika ma pumu yake na alitosha ku kinywa damu. Pempeni kivukutu urefu ilimubamba na alilekea sawa mishumaa.

Vile alitesa kupita mingi ya washahidi! Mateso yake ilikuwa wa miaka mengi na bila usimamisho. Mt. Sigklitiki aliteswa ya waakti miaka tatu na kipande pa kitanda na moto moja wa ndani ilimulungua mu tumbo na pumu yake!

Alivumilia hii mateso yake bila kusimama ya kufunda watawa wake na waaminifu ya monasteri yake.

Ilikua wakati na huyu mutawa aliyekuwa sawa chemchem ya fundisho ya Mungu ilisimama.. . ku mwanzo ilimuuma rino moja. Kisha hii malari yake ilienda na ma meno ingine. Kisha miezi mbili hii ugonjwa ilipita ndani ya mifupa yake. Sa harufu moja mubaya ilitoka ku mwilio yake na wa dada wake hakuna namna kumukaribisha na kumuvumilia. Juu ya kumukaribisha waliweka mbele ubani.

Sasa mtakatifu Sigklitiki alisaidia wa dada wake hapana na neno yake, lakini katika uvumilia yake.

Mungu alimupatia matulivu wa roho manene na alimustahili kujua siku na saa ya lufu yake. Hivi alikamata taji ya mashindani yake.

## Mtakatifu Monika

Mt. Monika (332-388) alizaliwa mu muji Tagasti ya Numidia wa inchi Livii na wazazi wakristu ya Mungu. Huyu alikuwa mama ya mt. Avgustinos, mutheologo na mwenye hekima mukubwa ya kanisa yetu.

Wazazi wake alimuowa mu mwaka 350 na mwanaume moja mupagano, aliyekuwa mtu na roho nzuri, lakini ilimubamba sana hasira. Mama Monika na uvumilia yake alishindana na alimuongoza bwana wake kwa imani ya Kristu. Tena na uvumilia na mapendo yake alimuvumilia na muke yake, aliyekuwa na tabia mubaya na jivuno na alimunyenyekesha..

Wakati mtoto wake mudogo Avgustinos aligonjwa na alikuwa karibu ya kufa. Waliwaza hile saa kumubatiza. Mama yake, alijua ya kama mtoto wake mu kipimo ujana wake atakuwa na mambo ya umri yake mingi na alikataa kumubatiza.

Pamoja na maziwa mama yake alimupatia na heshima na mapendo ya imani ya Kristu. Lakini mtoto yake alikuwa na ma zoezo ya baba yake. Alikomea mu kipimo yake na pamoja walikumea na ma zoezo mabaya ya mwili yake. Alifanya sala kwa Mungu mama Monika, lakini sasa sala yake Mungu hasikuisikie.

Avgustinos alienda mu muji Karkhidona juu ya kufunda. Kule alianguka ma zambi ya mwili. Mama yake alitangazwa ya kama mtoto wake anaishi uzima mubaya. Alienda karibu yake amusaidie, lakini roho ya mtoto yake iliisha kuharabika. Hasipotee lakini nguvu wake. Anakombana kumusaidia juu ya kuzarau zambi ya mwili. Lakini hakuna namna mususikia mtoto wake. Mama yake hasipotee kitumaini yake. Anasali kwa Mungu na anatosha machozi mingi mbele ya Mungu.

Alisikia uchungu mingi mu roho yake, wakati alisikia ya kama mtoto wake mu umri miaka yake 18, aliishi na mwanamuke moja mwenye zambi na alizamla na mtoto pamoja naye! Anatumainia kwa toba yake.

-Mtoto wangu, alimuwaambia, siku moja utakuja na weye kwa hii imani na uzima yangu.

Tangazo ingine ilikuja ku muji Karkhidona ya kama mttoo wake alifata fundisho wa uwongo. Alifanyika Manikheos! Alitaabu sana mama yake. Alienda mara ingine mu muji

Karkhidona, analia, anaomboleza anamuomba kurudia na kutubu mtoto wake. Lakini hakuna namna.

Utulivu yake sasa na kitumaini ni sala mbele ya Mungu. Alikimbilia kwa askofu moja na huyu alimushauria na alimutulivu hivi: Ku mwisho alimuwaambia:

-Uende mu baraka ya Mungu, mtoto wangu. Hasitapotee mwana wako, kwani mama yake alitosha machozi mengi juu ya toba na uzima mupya yake!

Mungu alitaka kupima tena uvumilia ya mama Monika. Avgustinos, alimusema, ya kama ataenda mi Italia. Mama yake alikamata mpango aende pamoja naye. Walishuka mu kikavu, lakini mwana wake alimulanda na alikimbia na chombo ingine.

Mama yake aliomba kwa Mungu:

-Ee Bwana wangu! anafokea kwa Mungu. Ninaacha mtoto wangu kwa bahari ya wema wako! Mawimbi ya neema Yake, ninatakia kuongoza mtoto wangu mu kikavu Yako!

Alizeka mama Monika mu masomo ya uvumilia na kitumaini. Aliacha inchi yake mu Livii ya Afrika na alikuja mu muji Mediolana ya Italia.

Pale ataangalia jambo ya kurudia mtoto wake kwa Mungu. FUraha moja inamufata ingine. Mtoto wake alizarau wale walifata fundisho ya uwongo na aliwaacha. Alianza kufata mahubiri ya askofu ya muji Mediolana, jina lake Amvrosios.

Avgustinos anakombana ndani yake. Minyororo ya zambi zake ndani ilianza kulekea, lakini bado kupasuka.

Avgustinos alikamata mpango kurudia mu Kanisa ya Kristu na kutumika juu ya utukufu Yake.

Nani sasa ataweza kusema furaha ngapi alisikia Mama Monika, wakati aliona mtoto wake kubatizwa? Hapa iliisha kazi yake sawa mama. Aliona mtoto wake ndani ya mikono ya Mungu.

Mama na mtoto walianza kurudia mu Afrika, lakini mama yake karibu ya hile fasi inatosha maji yake mutoni Tiveris ya inchi Italia, aligonjwa na alikufa na umri yake miaka 56, katika amani na alipatia nafsi yake kwa Mikono ya Kristu.

## Ma taji saba

Muzee moja mutawa alibaki ndani ya pango moja ya jangwa na alikuwa na karibu yake na mtoto wa roho moja. Muzee kila usiku alikuwa na zoezo kusema kwa mtoto wake ma shauria ya kuachana. Kisha alimupatia baraka na alimutuma kupumzika.

Siku moja walikuja kundi moja na waamnifu, wenye walikuja kusikia mafundisho ya huyu padri. Wakati waliondoka wale watu, muzee, katika zoezo yake, aliikaa na alifunda mtoto wake. Lakini, hile saaa limufunda, kwani alikuwa wa muchoko, alimubamba musingizi. Mtoto wake, lakini hasikuende kulala. Alibakia pale na alimuongojea muzee wake mpaka atalamuka juu amupatie baraka yake ya wenda kulala na yeye.

Saa ilipita na muzee hasikulamuke. Mawazo walianza kumuuzi huyu mtoto kijana juu ya aende na yeye kupumzika, bila kubeba baraka ya padri wa roho yake. lakini mtoto alikataa aende kupumzika. Uwazo hii ilikuja mara saba na mtoto alimufukuza hii uwazo mara saba.

wakati usiku ilipita, alilamuka muzee wake na aliona mtoto wa roho wake kuikaa karibu yake na alimuuliza:

-Bado kutoka ya musingizi?

-Hapana, alimujibu hule, kwa sababu bila baraka yako namna gani nitaenda kulala?

-Na juu ya nini usinikulamusha?

-Misikupende kumiuzi.

Hile saa walilamuka na walianza ibada ya asubui. Kisha Muzee alimutuma mtoo wake aende kupumzika. Na, waakti muzee alikuwa huyu wa pekee aliona kiti moja wa zahabu na juu yake walikuwa ma taji saba. Kisha muzee aliuliza malaika moja: Hii kiti ni ya nani pamoja na ma taji saba?». Hule malaika alimujibu: «Ni ya mtoto wa roho yako. Hii Kiti alimupatia Mungu tangu hile siku aliacha dunia na alifata hii uzima ya watawa. lakini hii ma taji wa saba, inapashw

akujua weye ya kama Mungu alimupatia hii usiku». Alishituka Muzee na aliogopa. Alimuita, basi, mtoto wa roho yake na alimuuliza:

-Uniambie, ulifanya nini hii usiku?

-Unihurumie, muzee wangu. Misikufanye kintu.

Na padri ya roho mukuzania ya kama kwa ajili ya unyenyekevu yake alisema hivi, alimusema:

-Misitakuache mpaka utanielejea, ulifanya nini hii usiku.

Na mwanafunzi wake, bila kuwa na kintu kimoja ndani ya zamiri yake na bila kujua atasema nini, alimujibu:

-Unihurumie, padri wangu. Misikufanye kintu paka hi: «Uwazo ilikuja mu akili yangu mara saba na iliniuzi niende kupumuzika na mimi, lakini niliijibu namna gani nitaenda, bila kubeba baraka ya padri wangu? Na hivi misikutoke.

Wakati alisikia hii sauti yake padri wake alifafanusha ndani yake juu ya hii ma taji saba aliona mu ono yake usiku. Kisha kila uwazo mtoto alimufukuza na Mungu alimupatia na taji moja. Ni kweli ya kama padri ya roho yake asikumwaambie kwa mtoto wake hii jambo, lakini aliisema hii ono kwa watu wengine juu ya faida ya roho yao. Ni kusema Mungu juu ya bugomvi wa roho yetu udongo anatupatia ma taji wa milele!

## Ma chawa na ma siafi

Mutawa moja toka Monasteri ya mt. Ekaterini ya Mulima Sinaya alitoka kuishi mu jangwa. lakini shetani tangu mwanzo alimukombana sana. Pango yake pa hile fasi alilala ilijaza na ma chawa! Kutoka chini mpaka mufuniko ya pango ilijaza na ma chawa. Mukate na maji na ma nguo yake yote ilijaza na ma chawa.

Muzee alivumilia na uhodari hii majaribu na alisema kwa shetani: Kama ni lazima nikufe huku, misitaondoke ya hii pango mapaka itafika Shangilio ya Paska.

Siku moja ya Juma wa tatu ya Kwarezima muzee aliona asubui moja ya kama pango yake ilijaza na ma siafi manene. Waliingia ndani ya pango na walianza bugomvi moja munene pamoja na ma chawa. Ma siafi waliuua wote ma chawa na waliwafukuza inje ya pango.

Mungu katika hii namna aliripa uvumilia ya hule mutawa wa jangwa na alimuuhuru ya majaribu ya shetani.

## Sauti ya kushitaki

Mutawa moja aliuliza padri  moja mkubwa:

-Namna gani shetani anafanya bugomvi kupigana ya watawa na watakatifu?

Na hule alimusimulia hii jambo ifwatayo:

-Mu Kilima Sinaya aliishi mutawa Nikon. Hile wakati mwanaume moja aliingia mu hema ya mwanaume mwingine, lakini ndani alikuwa paka binti yake. pamoja naye alifanya zambi ya uzini (zambi ya mwili). Mbele ya kuondoka alimuwaambia: «Kama mtu moja atakuuliza na mtu gani ulifanya hii zambi, utamujibu nilifanya hii zambi pamoja na mutawa Nikon».

Waakti baba wake alirudia mu hema yake na alimwaambia hii sauti binti yake, huyu alikamata kisu moja murefu na alienda mbio mu chumba ya hule mutawa Nikon. Alikokola mulango, alitoka inje muitawa na huyu mwanaume alinyanyua kisu kumuua. Lakini kwa rafla mukono yake ilibaki bila kutengwa, sawa kupooza! Alienda huyu mwanaume mu kanisa kusema hii jambo kwa watawa na wakubwa wengine. Wale walimuita hule mutawa wa jangwa. Wakati alikuja walimubamba na walimupiga sana na mwili yake ilijaza na vilonda! Kisha walitaka kumufukuza. Mutawa Nikon aliwaambia kuongojea kidogo.

-Muniacheni, wapadri wangu, huku kutubu.

Walimuacha kuikaa na yeye mu fasi mbali ya watawa wengine na amri hata mtu moja hapana kumutembelea!

Aliishi mutawa Nikon kule miaka tatu paka yeye wa pekee. Paka kila mu Juma alikuja mu Mukini ya watawa, alionyesha kitubio yake na aliomba ya watawa wote:

-Ninamiomba, mufanya sala juu ya mimi!

Lakini wakati moja, hule mtu alifanya zambi na binti ya mtu mwingine na alimushitaki huyu mutawa Nikon, sasa aliingia pepo buchafu ndani yake na alimuteswa sana! Basi, alikuja mbele ya watawa ya hile mukini na aliungama mbele yao:

-Mimi nilifanya hii zambi, lakini nilisema kwa binti kushitaki huyu mutumishi ya Mungu.

Basi, watawa wote waliondoka na walienda kumukuta huyu padri Nikon na walimuwambia:

-Utuhurumie, tunakuomba, padri wetu!

Na huyu na mapendo mingi aliwasamahe!! !

Ku mwisho alisema huyu muzee kwa hule mutawa kijana:

-Unaona sasa namna gani shetani anagombana na majaribu mengi watu wa Mungu?

## Chai ya mugonjwa moja

Muzee moja aligonjwa na hasikuweze kukula chakula.

Siku moja alisema kwa mtoto wa roho yake amupatie kunywe chai ya kivukutu. Hule alienda, alifanya maji ya kivukutu na, kwani hakuna chai, alitafuta sali. Lakini alifanya kosa na badala ya chupa ya sali alibeba chupa ya mafuta iliye iliisha kuharabika, kwani ilikuwa wa zamani.

Aliweka pa moto na alimuletea.

Mugonjwa aliipima, lakini hasikusema sauti. Aliicha na upole. Mtoto wa roho yake alimusukuma akunywe. Muzee yake alisukuma maungo yake akunywe. Na, wakati mtoto wake alimusukuma akunywe mara ya tatu, padri alimujibu:

-Misiweze na misitake mtoto wangu.

Mtoto wa roho yake juu ya kumwaambia ya kama hii maji na sali ni ya muzuri, alimusema:

-Ee Muzee, ni nzuri. Angalia, ninakunywa na mimi.

Lakini, wakati aliipima na alisikia alifanya ninyi, alianguka na uso yake chini mbele ya mpadri wa roho yake mukusema:

-Ole wangu, Muzee wangu, nilikuua! Na wewe bila kusmea sauti, ulitupa zambi juu yangu.. .

Kisha muzee wake alimujibu:

-Usitaabu mtoto wangu. Kama Mungu alitaka nikunywe sali, ilikuwa namna Mungu akuangazie akili yako ya kuweka sali na hapana mafuta uchungu!

## Padri mkubwa mugonjwa

Padri mkubwa Antonios ya njimbo Optina ya inchi Rusia (1795-1865), wakati alirudia mu monastyeri yake, kwani alilofa miaka mengi, alisikia furaha mingi na aliandika hivi:

«Sasa uzima wangu-utukufu kwa Mungu- ni wa ukimya na wa furaha, lakini magonjwa wangu walinilekehsa sana na maumivu pa miguu yangu na pa meno wanakomea sana. Lakini wananipatia faida ya roho. Kwa ajili ya zmabi zangu zote inagonjwa mwili inagonjwa na nafsi.. . Lakini utukufu kwa Mungu. Ninamushukuru. Ananipatia nguvu na ninaenda kila siku mu kanisa Yake. Kisha ninakula pamoja na wa ndugu wote mu meza. Mu chumba yangu misina na kintu, paka maji ya baraka! Ma panya wanazunguluka kutafuta chakula, lakini mimi ninakula mu meza. Ninaishi mu monasteir mimi wa pekee. Unipe, ee Mungu wangu kuishi hivi mpaka mwisho ya

uzima yangu! Ninasikitika paka ya mambo moja, ya kama kwa ajili ya maumivu ya miguu yangu, misiweze kutembea na kutumika».

VIle alikombana mu uzima yake padri Antonios wa Optina. Kwa ajili alisimama ma saa mingi ilifanyika pa miguu yake vilonda na ilitoka buchafu mbaya!

Huyu muzee ya wakati miaka makumi tatu (30) aliteswa na maumivu mengi. Alisikia ya kama sawa mtu moja alimukata miguu yake na kisu! Ilikuwa miguu yake ya kujaza na dami ya kunenepa na sawa mbau! Na tena walitosha na buchafu. Munganga aliyeona miguu yake alitosha ku ndani ya vilonda bilulu!

Alivumilia hii mateso yake, kwa sababu aliomba ya kwanza faida ya roho yake, utulivu ya roho na baraka ya utii.

Mtu moja alimutembelea na, wakati aliona namna gani aliteswa, alimwaambia:

-Kwako, ee Muzee inatimiwa neno ya Madioko Takatifu: «Mateso ya mwenye haki ni mengi! »

Padri Antonios alimujibu: Kwangu inatimizwa neno ya Nabii Daudi: «Mateso ya mwenye zambi ni wingi».

Watu wengine walimwaambia ya kama anafanana na mtu mwenye haki Yovu, lakni padri Antonio aliwajibu:

-Mateso yangu yote haina na stahili hata ombolezo moja ya Yovu mwenye haki».

Mtu mwingine alimujibu:

-Ninataabu mingi kwa maumivu yenu. Tena ninaona ya kama Mungu anamipenda, kwa sababu ya kila ombolezo na umivu yenu anatayarisha na taji moja wa milele.

-Ole kwangu, alimujibu hule. Misifanye kintu hata kidogo! Na kwa hile saa ya uhukumu Mungu atanihukumu sana kwa zambi zangu.

Padri mkubwa Antonioa alifuchika ma fazila yake na alionyesha mbele ya watu uso yake wa furaha na wa mwangaza. Alipokelea watu na uso wa mwangaza na mepndo. Alisuburia na wao paka wa furaha. Aliwasalimia na urafiki.

Aliteswa kabisa, lakini hasikulofe ya Ibada ya kanisa. Alikombana tena kuwa ndani ya kanisa mbele ya mwanzo ya kila Ibada.

Ilikuwa mambo ya ajabu kuona muzee moja na maumivu mingi na aliikaa ndani mpaka mwisho ya Ibada ya asubui. Kisha alirudia na maombolezo nyumbani yake.

Juu ya sala aliwafundisha watu hivi:

-Kama ilikuja saa ya sala, tunapashw akulamuka ku kitanda sawa kwa mfano nyumba yetu inawaaka ma moto! .. . Mwanzeni kufanya sala na mapendo. Mbio roho yenu itapata kivukutu, kwani Mungu ni moto wa roho! Analungua mawazo mabaya na analeta kivukutu mu roho yetu!

## Padri na wasaidizi wake

Mu muji Athina ya Grekia aliishi padri moja mtakatifu, jina lake Nikolaos Planas (1851-1932). Siku moja alienda mu kanisa moja kufanya p. Nikolaos Liturgia, lakini mpadri mwingine alisuburia na watu wakubwa ya kanisa juu ya kumutuma padri Nikolaos mu kanisa ingine, ya mt Georgios mu fasi Kukaki.

Wakati alisoma ibada ya Komonyo Takatifu walikuja na walimusema:

-Padri Nikolaos, leo utaneda kufanya liturgia mu kanisa ya mt. Georgios mu Kukaki.

-Na furaha mingi, alijibu padri mupole na aliendelea ibada ya asubui. Bado kuwa asubui.

Kisha saa moja alikuja mtu wa kanisa mwingine na alimwaambia:

-Padri Nikolaos tuligeuza mpango. Utafanya Liturgia huku.

-Na furaha mingi, alijibu mara ingine.

Ilipita saa moja. Kisha mazungumuzo na makelele yao mengi walikamata mpango. Walikuja kwa padri na walim, uwaambia:

-Padri Nikolaos, tuliwaza mara ingine na tulikamata mpango leo utaenda mu kanisa ya Mt. Georgios kufanya Liturgia.

-Na furaha mingi, aliwajibu mara ingine.

Ilikuja karibi ya kufika asubui. walikuja wakubwa ya kanisa na walimwaambia>

-Padri Nikolaos, hii ni mpango yetu wa mwisho: Utafanya litrurgia huku.

-Kuwa ubarikiwa, aliweajibu na unyenyekevu.

Waaminifu wenye walikuwa ndani ya kanisa na waliona hii jambo, walisirika na wlaikuwa tayari kufanya funjo ndani ya kanisa. Juu ya nini wanateswa huyu padri muzee na mupole?

Ku mwisho, wakati padri Nikolaos alianza kuvaa manguo matakatifu yake, walikuja na walimusema:

-Mbio, padri Nikolaos, utaenda mu kanisa ya mt. Georgios.

Hasikuseme sauti hata moja. Alianza kuondoka na alibeba njia ya mt. Georgios.

Wakati alivaa manguo matakatifu yake na alikuwa tayari kuanza Liturgia alikuja mbio mbio mtu moja ya hawa wakubwa ya kanisa na alimuwaambia ya kama inapaswa kurudia mbio na atafanya Liturgia mu kanisa ya Mt. Yoano! .. .

Mambo gani ilikuwa?

Mu Kanisa ya mt. Yoano, aliisha kuja mama moja mkubwa na alimutafuta. Aliuliza wakubwa ya kanisa eko wapi padri Nikolaos?

-Eko mu kanisa ya mt. Georgios. Pale sisi tulimutuma.

-Mulifanya nini? Leo hii siku mulilutuma kwa mt. Georgios?

Mwende mumuletee mbio hapa.

Kisha wakubwa walienda kumurudisha mukongo.

Na kweli padri Nikolaos alirudia na kichwa yake chini na muchoko mingi. Na hile siku alifanya mu hii Kanisa ya mt. Yoano liturgia moja ya utukufu mingi!

**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU**
**MWEZI YA SABA**
**GREKIA**
**2000**

Τό παρόν βιβλίο <Χαρίσματα καί Χαρισματούχοι> πού είναι συλλογή ιστορική καί Έκδοσις της ‘Ιεράς Μονής Παρακλήτου ’Ωρωπού ’Αττικής, μεταφράσθηκε τόν ’Ιούλιο τού 2000 στά σουαχίλλι πρός πνευματική ωφέλεια του Ορθοδόξου Αφρικανικού λαού.

‘Ο μεταφραστής Μον. Δαμασκηνός Γρηγοριάτης.